# TATHMINI YA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA UWASILISHAJI WA HABARI ZA MAZINGIRA KATIKA GAZETI LA *TAIFA LEO* LA KENYA

**NELLY NZULA KITONGA**

Tasnifu iliyowasilishwa katika Idara ya Lugha, Fasihi na Utamaduni kutosheleza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamifu katika Kiswahili, ya Chuo Kikuu cha Maasai Mara

2023

## UNGAMO NA IDHINI

**Ungamo ya Mwanafunzi**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kingine chochote.

SAINI………………………………….. TAREHE ................................................

Nelly Nzula Kitonga DA05/4001/2015

**Idhini ya Wasimamizi**

Tasnifu hii imewasilishwa katika Chuo Kikuu cha Maasai Mara kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya Uzamifu katika Kiswahili kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

1. SAINI ................................ TAREHE ..............................

   Mwalimu Silas Owala (PhD)
   Idara ya Lugha, Fasihi na Utamaduni
   Chuo Kikuu cha Maasai Mara

2. SAINI ................................. TAREHE ...............................

   Dkt. Jane Ombati
   Idara ya Lugha, Fasihi na Utamaduni
   Chuo Kikuu cha Maasai Mara

# TABARUKU

Kwa watoto wangu wapendwa Benjamin Matei Kitonga na Ann Mwende Kitonga.

# SHUKRANI

Kwanza kabisa ninamshukuru Mungu ambaye ameniwezesha kuikamilisha hii kazi. Ninakiri ya kwamba ‘hapo nimefika Bwana Yesu ni kwa nguvu na uwezo wako’.

Pili, ninawashukuru walezi na wasimamizi wangu, Mwalimu Silas Odhiambo Owala (Ph.D) na Dkt Jane Ombati kwa kunishauri na kunielekeza katika uandaaji wa makala dhanishi, uandishi wa pendekezo la utafiti na tasnifu. Asanteni sana kwa kujitolea kwa dhati kuhakikisha kuwa mradi huu umekamilika.

Tatu, ninatoa shukrani kwa wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Maasai Mara ambao walinielekeza kiakademia hadi nikakamilisha masomo katika kiwango hiki. Daktari Nancy Ayodi na Daktari Alexander Meitamei Mungu awabariki.

Ninatoa shukrani za dhati kwa mume wangu James Kitonga Mutisya na watoto wetu Benjamin Matei Kitonga na Ann Mwende Kitonga kwa kunivumilia na kunihimiza kuendelea katika safari ya masomo.

Ninawashukuru sana wazazi wangu Simon Nduu Ngundo na marehemu Rael Ngali Nduu kwa kunifunza umuhimu wa elimu tangu utotoni.

Shukrani zangu za dhati zimwendee mwalimu mwenzangu, Dkt. Alex Kevogo, kwa kunilea kitaaluma.

Ninawashukuru dada zangu Jane Nduku, Esther Mbithe, Evelyne Wayua, Mercy Wavinya na Lydia Kanini pamoja na wapwa wangu Faith Nthenya na Mercy Kambua kwa kunitia moyo wakati nikisoma.

# IKISIRI

Utafiti huu unahusu tathmini ya matumizi ya lugha katika uwasilishaji wa habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya. Gazeti la *Taifa Leo* huwasilisha habari kwa wasomaji kwa lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili inatambuliwa na Katiba ya Kenya kama lugha ya taifa na pia lugha rasmi sambamba na lugha ya Kiingereza. Mazingira ni suala mtambuko na nyeti kitaifa na kimataifa. Mazingira yanaathiri maisha ya kila kiumbe kila siku kwa njia moja au nyingine. Inatarajiwa kwamba, kwa vile vyombo vya habari, Gazeti la *Taifa Leo* likiwemo, vimetwikwa jukumu la kuwapasha wanajamii yale yanayoendelea duniani kuhusiana na mazingira, vitafanya hivyo kwa namna ambayo itawawezesha watu kufahamu umuhimu wa mazingira na hivyo kuingiliana nayo kwa njia chanya. Hoja hii inatokana na imani kwamba mtu huthamini na kutunza kile anachofahamu thamani yake. Uchunguzi huu ulinuia kubainisha iwapo matumizi ya lugha katika kueleza habari za mazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* hufanikisha mawasiliano. Uchunguzi huu ulidhamiria kutimiza malengo yafuatayo: kuchanganua vipengele vya lugha vinavyoteuliwa na waandishi wa habari katika kuripoti habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo,* kutathmini mtindo wa uwasilishaji wa habari za kimazingira na kubainisha ujumbe uliowasilishwa na waandishi wa habari katika gazeti la *Taifa Leo*. Nadharia zilizotumika katika utafiti huu ni Nadharia ya Uchanganuzi Usemi (NUU) iliyoasisiwa na Michel Foucault (1928) na baadaye ikaendelezwa na Norman Fairclough (1989) na Nadharia ya Umtindo (NU) ambayo iliasisiwa na Geoffrey Leech (1965-1966) na ikapaliliwa na Simpson (2004). Utafiti huu ulifanyika maktabani ambapo taarifa kuhusu habari za mazingira zilizochapishwa katika gazeti la *Taifa Leo* zilichanganuliwa. Magazeti ya *Taifa Leo* yaliyochapishwa kuanzia Januari 2021 hadi Machi 2022 yaliteuliwa kwa kudhamiria, hususan yale yaliyokuwa na habari kuhusu mazingira. Data ilikusanywa kwa kudondoa matumizi ya lugha, mtindo uliotumiwa katika uwasilishaji wa taarifa za mazingira kutoka magazeti ya *Taifa Leo* teule pamoja na aina na dhima za ujumbe uliojitokeza katika habari hizo. Utafiti huu ulichanganua matini 270 kutoka kwa magazeti ya *Taifa Leo* yaliyoteuliwa kimaksudi. Matini hizi ni zile ambazo zilifafanua taarifa zinazohusiana na mazingira. Data iliyokusanywa katika utafiti huu ilikuwa ya kithamano. Data ya kithamano ilikuwa zile habari zilizofafanua masuala ya mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Data ya kithamano ilichanganuliwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia mihimili ya nadharia teule. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa maelezo, jedwali na takwimu. Inatarajiwa kwamba matokeo ya utafiti huu yatafaidi wanafunzi, watafiti, wanaharakati wa kimazingira, taaluma za Uchanganuzi Usemi, Umtindo na Pragmatiki, wanahabari, wachapishaji wa habari katika magazeti, na wasomaji wa habari hizo. Umuhimu wa Kiswahili kama wenzo wa mawasiliano pia umeangaziwa.

## ABSTRACT

This study focused on the use of language in reporting environmental information in the *Taifa Leo* newspaper in Kenya. *Taifa Leo* presents information to readers in Kiswahili. Kiswahili is recognized by the Constitution of Kenya as the national language and also the official language alongside English. Environment is a cross-cutting and sensitive issue nationally and internationally. Environment affects the life of every creature on a daily basis in one way or another. Print media, the *Taifa Leo* included, has been tasked with informing the public about the world's environmental issues, and it should do so in a way that will enable people to understand the importance of environment and thus interact with it in a positive way. This argument stems from the belief that a person values and cares for what he or she understands. This study therefore aims to determine whether the language used in conveying environmental information in the *Taifa Leo* newspaper enable journalists to convey the intended environmental information. Precisely, it aimed at analysing the language features used by journalists to present environmental information in *Taifa Leo*, to evaluate the styles employed by journalists in reporting on environmental news in the *Taifa Leo* newspaper and to ascertain the information communicated. The theories used in this study were Discourse Analysis Theory propounded by Michel Foucault (1928) and later advanced by Fairclough (1989) and Stylistics Theory developed by Geoffrey Leech (1965-1966) and later advanced by Paul Simpson (2004).This study was conducted in a library where environmental discourse published in *Taifa Leo* newspaper was analysed. *Taifa Leo* newspapers published from January 2021 to March 2022 were selected purposively, by extracting texts from the selected newspapers that had environmental information. Data was analysed based on language used in the presentation of environmental information in selected texts from *Taifa Leo* newspapers and the information presented. This study analysed a total of 270 texts selected purposively from *Taifa Leo* newspapers. The data collected in this study was qualitative. Qualitative data comprised of texts that explain environmental issues in the *Taifa Leo* newspaper. Qualitative data was analysed descriptively based on the tenets of the Discourse Analysis and Stylistics Theories. The results of the study were presented descriptively using table and numbers. It is hoped that the results of this study will be beneficial to students, researchers, environmental activists, disciplines of Discourse Analysis, Stylistis and Pragmatics, newspaper readers, journalists and newspaper publishers. The importance of Kiswahili as a communication tool is also highlighted.

**YALIYOMO**

**UNGAMO NA IDHINI ......................................................................................ii**

**TABARUKU ..................................................................................................iii**

**SHUKRANI ...................................................................................................iv**

**IKISIRI .........................................................................................................v**

**ABSTRACT..................................................................................................vi**

**YALIYOMO ..................................................................................................vii**

**JEDWALI LILILOTUMIKA.........................................................................xii**

**VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA.................................................................xiii**

**UFAFANUZI WA DHANA ZILIZOTUMIKA ..........................................xiv**

**SURA YA KWANZA ....................................................................................1**

1.0 Utangulizi .......................................................................................................1

1.1 Usuli wa Mada ................................................................................................1

1.2 Suala la Utafiti ................................................................................................5

1.3 Malengo ya Utafiti ..........................................................................................6

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti .....................................................................................6

1.3.2 Malego Mahususi ya Utafiti .........................................................................6

1.4 Maswali ya Utafiti ...........................................................................................7

1.5 Umuhimu wa Utafiti ........................................................................................7

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti ...............................................................................8

**SURA YA PILI..............................................................................................11**

**MWAUO WA MAANDISHI .........................................................................11**

2.0 Utangulizi .......................................................................................................11

2.1 Historia Fupi ya Gazeti la *Taifa Leo* na Ripoti za Habari Kuhusu Mazingira .....11

2.2 Tafiti Kuhusu Matumizi ya Lugha katika Vyombo vya Habari ...........................13

2.3 Tafiti Kuhusu Matumizi ya Lugha katika Gazeti la Taifa Leo .............................28

2.4 Tafiti Kuhusu Mtindo .......................................................................................32

2.5 Uchanganuzi Usemi Kuhusu Mazingira .............................................................36

2.6 Misingi ya Kinadharia .......................................................................................41

2.6.1 Nadharia ya Uchanganuzi Usemi (NUU) ..........................................................41

2.6.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Usemi ...............................................42

2.6.2 Nadharia ya Umtindo (NU) ..............................................................................44

2.6.2.1 Mihimili ya Nadharia ya Umtindo ....... 45
**SURA YA TATU ....... 48**
**MBINU ZA UTAFITI ....... 48**
3.0 Utangulizi ....... 48
3.1 Muundo wa Utafiti ....... 48
3.2 Eneo la Utafiti ....... 48
3.3 Kundi Lengwa ....... 49
3.4. Utafiti wa Maktabani ....... 49
3.5. Uteuzi wa Sampuli ....... 50
3.6. Vifaa vya Utafiti ....... 51
3.7. Ukubalifu na Utegemeo wa Vifaa vya Utafiti ....... 51
3.7.1. Ukubalifu wa Vifaa vya Utafiti ....... 51
3.7.2. Utegemeo wa Vifaa vya Utafiti ....... 51
3.8. Mbinu za Ukusanyaji wa Data ....... 52
3.9. Mbinu za Uchanganuzi wa Data ....... 53
3.11. Uwasilishaji wa Data ....... 54
3.12. Maadili ya Utafiti ....... 54
3.12.1. Maadili ya Utafiti Yanayomhusu Mtafiti ....... 54
3.12.2. Maadili ya Utafiti Yanayowahusu Watafitiwa ....... 55
3.12.3. Maadili ya Utafiti Yanayohusu Mchakato wa Utafiti ....... 55
**SURA YA NNE ....... 56**
**UCHANGANUZI WA DATA, UFASIRI NA MATOKEO YA UTAFITI ....... 56**
4.0. Utangulizi ....... 56
4.1 Uchanganuzi wa Data na Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti ....... 56
4.2. Vipengele vya Lugha Teule Katika Ripoti za Habari za Mazingira Katika Gazeti la *Taifa Leo* ....... 57
4.2.1 Udhamiriaji ....... 58
4.2.1.1 Udhamiriaji Unaobainisha Ulazima ....... 59
4.2.1.2 Udhamiriaji unaobainisha Unuiaji ....... 60
4.2.1.3 Udhamiriaji unaobainisha Uwezekano ....... 62
4.2.1.4 Udhamiriaji unaobainisha Mazoea ya jambo fulani ....... 63
4.2.2 Matumizi ya Nafsi katika Masimulizi ....... 64

4.2.2.1 Usimulizi wa Nafsi ya Kwanza ....................................................................64
4.2.2.2 Usimulizi wa Nafsi ya Pili ............................................................................67
4.2.2.3 Usimulizi wa Nafsi ya Tatu ..........................................................................68
4.2.3 Matumizi ya Toni .............................................................................................69
4.2.3.1 Toni ya Huzuni .............................................................................................70
4.2.3.2 Toni ya Kukashifu .........................................................................................71
4.2.3.3 Toni ya Kutamauka........................................................................................73
4.2.3.4 Toni ya Kusikitisha ........................................................................................75
4.2.3.5 Toni ya Matumaini .........................................................................................77
4.2.3.6 Toni ya Kupongeza ........................................................................................78
4.2.4 Miundo ya Sentensi ..........................................................................................79
4.2.4.1 Miundo ya Sentensi Sahili ............................................................................79
4.2.4.2 Miundo ya Sentensi Changamani .................................................................82
4.2.4.3 Miundo ya Sentensi Ambatani.......................................................................84
4.2.5 Matumizi ya Takwimu.......................................................................................86
4.2.5.1 Matumizi ya Takwimu zinazoonyesha Idadi Mahsusi ..................................87
4.2.5.2 Matumizi ya Takwimu zinazoonyesha Kiwango au Kiasi Jumlifu ................88
4.2.6 Uteuzi wa Mada ................................................................................................90
4.2.6.1 Mada za Kimdokezo au Kimkato ..................................................................90
4.2.6.2 Mada za Kibalagha ........................................................................................93
4.2.6.3 Mada za Kitakwimu........................................................................................95
4.2.6.4 Mada za Kitaharuki.........................................................................................97
4.2.6.5 Mada za Kimaelekezo...................................................................................100
4.2.6.6 Mada za Kiistiari............................................................................................101
4.3 Mtindo wa Wanahabari katika Kuripoti Habari za Mazingira katika Gazeti la Taifa Leo ..........................................................................................................103
4.3.1 Sifa za Grafolojia ............................................................................................104
4.3.1.1 Mpangilio wa Aya .........................................................................................105
4.3.1.2 Mpangilio wa Kurasa.....................................................................................107
4.3.1.3 Nafasi Baina ya Sentensi ...............................................................................108
4.3.1.4 Matumizi ya Picha na Michoro......................................................................109
4.3.1.5 Matumizi ya Rangi Mbalimbali .....................................................................110
4.3.1.6 Upangaji wa Safu za Maneno ........................................................................111

4.3.2 Sifa za Kiothografia ....................................................................................113
4.3.2.1 Uakifishaji....................................................................................................113
4.3.2.2 Matumizi ya Herufi Ndogo na Kubwa ........................................................116
4.3.2.3 Tahajia na Sarufi ...........................................................................................117
4.3.2.4 Uteuzi wa Hati ..............................................................................................118
4.3.3 Sifa za Kileksia ...............................................................................................120
4.3.3.1 Uteuzi wa Msamiati .....................................................................................120
4.3.3.2 Matumizi ya Tamathali za Usemi ................................................................123
4.3.3.2.1 Matumizi ya Misemo au Nahau.................................................................123
4.3.3.2.2 Matumizi ya Sitiari ....................................................................................125
4.3.3.2.3 Matumizi ya Maswali ya Balagha .............................................................127
4.3.3.2.4 Matumizi ya Methali..................................................................................128
4.3.3.2.5 Matumizi ya Tashhisi ................................................................................130
4.3.3.2.6 Matumizi ya Kinaya ..................................................................................132
4.3.3.3 2.7 Uradidi ...................................................................................................133
4.3.4 Sifa za Kiusemi..............................................................................................135
4.3.4.1 Mshikamano ................................................................................................135
4.3.4.2 Muwala .........................................................................................................140
4.4 Ujumbe Ulioibuliwa Kutokana na Matumizi ya Lugha katika Kuwasilisha Habari za Mazingira katika Gazeti la *Taifa Leo*. ..................................................................142
4.4 1 Aina ya Ujumbe Ulioibuliwa Kutokana na Matumizi ya Lugha katika Kuwasilisha Habari za Mazingira katika Gazeti la *Taifa Leo*. ...................................142
4.4.1.1 Ujumbe wa Kimazingira wenye Maana Dhamirifu .....................................143
4.4.1.2 Ujumbe wa Kimazingira wenye Maana Akisifu .........................................144
4.4.1.3 Ujumbe wa Kimazingira wenye Maana Athirifu.........................................146
4.4.1.4 Ujumbe wa Kimazingira wenye Maana Kimtindo ......................................148
4.4.1.5 Ujumbe wa Kimazingira wenye Maana Halisi ............................................149
4.4.1.6 Ujumbe wa Kimazingira wenye Maana Ashirifu ........................................151
4.4.2 Dhima ya Ujumbe Ulioibuliwa Kutokana na Matumizi ya Lugha katika Kuwasilisha Habari za Mazingira katika Gazeti la *Taifa Leo*. ...................................153
4.4.2.1 Kushawishi Wasomaji ..................................................................................154
4.4.2.2 Kukashifu Matukio Anuwai .........................................................................156
4.4.2.3 Kutahadharisha Hadhira ...............................................................................157

4.4.2.4 Kuhamasisha Hadhira ....................................................................................158
4.4.2.5 Kutamausha Hadhira .....................................................................................160
4.4.2.6 Kuchochea Ari ya Pamoja ya Hadhira.........................................................161
4.5 Hitimisho ...........................................................................................................162
**SURA YA TANO .....................................................................................163**
**MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..................163**
5.0 Utangulizi ...........................................................................................................163
5.2 Mahitimisho ya Matokeo Muhimu ya Utafiti ....................................................164
5.2.1 Lengo la Kwanza Lilikuwa Uchanganuzi wa Vipengele vya lugha vilivyoteuliwa katika uwasilishaji wa habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. .........................................................................................................164
5.2.2 Lengo la Pili Lilikuwa Kutathmini Mitindo iliyotumiwa na Waandishi wa Habari za Mazingira katika Gazeti la *Taifa Leo* .......................................................175
5.2.3 Lengo la Tatu Lilikuwa Kubainisha maana ya Ujumbe Ulioibuliwa Kutokana na Uteuzi wa Lugha na Mtindo wa Kuwasilisha Habari za Mazingira katika Gazeti la *Taifa Leo* .........................................................................................................186
5.2.3.1 Aina za Jumbe Zilizoibuliwa Kutokana na Matumizi ya Lugha na Mtindo wa Uwasilishaji wa Habari za Mazingira katika Gazeti la *Taifa Leo* ............................186
5.2.3.2 Hitimisho Kuhusu Dhima ya Ujumbe Ulioibuliwa Kutokana na Matumizi ya Lugha na Mtindo wa Uwasilishaji wa Habari za Mazingira katika Gazeti la *Taifa Leo* ...........................................................................................................192
5.3 Mapendekezo ya Utafiti.........................................................................................194
5.4 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi ..............................................................................198
**MAREJELEO .........................................................................................................201**
**KIAMBATISHO 1: CHETI CHA IDHINI YA KUFANYA UTAFITI KUTOKA KWA NACOSTI ....................................................................................................209**
**KIAMBATISHO 2: BARUA YA IDHINI YA KUFANYA UTAFITI KUTOKA SHULE YA MAFUZU .........................................................................................210**
**KIAMBATISHO 3: BARUA YA IDHINI YA KUFANYA UTAFITI KUTOKA KWA KAMPUNI YA *NATION MEDIA GROUP*...............................................211**

## JEDWALI LILILOTUMIKA

Jedwali 1: Sifa za Kigrafolojia za Matini za Kimazingira katika Gazeti la *Taifa Leo* 109

## VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

| | |
|---|---|
| FEC | Federal Election Commission |
| NUU | Nadharia ya Uchanganuzi Usemi |
| NU | Nadharia ya Umtindo |
| T.L | Taifa Leo |
| Uk | Ukurasa |
| UNEP | United Nations Environmental Program |
| UU | Uchanganuzi Usemi |
| NMG | Nation Media Group |
| ICC | International Criminal Court |

## UFAFANUZI WA DHANA ZILIZOTUMIKA

**Lugha** Utafiti huu ulizingatia dhana ya lugha kwa ujumla wake wote ikiwa ni pamoja na sifa za kisarufi, sifa za kileksia, sifa za kiusemi, mwonekano wa vipengele vya lugha kama vile picha, michoro, rangi na hata viziada lugha

**Mtindo** Mtindo katika utafiti huu unahusiana na namna lugha inavyotumiwa, yaani, elimumtindo. Ni mtindo unaolenga masuala ya kiisimu. Dhana hii inatumiwa kurejelea namna ya kushughulikia jambo, au njia mbalimbali ambazo mwanahabari anatumia kupitisha taarifa za mazingira. Mtindo ulichunguzwa kwa kubainisha sifa za grafolojia na kiothografia miongoni mwa masuala mengine yanayojikita katika mtindo kwa mtazamo wa kiisimu.

**Mazingira** Mazingira ni jumla ya mambo yote yanayomzunguka kiumbe katika maisha yake. Mazingira yanajumuisha vitu vilivyo na uhai na visivyo na uhai, mathalan, hewa, anga, maji, mchanga, mito, bahari, milima, mijengo, barabara, misitu na hata viumbe wengine kama vile binadamu. Aidha, Mazingira huweza kuundwa na vitu mbalimbali: yanaweza kuwa maliasili (miti, milima, misitu, hewa, anga, mito, bahari mchanga, maziwa, mabonde) au ya kutengenezwa na binadamu (majengo, viwanda, barabara, mashamba, mimea na kadhalika).Mazingira yanaweza kuwa wanyama, wadudu, samaki miongoni mwa viumbe wengine.

**Mtambuko** Suala ambalo limekuwa katika jamii kwa muda, athari zake zilikuwa, zipo na zitaendelea kuwepo. Mazingira ni suala mtambuko.

**Athari** Neno hili linapotumiwa kuhusiana na habari, kwa mfano `athari za habari linakusudiwa kurejelea maana ya ujumbe. Kwingiineko lina maana ya `matokeo

**Dhanaawali** Ni hoja au mambo yaliyokubaliwa kimsingi na washiriki wa mazungumzo; yaani mtazamo wa maana ambapo mwandishi anachukulia kuwa msomaji anayajua mambo mambo yanayozungumziwa.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Sura hii imetoa maelezo kwa undani kuhusu usuli wa mada. Vilevile, ufafanuzi wa kina wa suala la utafiti umetolewa. Aidha, sura hii imebainisha malengo ya utafiti huu. Hali kadhalika, katika sura hii, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti pamoja na upeo na mipaka ya utafiti umefafanuliwa.

## 1.1 Usuli wa Mada

Habari ni matukio ya kila siku yaliyo na athari kwa binadamu na hatimaye kwa mazingira ya binadamu. Katika ulimwengu kuna habari ambazo ni za kimsingi zinazomhusu kila mtu na zinazohitaji kuwasilishiwa hadhira inayozisoma kwa uangalifu kwa sababu wasomaji hupata maana ya taarifa kutegemea jinsi zilivyowasilishwa, hasa uteuzi wa lugha katika uwasilishaji wa habari zenyewe. Kwa hivyo, mawasiliano yafaayo yana manufaa kwani yanaweza ama kuhatarisha au kunusuru maisha ya wapokezi wa habari husika. Maisha ya binadamu hutegemea hali ya mazingira moja kwa moja. Suala hili la mazingira ni suala mtambuko kitaifa na kimataifa. Mazingira ni jumla ya mambo yote yanayomzunguka kiumbe katika maisha yake. Mazingira yanajumuisha vitu vilivyo na uhai na visivyo na uhai, mathalan, hewa, anga, maji, mchanga, mito, bahari, milima, mijengo, barabara, misitu na hata viumbe wengine kama vile binadamu. Aidha, mazingira huweza kuundwa na vitu mbalimbali: yanaweza kuwa maliasili (miti, milima, misitu, hewa, anga, mito, bahari mchanga, maziwa, mabonde) au ya kutengenezwa na binadamu (majengo, viwanda, barabara, mashamba, mimea na kadhalika). Kwa sababu hii, ni muhimu binadamu kuwa na uelewa wa kina kuhusu mazingira yake. Ufahamu wa hali ya mazingira wa kila siku una manufaa si haba kwa kila mtu sasa na hata siku za usoni. Vyombo vya habari, yakiwemo

magazeti, hutumia lugha katika kuwasilisha habari za mazingira ambazo zina umuhimu wake kwa hadhira lengwa.

Aidha, habari hizi huwasilishiwa wasomaji kwa kuzingatia mitindo mbalimbali. Lugha na mitindo ya kuwasilisa habari huchangia jinsi wasomaji wanavyoelewa habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*.

Maoni haya yanaungwa mkono na Tripathi (2006) anaposema kwamba mawasiliano kupitia vyombo vya habari yana athari kuu kwa hadhira. Hili ni kwa mujibu wa nadharia aliyoiasisi kuhusu mawasiliano kupitia kwa vyombo vya habari aliyoiita '*Magic Bullet or Hypodermic Needle Theory.'* Nadharia hii inadai kuwa hadhira hupokea na kuamini kikasuku habari zote zinazoifikia pasipo kuichuja au kuziweka kwenye mizani yoyote ili kubainisha ukweli.

Mawasiliano kwa mujibu wa Maina (2011) ni tendo la kuarifu au kubadilishana mawazo, hisia, maoni au habari kwa usemi, uandishi au ishara nyinginezo. Mawazo haya yanasisitizwa na Berelson na Steiner (1969) katika Maina (2011). Hawa wanataja picha, michoro, na majedwali kama baadhi ya ishara zinazozingatiwa watu wanapowasiliana. Kwa mujibu wa Beeman (1977) katika Maina (2011), mawasiliano ni mchakato unaolenga kuwasilisha ujumbe miongoni mwa viumbe kwa nia ya kubadili tabia na mienendo ya wahusika wote kwenye mfanyiko huo. Kwa hivyo, mawasiliano hulenga kuathiri wanaoshiriki kwenye mchakato wa mawasiliano. Naye Finnegan (2002) katika Maina (*keshatajwa*) ameeleza kuwa mawasiliano hujumlisha namna zote za mahusiano na maisha ya binadamu kupitia kwa kusikiliza, kunusa, kuona, kuonja, mwendo na hata vifaa halisi. Ufanisi wa mawasiliano hukamilishwa na uwasilishaji na upokezi mwafaka. Mojawapo ya

njia za kuwasilisha ujumbe ni kutumia vyombo vya habari, magazeti yakiwemo.Utafiti huu ulikusudiwa kubainsha iwapo uteuzi wa lugha na mtindo wa kuwasilisha habari za mazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* ulifanikisha uwasilishaji wa ujumbe uliokusudiwa na waandishi wa habari.

Vyombo vya habari hutekeleza jukumu la kimsingi katika kutoa habari vikiwa na lengo la kuhamasisha jamii kuhusu masuala muhimu, (Oduor, 2016). Tafiti nyingi zimethibitisha kuwa habari kwenye vyombo vya habari ndicho chanzo kikuu au tegemeo kubwa la kupata taarifa kuhusu masuala ibuka. Vilevile, ufahamu, imani na mielekeo ya wanajamii kuhusu mifumo ya sheria (na mambo mengine muhimu duniani) kwa kiwango kikubwa huumbwa na habari zinazotolewa na vyombo vya habari (Oduor, *ameshatajwa*). Kwa msingi huu, pana haja ya kuchunguza aina ya yaliyomo kwenye vyombo vya habari na athari ya habari hizo kwa jamii. Utafiti wetu umepata msukumo mkubwa kutokana na maoni yanayotolewa na utafiti wa Oduor kwa kuwa tulichanganua matini zinazoeleza masuala ya mazingira katika magazeti ya *Taifa Leo* tukinuia kubainisha iwapo habari hizi zina mchango katika jamii.

Habari za mazingira ni za kimsingi kwa sababu ya athari zinazoweza kuzua katika ulimwengu tunaoishi na kwa hivyo zinafaa kuwasilishwa katika andiko la gazeti la *Taifa Leo* kama sehemu ya habari za kimsingi. Lugha ni wenzo muhimu katika uwasilishaji wa habari. Aidha, uteuzi wa vipengele vya lugha pamoja na mtindo wa kuwasilisha habari lengwa ndio unaamua aina ya ujumbe unaowasilishwa kwa wasomaji. Uelewa alionao mtu kuhusu mazingira ndio unaomwezesha kuamua jinsi atakavyotangamana na mazingira yake. Uelewa huu pia unaweza kuibua mtazamo ufaao kuhusiana na uhifadhi au uharibifu wa mazingira. Ufahamu ufaao wa mazingira ni muhimu katika kupambana na vitendo

vyote vinavyohatarisha mazingira. Asilimia kubwa ya ufahamu wetu wa mazingira unachangiwa na jinsi vyombo vya habari vinavyowasilisha taarifa kuhusu mazingira.

Uteuzi wa lugha katika kuripoti habari za mazingira pamoja na mtindo wa uwasilishaji wa habari hizo ni muhimu katika kutoa habari kwa wasomaji kwa sababu mambo haya yanaweza kuibua aina tofauti za ujumbe ambao unaweza kuwa na dhima mbalimbali kwa wasomaji. Hili hutokea kwa kuwa uelewaji wa matini kwa upande wa msomaji kwa kiwango kikubwa hutegemea jinsi ujumbe kwenye matini ulivyowasilishwa. Utafiti huu ulilenga kuhoji jinsi lugha inavyotumiwa na waandishi wa habari katika kuripoti taarifa za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya. Aidha, utafiti huu ulidhamiria kutathmini mitindo ya kuziwasilisha taarifa za kimazingira na ujumbe ulioibuliwa katika habari hizo.

Ili kueleza jinsi lugha ilivyopambanuliwa na waandishi wa habari katika kuripoti taarifa za mazingira, utafiti huu ulilenga kufafanua sifa za kisarufi kama vile upekee wa miundo ya maneno, mpangilo wa maneno, unyambuaji wa maneno, matumizi ya nafsi katika matini na udhamiriaji. Vilevile, ulieleza sifa za kileksia kama vile uteuzi wa msamiati, matumizi ya tamathali za usemi (sitiari, takriri, uhuishaji, tashbihi miongoni mwa tamathali za lugha nyingine). Matumizi ya lugha pia yalidhihirika kupitia uchanganuzi wa sifa za kiusemi zilizojumuishwa na waandishi wa habari kama vile mshikamano na muwala katika matini. Isitoshe, utafiti huu ulifafanua mwonekano wa vipengele vya lugha na mbinu zote zilizozingatiwa katika uwasilishaji wa habari za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* teule kama vile picha, michoro, rangi miongoni mwa masuala mengine ya mtindo kwa mtazamo wa kiisimu.

Kwa upande mwingine, mtafiti alipambanua mitindo mbalimbali iliyozingatiwa katika uwasilishaji wa habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya. Mtindo ni dhana ambayo huhusiana na namna lugha inavyotumiwa katika miktadha mbalimbali. Mitindo hiyo huwa ni pamoja na mitindo ya kilahaja, mitindo ya kiwakati, mitindo ya kieneo, kitaaluma au fani fulani, mitindo ya kiuwasilishaji, mitindo ya kihadhi na mitindo ya kibinafsi. Dhana hii pia huhusu namna mbalimbali za kushughulikia jambo. Katika utafiti huu, dhana ya mtindo ilitumiwa kuelezea masuala ya kiisimu zaidi, yaani, elimumtindo. Mtindo ulichunguzwa kwa kubainisha sifa za grafolojia kama vile mpangilio wa aya, mpangilio wa kurasa, nafasi baina za sentensi, matumizi ya picha na michoro, rangi mbalimbali, utaratibu unaotumiwa katika vichwa vya habari na upangaji wa safu za maneno. Aidha, mtindo ulidhihirishwa kupitia ufafanuzi wa sifa za kiothografia kama vile uakifishaji, matumizi ya herufi ndogo na kubwa, tahajia na uteuzi wa hati pamoja njia nyingine mbalimbali zinazozingatiwa katika kuwasilisha habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya.

Utafiti huu ulilenga kuchunguza na kuchanganua uteuzi wa vipengele vya lugha na mitindo ya uwasilishaji wa habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* na ujumbe ulioibuliwa na taarifa hizo.

**1.2 Suala la Utafiti**

Takriban kila siku gazeti la *Taifa Leo* husheheni taarifa kuhusu mazingira. Waandishi wa habari za mazingira huteua lugha pamoja na mtindo fulani ili kuwasilisha habari hizi kwa wasomaji. Uteuzi wa lugha na mtindo wa uwasilishaji unaweza kuathiri maana ya ujumbe unaotolewa. Uelewa wa maandishi wa wasomaji hutegemea lugha na mtindo wa kuwasilisha maandishi hayo. Dhamira ya utafiti huu ni kuchanganua uteuzi wa vipengele

vya lugha na mtindo unaozingatiwa katika kuwasilisha habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya kwa lengo la kubainisha iwapo uteuzi hu unaathiri aina na dhima za ujumbe uliokusudiwa katika habari hizo. Hili litakuwa na manufaa ya kufanikisha uwasilishaji wa habari za kimazingira kwa wasomaji kwa njia ifaayo kama inavyokusudiwa na waandishi wa habari.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na lengo kuu na malengo mahususi. Sehemu inayofuata imejadili kwa kina lengo kuu la utafiti pamoja na malengo mahususi.

#### 1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Utafiti huu ulihusu tathmini ya lugha iliyotumika katika kuwasilisha taarifa za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Lengo kuu kwa hiyo ni kuchanganua jinsi uteuzi wa vipengele vya lugha na mtindo unaotumika katika kuwasilisha habari za mazingira unachangia katika utoaji wa maana ya ujumbe katika taarifa za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*.

#### 1.3.2 Malego Mahususi ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi yafuatayo:

i) Kuchanganua vipengele vya lugha vilivyoteuliwa katika kuripoti taarifa za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*.

ii) Kutathmini mtindo uliotumiwa na waandishi katika kuripoti habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*.

iii) Kubainisha maana za ujumbe ulioibuliwa kupitia uteuzi wa lugha na mtindo wa kuwasilisha habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

i) Je, ni vipengele gani vya lugha vilivyoteuliwa katika kuripoti habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo?*

ii) Je, ni mtindo gani uliozingatiwa na waandishi katika kuripoti habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*?

iii) Je, wanahabari katika gazeti la *Taifa Leo* waliwasilishia wasomaji ujumbe wa kimazingira wenye maana gani?

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ulilenga kutoa mapendekezo kwa wanafunzi na wasomi kuhusu umuhimu wa kutumia lugha na mtindo unaofanikisha mawasiliano. Uhariri wa habari kabla ya kuzitoa kwa walengwa wa habari hizo utahakikisha makosa ya kimsamiati na kisarufi yataondolewa na hivyo kuhakikisha mawasiliano yametolewa kikamilifu na kulingana na jinsi yalivyokusudiwa. Jambo hili huenda litasaidia kukuza hadhi ya lugha ya Kiswahili.

Aidha, utafiti huu una manufaa kwa wasomaji wa habari katika gazeti la *Taifa Leo* kwani watafahamishwa kuhusu hali ya mazingira na wahamasishwe kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira. Hili litatokea wanahabari wanapotumia lugha na mtindo ufaao wa kuwasilisha habari za mazingira wanazokusudia.

Kadhalika, utafiti huu una manufaa kwa waandishi, wahariri, wachapishaji wa habari pamoja na wanaharakati wa mazingira kwa sababu utapendekeza mtindo wa kuwasilisha habari za kimazingira kwa njia itakayofikisha ujumbe kikamilifu kwa wasomaji wanaolengwa.

Utafiti huu utachangia kuendeleza taaluma ya Pragmatiki, Uchanganuzi wa Usemi na Umtindo, ikichukuliwa kwamba lugha huumbwa na jamii na vilevile huumba jinsi watumiaji wake watakavyoitumia kijamii.

Serikali ya Kenya kupitia wizara husika imekuwa ikihamasisha raia wake kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira. Raia hupata msimamo wa serikali kupitia habari katika vyombo vya habari. Matokeo ya utafiti huu ni jukwaa mwafaka la kuhakikisha kwamba serikali imefikia malengo yake.

Matokeo ya utafiti huu yanaangazia mapengo ya kitaaluma ambayo yanaweza kuzingatiwa na wasomi wengine kufanya tafiti nyingine ambazo zitaibua manufaa makubwa siku za baadaye, hususan matumizi ya lugha katika tasnia mbalimbali zinazotagusana na jamii.

**1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ulifanyika maktabani kwa kuchanganua taarifa za mazingira zinazoripotiwa katika magazeti ya *Taifa Leo* nchini Kenya. Gazeti la *Taifa Leo* liliteuliwa kuchunguzwa katika utafiti huu kwa sababu huandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili ni lugha ya Taifa na pia rasmi nchini Kenya. Hili linatokana na imani kwamba Wakenya wengi huwasiliana na kutagusana katika shughuli muhimu kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Aidha, lugha ya Kiswahili ina umuhimu sio nchini Kenya pekee lakini hata katika bara Afrika kwani lugha hii ni *Lingua Franka* Afrika Mashariki na Kati (Mukuthuria, 2006). Ingawa gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya huchapishwa kila siku, uteuzi wa magazeti yaliyoshirikishwa katika utafiti huu ulikuwa wa kimakusudi kwa vile ni makala 270 pekee kutoka magazeti ambayo yaliandikwa kuanzia Januari 2021 hadi Machi 2022.

Aidha, uteuzi wa makala 270 uliongozwa na uwepo wa taarifa zinazohusiana na mazingira katika makala lengwa. Hali kadhalika, uteuzi wa kipindi hiki ulishinikizwa na haja ya kutaka kuchanganua data ya wakati wa sasa zaidi kwani tayari kuna baadhi ya watafiti wengine ambao walichunguza taarifa kwenye gazeti la *Taifa Leo* hapo awali wakilenga masuala tofauti tofauti. Vilevile ni katika kipindi hiki ambapo taarifa muhimu kuhusiana na mazingira kimataifa na kitaifa zimetolewa. Miongoni mwa habari hizi ni zile zinazohusiana na majanga ya Corona, nzige na mafuriko ambayo yanaathiri mazingira moja kwa moja. Aidha, zipo habari muhimu zinazolenga mazingira ambazo zilitolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na mazingira, UNEP. Taarifa hizo zilikusudiwa kuhamasisha watu kuhusu upunguzaji wa matumizi ya gesi chafu na mipango ya kukabiliana na kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Isitoshe, Shirika hilo lilitoa kauli kuhusu harakati za kupunguza uwezekano wa madhara ya majanga kama vile Corona kwa kuongeza juhudi za kuelewa zaidi mambo yanayohatarisha mwingiliano wa binadamu na wanyama. Jambo hili linalengwa kuwezesha ulindaji wa mazingira na hata maadili ya kimazingira. Kadhalika, lilikusudiwa kuhimiza watu kuzingatia ilani iliyotolewa na baadhi ya wanasiasa kuhusiana na ukataji miti nchini Kenya. Masuala hayo yaliangaziwa katika vyombo vya habari kwa kina. Katika utafiti huu, taarifa zinazolenga mazingira na ambazo zilitokea katika gazeti la *Taifa Leo* katika kipindi teule pekee ndizo zilizozingatiwa. Hili lilitokana na hoja kwamba uchunguzi huu ulijikita katika habari zilizotolewa kwa lugha ya Kiswahili. Habari za kitaifa na kimataifa kuhusu mazingira zilishirikishwa kwenye utafiti huu.

Dhana ya mazingira ilizingatiwa kwa upana wake ili kujumuisha habari zinazohusu maji, hewa mchanga, milima, mito, bahari, mafuriko, kilimo, misitu na hata viumbe. Hususan

habari zilizochunguzwa ni zile zilizohusu majanga ya kiasili kama vile mafuriko, vimbunga, tufani, zilizala, kuzuka kwa nzige, na viwavi pamoja na ukame. Vilevile utafiti ulichunguza habari kuhusu milipuko ya maradhi duniani kama vile Corona, Kipindupindu, Ebola na Malaria. Utafiti pia ulizingatia uharibifu na utunzaji wa misitu na vyanzo vya maji, mito, maziwa na bahari, maji safi na maji taka, umwagaji wa taka, upanzi wa miti, utunzaji wa fuo za bahari, kilimo, ardhi na uharibifu wa mazingira kwa ujumla.

Uchanganuzi ulijikita kwenye uhakiki wa habari za kimazingira kwa misingi ya Nadharia ya Uchanganuzi Usemi hususan matumizi ya lugha na uzingatiaji wa mtindo wa uwasilishaji wa habari na ujumbe uliotolewa pamoja na maana za ujumbe huo. Hali kadhalika, Uchanganuzi Usemi ulisaidia kufichua hisia zilizofichwa katika matini ya mwandishi, jambo ambalo linachangia katika kuelewa matini kwa kina.

Vilevile, utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Umtindo. Msisitizo uliwekwa kwenye uchanganuzi wa mtindo kiisimu unaohusiana na namna lugha inavyotumiwa katika kuwasilisha taarifa za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*

# SURA YA PILI

# MWAUO WA MAANDISHI

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inahusu mwauo wa maandishi yanayohusiana na matumizi ya lugha katika vyombo vya habari. Masuala yanayofafanuliwa katika vyombo vya habari kwa kutumia lugha huenda yakawa yanahusu mazingira au mambo tofauti na mazingira. Mathalan, sura hii imetoa historia fupi ya gazeti la *Taifa Leo* na ufafanuzi wa yale yaliyoandikwa kuhusu matumizi ya lugha katika vyombo vya habari kwa ujumla. Pia inajadili na kuhakiki machapisho yanayohusu matumizi ya lugha katika gazeti la *Taifa Leo* pamoja na mtindo wa uwasilishaji wa habari za mazingira na ujumbe unaoibuliwa kwa msomaji. Hali kadhalika, maandishi yanayohusiana na uchanganuzi wa habari zinazohusiana na mazingira yalichunguzwa. Hali kadhalika, sura hii inaeleza Nadharia ya Uchanganuzi Usemi, Nadharia ya Umtindo pamoja na kuonyesha pengo ambalo utafiti huu ulitazamia kuziba.

## 2.1 Historia Fupi ya Gazeti la *Taifa Leo* na Ripoti za Habari Kuhusu Mazingira

Gazeti la Taifa Leo ni gazeti la Kampuni ya Nation Media Group (NMG) ambayo ina afisi zake Barabara ya Kimathi jijini Nairobi. Kulingana na Loughran (2010) gazeti la *Taifa Leo* lilichapishwa mara ya kwanza 1958, na Mwingereza Charles Hayes na mwenzake Tebbutt, wakati huo likiitwa *Taifa*. *Taifa* lilikuwa gazeti la kila wiki. Mwaka wa 1959, gazeti hili likanunuliwa na Aga Khan na likawa gazeti la kila siku na kuitwa *Taifa Leo* kufikia mwaka wa 1960. Gazeti la Kiingereza, *Sunday Nation* lilizinduliwa Machi 1960, na *Daily Nation* likazinduliwa Oktoba 1960. Hii leo, gazeti la *Taifa Leo* huchapishwa kila siku na husheheni habari za aina mbalimbali za humu nchini na nje ya nchi.

Magazeti ni chombo muhimu sana cha mawasiliano na umma. Hiki ndicho chombo cha mawasiliano ya umma kilicho kikongwe zaidi kuliko vyombo vingine kama vile redio, televisheni, sinema, video na kadhalika. Taarifa katika magazeti huweza kutumika kama aina ya utangazaji. Utangazaji ni namna ya kufahamisha ili kuuza au kubadilisha mielekeo (Maina, 2011). Matangazo yalianza kama maelezo yaliyoandikwa kwenye viingilio vya mahali pa kufanyia biashara. Baadaye yakawekwa magazetini na hata kwenye mabango. Matangazo katika vyombo vya habari huzingatia mitindo mbalimbali na pia mbinu za uteuzi wa lugha (King'ei, 2000) katika Maina (2011). Magazeti pia ni chombo kinachowashirikisha watu wengi sana kwa pamoja na kwa wakati mmoja katika kutoa mchango wao magazetini na kusoma yaliyoandikwa na wenzao. Kwa hali hii inaonekana kuwa magazeti ni chombo muhimu cha kuelimishia umma. Dhima hii ni kubwa sana. Ili iweze kutekelezwa vyema haitoshi tu kwa wale wanaowasiliana kwa kutumia chombo hiki kuwa na msamiati mwingi wa Kiswahili bali wanahitajika kuifahamu vyema sarufi ya Kiswahili. Kilicho muhimu zaidi ni kujua jinsi ya kuzitumia zana hizi za kiisimu kwa namna inayofaa na inayokidhi mazingira haya maalum ya mawasiliano.

Utafiti huu ulichunguza matumizi ya lugha na mtindo uliotumika kuripoti matukio ya kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* na ujumbe ulioibuliwa kwa wasomaji. Matukio tofauti ya kimazingira yalichunguzwa yalivyoripotiwa kila mwezi kuanzia Januari 2021 hadi Machi 2022. Matukio hayo ni: Majanga ya kiasili, wanyamapori, milipuko ya maradhi, utunzaji misitu, kilimo, uharibifu wa mazingira, mabadiliko ya tabianchi, majanga yanayosababishwa na moto, zilizala na maporomoko, vimbunga na upepo mkali, maji-safi na maji-taka, bahari na fuo zake, ukame na njaa, ardhi, uhifadhi wa mazingira, kawi na mazingira, mito na mabwawa, umwagaji taka na shughuli za ubomoaji na ajali.

Utafiti huu ulichunguza matini 270 zilizoteuliwa kimaksudi kuhusu matukio ya kimazingira yaliyotajwa kutoka katika gazeti la *Taifa Leo* kuanzia Januari 2021 hadi Machi 2022.

**2.2 Tafiti Kuhusu Matumizi ya Lugha katika Vyombo vya Habari**

Rube (2021) alichunguza mambo ambayo wanahabari nchini Kenya wanafikiria kuwa ndiyo yanaathiri maendeleo katika taaluma ya uanahabari na vilevile ni kwa njia gani mielekeo yao kama washikadau muhimu huathiri utekelezaji wa kazi zao. Utafiti huu pia ulitathmini ufahamu na ujuzi wa wanahabari kuhusu mafanikio ya kitaifa katika taaluma ya uanahabari. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa ujuzi, tajriba na mwegemeo hasi wa habari ndiyo mambo yanayotinga maendeleo ya taaluma hii; ingawa idadi ndogo ya wanahabari walitofautiana na wenzao katika mtazamo huu. Utafiti huu pia ulibainisha kuwa wanahabari katika kujitathmini wanajiweka katika ngazi ya juu kupindukia kuhusu ufahamu wa mafanikio yao ya kazi ikilinganishwa na hali halisi. Hata hivyo, walidunisha mafanikio ya kitaifa ya taaluma ya uanahabari. Utafiti wa Rube (*ametajwa*) unafaidi utafiti wetu kwa sababu tajriba na ufahamu wa mwanahabari ni muhimu katika uwasilishaji wa habari ambazo zinachora hali halisi ya mazingira ya mpokezi wa habari lengwa. Ufahamu wa hali halisi wa wanajamii huchangia utoaji wa maamuzi ambayo yanamfaidi mtu binafsi na mazingira yake. Hata hivyo, tafiti hizi mbili zinatofautiana katika aina za data na upeo na mipaka ya vyanzo vya data, kwani utafiti wetu unachunguza habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*.

Korir na Nabushawo (2021) walitathmini habari zilizochapishwa katika vyombo vya habari wakati wa janga la kimataifa la Corona. Korir na mwenzake *(keshatajwa*)

wanasadiki kuwa kwa muda mrefu habari zinazochapishwa katika vyombo vya habari zimechukuliwa kwamba zina uwezo au nguvu kuu za kuweza kuleta mabadiliko chanya katika jamii hasa kutokana na sifa yake ya jinsi habari zenyewe huwasilishwa. Hata hivyo, ingawa watu wengi wanaamini haya, kumekuwa na wasiwasi kuwa huenda vyombo vya habari vikashindwa kuendelea kutekeleza wajibu huo, na sanasana nyakati kunapotokea msambao wa majanga wa kiwango kikubwa. Korir na mwenzake (*keshatajwa*) walitafiti uripotaji wa habari za msambao wa janga la Corona katika gazeti kuu nchini la *Daily Nation* mwaka wa 2020. Uchunguzi huu ulijikita katika kipindi ambapo taarifa zilizolenga janga hili zilipochapishwa kwa wingi na ambazo zilionekana kuwa na athari kuu katika jamii. Data za utafiti huu zilichanganuliwa zikitawaliwa na imani na uzoefu wa kikaida wa jinsi ujumbe katika gazeti unatarajiwa kuwa. Katika habari hizi, waandishi wa habari walikusanya habari kutoka kwa maafisa wakuu serikalini pamoja na watu wengine mashuhuri. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa taarifa kuhusu suala husika katika gazeti hili zilizua hofu kuu na hali ya kupoteza matumaini miongoni mwa hadhira; na kwa sababu hii habari zenyewe zilinuiwa kuibuia hisia za msomji. Utafiti wa Korir na mwenzake (keshatajwa) ni muhimu sana kwa uchunguzi wetu kwa kuwa unatathmini iwapo mwandishi wa gazeti anasawiri hali halisi katika jamii kupitia yale anayoandika. Utafiti wetu ulikusudia kubainisha iwapo mwandishi wa habari katika gazeti la *Taifa Leo* anamchorea msomaji hali halisi ya mazingira kupitia lugha na mtindo anaoteua. Vilevile, utafiti wa Korir na mwenzake ulihusu ripoti za janga la ugonjwa wa Corona unaosambazwa kupitia anga (ambayo ni sehemu ya mazingira). Pamoja na hayo, tafiti hizi zinatofautiana kuhusiana na aina na chanzo cha data.

Shalini na Tushar (2020) walichanganua uhusiano uliopo baina ya majanga mbalimbali na dhuluma za kijinsia kwa kuchambua jinsi kesi za dhuluma za kijinsia zinavyoripotiwa kwenye vyombo vya habari na suluhu zinazotolewa kwa waathiriwa. Utafiti huo ulikuwa na mchango kwa utafiti wa sasa kwani tafiti zote mbili zinalenga matumizi ya lugha katika vyombo vya habari. Tafiti hizi zinatofautiana kwa mintarafu ya aina ya data inayochunguzwa.

Armando na Garcia (2017) walilinganisha uhusiano uliopo kati ya vyanzo vya data za ripoti za taarifa za habari na data zinatolewa na vyombo vya habari. Walibaini kuwa katika kuripoti habari, wanahabari hulenga kupata taarifa kutoka kwa watu au mashirika yanayochukuliwa kuwa yatatoa habari za kuaminika na kutegemewa. Hata hivyo, waligundua kuwa vyanzo vya habari huenda vikawa na nia tofauti na hivyo kuamua kuficha habari fulani na kutoa zingine kwa kuwa wanahofia huenda baadhi ya habari hizo zikaibua hisia au kuzua athari fulani kwa umma. Utafiti huo ulikuwa na manufaa kwa utafiti huu kwa kuwa unaeleza athari za taarifa za habari kwa wapokezi wa habari hizo. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana kwa msingi kuwa utafiti wa sasa ulilenga data mahsusi, habari za mazingira, huku utafiti huo wa awali ukiangazia data zinazokusanywa na wanahabari kwa ujumla wake.

Barasa (2016) alichunguza matumizi ya lugha na changamoto zinazoambatana na matumizi hayo katika majukwaa ya kijamii. Alijikita katika matumizi ya lugha kwenye simu, kompyuta na vifaa vingine vya kidijitali. Utafiti wa Barasa una data muhimu kwa uchunguzi wa sasa kwa kuwa tafiti zote mbili zinalenga matumizi ya lugha kueleza mambo yanayohusu jamii. Aidha, tafiti hizi zinahoji iwapo lugha inayotumiwa inafaulu kutimiza malengo ya mwandishi. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana kwa misingi ya muktadha wa

matumizi ya lugha. Isitoshe, Barasa ( *ametajwa*) alichanganua matumizi ya lugha kwenye vifaa vya kidijitali kwa ujumla huku utafiti wa sasa ukichanganua data ya habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* kati ya Januari 2021 na Machi 2022.

Oduor (2016), anasema kuwa vyombo vya habari hutekeleza jukumu la kimsingi katika kutoa habari vikiwa na lengo la kuhamasisha jamii kuhusu masuala muhimu. Anasema kuwa tafiti nyingi zimethibitisha kwamba habari kwenye vyombo vya habari ndicho chanzo kukuu au tegemeo kubwa la kupata taarifa kuhusu masuala ibuka. Vilevile, ufahamu, imani na mielekeo ya wanajamii kuhusu mifumo ya sheria (na mambo mengine muhimu duniani (*msisitizo ni wangu*) kwa kiwango kikubwa huumbwa na habari zinazotolewa na vyombo vya habari (Oduor, *ameshatajwa*). Kwa msingi huu, pana haja ya kuchunguza aina ya yaliyomo kwenye vyombo vya habari na pengine athari ya habari hizi kwa jamii. Oduor (*ameshatajwa*) alitumia Nadharia ya Uwakilishaji wa Kijamii ambayo inasaidia kuchanganua aina ya yaliyomo au ujumbe unaowasilishiwa jamii na vyombo vya habari. Nadharia hii inaelekeza uchanganuzi wa matini kwa kulenga madhumuni na msisitizo (utiaji nanga ) wa mwandishi. Mwandishi hufanya hivi akiwa na lengo la kuhamasisha na kuimarisha uelewa au ufahamu wa jambo fulani. Uchanganuzi wa aina hii huhusisha matumizi ya sitiari, ukinzani, majina, uhuishaji, usisitizaji wa maudhui, hisia na madhumuni; mambo ambayo husaidia uelewa wa ujumbe unapofasiriwa ipasavyo. Oduor (*ameshatajwa*) alibainisha haya alipokuwa akichunguza jinsi magazeti ya *the Standard* na *Daily Nation* yalieleza habari za utaratibu wa kesi za ICC kufuatia ghasia za baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi mwaka wa 2007-2008 nchini Kenya. Utafiti huu una data muhimu kwa uchunguzi wa sasa kwa kuwa tafiti zote mbili zinalenga jinsi waandishi wa habari katika magazeti wanavyotumia lugha kueleza mambo yanayohusu

jamii. Aidha, tafiti hizi zinahoji iwapo lugha inayotumiwa inafaulu kutimiza malengo ya mwandishi. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana kwa misingi ya nadharia zilizohusishwa kwani utafiti wa Oduor unatumia Nadharia ya Uwakilishaji wa Kijamii huku utafiti wa sasa ukitumia Nadharia za Uchanganuzi Usemi na Umtindo. Isitoshe, Oduor alichanganua data zinazofafanua ghasia baada ya uchaguzi katika magazeti ya *the Standard* na *Daily Nation* huku utafiti wa sasa ukichanganua data ya habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* kati ya Januari 2021 na Machi 2022.

Dorroh (2015) alichunguza mtindo wa matukio katika ulimwengu na kusema kuwa katika miaka michache ijayo, mabadiliko ya hali ya anga yana uwezo wa kubadilisha uchumi na kutenganisha washindi na wale watakaopoteza katika ngazi za ulimwengu. Pamoja na haya anasema kuwa wanahabari wameshindwa kuueleza ulimwengu hali ilivyo kuhusiana na masuala ya mazingira. Badala yake, wanahabari huzamia kuripoti na kuhamasisha ulimwengu kuhusu masuala ya siasa. Data za utafiti huu zina manufaa kwa utafiti wa sasa kwa sababu unadokeza kuwa jamii ya ulimwengu ina haja ya kuelewa hali ya kila siku ya mazingira ili iweze kuchukua hatua zinazofaa kuhusiana na utunzaji wa mazingira. Tafiti hizi mbili zinatofautiana katika sehemu ya chanzo cha data kwani Dorroh anazungumzia vyombo vya habari kwa ujumla. Pia, utafiti wa sasa ulichanganua lugha na mtindo katika uwasilishaji wa taarifa za mazingira ilhali utafiti wa Dorroh ulilenga kuhamasisha umma kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira.

Brandon na Wates (2015) wanasema kwamba sio kile kipande cha kikaratasi cha kizamani kilichotumwa kwa wote kwa njia ya posta au kilichotolewa kwenye ‘matukio’ ya vyombo vya habari, lakini toleo lililotayarishwa kwa makini kusema unachotaka kukisema kwa ufanisi kadri iwezekanavyo

Kauli hii inamaanisha kuwa inawezekana kwa mwanahabari kuunda ujumbe utakaowasilishwa katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Pamoja na hayo, idadi nyingi ya taarifa katika vyombo vya habari huwa hazina ujumbe, huwa zimeandikwa vibaya na ndefu mno. Brandon na mwenzake (*keshatajwa*) wanasisitiza kwamba ipo haja ya kutumia muda wa kuziandaa vyema, ili kwamba zihabarishe na kuvutia sio tu kwa vyombo vya habari vya jadi, bali kwa hadhira ya mitandao ya kijamii vilevile. Maoni haya yanafaa utafiti wetu kwa kuwa iwapo wasomaji wa *Taifa Leo* watafaidi kutokana na habari za mazingira zinazoripotiwa, sharti waandishi wa gazeti wamakinikie kazi yao. Kufaidika hapa kunamaanisha kule kuelewa habari zenyewe na kufanya kinachofaa kufanywa kuhusiana na kusudi la mwandishi wa habari husika.

Brandon na mwenzake (*keshatajwa*) wanapendekezea waandishi wa habari kuwa wanapoandaa habari, wazingatie muundo unaojulikana kama *Piramidi iliyopinduliwa*, ambayo aghalabu hutumiwa na mashirika mengi ya habari katika uandishi wa habari. Katika muundo huu, sehemu pana ya chini ya umbo la piramidi inawakilisha taarifa kubwa zaidi, ya kuvutia na iliyo muhimu inayojaribu kuwasilishwa. Habari ya aina hii lazima iwe kichwa cha matini, ilhali sehemu ya chini iliyochongoka inaonyesha kwamba habari nyingine zifuate kwa umuhimu unaopungua. Uandishi wa taarifa kwa wanahabari huonekana kuwa kazi ngumu. Mbali na kuwa na mengi yanayofanana na uandishi mzuri wa habari, inahitaji kufanywa vyema.

Kamenchu (2015) alichunguza jinsi utoaji wa habari kidijitali umesababisha mabadiliko katika mfumo mzima wa taaluma ya uanahabari nchini Kenya. Kamenchu (*ametajwa*) alichunguza uandishi wa habari katika magazeti ya *The Standard* na *The Daily Nation* na kubainisha kuwa wanahabari wameukumbatia mfumo wa teknolojia katika kila hatua ya

shughuli zao. Pamoja na haya, katika juhudi zao za kukumbatia teknolojia katika utekelezaji wa kazi zao, juhudi hizi zinatingwa na ile hofu ya madhara ambayo wanahisi yana uwezo wa kuathiri taaluma ya uanahabari kwa upande wa uwazi, umakinifu na malengo au azma ya kazi yao. Utafiti huu unafanana na utafiti wetu kwa kuwa tafiti zote zinalenga uwasilishaji wa habari kupitia magazeti. Masuala anayofafanua Kamenchu (a*metajwa*) ni kigezo kikuu cha kupimia kufaulu au kutofaulu kwa malengo ya utafiti wetu. Tofauti moja inayobainika katika tafiti hizi mbili ni chanzo na aina za data za utafiti.

Utafiti uliofanywa na Hoffman na Hawkins (2015) unakubali kuwa tafiti nyingi zimefanywa ambazo zinatoa mwanga kuhusu uhusiano uliopo kati ya vyombo vya habari, ghasia na vita. Hata hivyo, suala la amani halijafafanuliwa ipasavyo ikiwa litaeleweka kuwa ni ukosefu wa fujo au ghasia; kwani kuna amani chanya na amani hasi. Utafiti huu unasadiki kuwa uhusiano kati ya mawasiliano, ghasia na amani si jambo geni, lakini juhudi za kiakademia za kutaka kuelewa suala hili zinaashiria kwamba uzito mwingi huegemezwa kwenye uhusiano kati ya mawasiliano na ghasia zenyewe badala ya juhudi za kuleta amani. Data za uchunguzi huo zilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa sababu zinahusu jukumu lililotwikwa vyombo vya habari la kuufahamisha umma matukio katika jamii. Hata hivyo, tafiti hizi mbili zinatofautiana kwa vile utafiti huo ulilenga vyombo vya habari kwa jumla na pia habari za vita, ghasia na amani ilhali utafiti wa sasa ulijishughulisha na habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* na pia mtindo wa kuziwasilisha habari hizo.

Jamar (2015) alichunguza jinsi magazeti yalivyosawiri makundi tofauti ya kidini kuhusiana na mashambulizi ya kigaidi yaliyotokea Mandera Novemba 2014 na katika Chuo Kikuu cha Garissa Aprili 2015. Utafiti wa Jamar (*ametajwa*) ulithibitisha kwamba wanahabari walizingatia mbinu za kitaaluma katika kutoa habari hizo. Utafiti wa Jamar una data

muhimu kwa utafiti wa sasa kwa kuwa unahusu matumizi ya lugha katika vyombo vya habari. Hata hivyo, tafiti hizi mbili zinatofautiana kuhusiana na lugha za utafiti kwani Jamar alitumia lugha ya Kiingereza huku utafiti huu ukitumia lugha ya Kiswahili. Aidha , tafiti hizi zinatofautiana kuhusiana na vyanzo ana aina za data.

Kevogo A. na Kevogo S. (2014) walichunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye majukwaa ya kielektroniki wakilenga blogu za Kikristo. Utafiti huu ulionyesha kwamba Kiswahili kimekomaa hadi kiwango cha kutumika katika miktadha kama hii. Utafiti wa Kevogo na mwenzake (w*ametajwa*) unausaidia utafiti wetu kwa jinsi ambavyo tafiti hizi mbili zinajikita katika matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kutoa habari. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana kuhusiana na aina ya data na chanzo cha data hizo.

Utafiti uliofanywa na Media Council of Kenya (2014) ulichunguza makala katika baadhi ya magazeti na matangazo katika runinga za Kenya na kubainisha kwamba vyombo vya habari kwa kiwango kikubwa havikuzingatia sheria na kanuni zinazoongoza uwasilishaji wa habari kwa umma. Aidha,walibainisha kwamba ujumbe uliowasilishwa ulikuwa na uwezo wa kuwagawanya Wakenya kwa misingi ya kidini. Data za utafiti huo zilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa sababu zililenga uchanaganuzi wa matini katika vyombo vya habari. Utafiti huo ulikuwa na data ambayo ilisaidia utafiti huu kwa sababu ulihusu uwasilishaji wa habari kwa umma kupitia uchanganuzi wa matini katika vyombo vya habari kwa ujumla. Hata hivyo, utafiti huo unatofautiana na utafiti huu kwa vile utafiti wa sasa unajifunga kwenye chombo kimoja cha habari, gazeti la *Taifa leo*, na taarifa mahususi, habari za mazingira.

Kulingana na Kisang (2014), uwasilishaji wa habari katika runinga nchini Kenya, hasa hadithi za kipelelezi hauzingatii kanuni na sheria zinazotawala utoaji wa habari. Hili linaonyesha kwamba habari hizo zina uwezo wa kuzua vurugu katika misingi ya kidini kwa vile habari zenyewe zilitukuza ugaidi. Utafiti huo ulikuwa na manufaa kwa mada iliyolengwa kwa sababu ulihusu matumizi ya lugha katika runinga ( chombo cha habari ) nchini Kenya. Hata hivyo, ulitofautiana na utafiti wa sasa kwa kuwa ulichunguza matumizi ya lugha katika runinga ilhali utafiti wa sasa unalenga uchambuzi wa lugha na mtindo wa uwasilishaji wa habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*.

Ahuja (2014) anaeleza kuwa wanahabari wana uwezo kamilifu wa kupata habari yoyote kuhusu umma kwa kigezo kwamba umma una haki ya kufahamishwa yote yanayotukia katika mazingira yao. Wanaopinga kauli hii wanadai kwamba wanahabari mara nyingi wanapokusanya na kuripoti habari huwa na mwegemeo au ubaguzi wa aina fulani, kwamba kuna aina fulani ya habari ambazo ni muhimu kwao. Wanaounga mkono kauli hii wanasema kwamba si lazima umma ufahamishwe kuhusu kila tukio. Hata hivyo, Ahuja anasisitiza kuwa ni muhimu wanahabari kutafakari kwa kina kama ni vizuri au kuna haja na ni haki kisheria kuingilia uhuru wa mtu mwingine kwa lengo au kisingizio cha kutetea haki na uhuru wa kujieleza. Matokeo ya utafiti huo yana manufaa kwa utafiti wa sasa kwa sababu yanahusu utoaji wa habari kwa umma. Hata hivyo, tafiti hizi mbili zinatofautiana kwa vile utafiti wa Ahuja unalenga vyombo vya habari kwa ujumla na pia taarifa kwenye vyombo hivyo kwa ujumla ilhali utafiti wa sasa ulijishughulisha na habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*.

Utafiti na Patterson (2013) unaeleza kuwa habari ni mchakato changamano na telezi hivyo unahitaji utimizaji wa kiwango cha juu cha maadili mema. Data za utafiti huo zilifaa utafiti

huu kwa kuwa mazingira ni suala nyeti na linatakiwa lichunguzwe kwa umakini na uadilifu unaofaa na habari zinazotolewa zifikishiwe umma kwa njia na mchakato unaofaa. Hili linatokana na hoja kuwa uelewa mwafaka wa mazingira utamwezesha binadamu kutangamana na mazingira yake kwa njia bora.

Thapthiang (2013) alichunguza uripotaji wa habari kuhusu matukio mawili ya ulipuaji wa magari kwa bomu katika mahoteli mawili maarufu ya Hatyai na Pattani katika mwezi wa Machi na Julai 2012 mtawalia na athari zake kwa watu binafsi na jamii kwa jumla. Thapthiang alibainisha kuwa katika kuripoti visa hivi, vyombo vya habari vilipuuza matamanio ya raia na vilevile utangamano wa kijamii. Aidha, kwa sababu ya ukosefu wa uzoefu mpana wa kiutamaduni miongoni mwa wanahabari walioripoti visa hivi, Waislamu walisawiriwa vibaya. Uchanganuzi wa namna matukio haya yalivyoripotiwa unaonyesha kuwa vyombo vya habari huamua; hushurutisha jinsi hadhira ikatavyoelewa matukio katika ulimwengu. Hili linajitokeza kupitia jinsi wanahabari wanavyopanga agenda zao, kuumba na kuuwasilisha ujumbe pamoja na kupalilia imani fulani. Data ya utafiti wa Thapthiang ilikuwa muhimu kwa utafiti wa sasa kwa sababu ulihoji iwapo uteuzi wa lugha na mtindo wa uwasilishaji wa taarifa za mazingira una uhusiano na uelewa wa habari hizo. Tafiti hizi zinatofautiana kwa upande wa aina za data zilizochanganuliwa..

Ingram (2012) alisisitiza umuhimu wa lugha kama wenzo wa kuwasilishia ujumbe kwa msomaji. Anaeleza kuwa ni wajibu wa mwanahabari kuteua lugha kwa namna ambayo itamwezesha kumfikia msomaji na msikilizaji. Anahimiza kuwa katika harakati za kutoa taarifa, mwanahabari anapaswa kufasili yale masuala na matukio changamano na kuyaeleza kwa lugha ambayo ni rahisi kwa msomaji na msikilizaji kuelewa. Utafiti wa

Ingram ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa unahimiza matumizi ya lugha ipasavyo kwa manufaa ya suala lengwa na vilevile wapokeaji wa habari husika.

Njoroge (2012) alifanya utafiti linganishi katika magazeti ya '*The Standard* na *Daily Nation'* ambapo alinuia kubainisha mahali au eneo katika magazeti penye habari za kilimo zilipotokea (kurasa za mwanzo, katikati au katika kurasa za mwisho za magazeti husika). Aidha, Njoroge alipambanua maratokezi ya taarifa za kilimo zilizoandikwa katika kurasa za mwanzo, za katikati au za mwisho wa magazeti yote mawili. Matokeo ya utafiti huu ni kwamba habari za kilimo ziliwasilishwa kwa kuzingatia kategoria saba: matangazo, makala maalum, tahariri, barua kwa mhariri, habari motomoto, maoni na picha au michoro. Alibainisha kwamba habari hizi zote zilitokea katika kurasa za katikati (95%). Kadhalika, habari za kilimo zilizowasilishwa kwa kutumia picha au michoro ndizo zilichukua nafasi kubwa (35.1%). Utafiti huu una taarifa muhimu kwa utafiti wa sasa kwa kuwa tafiti zote mbili zinachunguza taarifa katika magazeti. Tafiti hizi zinatofautiana kwa kuwa utafiti wa sasa unalenga habari za mazingira ilhali utafiti wa Njoroge unahusu taarifa za kilimo ambacho ni sehemu tu ya masuala ya kimazingira. Aidha, utafiti wa sasa unachunguza matumizi ya lugha na mtindo wa uwasilishaji wa taarifa za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* huku ule wa Njoroge ukiangazia mahali habari za kilimo zinatokea katika magazeti ya *The Standard* na *Daily Nation*. Isitoshe, gazeti la *Taifa Leo* hutoa habari kwa wasomaji kwa lugha ya Kiswahili tofauti na magazeti ya`*The Standard* na *Daily Nation* ambayo huandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

Ireri (2012) alichunguza hali ya taaluma ya Uanahabari nchini Kenya katika karne ya 21. Ireri (*ametajwa*) alichunguza wanahabari 96 ili kuelewa usuli wa demografia zao, uridhikaji kikazi, hali ya mazingira ya kazini na kiwango cha matumizi ya teknolojia.

Uelewa wao wa maadili ya uanahabari, uhuru wa wanahabari na mambo yanayoathiri utendakazi wao pia yalifafanuliwa. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa 69.7% ya wale walihojiwa wameridhika kikazi. Kadhalika, asilimia ndogo ya sampuli husika ilitaja mshahara duni kama kikwazo kikuu kwa kazi yao. Aidha, wanahabari wanaume wengi walisema wameridhika kikazi ikilinganishwa na wanahabari wanawake. Vizuizi vikuu kwa uhuru wa wanahabari vilikuwa wamiliki wa mashirika ya vyombo vya habari na watangazaji. Walinzi wa vyumba vya habari walitekeleza jukumu kuu la kuamua thamani ya habari zilizowasilishwa. Uchunguzi wa Ireri (*ametajwa*) una data muhimu kwa utafiti wetu kwa kuwa tafiti zote mbili zinafafanua masuala yanayohusiana na uanahabari. Isitoshe, masuala yaliyohojiwa na Ireri (*ametajwa*) ni vigezo muhimu vinavyosaidia utafiti wetu kufikia malengo yake.

Xiaoquan na wenzake (2011) wanasema kwamba kuna uwiano kati ya utoaji wa habari za mazingira zinazohusiana na mabadiliko ya hali ya joto ya anga kwa kuzingatia mbinu za kisasa za kisayansi. Wanaendelea kusema kuwa utoaji wa habari zenye mwegemeo wa kisiasa kuhusiana na mabadiliko ya hali ya joto ya anga ni tofauti. Utafiti huu unaonekana kuashiria kuwa habari zinazotolewa kuhusu mazingira kama vile mabadiliko ya hali ya joto ya anga kwa kuzingatia sayansi ya kisasa zina ukweli na ni za kuaminika. Data za utafiti huu ni muhimu kwa utafiti wa sasa kwa vile tafiti zote mbili zinalenga suala la mazingira na manufaa ya mwanahabari kuzingatia mbinu zenye uwezo wa kutoa habari zenye ukweli na za kuaminika wakati wa utoaji wa habari. Tofauti kati ya tafiti hizi ni kuwa utafiti wa Xiaoquan na wenzake (2011) unahoji kipengele kimoja tu cha mazingira-mabadiliko ya hali ya joto ya anga, ilhali utafiti wa sasa unafumbata vipengele vyote vya mazingira, mradi vipengele hivyo vimeangaziwa na waandishi wa habari katika gazeti la *Taifa Leo*.

Watu hutegemea vyombo vya habari kama vile runinga, magazeti, majarida, redio na mitandao mingine ya kijamii ili kujaribu kupata au kuelewa uchangamano uliopo kuhusiana na sayansi ya kimazingira na utawala ambao kwa kukusudia au kutokusudia huumba maisha yao. Katika juhudi za kutaka kuuthibitishia umma ukweli wa hali hii, Maxwell (2009) alitalii dhima ya vyombo vya habari katika kuripoti habari za mazingira. Alichunguza jinsi mambo mengi na ya ngazi za juu yamefaulu kuumba na kuuelekeza utoaji wa habari katika njia changamano, zinazobadilika kila uchao na zisizo na mwelekeo mmoja. Utafiti wake umejengwa kwenye muktadha wa kihistoria pamoja na ruwaza za michakato ya siasa, ya kitamaduni na mabadiliko ya kimazingira. Hapa, mijadala pia hueleza jinsi vyombo vya habari husawiri athari za ufahamu na uhusika wa umma kwa yale yanayoendelea. Kazi ya Maxwell (*ametajwa*) pia inatalii jinsi habari zinazotolewa huathiri uwezekano wa miundo tofauti ya udhibiti wa mazingira. Data za utafiti wa Maxwell ni muhimu kwa utafiti wa sasa kwa sababu una data za mazingira na zaidi unalenga kuhamasisha umma kuhusu uhifadhi wa mazingira.

Mwathe na Wafula (2009) walikusanya habari zilizoripotiwa kwenye magazeti, majarida na vyombo vingine vya habari vilivyohusika katika kampeni za kutetea ziwa Natron. Kampeni hizi zilichochewa na mpango uliokuwa unanuia kujengwa kwa kiwanda cha simiti katika ziwa Natron. Ujenzi wa kiwanda hiki ungehatarisha maisha ya ndege wanaoishi ndani ya ziwa hili pamoja na jamii za wafugaji ambao walitegemea ziwa hili kwa mifugo wao na pia maisha yao. Ripoti ambazo zilihusu kampeni za kuokoa ziwa hili kutoka kwa vyombo mbalimbali vya habari zilikusanywa kuanzia mwaka wa 2006 hadi mwaka wa 2009. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa asilimia 82% ya kampeni hizo zilikuwa chanya (zikiunga mkono kulindwa kwa ziwa Natron), asilimia 16% zilikosa

msimamo na asilimia 2% zilikuwa hasi. Data za utafiti huu ni muhimu kwa utafiti wetu kwani zinahusu habari katika vyombo vya habari na pia zinalenga uhifadhi wa mazingira. Utafiti wetu unatofautiana na huu wa Mwathe na Wafula kwa kuwa tulichunguza matumizi ya lugha na mtindo wa uwasilishaji wa habari za mazingira katika chombo kimoja cha habari nchini Kenya (Gazeti la *Taifa Leo*).

Ansdabehere na wengine (2005) walichunguza ushahidi wa utaratibu wa kuteua sampuli au habari zinazoonyesha mwegemeo katika utoaji wa habari zinazoeleza matumizi ya fedha katika kampeni katika magazeti makuu matano kule Marekani. Magazeti haya ni yale ambayo yalieleza matumizi ya dola, michango au upokeaji wa pesa kati ya mwaka wa 1996 na 2000. Walilinganisha data yao na ile iliyokuwa imerekodiwa na Federal Election Commission (FEC). Utafiti huu ulionyesha kuwa data ya magazeti ilikuwa nyingi mara nane ikilinganishwa na data ya FEC. Aidha, magazeti yalisisitiza zaidi ushirikiano wa makundi ya wafadhili katika utoaji wa michango kwa pamoja na pia vilevile pesa zinazotumwa kupitia vifaa vya kidijitali kuliko michango ya watu binafsi, aina za michango na pia michango iliyohusu pesa taslimu. Utafiti huu pia ulibainisha kuwa umma ulionyesha mwegemeo fulani kuhusu masuala ya pesa za kampeni. Hili lilitokana na hoja kuwa kuna tofauti kubwa kati ya uelewa wa masuala ya pesa za kampeni baina ya ripoti za magazeti (zinazodhihirishwa na watu wanaosoma magazeti, na ambao ndio ukweli) ikilinganishwa na umma wasiosoma magazeti na ambao hutegemea maoni ya watu wengine. Utafiti huu ni muhimu kwa uchunguzi wa sasa kwa sababu mbili: a) unahusu 7utoaji wa habari kwa umma kupitia magazeti, jambo ambalo linahamasisha raia kuhusu jinsi mambo yalivyo katika maisha na; b) unaonyesha tofauti za uelewa wa mambo yayo hayo kati ya wale wanaosoma magazeti na wale wasiosoma magazeti. Data za utafiti huu

zinalenga moja kwa moja utafiti wa sasa kwa sababu uelewa wa habari za mazingira huenda ukachangia jinsi wasomaji wa habari za mazingira katika gazeti *Taifa Leo* watakavyotangamana na mazingira. Utafiti wa Ansdabehere (*keshatajwa*) hata hivyo una data tofauti na utafiti wa sasa kwa kuwa unafafanua masuala ya pesa zinazotumiwa wakati wa kampeni kule Marekani. Aidha, data ya uchnguzi huu baada ya kukusanywa ililinganishwa na data iliyorekodiwa na FEC kabla ya maamuzi kutolewa.

Kovach na Rosenstiel (2001) walichunguza maadili katika uanahabari na kusema kuwa uanahabari ni mchakato ambao huanzia na kule kuwa na nidhamu katika kukusanya na kuthibitisha taarifa. Baadaye mwanahabari anaweza kuwasilisha taarifa ambazo zinaweza kutegemewa sasa na baadaye. Data za utafiti huo zilifaa utafiti wa sasa kwa kuwa mazingira ni suala nyeti na linatakiwa lichunguzwe kwa umakini na uadilifu unaofaa na habari zifikishiwe umma kwa njia na mchakato unaofaa.

Vyombo vya habari ni kifaa muhimu kinachochangia jinsi watu na wakuza sera katika serikali wanavyoelewa na kuchangamkia mambo mbalimbali katika jamii (Capella na Jamieson, 1997). Hili linamaanisha kwamba ikiwa vyombo vya habari vitawasilisha habari za mazingira kwa njia ifaayo, vitakuwa dira inayoongoza jinsi watu, (wakiwemo Wakenya) (*msisitizo ni wa mtafiti* ) wanachukulia masuala yanayohusiana na hali ya kila siku ya mazingira. Utafiti huo ulikuwa na manufaa kwa uchunguzi wa sasa kwa sababu ulihusu matumizi ya lugha katika vyombo vya habari kwa ujumla lakini tafiti hizi mbili zinatofautiana pale ambapo utafiti wa sasa ulilenga matumizi ya lugha na mtindo wa uwasilishaji wa habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*.Aidha utafiti wa sasa ulilenga kubainisha ujumbe ulioibuliwa kwa wasomaji wa azeti hili

## 2.3 Tafiti Kuhusu Matumizi ya Lugha katika Gazeti la Taifa Leo

Outuoma (2019) alichanganua vibonzo katika gazeti la *Taifa Leo* vilivyotumiwa kupitisha ujumbe kuanzia mwaka wa 2010 hadi 2014. Utafiti huu ulinuiwa kubaini jinsi ambavyo vibonzo vinavyodhihirika katika kuleta dhana ya ugatuzi kwenye gazeti la *Taifa Leo*. Vilevile ulilenga kuonyesha jinsi mikakati hiyo inavyoathiri ufasiri wa ujumbe unaodhamiriwa na mwandishi wa vibonzo. Outuoma alihusisha Nadharia ya Utambulisho (Ujihusishaji) ya Giles katika kuchanganua data. Uchunguzi wa Outuoma (2019) una manufaa kwa utafiti wetu kwa kuwa unachanganua data katika gazeti la *Taifa Leo*, sawa na wetu. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana kuhusiana na aina za data na pia nadharia zinazotumiwa katika uchanganuzi wa data.

Chepkorir (2016) alichanganua mtindo katika Tahakiki ya gazeti la Taifa Leo. Alichanganua mtindo kwa kufafanua uteuzi wa maneno, virai na miundo ya sentensi iliyotumiwa na mwandishi wa tahariri ya *Taifa Leo*. Vilevile, alichunguza mbinu za lugha na tamathali za usemi. Utafiti wake ulitumia Nadharia ya Umtindo. Matokeo ya utafiti wake yalibainisha kuwa tamathali za usemi zilizotumika kwa wingi ni tashbihi, misemo, kinaya, maswali ya balagha tashhisi, kwelikinzani na taswira. Hali kadhalika, matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa mwandishi anateua maneno na virai, anatumia takwimu na miundo ya sentensi inayowasilisha ujumbe unaoonyesha mwelekeo na mtazamo wake. Utafiti wa Chepkorir unafanana na uchunguzi wa sasa kwa sababu tafiti zote zinalenga ufafanuzi wa mtindo wa habari zilizowasilishwa katika gazeti la *Taifa Leo* na pia kwa kuwa tafiti zote zinatumia Nadharia ya Umtindo. Matokeo ya utafiti wa Chepkorir yalibainisha kuwa mhariri anatumia lugha nyepesi inayoeleweka na wasomaji bila kusababisha utata wowote, mada zimetoa muhtasari wa ujumbe uliomo, na mhariri ameonyesha msimamo

wake kuhusu suala linalozungumziwa. Hata hivyo, uchunguzi huu umejifunga kwenye mtindo wa matumizi ya lugha katika tahakiki ya gazeti la *Taifa Leo* ilhali utafiti wa sasa ulilenga matumizi ya lugha katika kila aina za habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* pamoja mtindo wa uwasilishaji wa habari hizo kwa kuzingatia mbinu zote hata kama si lugha andishi. Kadhalika, Nadharia ya Uchanganuzi wa Usemi inatumiwa katika utafiti wa sasa tofauti na utafiti wa Chepkorir.

Gitau (2015) aliendeleza uchunguzi wa Maina (2011) alipochanganua gazeti la *Taifa Leo* na *Jarida la Kilimo* ili kubainisha lugha ya biashara kwa kutumia mtazamo wa Kipragmatiki. Utafiti huu uliangazia lugha ya kimaandishi na kimazungumzo na data ilifafanuliwa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia tatu: Nadharia za Uhusiano, Umaanisho na Vitendo Usemi. Utafiti huu unatufaa kwa vile mtafiti alichanganua matumizi ya lugha katika gazeti la *Taifa Leo*, sawa na utafiti wetu. Yanayotofautisha tafiti hizi mbili ni aina ya data na nadharia zilizoongoza ufafanuzi wa data.

Odongo (2015) anasema kwamba ingawa suala la kifo ni suala nzito, tanzu anuwai za Kiswahili huliwasilisha kwa namna tofauti na huibuliwa kwa lugha ya pekee yenye mnato wa hisia na mashiko zaidi. Odongo (*ametajwa*) alichanganua uwasilishaji wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili na kubainisha kuwa taswira ya kifo katika mashairi haya ni pamoja na dhoruba ya kifo, kifo kinatamausha, uchungu wa mauti, kifo ni hatima ya kila kiumbe, kina upweke, kifo si mwisho wa maisha, na kifo kina ukatili. Usawiri wa kifo pia hujikita katika mazingira ya mtunzi ambayo hujitokeza katika vipengee vya wakati, dini, utamaduni na lugha. Matokeo ya utafiti huu yanashabihiana na utafiti wetu kwa kiwango fulani kwani utafiti wetu umedhihirisha kuwa baadhi ya habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*, hasa zile zinazohusu majanga, kama janga la Corona na nzige, zinatamausha

na kukatisha tamaa. Utafiti huu pia ulijifunga kwenye uwasilishaji wa habari katika maandishi kwa kutumia lugha, sawa na utafiti wetu, ila aina za habari na chanzo cha habari zenyewe ni tofauti.

Macharia (2015) alitafiti uteuzi wa maneno pamoja na mtindo unaozingatiwa na waandishi wa magazeti yanayowalenga vijana nchini Kenya, yaani *Zuqka* na *Pulse* ili kubainisha jinsi vijana wanavyojitambulisha. Data za uchunguzi huo ni muhimu kwa utafiti wa sasa kwa kuwa tafiti zote mbili zinahusu matumizi ya lugha na mtindo wa kuwasilisha taarifa katika magazeti. Kwa upande mwingine, tafiti hizi zinatofautiana. Kwanza, data zinazochunguzwa katika magazeti ni tofauti katika tafiti hizi. Macharia (keshatajwa) analenga data inayotumiwa na vijana ili kujitambulisha. Anapata data hizi kutoka magazeti ya *Zuqka* na *Pulse*; magazeti ambayo yanawalenga vijana kama hadhira yake. Jambo hili ni tofauti na utafiti wa sasa ambao ulikusudia kuchanganua data inayohusu mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*.

Xianzhong na wengine (2015) walilinganisha na kulinganua uteuzi wa msamiati pamoja na mielekeo ya waandishi wa magazeti ya Uchina na Marekani katika kuripoti ajali. Data za uchunguzi huo ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa zinahusu matumizi ya lugha katika magazeti. Hata hivyo, uchunguzi wa Xianzhong na wenzake unafafanua habari za ajali ilhali utafiti wa sasa unachunguza taarifa za mazingira. Aidha, utafiti wa sasa ulijikita katika gazeti la *Taifa Leo* la Kenya huku utafiti wa Xianzhong na wenzake ukijifunga katika habari za magazeti ya Uchina na Marekani. Isitoshe, Xianzhong anapambanua mielekeo ya waandishi wa magazeti, jambo ambalo linautofautisha utafiti wao na utafiti wa sasa.

Odhiambo (2014) alichanganua athari za ripoti za ugaidi katika gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya. Alibainisha kwamba lugha iliyotumiwa kuandika habari za ugaidi ina ishara za mwegemeo. Mwegemeo huu una athari hasi miongoni mwa wasomaji. Data za utafiti wa Odhiambo ni muhimu kwa utafiti wa sasa. Hata hivyo, utafiti wake unatofautiana na utafiti huu kwa sababu utafiti wa sasa ulilenga habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* la Kenya.

Onyone (2014) alichunguza mtindo, uteuzi wa maneno na mielekeo ya waandishi wa magazeti katika kuripoti matukio ya vita vilivyoshuhudiwa kule Niger Delta baina ya 1997-2009. Data za uchunguzi huo ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa zinahusu mtindo na matumizi ya lugha katika magazeti. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana kuhusiana na aina za data, kwani Onyone anachunguza matukio ya vita kule Niger Delta ilhali uchunguzi wetu unalenga habari za mazingira katika gazeti la T*aifa Leo* la Kenya. Kadhalika, utafiti wa Onyone unachunguza mielekeo ya waandishi wa habari katika magazeti.

Owala, Mohochi na Indede (2013) wanatoa kauli kwamba habari za ugaidi katika gazeti la *Taifa Leo* zina mwegemeo hasi kwa vile zinawachora Waislamu kama wazua fujo na uhasama katika jamii. Utafiti huu una manufaa kwa utafiti wa sasa kwa kuwa tafiti hizi mbili zinachanganua habari katika gazeti la *Taifa Leo*. Hata hivyo, zinatofautiana kuhusu aina ya data, kwani utafiti wa sasa unafafanua taarifa za mazingira zilizoripotiwa kati ya Januari 2021 na Machi 2022.

Maina (2011) alichanganua mbinu za mawasiliano zinazotumiwa kwenye matangazo ya runinga nchini Kenya. Matangazo yaliyochanganuliwa ni yale ya biashara pekee na yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni kubainisha

mbinu za kiisimu na zisizo za kiisimu zinazotumika katika matangazo. Maina (*Keshatajwa*) alibainisha kuwa aina zote mbili za mbinu hutumika katika matangazo ya biashara na kuwa mbinu hizi huwa na dhima mahsusi. Mwingiliano wa mbinu katika matangazo ya biashara ulileta ufanisi wa mawasiliano. Data za utafiti huu zinatoa mwanga kwa utafiti wetu ambao pia ulibainisha kuwa uwasilishaji wa taarifa za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* huhusisha mbinu za kiisimu na zisizo za kiisimu. Mwingiliano huu wa mbinu ulisaidia uelewaji wa habari. Kwa hivyo utafiti wa Maina (*keshatajwa*) unaufaidi uchunguzi wetu kwa upande wa matumizi ya lugha katika vyombo vya habari na mtindo wa mawasiliano.

Conboy (2010) anafafanua matumizi ya lugha katika magazeti na kuonyesha jinsi umbo na yaliyomo kwenye lugha inayotumika katika magazeti yanaweza kuibua mijadala ya kijamii na kisiasa. Aidha, ameonyesha jinsi nguvu za kijamii na kisiasa zinavyoweza kuathiri lugha katika magazeti. Utafiti huo una manufaa kwa uchunguzi huu kwa sababu unahusu matumizi ya lugha katika magazeti. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana kuhusiana na aina za data na magazeti yaliyochunguzwa.

## 2.4 Tafiti Kuhusu Mtindo

Utafiti huu unachunguza mtindo unaohusiana na masuala ya kiisimu. Hata hivyo, kazi za kifasihi ambazo zilichunguza mtindo zimerejelewa kwa kuwa zinalenga kueleza ujumbe katika matini sawa na utafiti wetu. Yafuatayo ni baadhi ya maandishi yaliyochunguzwa ili kujenga msingi wa utafiti huu:

Gathenya (2018) alichanganua mtindo na mielekeo kwa kushughulikia matumizi ya uchimuzi na ukiushi katika riwaya teule za mwandishi Shafi Adam Shafi: *Kuli* (1979) na

*Haini* (2003). Gathenya (keshatajwa) aliteua riwaya hizo kwa kutumia mbinu kusudio kwa kuwa zilidhihirisha mtindo wa mwandishi kupitia matumizi ya uchimuzi na ukiushi ambazo zingetosheleza mahitaji ya utafiti huu. Mtafiti aliongozwa na Nadharia ya Umtindo kama ilivyoelezwa na Leech (1969) ili kubainisha aina za ukiushi wa uandishi wa riwaya husika. Kazi hii inafaa utafiti wetu kwa sababu inachanganua matini kwa kuongozwa na Nadharia ya Umtindo sawa na utafiti wetu. Hata hivyo, utafiti huu uliegemea mtindo kama unavyotumiwa katika tawi la isimu liitwalo Elimu-Mtindo. Aidha, tafiti zote mbili ziliteua data kwa kutumia mbinu kusudio. Hata hivyo, tafiti hizi zinalenga data tofauti na pia utafiti wetu unaongozwa na nadharia mbili kinyume na utafiti wa Gathenya.

Uchunguzi wa Gathenya (2018) unaendelezwa na Motanya na wengine (2021) walipochunguza ukiushi kama elementi ya mtindo kwenye riwaya nne za Kiswahili zilizoandikwa na Ken Walibora kwa kutumia mkabala wa kiisimu. Motanya na wenzake (*keshatajwa*) walifanya uchunguzi wa kimaelezo na uliongozwa na Nadharia ya Umtindo. Kwa mujibu wa Motanya na wenzake, Nadharia ya Umtindo ina nguzo za kuchanganua kazi za kifasihi kwa misingi ya kiisimu na hubainisha kanuni za kuelezea uteuzi uliofanywa na mwandishi katika matumizi yake ya lugha kuhusu mambo ya kijamii, utoaji na upokeaji wa maana na uhakiki wa diskosi. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kimakusudi, data ikakusanywa na kisha kudondoa mifano mwafaka na kuinakili kwa ajili ya kutoa maelezo kulingana na malengo ya utafiti. Utafiti wa Motanya na wenzake (keshatajwa) unaufaidi utafiti wetu kwa kuwa tafiti mbili zina malengo sawa ya kuchunguza matumizi ya lugha na nadharia, unazingatia utaratibu sawa wa uchunguzi wa mtindo, uteuzi na ukusanyaji wa data. Aidha, ingawa utafiti huu ni wa kifasihi, unatumia nadharia ya umtindo kuchanganua matumizi ya lugha ya kiisimu.

Nyamari (2016) alihakiki vipengele vya kimtindo katika *Utenzi wa Katirifu* na alifanya hivyo akitumia nadharia ya Umtindo. Data za utafiti huu ni za manufaa kwa utafiti wa sasa kwa sababu tafiti zote mbili zinachunguza mtindo kwa kutumia vipengele vya nadharia ya Umtindo. Tofauti kati ya tafiti hizi ni kuwa Nyamari (*ametajwa*) alikusanya data kutoka *Utenzi wa Katirifu* ambayo inahusiana na fasihi ilhali utafiti wa sasa ulitumia data za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* huku ukilenga masuala ya kiisimu.

Florin (2016) alibainisha mitindo mitatu inayozingatiwa wakati wa kutoa habari kuhusu kampeni za uchaguzi: mtindo wa kueleza taarifa huku mwanahabari akijitenga na yaliyomo, mtindo unaomlenga mwanasiasa husika na mtindo wa mwanahabari kujihusisha na yaliyomo kwenye habari husika. Florin (*ametajwa*) alifafanua haya alipofanya utafiti linganishi kwa kuchunguza yaliyomo kwenye uripotaji wa habari za kampeni za uchaguzi kule Uswizi, Ujerumani na Marekani. Data ya uchunguzi wa Florin ilifaidi utafiti wa sasa kwa sababu ulishughulikia suala la mtindo katika kuwasilisha ujumbe katika matini. Hata hivyo, unatofautiana na utafiti wa sasa kwa kuwa unaegemea mtindo katika habari za kampeni za uchaguzi tofauti na utafiti wa sasa ambao unalenga mtindo kwa mtazamo wa kiisimu huku ukitumia habari za mazingira.

Murumba (2013) alichambua vipengele mahususi vya kimtindo vinavyodhihirika katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012) na kutoa maelezo jinsi vinavyoathiri muundo wake. Riwaya hii ina mtindo unaojibainisha kwa matumizi ya vipengele mbalimbali vya fani kama usimulizi, mandhari, wahusika, matumizi ya lugha na ploti changamano. Pia, alichunguza namna mwandishi alivyotumia mtindo katika kukuza na kuendeleza ujumbe wake. Data ya uchunguzi wa Murumba ilifaidi utafiti wa sasa kwa sababu ulishughulikia suala la mtindo katika kuwasilisha ujumbe katika matini. Hata hivyo, unatofautiana na

utafiti wa sasa kwa kuwa unaegemea mtindo katika mtazamo wa kifasihi tofauti na utafiti wa sasa ambao unalenga mtindo kwa mtazamo wa kiisimu.

Musembi (2008) alitumia Nadharia ya Umtindo kuchunguza matumizi ya taswira na ukinzano kama kichocheo cha zinduko katika riwaya za G.K.Mkangi: *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Kazi hii inafaa utafiti wetu kwa sababu inachanganua matini kwa kuongozwa na Nadharia ya Umtindo, sawa na utafiti wetu ila mtindo unaosisitizwa katika utafiti wa sasa unahusiana na masuala ya kiisimu. Aidha tafiti zote mbili ziliteua data kwa kutumia mbinu kusudio. Hata hivyo, tafiti hizi zinalenga data tofauti na pia utafiti wetu unaongozwa na nadharia mbili kinyume na utafiti huu.

Wanyama (2007) alifafanua mtindo na maudhui katika utendi wa Wabukusu "*Khuswala Kumuse*" ili kubainisha mtindo uliozingatiwa katika kuwasilisha utendi husika. Kazi yake ina data muhimu kwa utafiti wa sasa kwa sasbabu tafiti zote mbili zilichunguza mtindo wa uwasilishaji wa ujumbe. Kazi ya Wanyama *(ameshatajwa*) ni tofauti na yetu kwa kuwa inatumia data tofauti na inaegemea masuala ya kifasihi ilhali utafiti wa sasa unachunguza mtindo unaohusiana na masuala ya kiisimu.

Kairu (2005) alichanganua uhalisia na mtindo wa Ken Walibora katika fasihi ya watoto akizingatia Nadharia ya Umtindo, jambo linaloufanya utafiti huu ufaidi utafiti wetu. Hata hivyo, data ya utafiti wetu ni habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*.

Weche (2000) alichambua vitabu vya fasihi kwa Kiingereza vya Ezekiel Alembi kwa kuzingatia mtindo na upokezi. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa vitabu hivyo vimeandikwa kwa weledi wa hali ya juu na kwa sababu hiyo vinavutia watoto kwa urahisi. Kazi ya Weche inatufaa kwa kuwa alifafanua matini kimtindo. Kwa upande mwingine,

kazi yake inatofautiana na yetu kuhusiana na aina na chanzo cha data ya utafiti kwani data yake ni ya kifasihi na imeandikwa katika vitabu huku data yetu ikiandikwa katika gazeti la *Taifa Leo.*

## 2.5 Uchanganuzi Usemi Kuhusu Mazingira

Kulingana na ripoti iliyotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na Mazingira (UNEP, 2021), robo tatu ya mataifa kote duniani yameweka mipango ya kukabiliana na kuhimili mabadiliko ya tabianchi. UNEP katika harakati za kupunguza uwezekano wa madhara ya majanga kama vile Corona, inajizatiti kuongeza juhudi za kuelewa zaidi mambo yanayohatarisha mwingiliano wa binadamu na wanyama ili kuweza kulinda mazingira. Mabadiliko katika mazingira huathiri maisha ya viumbe wote kwa namna fulani.

Katika kuthibitisha haya, UNEP (*keshatajwa* ) imeonya kuwa huenda maambukizi ya maradhi ya Corona yakahatarisha ukuaji wa kiuchumi, afya ya binadamu pamoja na wanyama na hata maadili ya kimazingira. Ifahamike kwamba kilimo, ufugaji na mvua huathiriwa na uchafuzi wa mazingira. Kwa upande mwingine, mazingira hutunzwa kwa njia mbalimbali kama vile kupanda miti kwa wingi, kutunza vyanzo vya maji pamoja na kutumia maji vizuri ili kuepuka tatizo la ukame.

Wakibia (2020) anaonekana akisisitiza wazo hili alipotoa kauli kwa Wakenya akiwarai watunzi mazingira kwa hali na mali. Anaipongeza Kenya kwa kupiga marufuku matumizi ya baadhi ya mifuko ya plastiki miaka mitatu iliyopita katika jitihada za kutunza mazingira. Anasema kwamba hatua hii imeifanya nchi ya Kenya kujizolea sifa kocho kocho kote ulimwenguni. Kariuki (2017) anakubaliana na maoni haya anaposema kwamba uhifadhi

wa rasilimali za kimazingira ili kufikia maendeleo endelevu ni jambo ambalo halifai kupuuzwa. Kauli hii imejengwa kwenye msingi kwamba mazingira na rasilimali ndanimwe ni urithi ambao unafaa kutunzwa, kuhifadhiwa na kulindwa, sio tu kwa ajili ya manufaa ya kizazi cha leo lakini hata kile cha siku sijazo. Kariuki (*keshatajwa*) anasisitiza kuwa mazingira yanaathiri maisha ya kila kitu duniani kwa njia moja au nyingine. Kwa hivyo, mazingira na rasilimali ndani yake zastahili kwa utaratibu kulelewa ili kuhakikisha kwamba afya yake haijatelekezwa kwa kisingizio cha maendeleo ya taifa.

Ong'ute (2014) anaonekana kupigia debe suala la utunzaji wa mazingira alipohakiki suala la uhifadhi wa mazingira katika tanzu teule za fasihi ya Kiswahili za Milenia Mpya. Utafiti huu ulilenga kubaini vile fasihi ya Kiswahili ya Milenia Mpya inavyoweza kutumika kuangazia suala hili. Utafiti huu uliongozwa na lengo kuu ambalo ni kuchunguza kazi ya kifasihi za milenia mpya za Kiswahili kwa mtazamo wa uhakiki wa kimazingira. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa uharibifu wa mazingira ni bayana katika jamii na tayari umeangaziwa na watunzi wa Kiswahili. Pia yaliangazia sababu za uharibifu wa mazingira, utawala unavyochangia uharibifu wa mazingira na pia athari za uharibifu wa mazingira. Alibainisha kuwa watunzi wa fasihi ya Kiswahili walilenga kuhamasisha jamii, kuzindua binadamu, kutabiri hali ya baadaye na pia kuburudisha jamii kuhusu mazingira yao. Utafiti huu ni muhimu kwa uchunguzi wetu kwa kuwa sababu moja kuu ni kuhoji iwapo habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* zina uwezo wa kuifanya hadhira kuelewa zaidi hali ya sasa ya mazingira na hatimaye itangamane na mazingira kwa njia chanya.

Dorroh (2015) anasisitiza kuwa mazingira ni kiungo muhimu sana katika maisha ya sasa na ya baadaye ya kila kiumbe. Kwa hivyo, mazingira yanahitaji kupewa kipau mbele na vyombo vya habari. Anahuzunika kwamba masuala ya mazingira huishia kuwekwa

pembeni na kukosa kupewa uzito unaostahili. Mashirika makubwa yanayohusika na upeperushaji wa habari hujishughulisha na habari za siasa, uhalifu, burudani na michezo. Ni muhimu kufahamu kuwa miaka michache ijayo watu duniani kote watakabiliana na changamoto zisizomithilika zinazohusiana na utumiaji wa rasilimali. Kudumu kwetu humu duniani kunategemea uwezo wetu wa kufikiria kwa pamoja kama ulimwengu na kiubunifu na kufanya kazi kwa pamoja ili kupata suluhu kwa matatizo ya kimazingira yanayoikumba dunia nzima (Dorroh, *keshatajwa*).

Pan (2012) aliangazia umuhimu wa mashirika ambayo yanashughulikia masuala ya mazingira na kushauri kuwa pana haja ya mashirika hayo kutoa habari kuhusiana na shughuli zao za utendakazi na ambazo zinalenga mazingira. Habari hizi zikifahamika na washika dau wa kimazingira zitasaidia katika juhudi za pamoja za kupambana na uharibifu wa mazingira.

Kibuga (2009) anathibitisha umuhimu wa kutunza mazingira alipoandika kitabu kwa wanafunzi wa shule za msingi nchini Tanzania, kitabu kinachotoa maelezo kuhusu hali halisi ya mazingira ya Milima ya Tao la Mashariki na kueleza umuhimu wa milima hii na vikwazo vinavyoikumba. Jambo hili linahakikisha wanafunzi watakua wakijua umuhimu wa mazingira yao na jinsi ya kutangamana na mazingira kwa njia ifaayo.

Kwa sababu hii, ni muhimu binadamu kuwa na uelewa wa kina kuhusu mazingira yake. Ufahamu wa hali ya mazingira wa kila siku ni muhimu sana. Hili linatokana na hoja kwamba, mawasiliano yafaayo yana manufaa kwani yanaweza ama kuhatarisha au kuokoa maisha. Vyombo vya habari, yakiwemo magazeti, hutumia lugha katika kuwasilisha habari za mazingira ambazo zina umuhimu wake kwa hadhira lengwa. Mfano mzuri wa jukumu

la vyombo vya habari katika kusaidia utunzaji na uhifadhi wa mazingira ni kazi iliyofanywa na Mwathe na Wafula (2009). Wawili hawa walikusanya habari zilizoripotiwa kwenye magazeti, majarida na vyombo vingine vya habari vilivyohusika katika kampeni za kutetea ziwa Natron. Kampeni hizi zilichochewa na mpango uliokuwa unanuia kujengwa kwa kiwanda cha simiti katika Ziwa Natron. Ujenzi wa kiwanda hiki ungehatarisha maisha ya ndege wanaoishi ndani ya Ziwa hili pamoja na jamii za wafugaji ambao walitegemea ziwa hili kwa mifugo wao na pia maisha yao. Ripoti ambazo zilihusu kampeni ya kuokoa ziwa hili kutoka kwa vyombo mbalimbali vya habari zilikusanywa kuanzia mwaka wa 2006 hadi mwaka wa 2009. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa asilimia 82 ya kampeni hizo zilikuwa chanya (zikiunga mkono kulindwa kwa Ziwa Natron), asilimia 16 zilikosa msimamo na asilimia 2 zilikuwa hasi. Matokeo ya utafiti huu ni muhimu kwa utafiti wetu kwani yanahusu habari za mazingira katika vyombo vya habari na pia unalenga uhifadhi wa mazingira.

Alexander (2008) aliwasilisha mkururo wa tafiti za kiasili na kiujarabati zinazohusu lugha na usemi uliotumika katika mijadala ya masuala ya kimazingira na kiekolojia. Uchunguzi huu ulitegemea matini na tanzu za aina mbalimbali zikiwemo tovuti za makampuni, matangazo, makala kwenye magazeti, hotuba na semi za wanaharakati ili kujadili na kuangazia changamoto ambazo zinaonekana kukumba na kuhatarisha ekolojia. Katika utafiti huu, Alexander anauliza: changamoto zinazoikumba ekolojia huwasilishwaje katika matini? Je, tunaelewa nini kuhusu changamoto zinazoikumba ekolojia kwenye matini zenye vianzo tofauti tofauti? Ni vipengele gani vya lugha vinavyohusishwa katika usemi wa kiekolojia katika miktadha na sajili mbalimbali? Utafiti huo unaonekana kuangazia na kutilia mkazo haswa pale ambapo masuala ya lugha na usemi wa kiekolojia

yanapotagusana na biashara, uchumi na siasa. Utafiti huo unahusiana na utafiti wa sasa kwa vile ulichunguza lugha na usemi unaotumika kufafanua masuala ya mazingira katika makala kwenye magazeti. Hata hivyo, ni tofauti na utafiti wa sasa kwa sababu unaenda nje ya mipaka ya utafiti wa sasa pale unapochunguza matumizi ya lugha inayowasilisha mazingira kama vile tovuti za makampuni, hotuba na semi za wanaharakati.

Varzari (2001) alichanganua usemi katika sheria za kimazingira. Mtafiti huyu alichunguza iwapo kulikuwa na mbinu za kiusemi ambazo zinawasilisha na kusambaza ubaguzi kwa walinda mazingira. Pia alitoa suluhu kwa usemi wa kisheria ambao tayari umekoleza ubaguzi wa kimazingira. Uchunguzi wa Varzari ulifaulu kwa sababu ulishirikisha Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi inayofafanuliwa na Van Djik. Data za utafiti huu ni muhimu kwa utafiti wetu kwa kuwa unalenga kutalii jinsi lugha inavyoweza kutumika kama chombo cha kufahamisha umma kuhusu yote yanayouzunguka na pia umuhimu wa kutangamana na mazingira kwa njia inayofaa.Tafiti hizi zinatofautiana kwa misingi ya nadharia zilizohusishwa katika tafiti husika.

Varzari (*ametajwa*) anaungwa mkono na Ong'ute (2014) anapochunguza suala la utunzaji wa mazingira kupitia uhakiki wa uhifadhi wa mazingira katika tanzu teule za fasihi ya Kiswahili ya Milenia Mpya. Utafiti huu ulilenga kubaini vile fasihi ya Kiswahili ya Milenia Mpya inavyoweza kutumika kuangazia suala hili. Utafiti huu uliongozwa na lengo kuu ambalo ni kuchunguza kazi za fasihi za Kiswahili za Milenia Mpya kwa mtazamo wa uhakiki wa kimazingira. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa uharibifu wa mazingira ni bayana katika jamii na tayari umeangaziwa na watunzi wa Kiswahili. Aidha yanafafanua sababu za uharibifu wa mazingira, utawala unavyochangia uharibifu wa mazingira na pia athari za uharibifu wa mazingira. Varzari (*ametajwa*) alibainisha kuwa watunzi wa fasihi

ya Kiswahili walilenga kuhamasisha jamii, kuzindua binadamu, kutabiri hali ya baadaye na pia kuburudisha jamii kuhusu mazingira yao. Utafiti huu ni muhimu kwa uchunguzi wetu kwa kuwa lengo kuu la utafiti huu ni kuhoji iwapo habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* zina uwezo wa kuifanya hadhira kuelewa zaidi hali ya sasa ya mazingira na hatimaye itangamane na mazingira kwa njia chanya.

## 2.6 Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Usemi (NUU), ( kama ilivyorejelewa katika kazi hii ) na Nadharia ya Umtindo (NU).

### 2.6.1 Nadharia ya Uchanganuzi Usemi (NUU)

Uchanganuzi wa usemi ni ile hali ya kufafanua lugha katika matumizi yake (Brown na Yule, 1983). Katika hali hii, tulichanganua jinsi binadamu hutumia lugha ili kuwasiliana. Zaidi ni kuwa, katika uchanganuzi wa usemi, kinachosisitizwa ni jinsi mzungumzaji anavyounda na kuwasilishia msikilizaji ujumbe wa kiisimu na namna msikilizaji hufasili huo ujumbe wa kiisimu. Hali kadhalika, uchanganuzi wa usemi unahusu jinsi miundo ya lugha inavyotumika katika mawasiliano. Uchanganuzi usemi ni mtazamo mpya wa kisayansi wa kuchunguza lugha katika vipengele vyake vyote , vikiwemo hata vile vikubwa kuliko sentensi, yaani ni uchanganuzi wa lugha katika kiwango cha usemi ( na matini (*msisitizo ni wangu*) (Ponton na Larina , 2017). Maelezo ya Ponton na Larina (*wametajwa*) yanaelekea kuonyesha kwamba uchanganuzi wa usemi hutegemea sana mwegemeo wa mtafiti na hasa kile ambacho analenga kueleza. Gee (1999) kwa upande mwingine anasema kwamba lugha ina sifa ya kimuujiza kwani wakati tunapozungumza au kuandika, kwanza hufikiria kile tunataka kusema ili kiafiki hali au muktadha wa mazungumzo. Hata hivyo, inatokea kuwa kile tunachozungumza ndicho huumba hiyo hali au muktadha. Hili

linaonyesha kwamba tunaweza kuifanya lugha yetu iafiki katika hali au muktadha ambao lugha yetu imeuumba.

#### 2.6.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Usemi

Utafiti huu ulitumia Nadharia ya Uchanganuzi Usemi (NUU) ili kufafanua matumizi ya lugha katika kuwasilisha taarifa za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. NUU iliasisiwa na Fairclough mwaka wa 1989. Taaluma hii hushughulikia namna lugha inavyotumiwa na wanajamii katika miktadha ya kijamii kwa kuitazama lugha kama uzoefu wa wanajamii. NUU huonyesha lugha kama kifaa muhimu katika shughuli za kijamii ambayo husaidia katika ufafanuzi wa maana katika jamii kwa kujadili mabadiliko yanavyotokea kijamii na kitamaduni. Nadharia hii huchukulia kwamba lugha huumbwa na jamii na vilevile huumba vile watumiaji wake wanavyoitumia kijamii. Nadharia ya Uchanganuzi Usemi ilichimbuka kutokana na Isimu Jadilifu ambayo ilianzishwa katika Chuo Kikuu cha East Anglia katika miaka ya 1970.

Nadharia ya Uchanganuzi Usemi ilitumiwa kutokana na uwezo wake wa kuwa kifaa cha kutegemewa cha kuchunguza uhusiano uliopo baina ya matumizi ya lugha na muktadha wa kijamii unaochangia matumizi hayo. Aidha, Nadharia ya Uchanganuzi Usemi ilifaa katika utafiti huu kutokana na uwezo wake wa kubainisha miundo na michakato ya kijamii na kitamaduni kwa upande mmoja na sifa za kimatini kwa upande mwingine (Fairclough na Wodak, 1997).

Usemi ni kule kujieleza kwa kutumia maneno. Ni jina linalopewa maumbo ya lugha yanayozidi sentensi moja (Brown na Yule, 1981). Usemi huhusisha matini, mahusiano na

miktadha. Katika Uchanganuzi Usemi, mchanganuzi sharti achanganue uhusiano kati ya matini, mahusiano na miktadha ili usemi huo uweze kueleweka.

Fairclough (2003) alibuni nadharia yenye mihimili mitatu ya kutafiti mazungumzo ambapo lengo lake ni kubaini aina tatu tofauti za uchambuzi.

Ifuatayo ni mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Usemi inayopendekezwa na Fairclough (2003) kama inavyotumikizwa katika utafiti huu:

i) Uchambuzi wa matini ya lugha (simulizi au andishi),

ii) Uchambuzi wa uzungumzaji (mchakato wa utoaji matini, usambazaji na utumizi) na

iii) Uchambuzi wa mijadala ya matukio kama shughuli katika jamii

Utafiti wetu ulidhamiria kubainisha vipengele vya lugha na mtindo unaozingatiwa katika uwasilishaji wa taarifa za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* na ujumbe ulioibuliwa. Nadharia ya Uchanganuzi Usemi ilitumika kwenye utafiti huu katika kuchambua matumizi ya lugha ya waandishi wa gazeti la *Taifa Leo* wanapowasilisha taarifa za mazingira. NUU haingewasaidia watafiti kuchanganua mitindo ya kuwasilisha habari za mazingira. Kwa sababu hii, watafiti walitumia Nadharia ya Umtindo ili kufidia pengo hili. Sehemu inayofuata inatoa maelezo kuhusu Nadharia ya Umtindo.

### 2.6.2 Nadharia ya Umtindo (NU)

Mtindo hutumiwa kuashiria jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha fulani, na mtu fulani na kwa lengo fulani (Leech na Short, 1981) wakinukuliwa na Murumba (2013). Mtindo unaweza kutumiwa kuchanganua matini za kifasihi au za kiisimu. Aidha, mtindo unaweza kuhusishwa na mazoea ya lugha ya mtu binafsi au upekee wa mtu katika matumizi ya lugha (Crystal na Davy, 1969) katika Murumba (2013). Kulingana na Barasa (2013), Umtindo huweka wazi sheria za kuelezea uchaguzi unaofanywa na watu katika matumizi yao ya lugha kuhusu mambo ya kijamii, utoaji na upokeaji wa maana na uhakiki wa kidiskosi.

Hali kadhalika, Umtindo unaweza kuelezwa kuwa ni ukiushi katika matumizi ya lugha. Unahusisha ukiushi kutoka kanuni za lugha ambazo zimezoeleka au za kimapokeo. Ukiushi huu pia hujitokeza katika matumizi ya sajili mbalimbali za lugha (McIntosh 1963; Kitsao 1975; Leech na Short 1981 na Wales, 1990) katika Murumba (2013).

Tunapofafanua mtindo huwa tunaeleza mwandishi husika, kuwa upekee wake ndicho kile kinachodhihirika katika matini alizoandika, yaani, mtindo ndio unaomtambulisha mtu.

Wamitila (2003) anaeleza Umtindo kama taaluma iliyoko kati ya uchunguzi wa lugha na uchunguzi wa fasihi au jinsi lugha inavyotumiwa katika matini. Leech (1969) anatumia istilahi `elimumitindo` kurejelea ule ufafanuzi wa maandishi kiisimu. Anasema kwamba msamiati katika upana wake huweza kuelezeka kikamilifu kwa kuzingatia dhana za kiisimu. Katika kazi hii, mtindo unaorejelewa ni ule unaohusiana na masuala ya kiisimu kwa ujumla wake ili kurejelea namna jambo fulani linavyoshughulikiwa, na hasa namna zote zinazozingatiwa katika kuwasilisha habari za mazingira.

#### 2.6.2.1 Mihimili ya Nadharia ya Umtindo

Nadharia ya Umtindo (NU) iliasisiwa mwaka wa 1904 na Viktor Shyklovsky alipogundua kuwa lugha hutumika kwa njia inayofanya mambo ya kawaida kuonekana mapya (Motanya, 2021).Wengine ambao waliishughulikia nadharia hii katika miaka ya awali ni pamoja na Geoffrey Leech baina ya miaka ya 1965 na 1969. Baadaye nadharia hii imeweza kupanuliwa na wasomi wengine. Miongoni mwa wasomi hawa ni Simpson (2004). Kwa upande mwingine, Leech (1969) anasema kuwa umtindo ni uchanganuzi na maelezo ya matini katika mtazamo wa kiisimu kama taaluma, unaoweka pamoja uhakiki wa kifasihi na kiisimu ingawa haujitegemei. Fowler (1975) anasema kuwa Nadharia ya Umtindo ilitajwa awali kama Nadharia ya Kimtindo kwa mujibu wa Buffon (1930). Mtindo ni namna lugha inavyotumiwa kupitisha ujumbe. Umtindo unaonyesha jinsi mpangilio wa maneno wa kisintaksia unavyoongoza utaratibu wa usomaji ili kupata maana (Gathenya, 2018). Mtindo ni namna ambavyo lugha hutumiwa kama mali ya mtu binafsi (Leech, 1981). Mtindo ni matumizi ya lugha kupitia uteuzi unaotumiwa na mwandishi mmoja katika uandishi wake wa matini ya aina fulani. Kwa hivyo mtindo unahusu uteuzi wa msamiati, misemo, tamathali za usemi, miundo ya sentensi, mbinu za uchimuzi, ukiushi miongoni mwa mengine. Mwandishi pia anaweza kuteua kauli yenye nguvu za kushawishi na kuteka makini ya msomaji. Hufanya hivi akiwa na lengo la kupamba kazi yake au labda kuvutia hadhira.

Hali kadhalika, mtindo pia hutegemea jinsi msomaji atakavyoelewa anachosoma kulingana na ubunifu wake mwenyewe (Gathenya, *keshatajwa*). Msomaji ndiye anayesoma kilichoandikwa na mwandishi, na kwa hivyo ni sharti aweze kufikiria kwa undani zaidi anayoyasoma ili aweze kuelewa anachokusudia mwandishi, kitakachomwezesha

kung’amua tatizo na suluhu la suala hili katika jamii yake. Uchaguzi wa mtindo hutegemea vile vipengele vya uteuzi wa kiisimu unaohusiana na njia tofauti za kuchunguza ujumbe sawa. Lodge (1972) anasema kuwa mtindo ni jinsi mwandishi anavyojifafanua. Mwandishi huteua vipengele fulani vya lugha ili kueleza fikira au maoni yake na kwa kufanya hivyo anawasilisha ujumbe fulani kwa wapokezi wa ujumbe huo.

Ifahamike kwamba mtindo sio tu uteuzi wa maneno bali pia ni mwingiliano wa maneno (Turner, 1984). Hili lilidhihirika pale ambapo wanahabari walipanga maneno kwa utaratibu fulani ili kuwasilisha ujumbe waliokusudia. Na hii ndio maana tunapata upekee fulani kutokana na utaratibu wa upangaji wa maneno katika matini zinazofafanua habari za mazingira. Mtindo ni uchunguzi wa makini wa maneno katika matini unaohusisha jinsi mtu anavyoangalia anachosema au kuandika. Aidha, ni mfuatano wa ruwaza za matini (Haynes,1995).

Leech (*keshatajwa*) anasema lugha huwasilisha hisia au tajriba fulani za mwandishi kwa hadhira yake. Isitoshe, lugha ni wenzo wa kutekelezea uelewa wa ujumbe ulionuiwa. Umtindo hulenga kuoanisha ujumbe na lugha. Lugha hufaulisha kazi ya mwandishi kwani huwasilisha fikira zake. Wazo hili linadhihirika katika utafiti wetu kupitia jinsi waandishi wa habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* wanavyoteua kimaksudi vipengele vya lugha ili kumwasilishia msomaji taarifa za mazingira kwa kusudi fulani. Malengo haya ni pamoja na kushauri, kuhimiza, kutahadharisha, kuhamasisha, kurai umma kuhusiana na masuala ya mazingira miongoni mwa madhumuni mengine.

Kimsingi, nadharia hii inaweza kuchunguza kile kinachosemwa au kuwasilishwa na jinsi kinavyowasilishwa (Motanya na wenzake, *keshatajwa*). Umtindo inazingatia mikabala

miwili. Upo mkabala wa jadi ambao unatenganisha baina ya yaliyosemwa (yaliyomo au maana au ujumbe) na jinsi yanavyosemwa (fani). Mkabala wa pili ambao ni wa kisasa unatazama mtindo kama taratibu za kitaaluma zinazochunguza jinsi ujumbe au maana inavyowasilishwa kwa matumizi ya njia na mbinu tofauti ambazo zinadhamiriwa kuwa na athari fulani za kiujumi kwa mlengwa au msomaji ,Wamitila (2010) na Simpson (2004). Ifuatayo ni mihimili ya Nadharia ya Umtindo kwa muhtasari:

i) Lugha hutumiwa kiufundi – lugha inaweza kuwa rahisi au gumu.
ii) Kuna matumizi ya nafsi ya kwanza, pili na tatu katika usimulizi.
iii) Hisia za mwandishi zinaonekana, zikionyesha dhihaka, mapenzi, matumaini, ukali au kejeli.
iv) Kuna mpangilio wa sura au matukio katika matini; sura fupi fupi au ndefu, nyingi zilizopangwa kwa nia fulani.
v) Kuna matumizi ya tamathali za usemi kama vile tashbihi, sitiari, tashhisi, na kadhalika kwa wingi.
vi) Kuna matumizi ya picha na michoro yenye rangi tofauti kwa lengo la kujenga uhalisia na kuvutia msomaji.
vii) Uteuzi wa msamiati uliotumika huleta mvuto kwa msomaji kwa kumtia ari ya kusoma.

Suala la mtindo wa uwasilishaji wa taarifa za mazingira lilichanganuliwa kwa kuzingatia kanuni za Nadharia ya Umtindo.

## SURA YA TATU

## MBINU ZA UTAFITI

### 3.0 Utangulizi

Sura hii inaangazia muundo wa utafiti, eneo la utafiti, na kundi lengwa katika utafiti huu. Aidha maelezo kuhusu utafiti wa maktabani, uteuzi wa sampuli, vifaa vya utafiti, ukubalifu na utegemeo wa vifaa vya utafiti, ukusanyaji data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data yamefafanuliwa. Pia maelezo kuhusu maadili kuhusiana na utafiti yametolewa.

### 3.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kimaelezo na ulidhamiria kuchanganua matumizi ya lugha, mtindo unaozingatiwa na waandishi wa habari katika gazeti la *Taifa Leo* katika kuripoti taarifa za mazingira pamoja na jumbe unaotolewa na habari hizo. Lengo hili lilitimizwa kupitia matumizi ya habari za mazingira zilizochapishwa kwenye magazeti ya *Taifa Leo* nchini Kenya kuanzia Januari 2021 hadi Machi 2022. Utafiti ulishirikisha matini 270 za gazeti la *Taifa Leo* ambazo ziliteuliwa kimakusudi ili kupata data lengwa. Mbinu ya utafiti wa maktabani ilitumiwa ili kutimiza malengo mawili. Kwanza, kuwekea utafiti huu msingi kupitia kuaua maandishi yanayohusiana na utafiti unaokusudiwa na pili, kuchanganua taarifa za mazingira katika magazeti ya *Taifa Leo* yanayofahamisha masuala ya mazingira ili kupata data lengwa.

### 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani. Kwanza, mtafiti alipekua majarida, vitabu, mtandao, makala na tafiti ambazo zimefanywa na zinahusiana na utafiti unaokusudiwa. Upekuaji huu wa maandishi ulibainisha kwamba kuna tafiti nyingi ambazo zimefanywa kuhusu

matumizi ya lugha katika vyombo vya habari kwa kulenga masuala tofauti tofauti. Masuala hayo ni kama vile ugaidi, ajali vita, visa vya ghasia, dhuluma za kijinsia, visa vya ulipuaji wa mabomu, mazingira, matumizi ya lugha, utambulisho kwa vijana, umuhimu wa vyombo vya habari, miongoni mwa mengine Macharia (2015), Onyone (2014), Conboy 2010), Odhiambo (2014). Upekuzi huu pia ulithibitisha kwamba mtindo unaozingatiwa katika kuripoti taarifa katika vyombo vya habari pia ulichunguzwa na watafiti katika miktadha inayotofautiana. Miktadha hiyo ni kama vile matukio ya ajali, vita na utambulisho kwa vijana, maudhui katika fasihi miongoni mwa mambo mengine. Hata hivyo, mtafiti alibaini kwamba pana haja ya kuchanganua matumizi ya lugha na mtindo wa uwasilishaji wa habari katika gazeti la *Taifa Leo* ili kufafanua jinsi taarifa za mazingira zilivyowasilishwa na ujumbe unaojitokeza katika taarifa hizo.

Pili, ili kupata data ya utafiti wa sasa, mtafiti alisoma na kuchambua magazeti ya *Taifa Leo* nchini Kenya ambayo yalichapishwa kuanzia Januari 2021 hadi Machi 2022 ili kubaini matumizi ya lugha, mtindo wa uwasilishaji wa habari za mazingira na ujumbe ulioibuliwa katika habari hizo.

### 3.3 Kundi Lengwa

Sehemu hii inahusu habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Matini ambazo zinalenga habari za mazingira zilichanganuliwa kwa mujibu wa nadharia teule.

### 3.4. Utafiti wa Maktabani

Mtafiti alitumia mbinu ya upekuzi wa vitabu, majarida na makala yanayofaa ili kudhibiti mada kabla ya kuchanganua matini za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Baada ya kusoma maandishi yanayohusiana na utafiti huu, ilibainika kwamba tafiti nyingi

zimefanywa kuhusu mazingira na pia matumizi ya lugha na mtindo katika vyombo vya habari ila yakihusiana na masuala tofauti. Kuna magazeti mengi nchini Kenya ambayo yanatoa habari za mazingira kwa matumizi ya lugha na kwa kuzingatia mitindo maalum. Magazeti hayo ni pamoja na *The Standard, The Daily Nation*, miongoni mwa mengine. Gazeti la *Taifa Leo* liliteuliwa kimaksudi kwa sababu utafiti huu ulinuia kuchanganua habari za kimazingira ambazo zinawasilishwa kwa lugha ya Kiswahili. Huu ni uteuzi wa kudhamiria kwa sababu mtafiti aliteua kile ambacho kinaakisi malengo ya utafiti husika.

## 3.5. Uteuzi wa Sampuli

Magazeti ya *Taifa Leo* yaliyochapishwa kati ya Januari 2021 hadi Machi 2022 yalichanganuliwa na taarifa zinazoshughulikia masuala ya mazingira zilichunguzwa. Kipindi hiki kinaafiki utafiti huu kwa kuwa taarifa muhimu kuhusiana na mazingira zilitolewa wakati huu. Aidha, palikuwa na haja ya kueleza hali ya sasa ya mazingira. Sampuli dhamirifu ilitumiwa ambapo matini 270 za gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya ziliteuliwa na kuchunguzwa. Hili lilifanywa kwa sababu utafiti huu ulilenga uchanganuzi wa matini zilizohusiana na mazingira na ambazo ziliandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Isitoshe, utafiti ulilenga kubaini iwapo matumizi ya lugha na mtindo wa kuwasilisha matini unamsaidia mwanahabari kuwasilisha ujumbe aliokusudia kwa msomaji. Ukweli ni kwamba kipindi teule kilikuwa na matini zaidi ya 270 ambazo zilieleza habari za mazingira ila matini zote hazikuhusishwa katika utafiti kwa kuwa watafiti walichuja baadhi ya matini. Hili lilifanywa ili kuepuka marudio na pia kwa lengo la kutaka kuzingatia matini zilizolenga habari lengwa.

### 3.6. Vifaa vya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani. Mtafiti alichanganua matini 270 za Gazeti la *Taifa Leo* zilizochapishwa kati ya Januari 2021 na Machi 2022. Matini 270 kutoka Gazeti la *Taifa Leo* ziliteuliwa kimakusudi ili kuchunguza masuala ya mazingira.

### 3.7. Ukubalifu na Utegemeo wa Vifaa vya Utafiti

Uchunguzi huu ulidhamiria kuhakikisha ukubalifu na utegemeo wa vifaa vya utafiti kwa kuzingatia yafuatayo:

#### 3.7.1. Ukubalifu wa Vifaa vya Utafiti

Ukubalifu wa vifaa vya utafiti ulizingatiwa kwa kuhakikisha kuwa vifaa vya utafiti vilipima kile kilicholengwa kwa njia iliyokusudiwa. Utafiti huu ulikusudiwa kuchanganua kwa kina uteuzi wa vipengele vya lugha na kutathmini mtindo wa kuwasilisha matini zilizohusu mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya katika kipindi teule. Lengo lilikuwa kubainisha iwapo taarifa hizo ziliibua ujumbe wa mazingira uliokusudiwa kwa msomaji wa matini hizo.

#### 3.7.2. Utegemeo wa Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya utafiti husemekana kuwa vya kutegemewa iwapo vimetumiwa na watafiti wengine na kuibua matokeo yaliyokusudiwa. Ili kuhakikisha kutegemewa kwa vifaa vya utafiti, mtafiti alifanya utafiti wa awali katika maktaba ya Nation Media Group kabla ya kuanza utafiti kamili. Katika utafiti wa awali, mtafiti alichambua taarifa za mazingira katika magazeti kadhaa ya *Taifa Leo*. Katika zoezi hili, mtafiti alilenga kuchanganua

matumizi ya lugha, mtindo wa kuwasilisha taarifa za mazingira na ujumbe ulioibuliwa na taarifa hizo na kuthibitisha kuwa angepata matokeo yaliyotarajiwa.

### 3.8. Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Ili kupata data za msingi za utafiti huu:

i) Mtafiti aliteua kimakusudi magazeti ya *Taifa Leo* yaliyochapishwa kati ya Januari 2021 na Machi 2022

ii) Mtafiti alisoma kila mojawapo ya magazeti aliyoteua na kudondoa kwa kudhamiria matini ambazo zilihusu masuala ya mazingira.

iii) Matini zote za kimazingira zilizoteuliwa ziliorodheshwa kulingana na mwaka na mwezi wa kuchapishwa na pia kulingana na aina zake. Kijumla mtafiti aliteua matini za kimazingira 270.

iv) Mtafiti alichunguza kila matini akiwa na lengo la kutathmini namna waandishi wa habari walivyotumia lugha na mtindo waliozingatia kuwasilisha masuala yaliyohusu mazingira na jinsi mambo haya yalivyohusiana na ujumbe.

v) Data ya kithamano na kitakwimu ndiyo ililengwa na ilihusu maelezo yaliyotolewa na waandishi wa habari kwenye magazeti la *Taifa Leo* yaliyosheheni taarifa za mazingira.

### 3.9. Mbinu za Uchanganuzi wa Data

Utafiti huu ulichanganua data ya kithamano kwa kuzingatia utaratibu ufuatao:

i. Data ilikusanywa kwa kudondoa vipengele vya matumizi ya lugha kimtindo katika kuwasilisha ujumbe kwenye matini zilizohusu mazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* katika kipindi kinachoanzia Januari 2021 hadi Machi 2022.

ii. Data hii ilikuwa inahusu maelezo ya masuala ya mazingira yaliyotolewa na waandishi wa habari na vilevile mtindo waliozingatia katika kuwasilisha matini hizo na uhusiano wa habari na ujumbe uliowasilishiwa wasomaji.

iii. Ili kurahisisha uchanganuzi wa data, mtafiti alizipanga data zilizokusanywa katika safu. Aliweka data katika safu ya mwaka data hiyo ilichapishwa.

iv. Aidha, data zilizochapishwa zilipangwa na kuchanganuliwa kulingana na aina ya lugha, sura ya maandishi, herufi kubwa na ndogo, picha aya, msamiati na kadhalika.

v. Data ilichanganuliwa kwa mujibu wa mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Usemi (NUU) na Nadharia ya Umtindo (NU).

vi. Nadharia ya Uchanganuzi Usemi ilikuwa faafu kwa utafiti huu kutokana na uwezo wake wa kubainisha uhusiano uliopo baina ya miundo na mchakato ya kijamii na kitamaduni kwa upande mmoja na sifa za kimatini kwa upande mwingine (Fairclough na Wodak, 1997).

vii. NUU huonyesha lugha kama kifaa muhimu katika shughuli za kijamii ambayo husaidia katika ufafanuzi wa maana katika jamii kwa kujadili mabadiliko yanavyotokea kijamii na kitamaduni. Nadharia hii huchukulia kwamba lugha huumbwa na jamii na vilevile huumba vile watumiaji wake wanavyoitumia kijami. Kimsingi, huchanganua lugha na namna inavyotumika.

viii. Kwa upande mwingine, suala la mtindo wa uwasilishaji wa habari za mazingira lilichanganuliwa kwa kuzingatia kanuni za Nadharia ya Umtindo. Kulingana na Nadharia ya Umtindo, uchunguzi wa mitindo huangaliwa kwa kuchunguza mikabala miwili.

ix. Upo mkabala wa jadi ambao unatenganisha baina ya ujumbe au maana na fani.

x. Mkabala wa pili ambao ni wa kisasa unatazama mtindo kama taratibu za kitaaluma zinazochunguza jinsi ujumbe au maana inavyowasilishwa kwa matumizi ya njia na mbinu tofauti ambazo zinadhamiriwa kuwa na athari fulani ya kiujumi kwa mlengwa au msomaji.

xi. Utafiti huu ulizingatia mikabala yote miwili katika kuchanganua mitindo ambayo waandishi wa habari walizingatia katika kuwasilisha habari za mazingira.

### 3.10. Uwasilishaji wa Data

Data ya utafiti huu ilikuwa ya kithamano na kitakwimu. Data hii iliwasilishwa kwa kutolewa ufafanuzi, maelezo na mifano ya matumizi ya lugha na mtindo wa kuripoti taarifa za mazingira.

### 3.11. Maadili ya Utafiti

Utafiti huu ulizingatia maadili yanayomhusu mtafiti, yaliyowahusu watafitiwa na yaliyohusu mchakato wa utafiti ifuatavyo:

#### 3.11.1. Maadili ya Utafiti Yanayomhusu Mtafiti

Mtafiti aliomba idhini ya kufanya utafiti kutoka kwa Shule ya Mafuzu ya Chuo Kikuu cha Maasai Mara. Vilevile aliomba kibali kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

kabla ya kuomba ruhusa ya kuchunguza matini lengwa kutoka kwa Shirika la Nation Media Group.

### 3.11.2. Maadili ya Utafiti Yanayowahusu Watafitiwa

Data ya utafiti ilikusanywa kutoka gazeti la *Taifa Leo*. Gazeti hili linamilikiwa na Shirika la Nation Media Group. Kwa hivyo, idhini ya shirika hili iliombwa kabla ya kuanza utafiti kamili. Mtafiti alihakikisha kuzingatia kanuni zote zilizohusiana na hakimiliki ya gazeti la *Taifa Leo*.

### 3.11.3. Maadili ya Utafiti Yanayohusu Mchakato wa Utafiti

Sehemu hii ilijumuisha kipindi chote kuanzia uandishi wa pendekezo la utafiti hadi uandishi wa tasnifu na kwa hivyo mtafiti alinukuu kazi zote alizorejelea katika utafiti huu na kuhakikisha kwamba amekusanya, amechanganua na kuwasilisha data kwa uadilifu unaotosha.

# SURA YA NNE

## UCHANGANUZI WA DATA, UFASIRI NA MATOKEO YA UTAFITI

### 4.0. Utangulizi

Sura hii inahusu uchanganuzi wa data na ufasiri wa matokeo ya utafiti. Inaanza kwa kueleza aina ya data iliyokusanywa. Aidha, inatoa maelezo kuhusu jinsi data ilivyokusanywa, ikachanganuliwa hatua kwa hatua na kutoa ufasiri wa matokeo ya utafiti kwa mujibu wa malengo ya utafiti.

### 4.1 Uchanganuzi wa Data na Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulitumia data ya kithamano. Data ya kithamano ilichanganuliwa kwa kutolewa ufafanuzi na maelezo ya kina. Uchanganuzi ulifanywa ili kubainisha vipengele vya lugha na mtindo uliotumiwa na wanahabari kuwasilisha ujumbe katika matini zilizohusu mazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* na ujumbe ulioibuliwa.

Dhana ya mazingira katika utafiti huu inatumiwa kufumbata takriban masuala yote yanayohusiana na mazingira, yaani kila kitu kinachokizingira kiumbe ( kilicho hai au kisichokuwa hai ). Data hii ilikuwa inahusu maelezo ya masuala ya mazingira yaliyotolewa na waandishi wa habari na vilevile mtindo waliozingatia katika kuwasilisha matini hizo na ujumbe ulioibuliwa. Data ilichanganuliwa kwa mujibu wa mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Usemi na Nadharia ya Umtindo.

Matini za usemi wa taarifa za habari katika gazeti zina upekee wake unaoonekana upande wa mtindo, muundo na uteuzi wa msamiati. Kutokana na itikadi zilizoshehenezwa katika matini hizo, huenda msomaji akakosa kubainisha taathira zake kutokana na uzingatiaji wa matumizi ya lugha kijuujuu na kupuuza undani wa matini zenyewe. Kwa hali hiyo, utafiti

huu ulizingatia mkabala wa kiuchanganuzi kuhakiki matumizi ya lugha katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo*.

Wanahabari hutumia mitindo mbalimbali kuwasilisha jumbe zao kwa wasomaji wanaowakusudia. Mitindo inayotumiwa inaweza kuchunguzwa kwa mujibu wa Nadharia ya Mitindo. Utafiti huu ulitumia Nadharia ya Umtindo kwa sababu inajikita kwenye uchunguzi wa matumizi ya lugha katika matini za aina mbalimbali. Uchunguzi wa matumizi ya lugha hunapania kubainisha ubunifu uliopo kwenye lugha iliyotumika katika matini fulani na kwa kuutekeleza kwa undani unasaidia kuelewa matini kwa urahisi (Simpson, 2004). Nadharia ya Umtindo hudhamiria kuchunguza na kuchanganua matini kwa kuzingatia taratibu za kisayansi pamoja na zile za kitaaluma. Utafiti huu ulichunguza matini 270 za kimazingira kutoka katika magazeti ya *Taifa Leo* kwa kuzingatia Nadharia ya Umtindo ili kubainisha jinsi lugha ilivyotumiwa kutoa ujumbe kwa walengwa.

Sehemu inayofuata inatoa maelezo ya kina kuhusu vipengele vya matumizi ya lugha kimtindo katika gazeti la *Taifa Leo*.

## 4.2. Vipengele vya Lugha Teule Katika Ripoti za Habari za Mazingira Katika Gazeti la *Taifa Leo*

Utafiti huu ulichunganua jinsi lugha ilivyotumiwa na wanahabari katika kuandika habari za kimazingira na uchanganuzi huo unaakisi matumizi ya lugha teule au yenye upekee wa aina fulani. Baadhi ya vipengele vya lugha teule vilivyochunguzwa ni:

i) Udhamiriaji

ii) Matumizi ya nafsi katika masimulizi

iii) Matumizi ya toni

iv) Miundo ya sentensi

v) Matumizi ya takwimu

vi) Uteuzi wa mada.

Vipengele hivi vimejadiliwa kwa kina katika sehemu inayofuata na mifano kutolewa pamoja na ufasiri wa mifano yenyewe.

### 4.2.1 Udhamiriaji

Udhamiriaji hurejelea njia za kiisimu zinazotumiwa kuvumishia au kuelezea nia aliyo nayo mtumiaji wa lugha (Wamitila, 2007). Kimsingi ni kuwa udhamiriaji ni njia ya kipekee ambayo huzingatiwa na mtumiaji lugha kuelezea mwonoulimwengu wake pamoja na itikadi yake. Lugha haimruhusu mzungumzaji au mwandishi kuzungumzia jambo lolote pasipo kuonyesha mwelekeo kuhusiana na jambo hilo (Fowler, 1986). Kwa hivyo, ni vigumu kupata maandishi au mazungumzo ambayo yana sifa za kiutobinafsi yaani yasiyo na upendeleo wala yasiyoegemea upande wowote. Katika maandishi yoyote yale, mtazamo wa mwandishi na mkabala anaochukua anapoandika hudhihirika katika kazi yake. Uchanganuzi wa kina wa matini iliyoandikwa unaweza kubainishia mtafiti upande unaoegemewa kimtazamo na mwandishi.

Tulivyoeleza awali, udhamiriaji hurejelea njia za kiisimu zinazotumiwa kuvumisha au kueleza nia aliyo nayo mtumiaji wa lugha. Udhamiriaji unaweza kuwa wa uwezekano, ulazima, unuiaji au mazoea (Wamitila, 2007). Udhamiriaji wenyewe unaweza kudhihirika kupitia kwa matumizi ya mikakati ya kimatini kama vitenzi vishirikishi, vielezi vya udhamiriaji, vivumishi na virai vilivyotumiwa na waandishi. Waandishi wa matini za kimazingira wa gazeti la *Taifa Leo* wametumia vitenzi vya udhamiriaji ili kuonyesha msimamo wao kuhusu masuala

wanayoyajadili. Matokeo ya utafiti huu yanabainisha aina zifuatazo za udhamiriaji katika habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*:

#### 4.2.1.1 Udhamiriaji Unaobainisha Ulazima

Udhamiriaji unaobanisha ulazima huonyesha kuwa mwandishi wa matini anakusudia kumfahamisha msomaji wake kuwa ni lazima jambo fulani litendeke; vinginevyo matokeo ya kutotenda jambo hilo yatakuwa na athari hasi (Portner, 2009). Mifano ifuatayo inaonyesha udhamiriaji unaoakisi nia ya ulazima iliyotumiwa na waandishi wa habari kuhusu mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* (T.L):

1. Serikali *izuie* wizi wa vyakula vya msaada kwa wahanga wa ukame (ulazima) (T.L 15/9/21 uk 4)
2. Serikali *iipe* kipaumbele miradi inayopunguza athari za mabadiliko ya tabianchi (ulazima) (T.L 13/12/21 uk 6)
3. Wataalam wa afya *wataka* bunge idumishe ushuru wa sigara (ulazima) (T.L 13/4/22 uk 5)
4. WHO *yaonya* Afrika dhidi ya kulegeza kanuni za kuzuia Corona. (ulazima) (T.L 26/3/22 uk 5)
5. Serikali *iwe* mstari wa mbele kukabili uharibifu wa misitu. (ulazima) (T.L 26/3/22 uk 7)
6. Miti ni uhai wa taifa letu, *tusipoitunza* tutaangamia. (ulazima) (T.L 24/3/22 uk 7)
7. Fueli za visukukuu *sharti* zisalie ardhini, wasema wanasayansi (ulazima) (T.L. 5/10/21 uk 14)

Mfano wa kwanza unaonyesha kuwa serikali haina budi kuzuia wizi wa chakula cha msaada katika maeneo yanayokabiliwa na ukame nchini. Kusudi lake ni kuonyesha umuhimu wa kuzuia wizi wa chakula cha msaada kinachotolewa kwa wahanga wa janga la ukame. Katika mfano wa pili, mwandishi anarai serikali kuipa kipaumbele miradi inayopunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Kitenzi 'wataka' katika mfano wa tatu kinaoonyesha kuwa kuna ulazima wa bunge kudumisha ushuru wa juu unaotozwa uuzaji na utengenezaji sigara ili kuzuia matumizi yake. Mfano wa nne unaonyesha kuwa lazima

mataifa duniani yaendelee kuzingatia masharti ya kudhibiti kuenea kwa ugonjwa wa Corona. Hali hii inabainika kupitia kwa matumizi ya kitenzi 'yaonya' ambacho kinaakisi ulazima wa kauli inayotolewa na endapo itakiukwa kutakuwa na madhara hasi. Mfano wa tano unaonyesha nia ya mwandishi kuishurutisha serikali kutilia maanani matukio ya kutunza misitu na kuzuia uharibifu wake. Mfano wa sita unaonyesha nia ya mwandishi kutaka kuwatahadharisha wanajamii wanaoharibu mazingira kwa kukata miti. Ukiukwaji wa onyo inayotolewa utasababisha maafa. Katika mfano wa saba, mwanahabari anasisitiza ulazima wa fueli zinazodhuru afya na mazingira kusalia ardhini. Katika mifano iliyotolewa kuna matumizi ya vitenzi vya udhamiriaji vinavyoonyesha ulazima ambavyo vimeonyeshwa kwa herufi za italiki. Lengo kuu la udhamiriaji wa ulazima katika matini za kimazingira ni kuonyesha udharura uliopo katika kutunza mazingira. Kutotunza mazingira kutasababisha mabadiliko ya tabianchi na maangamizi ya binadamu na viumbe wengine duniani.

Ujumbe huu kwa ujumla unaonyesha kuwa ikiwa msomaji atazipokea taarifa hizi ipasavyo, pana uwezekano mkuu wa asasi husika kuyatunza mazingira.

#### 4.2.1.2 Udhamiriaji unaobainisha Unuiaji

Udhamiriaji unaobanisha nia ya unuiaji hudhirika kupitia kwa vitenzi vinavyoonyesha kusudi la kutenda jambo ambalo litatendwa hivi karibuni. Kimsingi ni kuwa vitendo vyenyewe havijajafanyika lakini vinatarajiwa kufanywa na wahusika muda si mrefu kutoka wakati wa kutolewa kwa tamko (Portner, 2009). Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka kwa matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* inaakisi udhamiriaji unaobainisha unuiaji:

8. Raila *aahidi* kutunza misitu ya Kaya akichaguliwa. (unuiaji)
(T.L 30/12/21 uk. 2)
9. Tobiko *atangaza* mpango wa kusajili chemichemi za maji (unuiaji)
(T.L 5/2/21 uk 4)
10. Serikali *yatenga* Sh 450 m kukabili ukame. (unuiaji)
(T.L 24/12/21 uk 3)
11. Ukame: serikali *kutumia* Sh 350 m kusambaza maji. (unuiaji)
(T.L 19/10/21 uk 4)
12. Serikali *kufany*a mageuzi katika kilimo cha viazi (unuiaji)
(T.L. 17/1/22 uk 4)
13. Serikali *kuwekeza* katika kawi ya miale ya jua kuzalisha nguvu za umeme (unuiaji) (T.L. 15/1/22 uk 7)

Mfano wa 8 unaonyesha kuwa mgombea urais Raila Odinga anatoa ahadi kwa wakazi wa Pwani kuwa atatunza misitu ya Kaya inayothaminiwa na wenyeji endapo atachaguliwa kuwa rais. Mfano wa 9 unaonyesha nia ya waziri wa mazingira bwana Tobiko kutangaza mipango ya serikali kusajili chemchemi za maji ili kutunza vyanzo hivyo vya maji dhidi ya unyakuzi na uharibifu. Kwa upande mwingine, mfano wa 10 unaonyesha kusudi la serikali la kutaka kukabili ukame kwa kutenga shilingi milioni 450 kwa ajili ya shughuli hiyo. Mfano wa 11 unaonyesha nia ya serikali kutumia shilingi milioni 350 kusambaza maji katika maeneo kame. Mfano wa 12 unaoonyesha nia ya serikali kufanya mageuzi katika kilimo cha viazi. Kwa upande mwingine, mfano wa 13 unaoonyesha nia ya serikali kuanzisha miradi ya kawi ya miale ya jua. Matumizi ya kiambishi {ku-} katika vitenzi vilivyobainishwa kwa hati za italiki yanaoonyesha nia ya udhamiriaji unaoakisi unuiaji. Kumaanisha kuwa vitendo havijatendeka lakini vinatarajiwa kutendeka hivi karibuni. Viambishi {a-} na {ya-} katika mifano iliyotolewa vinaoonyesha udhamiriaji wa unuiaji. Katika matini za kimazingira kwenye Gazeti la *Taifa Leo*, wanahabari walitumia udhamiriaji unaoonyesha unuiaji kuripoti matukio yaliyotarajiwa kutendeka ambayo hayakuwa yametendeka tayari.

#### 4.2.1.3 Udhamiriaji unaobainisha Uwezekano

Udhamiriaji unaobainisha uwezekano ni ule unaonyesha kuwa huenda jambo fulani likatendeka au tukio fulani likafanyika au lisitendeke. Aidha, udhamiriaji wa aina hii huonyesha kuwa huenda tukio fulani likatendeka kutokana na athari za tukio lingine lililofanyika mwanzoni au lililotangulia (Portner, 2009). Mifano ifuatayo ya udhamiriaji unaoonyesha uwezekano ilikusanywa kutoka kwenye matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo*:

14. *Hofu* janga la Corona linaathiri unyonyeshaji watoto duniani. (uwezekano) (T.L 3/8/21 uk 3)
15. *Hofu* ya njaa nzige wakitua kijijini. (uwezekano) (T.L 8/2/21 uk 4)
16. *Hofu* Omicron ikienea katika nchi 89 duniani. (uwezekano) (T.L 20/12/21 uk 8)
17. *Hofu* wanafunzi wakikosa kuvaa maski shuleni (uwezekano) (T.L. 15/2/21 uk 3)
18. *Hofu* ya wakulima ugonjwa mpya ukishambulia nyanya.(uwezekano) (T.L. 22/2/21 uk.4)
19. *Hofu* chemchemi za majimoto kaunti ya Kwale zikianza kupoa. (uwezekano) (T.L 22/3/22 uk 10)

Mfano wa 14 unaonyesha kuwa mwandishi alikuwa na nia ya kufahamisha wasomaji kuwa kuna uwezekano mkubwa wa ugonjwa wa Corona kuathiri unyonyeshaji wa watoto duniani. Hali hii inamaanisha kuwa kuna uwezekano mkubwa japo hakuna ushahidi wa kutosha kutetea dai hili. Hali hii inaakisiwa kupitia kwa matumizi ya nomino '*hofu*' kuonyesha kuwa kuna wasiwasi kuwa huenda janga la Corona likaathiri afya ya watoto duniani kutokana na unyonyeshwaji hafifu. Hali sawia inaonekana katika mfano wa 15 ambapo neno hilohilo '*hofu*' linatumika kuonyesha kuwa kuna uwezekano mkubwa wa njaa kuzuka kutokana na uharibifu mkubwa wa mimea unaofanywa na nzige waliovamia kijiji. Mfano wa 16 unaonyesha kuwa mwanahabari anakusudia kuonya umma kuhusu uwezekano wa maafa yanayotokana na kuenea kwa aina mpya ya Corona ijulikanayo kama

‘Omicron’ katika mataifa 89 duniani. Mfano wa 17 unaonyesha uwezekano wa wanafunzi wengi kuambukizwa kwa kukosa kuvaa maski shuleni. Mfano wa 18 unaonyesha uwezekano wa ugonjwa mpya kuathiri ukuzaji wa zao la nyanya. Kwa upande mwingine, mfano wa 19 unaonyesha uwezekano wa chemchemi za maji moto katika Kaunti ya Kwale kupoa kutokana na shughuli za binadamu zinazoathiri mazingira. Udhamiriaji unaobainisha nia ya uwezekano unatumiwa katika matini za kimazingira na wanahabari kwa lengo la kuonya, kutahadharisha na kuwatia umakini wasomaji ili waepukane na madhara au athari fulani zinazotarajiwa. Kwa mfano iwapo mazingira hayatatunzwa vizuri, kuna athari ya maafa yatakayotokea kutokana na uharibifu huo.

#### 4.2.1.4 Udhamiriaji unaobainisha Mazoea ya jambo fulani

Udhamiriaji unaobanisha mazoea huonyesha kuwa jambo au tukio fulani hutendeka kila mara (Portner, 2009). Udhamiriaji huu huonyeshwa kupitia kwa mofu {hu-} inayowakilisha mofimu ya hali ya mazoea katika kitenzi cha Kiswahili. Hali hii huonyesha uradidifu wa vitendo au matukio fulani. Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka katika gazeti la *Taifa Leo* inaonyesha dhamira ya mazoea:

20. Hewa chafu *husababisha* mimba kuharibika na uzani mdogo-Utafiti. (mazoea) (T.L. 15/10/21 uk. 14)
21. Moshi wa kuni, makaa, magunia au mafuta una chembechembe za ‘Particulate Matter’ ($PM_{2.5}$) ambazo *huchangia* maradhi ya mapafu na moyo.(mazoea) (T.L 17/12/21 uk. 4)
22. (Mabadiliko ya tabianchi yanyima watoto virutubisho tosha)...wakati huu mambo yamekuwa mabaya kwelikweli. Hakujanyesha na kutokana na uhaba wa malisho, imebidi ng’ombe kukaa mbali na boma kwa zaidi ya miezi sita. Kukiwa na uhaba wa malisho, mifugo *huhamishwa* hadi Nairobi au hata nchini Tanzania...(Chifu wa kata ya Keekonyonyokie) (mazoea) (T.L 24/8/21 uk. 12)

Kupitia kwa matumizi ya kitenzi ‘husababisha’ katika mfano wa 20 tunapata ujumbe kuwa hili ni tukio linalotendeka kila mara. Kuna athari za kuharibika kwa mimba za wajawazito na watoto kuzaliwa wakiwa na uzani mdogo kutokana na kupumua hewa chafu. Mfano wa 21 unaonyesha kuwa moshi wa kuni, makaa na mafuta husababisha maradhi yanayoathiri mapafu na moyo. Kwa upande mwingine, mfano wa 22 unaoonyesha kuwa uhaba wa malisho husababisha jamii fugaji kuhamisha mifugo wao maeneo na hata nchi za mbali. Udhamiriaji wa mazoea katika matini za kimazingira unalenga kuwatanabahisha wasomaji kuhusu matukio yanayotendeka kila mara ambayo huenda wakayapuuza lakini yana madhara makubwa kwa afya na mazingira. Kwa kuchukua hatua mwafaka huenda umma ukaepukana na madhara au athari hizo. Udhamiriaji huu pia unatumika kuelimisha na kuhimiza jamii kuhusu vitendo chanya ambavyo huenda vikainua na kudumisha viwango bora vya afya na mazingira.

### 4.2.2 Matumizi ya Nafsi katika Masimulizi

Usimulizi unahusu nyenzo, mbinu au njia iliyotumiwa na mwandishi wa matini kusimulia au kueleza matukio au habari (Mieke, 1985). Utafiti huu ulibainisha mpaka uliopo baina ya mwandishi wa matini ya kimazingira na sauti au nafsi aliyoitwika jukumu la kusimulia matukio au taarifa zilizomo. Msimulizi wa matini za kimazingira anadhihirika kupitia kwa nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu. Nafsi hizi zimefafanuliwa na mifano kutolewa katika sehemu inayofuata:

#### 4.2.2.1 Usimulizi wa Nafsi ya Kwanza

Kitambulishi cha usimulizi wa nafsi ya kwanza ni kuwepo kwa kiambishi **–ni-/-tu-** cha nafsi ya kwanza katika masimulizi yanayotolewa. Usimulizi wa nafsi ya kwanza hujenga

ukaribu mkubwa baina ya mwanahabari msimulizi au mhusika anayesimulia habari za kimazingira na msomaji (Mieke, 1985). Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka katika gazeti la *Taifa Leo* inaonyesha usimulizi wa nafsi ya kwanza:

23. (Mabadiliko ya tabianchi yanyima watoto virutubisho tosha)...kutokana na mifugo wangu *ni*ngepata angalau chupa nne za maziwa kila siku kwa minajili ya kujumuisha kwenye lishe, na hata kuuza angalau ili *ni*weze kununua mboga na vyakula vingine...(Esther Roigo mkazi wa kata ya Keekonyonyokie) (T.L 24/8/21 uk. 12)
24. (Corona yasukuma maelfu kutumia kawi hatari)...Mkebe mmoja wa makaa unauzwa sh 100. Makaa hayawezi kuchemsha sufuria ndogo ya nyoyo (githeri). *Si*wezi kununua makaa ilhali watoto hawana chakula...(Martha Ouma, mkazi wa Korogocho, Nairobi) (T.L. 7/12/21 uk 14)
25. (Je, bora mitishamba?)...*ni*litafuna tembe tano za mbegu za mturituri miaka mitano iliyopita na *si*jawahi kupata ujauzito wala kuvuja damu tena. Mbegu hizo zime*ni*saidia sana maanake *si*umwi tena na tumbo, kichwa wala maradhi mengine yaliyoletwa na dawa za kupanga uzazi. Hazina athari yoyote kwangu.... (Josephine Karisa, mkazi Kilifi) (T.L 22/1/22 uk. 14)
26. *Tu*pande miti kukabili uchafuzi wa anga yetu. (T.L. 5/1/22 uk. 7)

Katika mfano wa 23, nafsi inayosimuliwa ni ya Esther Roigo mkazi wa kata ya Keekonyonyokie; eneo linaloshuhudia mabadiliko ya tabianchi. Mwanahabari anampatia mwathiriwa wa mabadiliko ya tabianchi nafasi ya kusimulia jinsi alivyoathiriwa na mabadiliko hayo. Matumizi ya kiambishi –ni- kunamfanya msomaji ajitie katika nafasi/hali halisi ya msimulizi. Kwa kufanya hivi, umbali kati ya msimulizi na msomaji unapungua. Kutokana na haya, ni rahisi mwanahabari kubadilisha mwelekeo, hisia, na tabia za msomaji kuhusu mazingira kupitia kile anawasilisha katika gazeti la *Taifa Leo* (Maina, 2011 (*ametajwa*). Katika mfano wa 24 nafsi inayosimuliwa ni ya Martha Ouma, mkazi wa Korogocho jijini Nairobi. Mwanahabari anampa Martha Ouma jukumu la kusimulia ugumu wa maisha kutokana na Corona unaomsukuma kutumia kawi hatari kwa mazingira. Nafsi inayosimulia katika mfano wa 25 ni ile ya Josephine Karisa, mkazi Kilifi. Mwanahabari anamtwika Bi Karisa jukumu la kusimulia umuhimu wa mitishamba na faida

za kutunza miti ya kiasili ambayo hutoa dawa hizo. Kwa upande mwingine, nafsi inayosimulia katika mfano wa 26 ni ile ya mhariri anayewahimiza wasomaji kupanda miti ili kukabiliana na uchafuzi wa anga. Mifano hii inaonyesha wazi kuwa wanahabari wanawapa waathiriwa wa matukio husika jukumu la kusimulia wenyewe matukio au mikasa iliyowakumba.

Sauti inayosikika katika taarifa inayowasilishwa kwa nafsi ya kwanza ni ile ya mhusika aliyeshuhudia au kuathiriwa na matukio yanayosimuliwa na mwanahabari. Kwa kufanya hivyo mwanahabari anayafanya matukio yanayosimuliwa yawe ya kusadikiwa na kuaminika kwa urahisi. Matukio hayo yanafanywa kuwa halisi kabisa kwa msomaji. Vilevile, mwanahabari anafanikiwa kukuza athari anayolenga kuibua kwa msomaji. Katika mfano wa 23 msomaji anawasikitikia waathiriwa wa mabadiliko ya tabianchi wanaokosa lishe bora na hasa watoto wanakosa virutubisho bora vya afya. Kwa upande mwingine, msomaji anawasikitikia wakaazi wa vitongoji duni wanaolazimika kutumia kawi hatari kwa afya na mazingira yao kutokana na ugumu wa maisha uliosababishwa na janga la Corona. Kiambishi **–ni-** cha nafsi ya kwanza katika umoja kinarejelea mwathiriwa wa matukio yanayosimuliwa katika taarifa za habari. Mwanahabari anapoipa nafsi ya kwanza kusimulia matukio yaliyotendeka, msomaji anaathiriwa kihisia kutokana na usimulizi huo. Kwa njia hii mwanahabari anafanikiwa kumshawishi, kumwelekeza kifikra na kumbadilisha kimawazo msomaji wake kuhusu matukio ya kimazingira yanayosimuliwa (Maina, 2011 (*ametajwa*).

#### 4.2.2.2 Usimulizi wa Nafsi ya Pili

Usimulizi wa nafsi ya pili hutambulika kupitia kwa matumizi ya kiambishi **–u-** cha nafsi. Kwa kutumia nafsi ya pili, msimulizi hurejelea ulimwengu wa msomaji au mlengwa wa taarifa. Hali hii inamaanisha kuwa mwandishi huvunja mpaka uliopo kati ya ulimwengu wa uandishi na ulimwengu halisi au ulimwengu wa nje ya matini (Mieke, 1985). Kwenye matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* wanahabari walitumia nafsi ya pili kumshirikisha msomaji katika matukio yaliyosimuliwa. Kwa mfano:

27. *U*nahatarisha afya yako ya uzazi *u*napopumua hewa chafu... (T.L. 2/11/21 uk. 8)
28. *Ji*andaeni kwa kiangazi na njaa, shirika laonya. (Shirika la utabiri wa hali ya anga) (T.L. 5/8/21 uk 5)
29. 'Smoker' ita*ku*saidia kukaribia mzinga na kuvuna asali murwa. (T.L. 23/3/22 uk16)
30. Apu ya simu ya 'Kalro Banana Varieties' ita*ku*saidia kupata maarifa na kuongeza maarifa yako. (T.L. 23/3/22 uk. 16)

Katika mfano wa 27, matumizi ya kiambishi cha nafsi **–u-** yanarejelea msomaji wa taarifa ya habari. Tukio linalofafanuliwa ni lile la uchafuzi wa hewa jijini Nairobi kiasi cha kuhatarisha afya ya wakazi wa jiji hilo. Mwanahabari anamshirikisha msomaji wa habari katika muktadha wa mazingira anayoyasimulia. Taswira inayojitokeza ni ile inayonuiwa kuathiri hisia za msomaji. Mwanahabari anamtaka msomaji kuhisi kuwa anapopumua hewa chafu anaathiri afya yake ya uzazi. Mwanahabari analenga msomaji wake ahisi kughasiwa endapo atapumua hewa chafu na kwa njia hiyo kuchochea hatua za dharura zichukuliwe na vyombo vya dola vinavyohusika kuwaondolea wakazi wa jiji kero hilo. Katika mfano wa 28, mwanahabari aliyetunga makala anamtahadharisha msomaji wake kuwa kuna kiangazi na njaa ambavyo vitatokea hivi karibuni kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na shirika la utabiri wa hali ya anga. Katika mfano huo wa 28, kiambishi **–ji-**

kinaonyesha nafsi jirejelevu inayosimamia nafsi ya pili (nyinyi) katika wingi. Katika muktadha huo anayerejelewa ni msomaji wa kifungu cha taarifa ya habari. Mwanahabari anakusudia kumshirikisha msomaji katika matukio yanayosimuliwa kuhusu kuzuka kwa kiangazi na njaa. Katika mifano ya 29 na 30 matumizi ya kiambishi **–ku-** katika kitenzi 'ita**ku**saidia' yanaonyesha nafsi ya pili (wewe) inayorejelea msomaji. Matumizi ya nafsi ya pili kwenye matini za habari ya mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* yanakusudiwa kumshirikisha msomaji katika matukio yanayosimuliwa ili kumwathiri kwa njia inayokusudiwa na mwandishi wa makala.

#### 4.2.2.3 Usimulizi wa Nafsi ya Tatu

Usimulizi wa nafsi ya tatu hutambulika kupitia kwa matumizi ya kiambishi **–a-** cha nafsi ya tatu umoja. Usimulizi huu unawezesha waandishi wa matini husika kuwa na mtazamo mpana wa matukio yanayopatikana katika ulimwengu halisi au wa kiubunifu wanaoutungia (Mieke, 1985). Kiambishi **–wa-** cha nafsi ya tatu katika wingi kikitumiwa katika matini kinarejelea nafsi ya kijamii. Nafsi ya kijamii inaweza pia kutumiwa na wanahabari kama njia ya kumshirikisha msomaji kwenye masimulizi na kumfanya ashirikiane na mtunzi wa matini husika. Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* inaonyesha matumizi ya nafsi ya tatu katika usimulizi:

31. *A*jifungulia mlango wa ajira kwa kuotesha mbegu na kuuza miche.
    (T.L. 5/1/22 uk. 13)
32. Wakulima *wa*elimishwa jinsi ya kukabili mabadiliko ya hali ya anga.
    (T.L. 12/1/22 uk. 14)
33. Mkazi wa eneo la Hegen, Ujerumani *a*tembea kando ya gari lililozama ndani ya vifusi kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha katika magharibi ya nchi hiyo. (T.L. 16/7/21 uk. 5)

Katika mfano wa 31, kiambishi **–a-** kinarejelea nafsi ya mjasiria mali aliyeanzisha biashara ya kuotesha mbegu na kuuza miche. Katika mfano huo, sauti inayosikika ni ile ya mwanahabari anayesimulia matukio kuhusu mhusika aliyeanzisha biashara ya kukuza na kuuza miche. Mwanahabari anasimulia kuhusu matukio aliyoyashuhudia na kuyaona lakini yanayomzingira mtu mwingine. Katika mfano wa 32, matumizi ya kiambishi cha nafsi ya tatu katika wingi **–wa-** yanarejelea wakulima wanaoathiriwa na mabadiliko ya hali ya anga. Kimsingi ni kuwa, mfano wa 32 unabainisha matumizi ya kiambishi **–wa-** cha nafsi ya tatu katika wingi kinachorejelea nafsi ya jamii. Katika mfano huo wa 32, nafsi ya jamii inayorejelewa ni ile ya wakulima ambao shughuli yao ya kilimo imeathiriwa na mabadiliko ya hali ya anga. Kwa kutumia kiambishi cha nafsi ya tatu **–a-** mwanahabari katika mfano wa 33, anakuwa huru kusimulia kwa mitazamo mipana matukio yanayotendeka katika ulimwengu halisi anaotangamana nao. Katika muktadha wa mfano wa 33, mwanahabari anasimulia kuhusu athari za mafuriko baada ya mvua kubwa kunyesha.

### 4.2.3 Matumizi ya Toni

Lugha andishi inayotumika katika matini za kimandishi huakisi toni fulani. Kimsingi, toni hurejelea suala linalozungumziwa katika matini husika ambalo huibua hisia fulani kupitia kwa maneno yaliyoteuliwa na mtunzi wa matini (Wamitila, 2007). Hili linamaanisha kuwa, mtunzi wa matini huteua maneno ili kuibua maana maalum kutegemea muktadha wa matumizi ya maneno hayo. Maana inayowasilishwa katika matini huibua hisia fulani ambazo zinaweza kuwa kwa mfano dhihaka, kicheko, kashfa au huzuni. Uteuzi wa maneno au visawe vyake haudhibitiwi tu na maana ya maneno hayo pekee bali pia na athari inayoibuliwa na maneno yenyewe. Hali hii ina umuhimu katika ujenzi wa toni ya matini ya kimazingira ili kuathiri hadhira ya wasomaji kwa njia inayokusudiwa na mwanahabari.

Kwa mfano mwandishi wa makala atatumia maneno ya kashfa anapokusudia kukashifu uharibifu wa mazingira. Kwa upande mwingine, atatumia maneno ya kusifu, kupongeza na kuhimizi akitaka kukuza tabia ya kutunza na kujali mazingira. Kimsingi, kwenye matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* utafiti huu ulibainisha matumizi ya toni ya kichomi, huzuni, kukashifu, kutamauka au kukata tamaa, kusononeka, kusikitisha, kutumaini, na kupogeza. Matumizi ya aina mbalimabali za toni katika gazeti la *Taifa Leo* yamejadiliwa kwa kina katika sehemu inayofuata:

#### 4.2.3.1 Toni ya Huzuni

Matini za kifasihi ( na zisizo za kifasihi ) (*msisitizo ni wangu* ) hukusudiwa kuibua hisia fulani kwa msomaji. Suala la hisia katika matini hizo hufungamana kwa kiasi kikubwa na dhana za toni (Wamitila, 2007). Toni ya huzuni inakusudiwa kuibua hisia za huzuni kwa wasomaji. Toni ya huzuni inaweza kudhihirika katika matini inayochunguzwa kupitia kwa uteuzi wa maneno ambayo mwandishi wa matini ya kimazingira anayatumia kutoa ujumbe anaokusudia. Athari inayotokana na usomaji wa maneno yaliyotumika ni ile ya kuhuzunisha inayoibuliwa na hisia za huzuni. Mifano ifuatayo kutoka katika gazeti la *Taifa Leo* inaakisi toni ya huzuni:

34. *Mafuriko* **yaua** 70 wengine 45 watoweka (Ankara, Uturuki) (T.L 17/8/21 uk 7)
35. Watoto 350,000 hatarini **kufa** *njaa* (T.L. 13/3/22 uk. 6)
36. Wanafunzi 26 **wateketea** madarasa yaliposhika *moto*. (T.L. 10/11/21 uk. 8)
37. *Mlipuko* wa oksijeni **waua** 64, **wajeruhi** 100 katika hospitali (Iraq) (T.L 14/7/21 uk 6)
38. *Radi* **yaua** 60 wakiwemo 11 waliokuwa wakipiga 'selfie' (New Delhi) (T.L. 13/7/21 uk 5)

Mfano wa 34 unaakisi hisia za huzuni zinazotokana na matumizi ya maneno '*mafuriko yaua 70*' na '*wengine 45 watoweka*'. Kauli hizi mbili zimeteuliwa kwa uangalifu ili kutoa

taswira ya uoni katika akili ya msomaji itakayomhuzunisha msomaji. Msomaji anapata picha ya mauti yaliyosababishwa na uharibifu wa mafuriko. Kitenzi '*watoweka*' kinaibua hisia kwamba hawajulikani walipo; kuna uwezekano mkubwa kwamba wamekabiliwa na mauti. Neno hilo ni la kitasfida kwa vile linapunguza makali ya kutaja mauti yasiyobainishwa kwa uhakika. Kwa upande mwingine, kauli '*hatarini kufa njaa*' linaibua taswira ya watoto wanaokabiliwa na madhara ya utapia mlo kwa kukosa chakula. Mwanahabari kwa kutumia takwimu '*350,000*' katika mfano wa 35 anakusudia kusisitiza wingi wa idadi ya watoto walio katika hali hatari ya kufa njaa. Kwa kutumia neno '*watoto*' kama kiima cha sentensi, mwanahabari anasawiri hali ya kutoweza kujiauni kutoka kwa hatari inayowakabili kwa sababu wao hutegemea wazazi kupata chakula. Katika mfano wa 36 matumizi ya kitenzi '*wateketea*' ni ya kimaksudi ili kuonyesha hali ya kuchomeka kwa kasi. Taswira inayoibuliwa ni ile ya wanafunzi hao kukabiliwa na mauti ya kuchomeka kwa kasi darasa lao liliposhika moto. Katika mfano wa 37 matumizi ya vitenzi '*waua*' na '*wajeruhi*' yanazua huzuni kwa msomaji. Mwanahabari ameteua maneno yaliyotumiwa katika kichwa cha habari ili kuibua hisia za huzuni. Msomaji anapatwa na huzuni anaposoma kuhusu mlipuko wa tanki la oksijeni unaotokea hospitalini na kuua na kujeruhi wagonjwa na wauguzi. Mfano wa 38 unaibua hisia za huzuni na majonzi kutokana na tukio la kitanzia linalowapata watu sitini wanaouawa na radi. Hili ni janga la kimazingira linalowaangamiza raia wanaoendelea na shughuli zao.

#### 4.2.3.2 Toni ya Kukashifu

Toni ya kukashifu ni ile inayohusu uteuzi wa maneno yanayokusudia kufichua jambo lisililojulikana lenye uovu au la kuzua aibu na kulifanya lijulikane kwa kuibua hisia za kushutumu (Wamitila, 2007). Toni ya kukashifu ilidhihirika kupitia kwa maneno ya

kushutumu au kukashifu yaliyoteuliwa na waandishi wa matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Maneno hayo yalinuiwa kuibua hisia za chukizo na kukereka dhidi ya vitendo vya baadhi ya wanajamii kuharibu au kuchafua mazingira. Mifano ifuatayo iliyonukuliwa kutoka katika gazeti la *Taifa Leo* inadhihirisha toni ya kukashifu:

39. Uhifadhi wa mazingira usiwe wa siku moja (T.L. 7/6/21 uk. 8)
40. Tatizo la maji Turkana ni ***aibu*** (T.L. 4/11/21 uk. 10)
41. Siasa tu, Corona ikifyeka nchi (T.L. 6/8/21 uk 1)
42. Mapuuza ya wakazi tishio katika vita vya kukabiliana na Corona (T.L. 11/8/21 uk 4)
43. Wakazi wageukia maji machafu katika vidimbwi baada ya mradi wa sh 11 milioni kukwana Galole. (T.L. 18/8/21 uk 4)
44. Raia wafa njaa viongozi wakipiga domo (T.L. 24/8/21 uk 1)

Mfano wa 39 uliokusanywa kutoka kwa tahariri ya gazeti la *Taifa Leo* unadhihirisha toni ya kukashifu. Hili linabainika wazi katika kichwa cha tahariri '*Uhifadhi wa mazingira usiwe tukio la siku moja*'. Matumizi ya kauli '*tukio la siku moja*' yanaakisi kinaya; kwamba serikali huadhimisha siku ya mazingira duniani mara moja tu kwa kuhamasisha raia na kisha kukomea hapo. Mhariri anakashifu tukio hili la kusingizia kutunza mazingira kwa siku moja tu. Mhariri anakashifu uzembe wa vyombo hivyo vya dola vyenye utepetevu katika utunzaji mazingira na utekelezaji wa majukumu yanayohusu uhifadhi wa mazingira. Anwani ya tahariri inasheheni kinaya kwa sababu wizara hukurupuka kuhusu shughuli za kimazingira siku ya mazingira duniani. Mhariri anakejeli serikali kwa kukosa kuchukua hatua za kuhifadhi na kutunza mazingira kila mara. Mfano wa 40 unakashifu kero ya ukosefu wa maji katika kaunti ya Turkana ilhali kuna ziwa Turkana pamoja na uvumbuzi wa bwawa la maji chini ya ardhi. Matumizi ya neno '*aibu*' yanaonyesha kuwa ukosefu wa maji ni tatizo lisilopaswa kuwepo. Mhariri anakejeli Serikali ya Kaunti pamoja na Wizara ya Maji kwa uzembe wa kutolishughulikia tatizo hilo ambalo suluhu yake ipo karibu.

Mfano wa 41 unabainisha toni ya kukashifu kupitia kwa uteuzi wa maneno yaliyotumiwa pamoja na muundo wa sentensi. Sentensi imegawanya katika vipande viwili kupitia kwa matumizi ya koma. Sehemu ya kwanza inadhihirisha shughuli inayotiliwa maanani na viongozi wa ngazi za juu. Shughuli yenyewe ni siasa ambayo imewafanya wapuuze kuenea kwa kasi kwa ugonjwa wa Corona ambao unawaangamiza wananchi. Kauli '*siasa tu*' inasheheni kejeli na kuakisi kinaya; kuonyesha kuwa viongozi wanapiga siasa bila kuwajibikia maafa ya raia kutokana na janga la Corona. Katika kauli '*Corona ikifyeka nchi*' kuna matumizi ya tashihisi yanayolenga kujenga taswira ya mtu anayefyeka nyasi kuonyesha jinsi gonjwa hilo linavyoangamiza wengi. Kwa kutumia taswira hii, mwanahabari anafanikiwa kufichua kutowajibika kwa viongozi wanaothamini nyadhifa zao bila kuwajali raia wanaoangamizwa na janga la Corona bila msaada wowote. Mfano wa 42 unadhihirisha kuwa mwandishi anakashifu tabia ya wakazi ya kuwa na mapuuza inayochangia kuongeza kwa maambukizi ya Corona. Mfano wa 43 unaonyesha toni ya kukashifu kutokana na matumizi ya kauli '*wakazi wageukia maji machafu katika vidimbwi*' inayoonyesha utepetevu wa serikali kutokamilisha mradi wa kusambaza maji uliogharimu pesa nyingi. Katika mfano wa 44 mwanahabari anatumia toni ya kukashifu kushutumu vitendo vya viongozi serikalini kujihusisha katika siasa wananchi wakifa njaa.

#### 4.2.3.3 Toni ya Kutamauka

Toni ya kutamauka hudhihirika wakati ambapo waandishi wa matini hutumia maneno yanayolenga kuibua hisia za kukatisha tamaa (Wamitila, 2007). Toni ya kutamauka ilibanika katika matini za kimazingira zilizokusanywa na ambazo zilionyesha kuwepo kwa fadhaa, pekecho, wasiwasi na kukithiri kwa viwango hasi ambavyo havikutoa matumaini yoyote. Waandishi walitumia toni hii huibua hisia za ghadhabu ili wanajamii wabadili

mielekeo na vitendo hasi dhidi ya mazingira. Mifano ifuatayo iliyodondolewa kutoka gazeti la *Taifa Leo* inaonyeha toni ya kutamauka:

45. Mochari *zajaa wafu* wa Covid (...watengenezaji majeneza wasema *wameshindwa* kutosheleza mahitaji ya wateja...) (T.L 1/9/21 uk 1)
46. Machozi yatiririka wakazi wakihadithia *ugumu wa kutamausha* (kiangazi Marsabit) (T.L. 24/1/22 uk 4)
47. Hawakustahili *kufa namna ile* katika ajali ya basi mtoni Kitui (T.L. 6/12/21 uk 6)
48. Putin *azua hofu* duniani akitisha *kulipua nyuklia* (T.L 1/3/22 uk 1)
49. Shule *zalemewa* kulinda watoto dhidi ya Corona. (T.L 15/10/21 uk. 3)
50. Serikali *imeshindwa* kutuliza makali ya njaa (T.L. 18/11/21 uk. 7)

Mfano wa 45 unaonyesha hali ya kutamauka kwa wanajamii walioshuhudia maafa mengi kutokana na ugonjwa wa Corona. Seremala wanaotengeneza majeneza walitamaushwa na idadi kubwa ya wafu wakashindwa kutosheleza uhitaji wa majeneza yaliyohitajika. Mfano wa 46 unadhihirisha hisia za kutamausha kutokana na masaibu ya njaa, ukame na kiangazi yaliyoshuhudiwa maeneo ya Marsabit. Mfano wa 47 unabainisha matumizi ya kauli ya kidhanaawali '*hawakustahili kufa namna ile*' ambayo inarejelea vifo vya kusikitisha cha wakazi wa Kitui waliosombwa na mafuriko basi lao lilipojaribu kuvuka mto. Katika kauli hiyo, mwanahabari anachukulia kuwa wasomaji wanajua jinsi ajali hiyo ilivyotendeka kwa vile vyombo vya habari viliangazia tukio hilo lililohuzunisha taifa zima. Mfano wa 48 unarejelea vita vya Urusi na Ukraine ambavyo vilihuzunisha ulimwengu mzima kutokana na raia wa Ukraine wasio na hatia kuvamiwa na majeshi ya Urusi yaliyozua uharibifu mkubwa wa kimazingira likiwemo tishio la kutumia silaha la kinuklia.

Matumizi ya maneno '*zalemewa kulinda watoto*' katika mfano wa 49 yanaonyesha hali ya shule kutamaushwa na maambukizi ya watoto ya ugonjwa wa Corona. Serikali kupitia kwa vyombo husika vya kupambana na janga la Corona vikishirikiana na shule vilishindwa kudhibiti na kuzuia maambukizi ya Corona miongoni mwa watoto shuleni. Mfano wa 50

unaonyesha hali ya serikali kutamaushwa na tatizo la njaa na uhaba wa chakula katika maeneo mengi nchini yakiwemo Kaunti za Baringo, Marsabit, Mandera, Wajir, Garissa na Tana River. Matumizi ya kitenzi '*imeshindwa*' katika matini husika yanaonyesha hali ya kukata tamaa. Serikali imeshindwa kukabiliana na janga la ukame lililosababisha njaa na maafa ya wanyama na binadamu. Serikali imekosa uwezo wa kulikabili janga hilo. Hali ya kutamaushwa na tatizo la kukosa chakula ambaco kingetolewa kwa wahanga wa njaa ni wito wa dharura unaotolewa na mwanahabari kwa mashirika yasiyo ya kiserikali na wananchi binafsi ili kuwaondolea waathiriwa kero lenyewe. Kimsingi ni kuwa wanahabari walipotumia toni ya kutamausha katika habari walizotoa walilenga kuangazia kero za wananchi na wakati huohuo kutoa wito wa dharura kwa serikali ishughulikie majanga ya kimazingira yaliyotishia kuwaangamiza raia.

#### 4.2.3.4 Toni ya Kusikitisha

Toni ya masikitiko hubainika katika matini za kifasihi kupitia kwa matumizi ya maneno yanayoonyesha masikitiko kutokana na hali zinazosimuliwa na waandishi (Wamitila, 2007). Toni ya kusikitisha ilibainika katika matini za kimazingira zilizochunguzwa katika utafiti huu. Kwa mfano, wanahabari waliporipoti taarifa zilizohusu majanga ya kiasili kama vile: uvamizi wa nzige, njaa, mafuriko na mikurupuko ya maradhi, walitumia maneno ya kuonyesha kusikitika kutokana na utepetevu wa serikali katika kuyashughulikia majanga haya. Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka gazeti la *Taifa Leo* inaonyesha matumizi ya toni ya kusikitisha katika kuripoti matukio husika:

51. Njaa *yaua* watoto 11 wiki moja-NDMA (T.L. 26/3/22 uk. 3)
52. Eneo la kutupia taka lililo *hatari* kwa wakazi wa Kisii (T.L. 28/3/22 uk. 10)
53. 28 milioni katika *hatari* ya kufa njaa (T.L. 24/3/22 uk 5)
54. Daraja la 100m *labomoka* siku tano baada ya kuzinduliwa (T.L. 25/3/22 uk 5)

55. Idadi ya *waliouawa* na mafuriko yapanda (T.L. 9/3/22 uk. 8)

Mfano wa 51 unaakisi toni ya kusikitika kutokana na matumizi ya neno '*yaua*' ambalo linaibua hisia za masikitiko katika matini. Neno hili linaonyesha hisia zinazowasilishwa na mwanahabari kutokana na janga la njaa linalowaua watoto ndani ya wiki moja. Hali hii ilitokana na utepetevu wa serikali kulishughulikia janga hilo. Mwanahabari anasisitiza kuwa ukame na kiangazi ni majanga ya kimazingira ambayo yanasababisha mkururo wa madhara yakiwemo njaa, magonjwa na maafa. Matumizi ya neno '*hatari*' katika mifano ya 52 na 53 yanaashiria lengo la wanahabari kutilia mkazo wito unaotolewa kwa serikali kuhusu hali zinazowakabili wananchi. Mwandishi wa makala katika mfano wa 52 anatoa wito kwa serikali kushughulikia hali ya kusikitisha ya eneo la kutupia taka ambalo linahatarisha maisha ya wakazi wa Kisii. Kwa upande mwingine, mwanahabari katika mfano wa 53 anatoa wito kwa seikali kulikabili janga la njaa linalotishia maisha ya watu takribani milioni ishirini na nane. Mfano wa 54 unaonyesha masikitiko aliyonayo mwanahabari kutokana na kubomoka kwa daraja lililogharimu mamilioni ya pesa kulijenga ambalo linaporomoka siku tano baada ya kuzinduliwa. Mwanahabari anasikitikia utepetevu wa mhandisi aliyejenga daraja hilo. Kauli ya kusikitisha '*yaendelea kupanda*' inaashiria ongezeko katika idadi ya vifo vya wahanga wa mafuriko. Idadi hiyo inaendelea kuongezeka kila siku.

#### 4.2.3.5 Toni ya Matumaini

Toni ya matumaini ni ile iliyo kinyume cha toni ya kutamausha. Toni hii huonyesha faraja, matumaini au imani kuwa hali hasi itabadilika na kuwa chanya. Maneno yanayotumiwa katika matini za kifasihi huonyesha matumaini au kuimarika kwa hali ambazo awali zilionekana kuwa hasi kabisa (Wamitila, 2007). Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka katika gazeti la *Taifa Leo* inaoonyesha matini za kimazingira zinazoakisi toni ya matumaini:

56. Mikakati ya haraka *ilinusuru* nchi kutokana na janga la Covid-Rais (T.L. 1/12/21 uk. 6)
57. Kenya *yapewa* Sh 3B kupambana na nzige. (Shirika la World Bank). (T.L. 16/2/21 uk. 2)
58. WHO yasema idadi ya visa vya Corona yaendelea *kushuka*. (T.L 18/2/21 uk. 5)
59. *Afueni* kwa familia mahindi *kushuka bei* (Uasin Gishu) (T.L 22/2/21 uk. 4)
60. Mombasa Cement *inavyorembesha* jiji. (T.L 2/3/22 uk. 10)
61. Familia zaidi ya 170,000 Kitui *zapokea* chakula cha msaada (T.L.7/3/22 uk. 5)

Toni ya matumaini ni toni chanya ambayo inaashiria hali ya afueni baada ya janga au msiba fulani. Katika mfano wa 56 kuna hali ya afueni baada ya janga la Corona lililokuwa kero kitaifa kukabiliwa na mikakati ya haraka iliyowekwa na serikali. Matumaini yanaonekana kupitia kwa matumizi ya neno '*ilinusuru*' ambalo linaashiria kuwa dalili zote zilionyesha kuwa kungekuwa na vifo vingi kutokana na ugonjwa wa Corona. Katika mfano wa 57 matumaini yanaonekana baada ya taifa la Kenya kupewa msaada wa kiasi cha shilingi bilioni tatu na Shirika la World Bank ili kupambana na janga la nzige. Kauli '*yaendelea kushuka*' iliyotumika katika mfano wa 58 inaashiria matumaini kutokana na ripoti iliyotolewa na Shirika la Afya Duniani kuwa idadi ya visa vya maabukizi ya Corona vinaendelea kushuka. Matumaini yanaonekana baada ya kuwa na idadi ya chini ya

maambukizi iliyoendelea kupaa kimataifa kwa muda mrefu. Toni ya matumaini inabainika katika mfano wa 59 kupitia kwa matumizi ya maneno '*afueni*' na '*kushuka bei*' ambayo yanaonyesha kuwa wakazi wa Uasin Gishu walikuwa wamesikitishwa na kupanda kwa bei ya mahindi kutokana na ukame. Kwa upande mwingine, mifano ya 60 na 61 inaakisi toni ya matumaini kutokana na maneno yaliyoainishwa kwa hati za italiki. Toni ya matumaini inatumiwa na wanahabari kuonyesha kuwa, licha ya kuwa na uharibifu mkubwa wa mazingira unaotokana na vitendo vya wanadamu pamoja na majanga; lakini pia kuna afueni na matumaini ya kunusuru uharibifu huo.

#### 4.2.3.6 Toni ya Kupongeza

Toni ya kupongeza ni ile inayotumiwa kuhimiza matendo mema yanayofanywa na watu mbalimbali katika jamii. Toni hii inatumiwa kusifia vitendo vya hisani na utu vinavyofanywa na watu binafsi, mashirika au taasisi mbalimbali (Wamitila, 2007). Katika matini za kimazingira zilizokusanywa na utafiti huu, wanahabari walitumia maneno yaliyokusudiwa kuibua toni ya kupongeza ili kusifu vitendo bora vya kutunza au kujali mazingira vilivyofanywa na watu au mashirika katika jamii. Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka katika gazeti la *Taifa Leo* inaonyesha toni ya kupongeza:

62. Mradi wa maji *kufaa* kaunti 6 katika maeneo kame nchini. (T.L. 28/3/2022 uk. 5)
63. Teknolojia mpya ya 'Lab in Box' *inasaidia* wakulima kupima viwango vya rutuba katika mashamba yao. (T.L. 2/3/22 uk. 16)
64. Wafugaji *wapata msaada* kuepuka hasara ya ukame (T.L. 13/3/22 uk. 14)
65. Serikali yaanza *kusambaza aina mpya ya korosho inayofaa* maeneo kame. (T.L. 13/3/22 uk. 15)
66. Kaunti ya Trans Nzoia *yakabili* uchafuzi wa mazingira mjini (T.L. 24/3/22 uk. 4)

Katika mfano wa 62 toni ya kupongeza inaonekana bayana kupitia kwa matumizi ya neno 'kufaa' ambalo linaashiria kuwa kuna hali ya heri baada ya kuanzishwa kwa mradi wa

kusambaza maji katika maeneo kame ya kaunti sita. Katika mfano wa 63 mwanahabari anawapongeza wavumbuzi wa teknolojia mpya inayowasaidia wakulima kujipimia wenyewe viwango vya rutuba katika mashamba yao. Katika mfano wa 64 kuna matumaini kwa wafugaji kutoka katika maeneo kame waliopata msaada kutoka kwa serikali kukabiliana na hasara zinazotokana na makali ya ukame. Katika mfano wa 65 mwanahabari anatumia maneno yanayotoa matumaini kwa wakulima wa korosho ambao wangepata aina mpya ya zao hilo inayostahimili maeneo kame. Kwa upande mwingine, matumizi ya kauli '*kukabili uchafuzi wa mazingira*' katika mfano wa 66 yanatoa matumaini kwa wakazi wa Trans Nzoia waliokumbwa na tatizo la kimazingira. Kimsingi ni kuwa, katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo*, wanahabari walitumia toni ya kupongeza kusifu juhudi zilizofanywa na watu binafsi, viongozi na mashirika katika kukabiliana na majanga au kuwasaidia waathiriwa wa majanga hayo.

### 4.2.4 Miundo ya Sentensi

Nyenzo kuu inayotumiwa na wanahabari kuumba matini zao ni lugha. Matumizi ya lugha huonekana kupitia kwa namna wanavyounda sentensi zinazojenga matini husika. Kuna miundo mikuu ya sentensi ambayo ni muundo sahili, muundo changamani na muundo ambatani (Habwe na Karanja, 2004). Katika sehemu inayofuata tumejadili aina hizi za miundo ya sentensi na kutoa mifano na maelezo jinsi ilivyobainika katika data tuliyokusanya kutoka gazeti la *Taifa Leo*.

#### 4.2.4.1 Miundo ya Sentensi Sahili

Sentensi sahili ni ile ambayo ina kitenzi kimoja, ambacho maana yake ni kamilifu. Sentensi sahili huwa na kitenzi kikuu kimoja. Hata hivyo, si lazima sentensi sahili iwe rahisi

kueleweka kimaana wala iwe fupi katika muundo wake (Habwe na Karanja, 2004). Sentensi sahili hueleza wazo moja tu ambalo hubebwa na kishazi kikuu kimoja. Mifano ifuatayo ya sentensi sahili ilikusanywa kutoka matini zilizoripoti habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*:

67. Uhifadhi misitu mashakani. (T.L. 8/6/21 uk. 11)
68. Magavana walenga ufugaji samaki (T.L. 14/7/21 uk. 4)
69. Ukame udhibitiwe mapema. (T.L. 19/10/21 uk. 10)
70. Wakulima wakadiria hasara ya viwavi jeshi (Kisumu) (T.L. 12/4/22 uk. 5)
71. Hasara za mafuriko zipunguzwe (T.L 16/12/21 uk. 6)
72. Hofu ya kimbunga kukaribia Msumbiji (T.L. 12/3/22 uk. 5)

Katika matini za mazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo*, sentensi sahili zilitumika katika baadhi ya vichwa vya habari ili kutoa ujumbe wa haraka kwa kutumia maneno machache yaani kudumisha iktisadi. Mfano wa 67 unaakisi kichwa cha habari kinachotoa onyo kwa wananchi kuwa shughuli za kuhifadhi misitu zimo mashakani. Usemi '*mashakani*' unamaanisha kuwa kuna watu wanaohujumu au kutatiza shughuli zinazofanywa kuhifadhi misitu. Kwa kutumia tamathali hii, mwanahabari anadumisha iktisadi na wakati uo huo kutoa ujumbe unaomdokezea msomaji ujumbe atakaoupata kikamilifu iwapo. Hii ni taarifa ya kidhana awali ambayo inayofahamika awali kwa msomaji hata iwapo hatafafanuliwa ni mashaka yapi ambayo yanakabili shughuli za uhifadhi wa mazingira nchini Kenya. Kimsingi, sentensi inayotumika inatoa wazo kamilifu kwa msomaji.

Mfano wa 68 unatoa taarifa kamili kwa msomaji. Sentensi hii ni ya kitaharuki na inayolenga kumchochea msomaji kusoma matini ili kujua kinachomaanishwa na kauli '*walenga ufugaji samaki*'. Taarifa inayotolewa ni kuwa magavana wa kaunti za magharibi mwa Kenya wanalenga kuimarisha shughuli za ufugaji wa samaki ili kuimarisha hali za kiuchumi za wakazi wa maeneo hayo. Mfano wa 69 unadokeza taarifa za habari kwa lengo

la kumchochea msomaji kusoma zaidi ili apate kile kinachodokezwa. Kwa msomaji anayekiona kichwa hiki cha habari kwa haraka, atajiuliza: ukame umezuka wapi? Kwa nini ukame huo udhibitiwe mapema? Nini kitatendeka iwapo ukame huo hautadhibitiwa mapema? Ili kupata majibu ya maswali haya, itamlazimu msomaji asome matini husika.

Mfano wa 70 unatoa taarifa kuhusu uvamizi wa viwavi jeshi maeneo ya Kisumu. Muundo wa sentensi hii umebadilishwa kimaksudi na mwanahabari ili kutimiza malengo fulani ya kimawasiliano. Kwa hali ya kawaida angesema: 'Viwavi jeshi vyasababishia wakulima hasara kubwa' badala yake anaanza na kauli 'Wakulima wakadiria hasara'. Hali hii inamaanisha kuwa msisitizo wa ujumbe unaotolewa upo kwenye hasara inayosababishwa na uvamizi wa viwavi jeshi. Hali inaonyesha kuwa wakulima walipata hasara kubwa kufuatia uharibifu wa mazao yao uliofanywa na viwavi jeshi. Mifano ya 70 na 71 inazungumzia majanga ya kimazingira yanayohusu mafuriko na kimbunga. Ujumbe unaotolewa katika mifano hii unaeleweka kwa uwazi kwa msomaji kutokana na miundo sahili ya sentensi zilizotumika.

Sentensi sahili zilitumiwa na wanahabari walioripoti matukio ya kimazingira kutoka taarifa kimilifu wakitumia maneno machache. Hali hii ilibainika kwenye vichwa vya habari vilivyofinyangwa kwa mitindo ya kiiktisadi ili kutoa taarifa za kuvuta nadhiri ya wasomaji kwa kutumia maneno machache. Baadhi ya vichwa hivyo vilidokeza tu taarifa zenyewe na vingine vikatumia lugha ya mkato kupitia kwa matumizi ya sentensi sahili. Maelezo yaliyotolewa katika matini za mazingira yalichanganya sentensi sahili, changamani na ambatani kutegemea ujumbe.

#### 4.2.4.2 Miundo ya Sentensi Changamani

Sentensi changamani ni aina ya sentensi yenye vitenzi viwili. Kitenzi cha kwanza maana yake si kamilifu ilhali cha pili maana yake ni kamilifu. Aina hii ya sentensi huundwa kwa kishazi tegemezi na kishazi huru. Kimuundo, sentensi changamani huwa na angalau kishazi huru na kishazi kingine tegemezi. Aidha, sentensi hii inaweza kuwa na vishazi tegemezi viwili (Habwe na Karanja, 2004). Mifano ifuatayo ya sentensi changamani ilikusanywa kutoka katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo*:

73. Waziri aonya vikali dhidi ya jaribio la kujaza bwawa ambalo linazozaniwa. (T.L. 3/12/21 uk. 5)
74. Afisa wa kijiji anusuru mtoto kutoka kwa mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa iliyonyesha maeneo ya Dazhou nchini Uchina siku mbili mfululizo. (T.L. 14/7/21 uk 6 )
75. Mabadiliko ya tabianchi yanavyoathiri kilimo cha pilau nchini. (T.L 12/1/22 uk. 3)
76. Kati ya vijito 21 vilivyokuwa vikitiririka kutoka vilima vya Maragoli, ni vichache tu vilivyosalia. (Vihiga) (T.L. 8/7/21 uk. 12)

Matumizi ya sentensi changamani katika matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* yalibainika katika maelezo yaliyotolewa kufafanua matukio yaliyokuwa yanasimuliwa na wanahabari. Sentensi changamani zilizotumika zilikuwa na vishazi huru na vishazi tegemezi. Vishazi huru vilitoa taarifa kamili kuhusu matukio yaliyosimuliwa na wanahabari. Kwa upande mwingine, vishazi tegemezi vilitoa habari za ziada kuhusu matukio yaliyotolewa katika vishazi huru.

Mfano wa 73 una kishazi huru: 'Waziri aonya vikali dhidi ya jaribio la kujaza bwawa.' Kishazi hiki kinatoa habari kamili zinazokusudiwa na mwanahabari. Kishazi tegemezi hakitoi taarifa zilizo kamilifu hadi kichopekwe kwenye kishazi huru. Katika sentensi hiyo kishazi tegemezi ni: 'ambalo linazozaniwa'. Kishazi hiki kinafafanua zaidi habari

zilizotolewa kwenye kishazi huru. Kishazi tegemezi hudhihirishwa kutokana na matumizi ya virejeshi **amba-** na **–o-/-ye-** (Mohamed, 1986). Virejeshi hivi vinaturudisha kwa matukio au wahusika waliotajwa katika vishazi huru. Mwanahabari ametumia kishazi tegemezi kumfafanulia msomaji wake kuhusu chanzo cha zogo la shilingi milioni tatu za wahasiriwa wa maporomoko.

Mfano wa 74 vilevile una kishazi huru na vishazi tegemezi viwili. Kishazi huru ni: 'Afisa wa kijiji anusuru mtoto kutoka kwa mafuriko'. Katika kishazi huru mmeshehenezwa vishazi tegemezi: 'yaliyosababishwa na mvua kubwa' pamoja na 'iliyonyesha maeneo ya Dazhou nchini Uchina siku mbili mfululizo' ambavyo vinatoa taarifa za ziada kuhusu mafuriko. Taarifa zinazotolewa katika kishazi tegemezi ni muhimu kwa sababu zinamfahamisha msomaji kuwa mafuriko yalisababishwa na mvua iliyonyesha kwa siku tatu mfululizo huko Uchina. Katika mfano wa 75 kuna kishazi huru: 'mabadiliko ya tabianchi nchini'. Kishazi tegemezi ni: 'yanavyoathiri kilimo cha plamu'. Msomaji wa makala anajulishwa mengi zaidi kuhusu mabadiliko ya tabianchi na jinsi yanavyoathiri ukuzaji wa zao la plamu nchini Kenya. Mabadiliko ya tabianchi yametajwa katika kishazi huru.

Mfano wa 76 una kishazi huru: 'kati ya vijito 21 ni vichache tu vilivyosalia' na kishazi tegemezi: 'vilivyokuwa vikitiririka kutoka vilima vya Maragoli'. Tunapata taarifa zaidi kuhusu vijito 21 vilivyokauka katika vilima vya Maragoli kupitia kwa kishazi tegemezi. Tunaweza kuhitimisha kuwa, vishazi tegemezi katika sentensi changamani zilizobainishwa kwenye mifano vinatoa taarifa za ziada zinazofafanua matukio ya kimazingira yanayosimuliwa katika vishazi huru ili kumwondolea msomaji tashwishi kuhusu matukio hayo. Kwa njia hii, ujumbe mkamilifu unatolewa kwa msomaji na mwandishi wa matini.

#### 4.2.4.3 Miundo ya Sentensi Ambatani

Sentensi ambatani huitwa hivi kwa sababu kuna tungo nyingi na sentensi nyingi zilizoambatanishwa. Muundo wa sentensi ambatani ni kwamba inaundwa na sentensi sahili na sentensi sahili nyingine au sentensi sahili tatu. Kimsingi ni kuwa sentensi ambatani huwa na vishazi huru viwili au zaidi ndani yake (Habwe na Karanja, 2004).Vishazi huru ambavyo vyenyewe huwa sentensi sahili huambatana kwa kutumia viunganishi (Omondi, 1992). Mifano ifuatayo ya sentensi ambatani ilikusanywa kutoka katika matini zilizoripoti habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*:

77. Takataka za bidhaa za kimatibabu zinatupwa katika jaa la Gikeu mjini Othaya *huku* wenyeji wakilalama kuhusu utupaji taka zinazotoka hospitalini katika eneo hilo *na* kuitaka serikali ya Kaunti ya Nyeri kufunga jaa hilo, wakihofia huenda likachangia kueneza maradhi ya kuambukiza.
    (T.L. 2/12/21 uk. 5 )
78. Matunda yake huwaniwa sokoni, na kuna sababu (...*Tofauti na* matunda mengine yaliyo na uchachu, ya Kiarie yana utamu wa kipekee anaosema umetokana na 'kilimohai' kisichotumia dawa au mbolea za kemikali.)
    (T.L 26/1/22 uk. 13)
79. Mlipuko 2020 waletea raia umaskini (Beirut, Lebanon). Mamia ya watoto wanaendelea kulala njaa *huku* familia nyingi zikikosa umeme wa kuwasaidia kuhifadhi dawa na vyakula *na* maradhi yakizidi kuongezeka. (T.L. 30/7/21 uk. 6)
80. Wingu la maangamizi limetanda kote nchini *huku* aina mpya ya Corona maarufu kama 'Delta' ikiua watu kwa mia. (T.L. 13/8/21 uk. 1)

Sentensi ambatani zilizotumika katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* ziliwawezesha wanahabari kutumia sentensi moja kutoa ujumbe wenye maelezo yaliyokamilika kabisa. Hali hii iliwaondolea uwezekano wa kuligawa wazo moja linaloweza kuelezeka kikamilifu katika sentensi mbili au zaidi. Hali hii iliondoa uradidi na uziada ambao ungepotosha maana ya matini. Sentensi ambatani zilizotumiwa katika matini za kimazingira zilizokusanywa katika utafiti huu zilikuwa na vishazi viwili au zaidi vilivyounganishwa pamoja.

Katika mfano wa 77, kuna vishazi huru vinne vilivyounganishwa na maneno 'huku' na 'na'. Kishazi huru cha kwanza ni: 'Takataka za bidhaa za kimatibabu zinatupwa katika jaa la Gikeu mjini Othaya'. Kishazi huru cha pili ni: 'wenyeji wakilalama kuhusu utupaji taka zinazotoka hospitalini katika eneo hilo'. Kishazi huru cha tatu ni: (wenyeji) 'waitaka serikali ya Kaunti ya Nyeri kufunga jaa hilo' na kishazi huru cha nne ni: '(wenyeji) wahofia huenda (jaa) likachangia kueneza maradhi ya kuambukiza'. Sifa inayoleta pamoja vishazi vya kwanza na vile vitatu vinavyofuata ni kuwa, kishazi cha kwanza kinazungumzia takakata za bidhaa za matibabu. Kwa upande mwingine, vishazi huru vitatu vinavyofuata vinazungumzia jambo moja linalohusu lalama za wenyeji wa Gikeu mjini Othaya. Hiki ndicho kiima cha vishazi huru vitatu vilivyotumika katika sentensi hiyo ambatani. Hata hivyo, kiima chenyewe kinadondoshwa katika kishazi huru cha tatu na cha nne ili kuondoa uradidi.

Mfano wa 78 una sentensi mbili changamani zilizounganishwa. Sentensi changamani ya kwanza ni: 'Matunda ya Kiarie yana utamu wa kipekee tofauti na matunda mengine yaliyo na uchachu'. Sentensi hii changamani ina vishazi viwili, kishazi cha kwanza ni huru ambacho ni: 'Matunda ya Kiarie yana utamu wa kipekee'. Kishazi cha pili ni tegemezi ambacho ni: 'tofauti na matunda mengine yaliyo na uchachu'. Sentensi changamani ya pili ni: '(Matunda ya Kiarie) yana utamu wa kipekee anaosema umetokana na 'kilimohai' kisichotumia dawa au mbolea za kemikali'. Sentensi hii changamani ina kishazi huru: '(Matunda ya Kiarie) yana utamu wa kipekee unaotokana na kilimohai. Kwa upande mwingine, kishazi tegemezi ni: '(kilimohai) kisichotumia dawa au mbolea za kemikali'. Kiima cha sentensi mbili changamani zilizounganishwa ni 'matunda ya Kiarie' ambacho hakikaririwi ili kuondoa uradidi katika sentensi.

Mfano wa 79 una vishazi huru vitatu. Kishazi huru cha kwanza ni: 'Mamia ya watoto wanaendelea kulala njaa'. Kishazi hiki ni sentensi sahili. Kishazi huru cha pili ni: 'familia nyingi zakosa umeme wa kuwasaidia kuhifadhi dawa na vyakula'. Kwa upande mwingine, kishazi huru cha tatu ni: 'maradhi yakizidi kuongezeka'. Kishazi huru cha pili ni sentensi changamani iliyo na kishazi huru: 'familia nyingi zakosa umeme' na kishazi tegemezi: 'wa kuwasaidia kuhifadhi dawa na vyakula'. Kishazi tegemezi kinatoa habari zaidi kuhusu ukosefu wa umeme. Hali hii inaonyesha kuwa matumizi ya sentensi ambatani huunganisha sentensi sahili mbili au zaidi zilizo na kiima kimoja na kuondoa uradidi wa kukariri kiima chenyewe katika mawasiliano.

Mfano wa 80 una vishazi huru viwili ambavyo ni: 'Wingu la maangamizi limetanda kote nchini' na: 'aina mpya ya Corona maarufu kama 'Delta' inaua watu kwa mia'. Vishazi huru viwili vilivyotumika katika sentensi hii ni sentensi mbili sahili ambazo zimeunganishwa na neno 'huku' kwa vile zinazungumzia jambo moja linalohusu madhara ya aina mpya ya Corona.

### 4.2.5 Matumizi ya Takwimu

Van Dijk (1988) anarai kuwa takwimu hutolewa katika matini za habari wakati wa kunukuu kutoka kwa wanaohusika ili kujenga taswira ya uhalisia wa matukio yanayoripotiwa. Katika hali hiyo, matukio yaliyoshuhudiwa moja kwa moja, mahojiano kutoka kwa walioshuhudia na kutoka kwa ripoti rasmi zilizopokelewa kutoka kwa watu na taasisi zilizo na nguvu na hadhi ya juu hufafanuliwa yakiambatana na takwimu zinatoa idadi au kiasi kamili ya kile kinachoripotiwa. Van Dijk anafafanua zaidi kuwa matumizi ya takwimu hudhihirisha usahihi wa ujumbe unaotolewa na huonyesha umuhimu wa

ujumbe wenyewe. Kwa hivyo, takwimu ni mbinu muhimu inayotumiwa katika uandishi wa habari kudumisha uhalisia, uhalali na utegemeo wa habari zinazotolewa (Van Dijk, 1988). Utafiti huu uliainisha matumizi ya takwimu katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* katika makundi mbalimbali. Sehemu ifuatayo imejadili aina za takwimu kwa kuzitolea mifano na ufafanuzi:

#### 4.2.5.1 Matumizi ya Takwimu zinazoonyesha Idadi Mahsusi

Takwimu za kiidadi zilitolewa kwa kuzingatia vivumishi vya idadi. Vivumishi vya idadi ni vile vinavyotaja idadi ya nomino husika. Kuna aina mbili za vivumishi vya idadi yaani, vivumishi vya idadi mahususi na vivumishi vya idadi isiyo mahususi. Vivumishi vya idadi mahususi hudhihirika kupitia kwa maneno yanayotaja idadi kamili ya vitu kwa mfano *kimoja*, *viwili*, *vitatu* au *tisa*. Kimofolojia vivumishi vya idadi mahususi huundwa kwa kuambatisha kiambishi patanishi cha msingi kwenye mizizi ya vivumishi vinavyotaja idadi mahususi (Wesana-Chomi, 2013). Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka katika gazeti la *Taifa Leo* inaakisi matumizi ya takwimu zinazoonyesha idadi mahususi:

81. *4.4* m wakabiliwa na njaa kutokana na uvamizi wa magaidi. (T.L 6/8/21 uk. 6)
82. Watu *52* wafa kutokana na janga la mafuriko Niger. (T.L 13/8/21 uk.5)
83. Covid-19 kuua *236,000* kufikia Disemba, WHO yasema. (T.L. 31/8/21 uk 5)
84. Idara yaonya kaunti *15* kuathiriwa na mvua nyingi wiki hii. (T.L. 21/12/21 uk. 3)
85. Waliofariki kimbungani Ufilipino sasa wafika *375* (T.L. 22/12/21 uk.8)
86. Mlipuko wa volkeno waua *13* Indonesia (T.L. 6/12/21 uk 8)
87. Dhoruba lauwa *watatu* na kukatiza huduma za umeme (T.L. 18/2/21 uk. 5)
88. Mafuriko yaua *wanane* huku maelfu wakiokolewa (Sydney) (T.L. 2/3/22 uk. 8)

Mifano ya 81, 82, 83, 84, 85 na 86 inaonyesha idadi mahususi kwa kutumia nambari 4.4, 52, 236,000, 15, 375 na 13 mtawalia. Lengo la kutumia nambari kuonyesha takwimu za

idadi ni kutumia maneno machache kueleza jambo. Kwa kutumia nambari mwanahabari anaepuka kutumia maelezo marefu na wakati huo huo kudumisha iktisadi katika taarifa zinazotolewa. Katika mfano wa 83 na 85 mwanahabari angetumia maneno mengi kutoa maelezo ya kiufafanuzi kuhusu takwimu zinazotolewa kwa mfano 'laki mbili mia tatu na sita elfu' na vilevile 'mia tatu sabini na tano'. Iwapo takwimu za nambari zitatumika katika vichwa vya habari vya matini husika, kuna uwezekano wa vichwa hivyo kuvuta makini ya msomaji ambaye ataviona kwa haraka.

Mifano ya 87 na 88 inadhihirisha matumizi ya takwimu za maneno zinazoonyesha idadi mahususi. Katika mifano hiyo neno mojamoja linalotaja idadi limetumiwa. Hii ina maana kuwa takwimu zinazotajwa kwa maneno hayo hazihitaji maelezo marefu. Kimsingi, matumizi ya takwimu zinazotaja idadi mahususi katika matini za kimazingira huimarisha uhalisia wa matukio yanayosimuliwa. Isitoshe, takwimu hizo za idadi mahususi hudhihirisha usahihi wa matukio yanayoripotiwa na wanahabari. Matini za kimazingira husheheni uhalisia na zinahitaji ushahidi wa kitakwimu kuondolea wasomaji shauku kuwa ujumbe huo ni ghushi. Baadhi ya matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* ni safu za kisayansi kwa mfano 'Mazingira na sayansi', 'Afya na Uhai', 'Shina la Uhai', 'Kilimo' na 'Akilimali' ambazo ujumbe wake hutolewa kwa mtindo unaotumia sajili ya kisayansi inayohitaji kuambatana na takwimu. Sajili ya sayansi hutegemea data inayotokana na utafiti wa kina ili kuonyesha uhalali, uhalisi na kutegemewa kwa taarifa inayotolewa.

#### 4.2.5.2 Matumizi ya Takwimu zinazoonyesha Kiwango au Kiasi Jumlifu

Takwimu zinazohusu kiwango zilionyeshwa kwa kutumia vivumishi vya idadi isiyo dhahiri yaani uchache au wingi. Vivumishi vya idadi isiyo dhahiri hudhihirika kupitia kwa

maneno yasiyotaja idadi kamili ya vitu kwa mfano –**chache** au **-ingi**. Kimofolojia vivumishi vya idadi isiyo dhahiri huundwa kwa kuambatisha kiambishi patanishi cha msingi kwenye mizizi ya vivumishi visivyotaja idadi dhahiri au mahususi (Wesana-Chomi, 2013). Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka gazeti la *Taifa Leo* inaonyesha matumizi ya takwimu katika matini za kimazingira ambazo zinaoonyeha idadi isiyo dhahiri:

89. Huenda *maelfu* wakafa njaa Tigray, UN yaonya. (T.L. 22/2/21 uk 5)
90. *Mamia* wahama Kerio mashambulizi yakizidi. (T.L. 22/3/22 uk. 4)
91. Teknolojia mpya kunusuru *maelfu* na makali ya joto. (T.L. 23/11/21 uk. 13)
92. *Maelfu* watoroka makwao baada ya volkano kulipuka. (T.L. 24/5/21 uk. 5)
93. 12 wafa *maelfu* wakihamishwa kwenye mafuriko. (T.L. 22/7/21 uk. 6)
94. Wanaharakati walalamikia uchafuzi *mkubwa* wa bahari. (T.L. 24/12/21 uk. 4)
95. Jua kuwaka sehemu *nyingi* za nchi-Utabiri (T.L. 7/2/21 uk. 4)
96. Kiangazi kinateketeza *wengi* Kitui lakini ameonyesha kilimo bado chawezekana. (T.L. 16/9/21 uk 13)
97. Wanajeshi *wengi* wakataa kupokea chanjo ya Corona (Amerika) (T.L. 19/2/21 uk. 5)

Baadhi ya wanahabari walitumia takwimu za jumla kuelezea matukio ya kimazingira. Mifano ya 89, 90, 91, 92 na 93 inaakisi vivumishi vya idadi ya jumla ya nomino zinazozungumziwa. Katika mifano hiyo, ni dhahiri kuwa haikuwa rahisi kwa wanahabari kuzungumzia idadi kamili ya nomino zinazozungumziwa kwa vile ni jambo lisilowezekana. Hata hivyo, wasomaji wanaweza kupata picha kamili ya kiwango au idadi ya kile kinachowasilishwa na wanahabari katika matini kupitia kwa idadi inayokadiriwa kupitia kwa matumizi ya maneno 'mamia' na 'maelfu'. Mifano ya 94, 95, 96 na 97 inatumia vivumishi vya idadi ya jumla ya kile kinachozungumziwa. Kwa kutumia kauli *'wengi*', '*nyingi*' na '*mkubwa*', mwanahabari anatumia taswira kama ya idadi ya jumla ya vitu au viwango vya hali zinazozungumziwa. Kupitia kwa taswira hizi, wanahabari wanafanikiwa kutoa picha ya uharibifu mkubwa na madhara ya kimazingira yaliofanywa na shughuli za binadamu zinazozungumziwa.

### 4.2.6 Uteuzi wa Mada

Kimsingi, mada ya habari au vichwa vya habari ni muhtasari au ufupisho wa taarifa zinazotolewa ambao huandikwa juu ya makala husika katika gazeti. Mara nyingi mada za habari haziandikwi kama sentensi kamili (Richardson, 2007). Mtafiti alibainisha kuwa vichwa hivi viliweza kukosa nomino au vitenzi fulani. Sababu ya kuacha maneno hayo inaweza kuwa ni kufanya mada hiyo kuvutia zaidi na isiwe na maneno mengi. Utafiti huu ulibainisha kuwa wanahabari walitumia lugha na mitindo tofautitofauti katika kuandaa mada za matini walizotunga. Utafiti huu umegawa mada za habari zilizochunguzwa katika makundi yaliyojadiliwa katika sehemu inayofuata.

#### 4.2.6.1 Mada za Kimdokezo au Kimkato

Mada za kimdokezo au kimkato huwa na maneno yaliyoachwa ambayo yanabeba ujumbe ulio muhimu au mzito. Aghalabu maneno huachwa kimaksudi ili kusababisha taharuki na hivyo kuchochea msomaji kuendelea kusoma ili apate ujumbe kamili (Conboy, 2010). Maneno ambayo huachwa kwenye mada ni vihusishi, vitenzi visaidizi, vivumishi, vimilikishi na viunganishi. Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka katika gazeti la *Taifa Leo* inaonyesha vichwa vya habari vilivyo na mada za kimdokezo au kimkato:

98. JOTO: Jua lawaka Mombasa! (T.L. 10/12/21 uk. 6)
99. Wenye njaa watelekezwa (T.L. 24/8/21 uk. 2)
100. MAFURIKO: Baada ya mbingu kupasuka (T.L. 29/7/21 uk. 6)
101. VIMBUNGA: Bidens atangaza dharura (T.L. 14/12/21 uk 8)
102. CORONA: mwenye macho aone... (T.L. 5/2/21 uk. 5)
103. ‘Covid mpya’ itahitaji maski mbili-Watafiti (T.L. 10/2/21 uk. 5)
104. Mazingira: Tusiache mtu yeyote nyuma (T.L. 3/11/21 uk. 2)
105. Kongamano kuu la mazingira lizindue viongozi usingizini (T.L. 2/11/21 uk. 8)

Mfano wa 98 unabainisha kichwa cha habari ambacho kinamdokezea msomaji lakini hakitoi ujumbe kamili. Kwa hali hiyo, msomaji anabaki akijiuliza maswali kama vile: kwa nini jua lawaka Mombasa? Ni nini hicho kinachohusu '*jua kuwaka*' ambacho kilifanya jiji la Mombasa kuwa na joto lisilokuwa la kawaida? Majibu ya maswali haya yatamchochea msomaji kudurusu matini nzima ili apate ujumbe wa mwanahabari aliyatunga makala. Matumizi ya alama ya mshangao pia ni ya kitaharuki. Lengo la kuandika kauli '*Jua lawaka Mombasa!*' kwa alama ya mshangao ni kuonyesha hali ya kustaajabisha au isiyo ya kawaida kwa msomaji. Aidha, matumizi ya kihisishi yanaashiria kuwa jua kuwaka kwa njia isiyo ya kawaida ndicho kiini cha joto kali Mombasa. Mwandishi anakusudia kumfahamisha msomaji wake kuwa, kiini cha kuongezeka kwa viwango vya joto Mombasa ni jua linalowaka kwa njia isiyo ya kawaida. Neno 'joto' limeandikwa kwa herufi kubwa kuashiria kuwa ndilo linaloakisi ujumbe unaowasilishwa na mwandishi wa makala.

Mfano wa 99 unatumia udondoshaji wa maneno kudokeza ujumbe ambao si mkamilifu. Kauli 'wenye njaa' imefupishwa kwa lengo la kujenga taharuki. Kauli hii ya kitaharuki inamchochea msomaji wa matini kusoma zaidi ili kujua ni kina nani wenye njaa na wametelekezwa na nani? Isitoshe, kwa msomaji anayefuatilia matukio ya kimazingira yanayotendeka nchini, kauli hiyo itakuwa ya kidhanaawali kwake. Msomaji huyo atafahamu hata bila kujulishwa kuwa ukame ulioshuhudiwa nchini ulisababisha njaa na kwa hivyo wahanga wa njaa wametelekezwa na serikali.

Katika mfano wa 100, neno 'mafuriko' limeandikwa kwa herufi kubwa ili kumdokezea msomaji kuwa ndilo linalotoa ujumbe unaosisitizwa. Kauli inayofuata neno hilo ni ya kitamathali kuwa, 'baada ya mbingu kupasuka'. Msomaji anajiuliza kuwa inawezekanaje mbingu kupasuka? Kauli hii inasheheni matumizi ya semi inayotoa taswira ya mafuriko.

Picha inayotolewa na taswira hii ni ile ya kuonyesha mvua iliyonyesha kwa wingi kupindukia. Kupitia kwa taswira hii msomaji anapata ujumbe wa mafuriko yaliyotokana na mvua kubwa iliyonyesha. Ujumbe unaohusu madhara ya mafuriko unatolewa kwa kudokezwa na mwanahabari aliyeandika makala hiyo. Mfano wa 101 unatumia herufi kubwa kusisitiza ujumbe kuhusu kuzuka kwa vimbunga Marekani. Neno 'vimbunga' limeandikwa kwa herufi kubwa kuonyesha ndicho kiini cha ujumbe unaotolewa.

Mfano wa 102 unatumia uakifishaji maalum kudokeza ujumbe unaotolewa. Neno 'Corona' limeandikwa kwa herufi kubwa ili kulisisitiza. Kauli 'mwenye macho aone' inatokatana na methali ya Kiswahili 'mwenye macho haambiwi tazama'. Kauli hiyo inamaanisha kuwa jamii yenyewe inashuhudia madhara ya Corona hata bila kusimuliwa. Mwisho wa kauli yenyewe una alama za dukuduku kuonyesha kuwa kuna maneno yaliyodondoshwa. Hili ni kusudi la mwanahabari aliyeandika makala la kujenga taharuki. Msomaji atajiuliza kuwa, mwenye macho aone nini? Katika mfano wa 103 kauli 'Covid mpya' imewekwa katika alama za mtajo kuonyesha kauli yenyewe imetumiwa kwa njia maalum kuashiria kuzuka kwa aina mpya ya ugonjwa huo inayojulikana kama 'Omicron'.

Mifano ya 103 na 104 inaashiria matumizi ya udondoshaji wa maneno katika sentensi kudokeza ujumbe unaotolewa. Katika mfano wa 103 msomaji atajiuliza ni nani anayeachwa nyuma katika shughuli za kimazingira? Kwa upande mwingine, katika mfano wa 104 msomaji atajiuliza ni viongozi gani wanaozinduliwa usingizini? Hali hizo zinazodokezwa zinakusudiwa kujenga taharuki. Kimsingi, matumizi ya vichwa vya habari vya kimdokezo katika matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* yalilenga kujenga taharuki na hivyo kuchochea msomaji kuendelea kusoma ili apate ujumbe kamili kuhusu matukio yaliyosimuliwa. Kwa njia hii wasomaji watapata ari ya kutaka kujua ujumbe

uliotolewa kwa njia ya mkato. Vyombo vya habari hukusudia kujiuza kwa wasomaji. Njia mojawapo ya kuhakikisha lengo hili limetimia ni kutumia vichwa vya kimkato vinavyovutia macho ya wasomaji.

#### 4.2.6.2 Mada za Kibalagha

Mada za kibalagha huchukua muundo wa swali ambalo halihitaji jibu. Swali linalotolewa katika kichwa cha habari hulenga kuchochea hadhira ya wasomaji kutafakari kwa kina kuhusu ujumbe unaotolewa na kwa njia hiyo huathiriwa kwa njia inayokusudiwa na mwandishi. Aidha, swali la balagha linaweza kuwa na dhamira ya kuchochea hisia fulani kwa wasomaji kwa mfano kusikitika, kukereka au kustaajabu (Timucin, 2010). Mifano ifuatayo ya vichwa vya habari vyenye mada za kibalagha kuhusu habari za kimazingira ilikusanywa kutoka katika gazeti la *Taifa Leo*:

106. Je, bora mitishamba? (T.L. 22/2/22 uk. 4)
107. Tutawahi kujifunza? (T.L. 19/7/21 uk.2)
108. Tutajifunza lini? (T.L. 19/7/21 uk. 1)
109. Kafyu ya nini na ushuru juu? (T.L. 28/9/21 uk. 10)
110. Mbona kuongeza kafyu ilhali ni wanasiasa wanaopepeta Covid? (T.L. 7/10/21 uk. 10)
111. Utoaji chanjo ya HPV nchini wasuasua, kunani? (T.L. 25/1/22 uk. 15)

Mfano wa 106 unaakisi swali la kibalagha linaloulizwa na mwanahabari aliyeandaa makala maalum kuhusu tiba za kiasili maarufu kama 'mitishamba'. Kichwa cha habari kinavuta umakini wa msomaji kwa sababu matumizi ya tiba za kiasili yamekuwa jambo la kawaida katika jamii kutokana na ongezeko la gharama ya tiba za kisayansi hospitalini. Msomaji wa gazeti anapokumbana na kichwa hicho cha habari atataka kujua kiini cha miti shamba kuwa bora. Msomaji atatafakari kuhusu tukio la ubora na athari za kutumia mitishamba kutibu magonjwa. Tafakuri hiyo inakusudia kulitafutia suluhisho la kudumu kuhusu kufaa

kwa matumizi ya tiba za kiasili katika utabibu. Msomaji atastaajabishwa na ukweli kuwa kumbe matumizi ya mitishamba yana manufaa mengi yakilinganishwa na tiba zinazotokana na ufumbuzi wa kisayansi.

Mifano ya 107 na 108 inaoonyesha maswali ya kibalagha ambayo yanalenga jamii nzima kuhusu uporaji wa petroli kutoka kwa malori yanayosafirisha shehena hiyo. Uporaji huo huzua majanga ya moto ambayo huangamiza waporaji na kuzua uharibifu mkubwa wa mazingira. Matukio ya kuchota petroli kwenye malori yaliyopata ajali katika barabara kuu yamekithiri nchini na kusababisha vifo na hasara kubwa kimazingira. Licha ya vifo hivyo wananchi huendelea na wizi huo bila kujali hatari iliyopo. Kwa hivyo, mwanahabari anaichochea jamii kujifunza kutoka kwa majanga ya awali yaliyoathiri mazingira na kuua watu wengi ili kujiepusha na uporaji huo. Maswali yanalenga kuibua masikitiko na majuto ili jamii nzima ihamasishwe kuhusu athari za wizi wa petroli kutoka kwa malori yaliyopata ajali barabarani.

Mifano ya 109 na 110 inalenga serikali kwa kusaili umuhimu wa kafyu nchini ilhali uchumi umedorora na wasiasa wanakiuka masharti ya kafyu. Wanahabari wanapendekeza kuwa kafyu inamuumiza mwananchi wa tabaka la chini na haitekelezi malengo ya kuzuia maenezi na maambukizi mapya ya Corona. Vichwa hivi vya habari vinakejeli hali ya kuwadhibiti wananchi kusafiri na kuendesha shughuli za kujikimu ilhali wanatozwa ushuru wa viwango vya juu. Vilevile, serikali imehalalisha usafiri wa wanasiasa wanaokiuka masharti ya afya ya kuzuia kuenea kwa Corona katika mikutano ya kisiasa.

Mfano wa 111 unabainisha kichwa cha habari chenye swali la balagha linalodadisi chanzo cha kusuasua kwa utoaji na upokeaji wa chanjo ya HPV nchini Kenya. Mwanahabari

analipa uzito janga la saratani inayowaathiri wanawake inayosababishwa na virusi vya HPV. Katika makala, mwanahabari anashangaa kuwa upokeaji na utoaji wa chanjo inayozuia maambukizi ya saratani hiyo unasusua nchini Kenya. Kwa kutumia swali la balagha, mwanahabari analenga kumchochea msoamji kutafakari kuhusu janga la saratani ya HPV na jinsi linavyoweza kumalizwa kupitia kwa utoaji chanjo. Tunaweza kufikia hitimisho kuwa vichwa vya habari vya kibalagha katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* vilikusudiwa na wanahabari kuchochea hisia fulani kwa wasomaji, kwa mfano, kusikitika, kukereka au kustaajabu kuhusu matukio yaliyosimuliwa.

#### 4.2.6.3 Mada za Kitakwimu

Mada za kitakwimu ni zile zinazotaja idadi au kiwango cha vitu na hali zinazozungumziwa katika kichwa cha habari. Takwimu hizi zinaweza kuwa kiasi mahususi cha fedha, umaratokezi wa tukio fulani au kiwango cha athari ya jambo fulani. Vichwa vya habari vyenye mada za kitakwimu hutaja idadi hiyo kwa hali mahususi au ujumla wake. Lengo la kutumia takwimu mahususi ni kuonyesha uhalisia wa jambo. Aidha, taarifa za kitakwimu hutoa ithibati inayoonyesha kuwa matukio yanayoripotiwa yanasadifu ukweli usiopingika (Van Djik, 1988). Ifuatayo ni mifano ya vichwa vya habari vyenye mada za kitwakimu iliyokusanywa kutoka kwa gazeti la *Taifa Leo*:

112. Tahadhari mafuriko yakiua *3* Makueni (T.L 1/12/21 uk 4)
113. Mafuriko yaua *18,* wengine *200* hawajulikani walipo. (T.L. 9/2/21 uk. 5)
114. Familia 15 zalala nje baada ya nyumba kusombwa usiku na mafuriko (T.L. 20/7/21 uk. 6)
115. *17* waangamia baada ya trela za vilipuzi kulipuka (Accra). (T.L. 22/1/22 uk. 5)
116. Ajali ya moto yaangamiza watu *16* klabuni. (T.L. 25/1/22 uk. 8)
117. Mlipuko wa trela la mafuta waua *77* Haiti (T.L 17/12/21 uk. 6)
118. Homa ya ubongo yaua watu *120* DRC (T.L. 10/9/21 uk. 5)

119. Watu *24* wafa jamii zikizozania malisho jimboni (T.L. 7/1/22 uk. 8)
120. Wahamiaji *57* wazama baharini. (T.L. 28/7/21 uk. 6)
121. Wavuvi 3 wafa ziwani, 2 wanusurika katika ajali ya usiku (T.L. 11/10/21 uk. 5)

Vichwa vya habari vinavyobainika katika mifano ya 112, 113 na 114 vinaonyesha idadi mahususi ya matukio yanayotokana na athari za janga la mafuriko. Hali hii inaimarisha uhalisia wa taarifa zinazotolewa. Isitoshe, wanahabari wanafanikiwa kutoa picha kamili ya madhara ya janga la mafuriko kwa jamii ili msaada wa dharura utolewe kwa waathiriwa. Kwa kutaja idadi hiyo, raia wanatambua madhara ya mafuriko yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi kutokana na shughuli hasi za binadamu. Kwa njia hii, wanahabari wanahamasisha jamii kuhusu jinsi ya kutunza mazingira na kujiepusha na madhara ya uharibifu wa mazingira.

Katika mifano ya 115, 116 na 117, vichwa vya habari vinatoa taarifa za idadi kamili ya watu waliokufa kutokana na majanga ya milipuko na moto. Taarifa hizi hazilengi tu wasomaji binafsi katika jamii, bali pia taasisi za kiserikali mbazo hushughulikia majanga kama yale ya moto katika jamii. Kwa kuonyesha idadi kamili, wanahabari wanafahamisha serikali pamoja na umma kwa jumla kuhusu kima cha janga la moto na kwa njia hiyo kutoa wito wa kujiandaa awali kulikabili katika jamii. Kwa kutumia takwimu zinazobainisha idadi kamili, wanahabari wanafanikiwa kufahamisha umma kuhusu uzito wa janga la moto na jinsi ya kuwa na vyombo vya kulikabili katika jamii zetu. Uhalisia wa madhara ya janga hilo kimazingira, kiuchumi na kijamii unaonekana bayana kupitia kwa takwimu zinazotolewa.

Vichwa vya habari vinavyoakisiwa katika mifano ya 118, 119, 120 na 121 vinaonyesha maafa yanayotokana na uharibifu wa mazingira. Taarifa hizi ni muhimu ili mipango ya

dharura ya kuwaauni wahanga ifanywe na vyombo vya kiserikali pamoja na mashirika yanayokabiliana na majanga hayo. Takwimu zinaonyesha uzito wa majanga yenyewe. Kimsingi, tunaweza kufikia hitimisho kuwa vichwa vya habari vya kitakwimu vilivyotumiwa katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* vililenga kutoa ithibati inayoonyesha kuwa matukio yaliyoripotiwa yalisadifu ukweli na uhalisia wa mambo.

#### 4.2.6.4 Mada za Kitaharuki

Mada za kitaharuki ni zile zinazoamsha ari ya msomaji kutaka kujua kinachojiri katika matini. Mada hizi hufinyangwa kwa uteuzi teule wa maneno yanayonuiwa kuteka makini ya msomaji ili asome zaidi kilicho katika matini. Mada za aina hii huzua taharuki kwa kumchochea msomaji kusoma matini nzima ili kujua kinachosimuliwa. Mada hudokeza tu jambo ambalo linamsisimua msomaji na inamlazimu asome makala nzima ili kujijazia mianya ya kiusimulizi iliyodokezwa katika kichwa cha habari (Bednarek, 2006). Hata hivyo, huenda kilichodokezwa katika kichwa cha habari kikasimuliwa kwa njia tofauti kabisa na matarajio ya msomaji. Lengo la taharuki ni kuchochea ari ya msomaji na kuvuta umakini wake kwenye matini husika. Mifano ifuatayo ya vichwa vya habari vyenye mada za kitaharuki zilizohusu mazingira ilikusanya kutoka kwa gazeti la *Taifa Leo*:

122. Ajabu ya raia kuchanjwa 'chumvi' kukabili Corona (Berlin, Ujerumani) (T.L 12/8/21 uk.5)
123. Polisi wapuliza Covid kwa sh 2,000 tu. (T.L 3/8/21 uk. 3)
124. 'Omicron imetua Kenya lakini hatutafunga nchi' (T.L. 16/12/21 uk. 4)
125. CORONA: Sikukuu kuwa tishio kuu (T.L. 22/12/21 uk. 8)
126. Raia njaa tu, vigogo nao siasa tu! (T.L. 3/2/21 uk. 2)
127. Uwanja wa ndege hutegemea vibuyu vya maji (T.L 17/2/21 uk. 4)
128. Polisi walaumiwa kuhusu wizi usiku nyakati za kafyu(T.L. 6/8/21 uk. 4)
129. Watoto wawili waliwa na fisi, ng'ombe 500 wafa njaa (Kwale) (T.L. 15/9/21 uk. 4)

130. Baa la njaa lazidi kuwa baya, msaada wa dharura wahitajika haraka.
(T.L. 15/10/21 uk. 6)

131. Kaunti yafunga hospitali ya kujifungulia kina mama kwa sababu ya ukame.
(T.L. 20/10/21 uk. 4)

Mfano wa 122 unabainisha kichwa cha habari ambacho kinadokeza habari za kumsisimua msomaji asome matini nzima. Msomji atajiuliza raia alichanjwaje chumvi kuzuia Corona? Kwa nini? Vipi? Lini? Maswali haya yatamchochea kusoma matini husika ili apate majibu. Kichwa hiki cha kimafumbo kina umbo wazi na umbo fiche. Kwa msomaji asiyefuatilia masuala ya kisayansi kuhusu utoaji chanjo atadhani kuwa mwanahabari anatoa taarifa kuhusu watu watakaochanjwa wakitumia chanjo ya chumvi ili kuzuia Corona. Hata hivyo, baada ya kusoma matini msomaji atagundua kuwa kinachozungumziwa ni kundi maalum litakalopokea chanjo iliyotengenezwa kwa maji yaliyotiwa chumvi katika majaribio ya kisayansi ya chanjo iliyotengenezwa Ujerumani. Kundi hili halitajua bali litalinganishwa na kundi lingine lililopokea chanjo halisi inayofanyiwa majaribio. Kwa upande mwingine kichwa cha habari katika mfano wa 123 kinatoa habari za kitaharuki kuhusu utepetevu uliofanywa na polisi wafisadi kwa kuwaruhusu raia wa kigeni kuvuka mpaka na kuingia nchini bila ithibati ya kuonyesha wamechanjwa na hawajaambukizwa Corona. Kitenzi ‘wapuliza’ kinatoa taswira ya mtu anayechochea moto kuwaka zaidi.

Kichwa cha habari katika mfano wa 124 ni cha kitaharuki kwa sababu kinanukuu taarifa zilizotolewa na waziri wa afya kuhusu ugonjwa wa aina mpya ya Corona ijulikanayo kama ‘Omicron’. Msomaji atajiuliza: ugonjwa huo ulifikaje nchini Kenya? Je, una madhara yepi ukilinganishwa na ule wa mwanzo? Kwa kutumia kichwa hiki, mwanahabari anafanikiwa kumchochea msomaji kusoma matini kuhusu chanjo ya ugonjwa wa Corona. Katika hali hiyohiyo, kichwa cha habari katika mfano wa 125 kinatoa habari za kitaharuki. Msomaji atajiuliza kuwa: sikukuu iwe tishio kuu? Kauli ‘tishio kuu’ ni usemi unaoashiria kuwa

huenda sherehe za Krismasi zikawa tishio kuu kiafya kwa kueneza Corona kwa vile watu husafiri kutoka maeneo ya mijini kwenda vijijini. Kuna uradidi wa silabi za mwisho katika maneno 'siku*kuu*' na '*kuu*' ili kuvuta makini ya msomaji. Kwa upande mwingine, kuna taharuki katika mfano wa 126 kwa vile msomaji atajiuliza ni raia gani hao walio na njaa? Ni vigogo wepi wanaopiga siasa wakati raia wanakumbwa na njaa? Hali hii itamchochea kusoma zidi makala apate majibu kamili.

Mfano wa 127 unaonyesha kichwa cha habari kilicho na taharuki. Taharuki inatokana na kauli 'hutegemea vibuyu vya maji'. Msomaji anajiuliza maswali kuwa, ni kwa nini uwanja wa ndege unategemea vibuyu vya maji? Maji yenyewe yana jukumu lipi? Wapi? Vipi? Haja ya kupata majibu ya maswali haya itamchochea kusoma matini ili apate ujumbe unaotolewa. Mwanahabari aliyeandika makala analenga kufichua kero la uhaba wa maji katika uwanja wa ndege. Wafanyakazi wanalazimika kuchota maji kwenye vibuyu kutoka mbali na kuyasafirisha yatumike katika uwanja huo. Mfano wa 128 unadhihirisha kichwa cha habari cha kitaharuki ambacho kinatumia kejeli na kinaya kukashifu wizi unaofanywa na polisi wakati wa kafyu. Kwa upande mwingine, mifano ya 129 na 130 inadhihirisha matumizi ya taharuki kusawiri athari za ukame katika Kaunti ya Kwale. Msomaji anaposoma mada hizi anajiuliza ilikuwaje watoto wawili wakaliwa na fisi huko Kwale? Mwandishi anakusudia kuibua hisia za huruma ili msaada wa dharura utolewe kwa wahanga wa njaa katika Kaunti ya Kwale. Mfano wa 131 unaibua taharuki kutokana na ujumbe unaotolewa kuhusu hospitali ya kipekee ya kujifugua kina mama kufungwa kwa sababu ya ukame. Mwanahabari anaangazia utepetevu wa serikali katika kutoa huduma kwa wananchi wake. Tunaweza kuhitimisha kuwa matumizi ya vichwa vya habari vya kitaharuki katika matini za kimazingira kwenye Gazeti la *Taifa Leo* yanalenga kuchochea

ari ya msomaji na kuvuta umakini wake kwenye matini husika na kwa njia hii akapata ujumbe unaotolewa kwa urahisi.

#### 4.2.6.5 Mada za Kimaelekezo

Mada za kimaelekezo ni zile zinazomwongoza msomaji kupata habari fulani ambazo huenda angezipuuza katika chombo cha habari. Msamiati unaoteuliwa na vilevile lugha inayotumiwa hulenga kumwelekeza msomaji kupata habari fulani ambazo huenda hazingetiliwa maanani iwapo zingewasilishwa kwa njia tofauti (Timucin, 2010). Katika gazeti la *Taifa Leo* kwa mfano, habari zinazohusu utunzaji na uharibifu wa mazingira zilitangulizwa kwa vichwa vya habari vilivyowaelekeza wasomaji kutahadhari, kubadili mielekeo na kuwa makini ili kutunza mazingira. Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka kwa gazeti la *Taifa Leo* inaonyesha vichwa vya habari vyenye mada za kimaelekezo kuhusu matukio ya kimazingira:

132. Hewa chafu ni hatari kwa mbegu za kiume, wataalam waonya. (T.L. 2/11/21 uk. 14)
133. Moshi wa magari wasababisha pumu kwa watoto-Utafiti. (T.L. 11/1/22 uk. 17)
134. Wito wakazi walinde vyanzo vya maji kupunguza uhaba. (T.L. 4/11/21 uk. 3)
135. Wakazi walalamikia uhaba wa maji wa mara kwa mara, wataka kaunti ipate suluhisho la kudumu. (Mombasa) (T.L. 19/7/21 uk. 4)
136. Hali ya anga yahatarisha utalii kwa kuathiri uhamaji wa kongoni. (T.L. 16/7/21 uk. 3)
137. Wakenya wanaendelea kupoteza maisha kwa kupora trela za petroli zilizoanguka barabara kuu. (T.L. 19/7/21 uk. 1)

Mifano ya 132 na 133 inatoa tahadhari kuhusu uchafuzi wa hewa. Maelekezo yanayotolewa katika mfano wa 132 ni kuwa, hewa chafu huathiri mbegu za kiume kwa mujibu wa utafiti wa wataalam wa kiafya. Kwa upande mwingine, mfano wa 123 unatoa maelekezo kuwa, hewa iliyochafuliwa na moshi wa magari ni hatari kwa afya ya watoto

kwa vile husababisha pumu. Mifano ya 134 na 135 inatoa tahadhari kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji na utafutaji wa suluhu ya kudumu kwa tatizo la uhaba wa maji. Hali hizi zinatokana na ukosefu wa uangalifu katika shughuli za binadamu ambazo huhujumu vyanzo vya maji na kusababisha uhaba wa maji.

Mifano ya 136 na 137 inatoa tahadhari kuhusu shughuli za binadamu zinazoathiri mazingira. Katika mfano wa 136 unatahadharisha kuhusu vitendo vya binadamu vinavyoathiri hali ya anga na kuhujumu uhamaji wa wanyama pori kama kongoni. Hali hii huathiri utalii chini. Mfano wa 137 unaelekeza wananchi kutahadhari kuhusu uporaji wa petroli katika malori yaliyoanguka. Kitendo hiki husababisha maafa na uharibifu wa mazingira kutokana na janga la moto.

#### 4.2.6.6 Mada za Kiistiari

Mada za kiistiari ni zile zilizotumia tamathali za ulinganishi bila kutumia maneno yanayoashiria ulinganishi huo.Istiari ni ulinganisho ambao hautumii maneno maneno kama vile 'kama, mfano wa, na mithili ya', yaani, kitu kimoja huitwa kingine. Msingi wa sitiari ni uhamishaji wa maana (Wamitila, 2007). Kwa mfano tunaposoma katika gazeti kuwa, 'jeshi la nzige lavamia ardhi eneo la Samburu' pana uhamishi wa maana yaani 'nzige' kupewa sifa ya 'jeshi'. Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka kwa gazeti la *Taifa Leo* inaonyesha vichwa vya habari vyenye mada za kiistiari kuhusu matukio ya kimazingira:

138. *Waliopepeta* Covid Kisumu (T.L. 18/6/21 uk. 1)
139. Serikali yashinda nzige *vita* (T.L. 15/10/21 uk. 2)
140. Corona *ilimeza* sh 112 M za uvuvi (T.L. 12/10/21 uk. 5)
141. Tujihadhari hili *zimwi* la matumizi ya pufya lisitumeze (T.L. 3/8/21 uk. 6)
142. Vitisho vya serikali ni *sumu* kwa utoaji chanjo (T.L. 23/8/21 uk. 8)

Msingi mkuu wa istiari ni uhamishaji maana na sifa kutoka kwa kitu kimoja hadi kitu kingine kwa kuvilinganisha. Katika mfano wa 138, ugonjwa wa Corona unalinganishwa na moto. Kwa kutumia mfano wa moto ambao unaweza kupepetwa ili kuuchochea kuwaka kabisa, mwanahabari aliyetunga makala analinganisha Corona na moto unaoanza kuwaka polepole lakini hupepetwa ukawa mkubwa na kusababisha uharibifu na hasara. Lengo la mwanahabari ni kutahadharisha wanasiasa nchini Kenya wanaoendesha mikutano ya kisiasa bila kuzingatia masharti ya wizara ya afya ya kuzuia maambukizi ya Corona. Katika mfano wa 139 nzinge wanalinganishwa na jeshi lenye uwezo wa kupigana vita. Katika vita hivyo, jeshi la nzige liko upande mmoja na jeshi la serikali liko upande wa pili. Hata hivyo jeshi la serikali linapata ushindi dhidi ya lile la nzige.

Mfano wa 140 unalinganisha Corona na zimwi lenye uwezo wa kumeza. Mfano huo unatoa taswira ya zimwi lililomeza kima cha shilingi milioni 112 ambazo zingetokana na shughuli za uvuvi zilizodumazwa na Corona. Mfano wa 141 unalinganisha matumizi ya pufya miongoni mwa wanariadha na zimwi linaloangamiza. Msomaji anapata picha ya madhara ya matumizi ya dawa za kututumua misuli miongoni mwa wanariadha. Madhara hayo yanafananishwa na zimwi linaloangamiza. Mfano wa 142 unafananisha vitisho vya serikali kwa wananchi ambao hawajapata chanjo ya Corona na sumu. Kwa kutumia ufananisho huo, mwanahabari anafanikiwa kujenga picha ya sumu inayohujumu harakati za utoaji chanjo. Ujumbe unaotolewa ni kuwa serikali inapaswa kuhamasisha raia kuhusu umuhimu wa chanjo hiyo badala ya kutumia vitisho.

Sehemu hii imechanganua vipengele vya lugha vinavyoteuliwa na waandishi wa habari wanaporipoti masuala ya kimazingira katika gazeti la Taifa Leo. Sehemu inayofuata inachunguza mitindo inayozingatiwa na wanahabari katika kuziwasilisha habari hizo.

## 4.3 Mtindo wa Wanahabari katika Kuripoti Habari za Mazingira katika Gazeti la Taifa Leo

Matini za taarifa za habari zina upekee wake unaoonekana upande wa mtindo, muundo na uteuzi wa msamiati (Van Djik, 1998). Kutokana na itikadi zilizoshehenezwa katika matini hizo, huenda msomaji akakosa kubainisha taathira zake kutokana na uzingatiaji wa matumizi ya lugha kijuujuu na kupuuza ubatini wa matini zenyewe. Kwa maana hiyo, kuna haja ya kuzingatia mkabala wa kihakiki tunapochunguza matumizi ya lugha ili kuonyesha uhusiano uliopo baina ya mtindo uliotumiwa na mwandishi wa matini, uteuzi wake wa lugha na itikadi inayojengwa (Van Djik, *ameshatajwa*).

Wanahabari hutumia mitindo mbalimbali kuwasilisha ujumbe wao kwa hadhira wanayoikusudia. Mitindo inayotumiwa inaweza kuchunguzwa kwa mujibu wa Nadharia ya Mitindo. Utafiti huu ulitumia Nadharia ya Mitindo kwa sababu inajikita kwenye uchunguzi wa lugha kwa kiasi kikubwa (Wamitila, 2007). Uchunguzi huo wa lugha unapania kubainisha ubunifu uliopo kwenye lugha hiyo na kwa kuuchunguza kwa undani unasaidia uelewekaji wa matini husika (Simpson, 2004). Nadharia ya Mitindo hudhamiria kuchunguza na kuchanganua matini kwa kuzingatia taratibu za kisayansi pamoja na zile za kitaaluma.

Watafiti wanaochunguza mitindo wanaweza kutumia mikabala miwili kufanikisha uchunguzi wao (Wamitila, 2007). Mkabala wa kwanza ni ule wa jadi ambao hutenganisha maudhui au yaliyomo kwenye matini ili kubainisha ujumbe au maana inayojitokeza pamoja na fani iliyotumiwa na mtunzi wa matini. Kupitia kwa mkabala huu, mtindo huchunguza jinsi ujumbe au maana hiyo inawasilishwa kwa matumizi ya mbinu tofauti ambazo

zinadhamiriwa na mtunzi kuibua athari fulani ya kiujumi kwa mlengwa au msomaji wa matini.

Mkabala wa pili ni ule wa kiisimu. Kwa kuzingatia mkabala huu, maarifa ya kiisimu hutumiwa kubainisha sifa za kimtindo za matini (Carter & Nash, 1990). Sifa hizo zinaweza kuwa za kifonolojia kwa mfano; ruwaza za sauti, vina na mizani pamoja na zile za grafolojia. Aidha, sifa za kisintaksia kwa mfano miundo ya sentensi, virai, vishazi na aina za sentensi zilizotumiwa zinaweza kuchunguzwa. Mtafiti anaweza kuchunguza sifa za kimsamiati kwa mfano uteuzi wa maneno na kategoria za maneno yaliyotumiwa katika matini. Isitoshe, mtafiti anaweza kuchunguza sifa za kisemantiki, sifa za kiusemi au diskosi na zile za kimuktadha au kipragmatiki. Utafiti huu ulitumia mkabala wa kiisimu kuchunguza sifa zifuatazo za kimtindo kwenye matini za kimazingira zilizochunguzwa:

### 4.3.1 Sifa za Grafolojia

Uchunguzi unaolenga grafolojia huchunguza mwonekano wa matini yaani abjadi au hati zilizotumiwa pamoja na upangaji wa taarifa kwenye safu za matini. Matini inaweza kuwa na sifa maalum za kimaandishi ambazo zinachimuzwa na kwa njia hii kukifanya kiwango hiki kuwa muhimu katika uchunguzi wa kimtindo wa matini yenyewe (Wamitila, 2007; Musotsi, 2017; Musotsi, Miruka & Okal, 2021). Sifa za kigrafolojia zinahusisha mpangilio wa aya, mpangilio wa kurasa, nafasi baina ya sentensi, matumizi ya picha na michoro, rangi mbalimbali, utaratibu uliotumiwa katika vichwa vya habari pamoja na upangaji wa safu za maneno zilizochunguzwa katika matini za habari katika gazeti la *Taifa Leo*. Matokeo ya utafiti yamejadiliwa kwa kina katika sehemu zinazofuata.

#### 4.3.1.1 Mpangilio wa Aya

Uchunguzi wa mpangilio wa aya za matini kwenye gazeti la *Taifa Leo* zilizohusu habari za kimazingira unadhihirisha umakini uliotumiwa katika ujenzi wa matini zenyewe na wanahabari. Taarifa za habari katika gazeti la *Taifa Leo* zimepangwa kwa uangalifu, umakini na utaratibu mwafaka katika gazeti lililochapishwa. Gazeti la *Taifa Leo* limezingatia mpango mahususi wa safu zenye aya zilizoratibiwa vyema. Gazeti la *Taifa Leo* limezingatia taarifa za habari kuhusu mazingira zilizopangwa katika aya maalum. Aya ya kwanza ina taarifa zilizokolezwa wino kusisitiza kiini cha habari kwenye matini. Baadhi ya taarifa ziliandikwa katika hati za kiitaliki kusisitiza ujumbe fulani uliotolewa na mwanahabari. Hata hivyo, uchunguzi wa kina wa habari katika aya zenyewe ulibainisha kuwa taarifa za habari kwenye matini zote zilizochunguzwa zilipangwa kwa aya fupi na kwa kuzingatia utondoti kutokana na ubanifu wa matini. Kwa hali hii, msomaji anaelekezwa kwa kudokezewa kilichojiri badala ya kufafanuliwa na kufahamishwa kilichotendeka. Mwandishi anamwelekeza msomaji kujijazia mianya ya kimawasiliano katika matini bila kumweleza kwa kina kinachosimuliwa. Kwa njia hii mwandishi anaweza kumshawishi, kumchochea au kumwongoza msomaji kifikra pasipo msomaji mwenyewe kujua.

Mfano wa kielelezo cha kwanza unaonyesha matini ya kimazingira katika safu ya ‘Shina la Uhai’ kuhusu ‘Afya ya jamii’ iliyoandika na Winnie Atieno katika gazeti la *Taifa Leo* la Februari 22, 2022 kwenye ukurasa wa 14-15. Katika matini hiyo, aya ya kwanza imeandikwa pembeni na kwa hati za italiki zilizokolezwa wino wa samawati. Aya hii ndiyo kiini cha ujumbe wa matini. Inasema kuwa: ‘*Wanasayansi na watafiti wa Makavazi ya Kitaifa wakishirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Matibabu Nchini (KEMRI) wanasema*

*wamegundua kuwa mbegu za mturituri zimekuwa zikitumiwa na jamii za Asia hasa nchini India kupanga uzazi*.' Sifa za kigrafolojia hukusudia kuvuta jicho la msomaji kwa taarifa zinazotolewa (Gerhard, 1986). Katika matini kwenye kielelezo cha 1 kuna aya inayoorodhesha manufaa ya tiba za kiasili kwa afya ya binadamu. Manufaa hayo yameorodheshwa kwa kiaya ili kutoa taarifa haraka kwa msomaji ambaye huenda akakosa muda wa kusoma matini nzima.




*Kielelezo cha 1*: Makala kutoka safu ya 'Shina la Uhai', *Taifa Leo*, Februari 22, 2022 uk. 14-15

#### 4.3.1.2 Mpangilio wa Kurasa

Matokeo ya utafiti yanaonyesha mpangilio wa kurasa za safu kuhusu mazingira kwa utaratibu mahususi katika gazeti la *Taifa Leo*. Kila ukurasa unaonyesha taarifa za habari za matukio ya aina mbalimbali. Kila ukurasa unaonyesha safu ya habari, mwandishi wa habari zenyewe, tarehe ya kuchapishwa kwa taarifa zenyewe na ukurasa husika.


Shina la uhai

Juhudi za kurejesha msitu

*Kilelezo 2*: Makala kutoka safu ya 'Shina la Uhai', *Taifa Leo*, Juni 8, 2021 uk. 12-13

Katika gazeti la *Taifa Leo* safu ya 'Shina la Uhai' huchapishwa kila Jumanne kuanzia ukurasa wa 12 hadi ukurasa wa 15/16. Safu hiyo inaanza na sehemu ya 'Afya ya Jamii' ambayo huzungumzia masula ya afya ya binadamu na jinsi inavyoathiriwa na mazingira

anamoishi. Safu ya shina la uhai huangazia kwa kina shughuli za kibinadamu zinazoathiri mazingira na kuhujumu afya.

#### 4.3.1.3 Nafasi Baina ya Sentensi

Matini zilizochapishwa huzingatia utaratibu maalum wa kuacha nafasi baina ya maneno na vilevile kutoka sentensi moja hadi nyingine au safu moja na nyingine. Sifa hii inazifanya zionekane nadhifu na zenye mvuto kwa msomaji (Hojjati & Muniandy, 2014). Kwa upande mwingine, matini zinazohusu habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* zinaacha nafasi baina ya sentensi kwa utaratibu wa kawaida unaozingatiwa katika matini zilizopigwa chapa katika vitabu. Mwonekano huu unazifanya matini hizi zionyeshe unadhifu unaorahisisha usomaji wake.


Shina la uhai
Afya Jamii
Wanavyokabili janga
H
Paul Wanjohi[Kushoto] na Paul Muriuki wakikusanya uchafu wa plastiki kutoka Mto Nairobi kisha baadaye huuzia
Picha/ HISANI

*Kilelezo 3*: Makala kutoka safu ya 'Shina la Uhai', *Taifa Leo*, Julai 6, 2021 uk. 12-13

Mfano wa matini kuhusu Mazingira na Sayansi uliotolewa katika kielelezo cha tatu unadhihirisha makala yenye safu na aya zilizopangwa kwa utaratibu nadhifu na maalum. Kuna matumizi ya aya zenye maneno machache yaliyopangwa kwa nafasi inayomwezesha msomaji kusoma taarifa kwa wepesi. Katika mfano huo kuna matumizi ya kielelezo cha picha na maneno kinachofafanua kwa muhtasari jinsi shirika la kibinafsi linavyokabiliana na janga la taka za plastiki jijini Nairobi.

**4.3.1.4 Matumizi ya Picha na Michoro**

Matumizi ya picha za rangi yanazingatiwa ili kutimiza malengo mbalimbali ya kimawasiliano (Gerhard, 1986). Taarifa zinazotolewa huambatishwa picha za matukio yanayosimuliwa. Sifa hii inaongeza uhalisia wa habari za kimazingira zinazotolewa kwenye gazeti la *Taifa Leo*. Kurasa na safu zinazotoa habari za matukio ya kimazingira zinatumia rangi mbalimbali kuvuta jicho la msomaji. Mbali na kuvuta umakini wa msomaji kwenye habari zinazotolewa, matumizi ya picha na michoro yanaimarisha uelewekaji wa habari za kimazingira zinazotolewa. Aidha, hali hii inajenga uhalisia kwa vile msomaji anajionea kile kinachofafanuliwa. Isitoshe, matumizi ya picha na michoro yanafanya matini kutoa taarifa za habari kwa msomaji kwa muhtasari.


MAKALA MAALUM

Hofu chemchemi za majimoto Kaunti ya Kwale zikianza kupoa

*Kilelezo 4*: Makala kutoka safu ya 'Makala Maalum', *Taifa Leo*, Machi 22, 2022 uk. 10

Mfano wa matini iliyoko kwenye kielelezo cha 4 kuhusu chemchemi za majimoto katika kaunti ya Kwale ambazo zimeanza kupoa kutokana na shughuli za binadamu zinazoathiri mazingira. Msomaji wa matini hii anahamasishwa kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira.

#### 4.3.1.5 Matumizi ya Rangi Mbalimbali

Matumizi ya picha za rangi yanazingatiwa katika matini za habari za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Taarifa zinazotolewa zinaambatishwa na picha za rangi za matukio yanayosimuliwa. Aidha, kurasa zenyewe zina rangi mbalimbali zinazojenga taswira inayokusudiwa na mwandishi wa matini. Sifa hii inaongeza uhalisia wa habari zinazotolewa kwenye matini husika. Aidha, matini hizi zinatumia rangi mbalimbali kuvuta jicho la msomaji. Rangi ni taashira au ishara mbalimbali zinazotoa ujumbe na maana fulani kwa msomaji (Oluwakemi & Omoniyi, 2015; Adegoju, 2008). Rangi nyekundu inaweza kuashiria hali hatari. Kwa upande mwingine rangi ya bluu, kwa mfano, ikaashiria kuwepo kwa matumaini.




*Kilelezo 5*: Makala kutoka safu ya 'Shina la Uhai', *Taifa Leo*, Novemba 23, 2021 uk. 14-15

Matumizi ya rangi za samawati na nyekundu katika mchoro wa kielelezo cha 5 yanatimiza malengo ya kimawasiliano. Rangi ya bluu iliyotumika katika mada ndogo inaonyesha hali shwari na matumaini katika mazingira ya binadamu kutokana na uvumbuzi wa rangi hiyo ya bluu inayozuia joto. Matumizi ya rangi nyekundu yanaashiria hali hatari inayotokana na ongezeko la joto linalosababishwa na mabadiliko ya anga. Kuziweka hali hizi mbili kwa usambamba kunalenga kuonyesha ukinzani uliopo binadamu anapotunza mazingira na anapoyaharibu kupitia kwa vitendo vyake.

#### 4.3.1.6 Upangaji wa Safu za Maneno

Upangaji wa safu za maneno kwenye ukurasa unaokusudiwa kupigwa chapa huzingatia utaratibu maalum. Mpangilio huo wa mikururo ya safu kwenye ukurasa uliochapishwa hukusaidia kuvuta jicho la msomaji kwenye matini husika (Gomez-Jimenez, 2015). Katika gazeti la *Taifa Leo*, kichwa cha habari kinachotangulia makala yenyewe kilifuatwa na picha

pamoja na jina la mwandishi wa makala. Herufi ya kwanza ya neno la kwanza katika aya ya kwanza ni kubwa ikilinganishwa na herufi zingine za neno hilo. Taarifa muhimu kwenye aya za safu zinasisitizwa kwa kutumia hati za kiitaliki, zilizokolezwa wino au zinazotumia wino wa rangi tofauti jinsi ilivyo katika mfano wa kielelezo cha 6.




*Kilelezo 6*: Makala kutoka safu ya 'Shina la Uhai', *Taifa Leo*, Septemba 21, 2021 uk. 12

Sifa za kigrafolojia za kimtindo kwenye matini za taarifa za kimazingira katika gazeti la Taifa Leo zinakusudia kutimiza malengo fulani ya kimawasiliano. Ukusara umepangwa kwa utaratibu maalum unaogawa safu, aya na mikururo ya maneno katika utaratibu mahususi unaokusudiwa kuteka jicho na umakini wa msomaji kwa haraka. Kuna matumizi ya picha, michoro na vielelezo vinavyomsaidia msomaji kupata habari kwa urahisi na kwa njia ya kasi. Uteuzi wa rangi zinazotumiwa na hata mpangilio wake katika matini unatimiza malengo ya kimawasiliano ya mwandishi wa makala. Tunaweza kuhitimisha ubainikaji wa sifa za kigrafolojia katika gazeti la *Taifa Leo* kupitia kwa jedwali lifutalo:

**Jedwali 1: Sifa za Kigrafolojia za Matini za Kimazingira katika Gazeti la *Taifa Leo***

| Matini za Kimazingira | Mwonekano wa hati | Utaratibu wa Kurasa zilivyopangwa | Nafasi baina ya sentensi | Picha Michoro vielelezo | Matumizi ya Rangi Mbalimbali | Sifa za Vichwa vya Habari |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Majanga Asilia | nadhifu | maalum | kawaida | zipo | anuwai | mvuto |
| Wanyamapori | nadhifu | maalum | kawaida | zipo | anuwai | mvuto |
| Mikurupuko Maradhi | nadhifu | maalum | kawaida | zipo | anuwai | mvuto |
| Utunzaji misitu | nadhifu | maalum | kawaida | zipo | anuwai | mvuto |
| Umwagaji taka | kawaida | kawaida | kawaida | zipo | moja | kawaida |
| Kilimo | nadhifu | maalum | kawaida | zipo | moja | mvuto |
| Uchafuzi mazingira | nadhifu | maalum | kawaida | zipo | anuwai | mvuto |
| Tabianchi | nadhifu | maalum | kawaida | zipo | anuwai | mvuto |
| Janga la moto | kawaida | kawaida | kawaida | zipo | anuwai | mvuto |
| Maporomoko | nadhifu | kawaida | kawaida | zipo | anuwai | mvuto |
| Uvuvi | kawaida | kawaida | kawaida | zipo | moja | kawaida |
| Kimbunga/Tufani | kawaida | kawaida | kawaida | zipo | moja | kawaida |
| Maji (safi/taka) | nadhifu | kawaida | kawaida | zipo | moja | kawaida |
| Bahari/Ufuo | kawaida | kawaida | kawaida | zipo | moja | kawaida |
| Ukame/Njaa | nadhifu | kawaida | kawaida | zipo | anuwai | mvuto |
| Ardhi/Mashamba | kawaida | kawaida | kawaida | zipo | moja | kawaida |
| Utunzaji mazingira | nadhifu | kawaida | kawaida | zipo | anuwai | mvuto |
| Kawi (safi/chafu) | kawaida | kawaida | kawaida | zipo | moja | kawaida |
| Maziwa/Mito/Mabwawa | nadhifu | kawaida | kawaida | zipo | moja | kawaida |
| Ubomozi/Milipuko | kawaida | kawaida | kawaida | zipo | anuwai | mvuto |

*Asili: Matokeo ya Utafiti, 2023*

### 4.3.2 Sifa za Kiothografia

Sifa za kiothografia zinahusisha suala la uakifishaji, matumizi ya herufi ndogo na kubwa, tahajia na uteuzi wa hati (Gerhard, 1986). Katika sehemu inayofuata baadhi ya sifa za kiothografia zilizobainika katika matini zilizochunguzwa zimejadiliwa na mifano kutolewa. Baadhi ya sifa hizo ni zifuatazo:

#### 4.3.2.1 Uakifishaji

Uakifishaji huathiri uwasilishaji wa ujumbe kwa msomaji (Chukwu, 2010). Kwa hivyo, ni wenzo muhimu katika uandishi wa matini za habari kwenye gazeti la *Taifa Leo*. Uakifishaji kwa msingi huu unaweza kutumiwa kama mkakati wa kudengua matini na kuchochea mtazamo mwingine wa msomaji. Udenguzi ni mtazamo wa kifalsafa na kitaaluma wa kudadisi, kuchunguza na kuonyesha kuwepo kwa ukinzani, uchangamano au utata katika hali zinazoonekana kuwa za kawaida (Wamitila, 2007). Viakifishi kama alama za

dukuduku, koloni, vihisishi na alama ya kuuliza ni nyenzo muhimu zinazoweza kudenguliwa ili kuonyesha hisia za mwandishi (Wamitila, *ameshatajwa*). Katika sehemu inayofuata mtafiti anatoa mifano ya viakifishi mbalimbali vilivyotumika katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* na kutoa maelezo kuhusu sababu za kimawasiliano za kutumia viakifishi vyenyewe:

143. Covid-19: UN yarai Mataifa kuanza kufungua shule zao.(T.L 29/7/21 uk 6)
144. ''Jiandaeni kwa kiangazi na njaa,'' Shirika laonya (T.L. 5/8/21 uk. 5)
145. "Corona 'huharibu' mioyo ya waathiriwa,'' wasema watafiti(T.L. 23/2/21 uk. 14)
146. Je, bora mitishamba? (T.L. 22/2/22 uk. 4)
147. Hewa chafu inaangamiza watu 160,000 mwaka jana-Shirika (Malaysia) (T.L. 19/2/21 uk 5)
148. 'Corona ya punda' yalipuka na kuzua hofu kubwa Lamu. T.L. 6/10/21 uk. 1
149. Ameunda jina kwa kuwa bingwa wa asali 'legit' (T.L. 26/1/22 uk. 17)
150. *Kafyu*: raia kuumia zaidi vigogo wakieneza Corona kijeuri. (T.L. 5/10/21 uk. 1)
151. CORONA: mwenye macho aone.... (T.L. 5/2/21 uk. 5)
152. Majanga ya nzige, Covid-19, mafuriko, maporomoko....yatikisa maisha ya wakenya (T.L 18/7/21 uk.6)
153. JOTO: Jua lawaka Mombasa! (T.L. 10/12/21 uk. 6)

Matumizi ya koloni katika mfano wa 143 yanaashiria kuwa kiafikishi hiki kimetumiwa ili kufupisha kauli ambayo ingekuwa ndefu. Isitoshe neno 'Covid' lililotengwa na kauli inayofuata kupitia kwa koloni limesisitizwa kwa sababu ndilo lenye ujumbe muhimu. Matumizi ya alama za mtajo katika mfano wa 144 yanaashiria maneno halisi yaliyosemwa na Shirika la Utabiri wa Hali ya Anga. Mwandishi wa matini kwa kunukuu kilichosemwa na shirika hilo, amefanikiwa kuipa kauli iliyosemwa mamlaka ya kufahamisha umma ujumbe unaokusudiwa unaotokana na matokeo ya utafiti. Kauli hiyo yenye ujumbe mzito inanukuliwa moja kwa moja jinsi ilivyosemwa na shirika la utabiri ili hadhira isiipuze kuwa ni ujumbe uliotolewa na mwanahabari binafsi. Matumizi ya alama ya kuuliza katika kauli ya mfano wa 145 yanaashiria swali la balagha linalolenga kuwafanya wasomaji kuwaza na

kutafakari kuhusu ubora wa tiba za kiasili zinazojulikana kwa wengi kama mitishamba. Swali hilo linakusudiwa kuvuta makini ya hadhira kuhusu manufaa ya kiafya ya kutumia mitishamba kutibu magonjwa. Matumizi ya kistari kifupi katika mfano wa 146 yanaonyesha kutenganishwa kwa kauli yenye ujumbe unaotolewa na mwanahabari na chanzo cha taarifa zenyewe. Kistari kifupi kinatenganisha ujumbe kuhusu athari za hewa chafu kwa afya ya binadamu na chanzo chake ambacho ni utafiti wa kitaalamu uliofanywa na Shirika la Afya Duniani. Kwa kutumia kistari kifupi, mwanahabari anamfahamisha msomaji kuwa hiyo si kauli yake binafsi bali inatokana na utafiti uliofanywa na wataalamu wa afya. Hili linabainisha kuwa kauli hiyo ni ya kimamlaka na si kauli ya kijumla inayotolewa na mwanagenzi.

Katika mfano wa 148, neno *Corona ya punda* limewekwa katika alama za mtajo kuonyesha kuwa neno hilo lina maana isiyo halisi. Matumizi haya yanabainisha maana nasibishi kwa vile msomaji atahusisha 'Corona ya punda' na ile inayoaathiri binadamu. Kwa njia hii ujumbe unaokusudiwa utaeleweka kwa urahisi. Mfano wa 149 unaonyesha matumizi ya neno *legit* ambalo limewekwa katika alama za mtajo. Mwanahabari anatumia msimu 'legit' kumaanisha kitu halali au kisicho ghushi. Msimu huu ulipata umaarufu kutokana na waigizaji wa futuhi waliokejeli matukio ya watu wengi kutapeliwa pesa zao kwa ahadi za kuzirudufu. Wasomaji wengi wanaweza kunasibisha msamiati huo na msimu uliopata umaarufu nchini Kenya. Katika mfano wa 150 neno 'kafyu' limeandikwa kwa hati za italiki au mlazo ili kuonyesha kuwa neno hilo limetoholewa kutoka kwa neno la Kiingereza *curfew*. Kwa kukosa kisawe cha moja kwa moja katika Kiswahili, mwanahabari analazimika kutohoa neno hilo la Kiingereza ili ajiepushe kutumia maelezo marefu kufafanua dhana hiyo. Hali hii inamaanisha kuwa wanahabari walilazimika kukopa

msamiati, kutafsiri, kutohoa na hata kubuni maneno ili kukabiliana na tatizo la kukosa istilahi za dhana zilizojitokeza kutokana na kuzuka kwa ugonjwa wa Corona. Ili kumwezesha msomaji kubainisha istilahi hizo mpya zilizotumiwa, wanahabari walitumia viakifishi mahususi katika matini kumwelekeza msomaji ipaswavyo. Mfano wa 151 unaonyesha matumizi ya alama za dukuduku mwishoni mwa sentensi. Matumizi ya kiakifishi hicho yanakusudiwa kuifanya kauli hiyo kuwa ya kimdokezo na inayomfanya msomaji atafakari kwa kina kuhusu athari za ugonjwa wa Corona. Katika mfano wa 152 kuna matumizi ya alama za dukuduku yanayokusudiwa kuonyesha mkururo wa majanga yanayofuatana yaliyolikumba taifa la Kenya. Alama za dukuduku mwishoni mwa orodha yanaashiria ukosefu wa uhakika kuhusu janga jipya linalotarajiwa kuzuka. Hali hii inaashiria hali ya kutamauka kwa wanajamii kutokana na majanga hayo yanayofuatana. Kwa upande wake, mfano wa 152 una matumizi ya alama ya mshangao yanayolenga kuonyesha hali ya kustaajabisha ya jua kuwaka kwa namna isiyokuwa ya kawaida.

Tunaweza kuhitimisha kuwa matumizi ya viakifishi kama alama za dukuduku, koloni, vihisishi na alama ya kuuliza ni nyenzo muhimu zinazoonyesha hisia za mwandishi wa makala. Aidha, viakifishi hivyo vinatumiwa kwa njia maalum ili kutimiza malengo fulani ya kimawasiliano jinsi tulivyobainisha katika maelezo yaliyotolewa.

#### 4.3.2.2 Matumizi ya Herufi Ndogo na Kubwa

Matumizi ya herufi kubwa na ndogo huathiri ujumbe unaowasilishwa kwa msomaji. Herufi kubwa zinaweza kuashiria msisitizo wa ujumbe fulani. Hii ina maana kuwa matumizi ya herufi kubwa na ndogo katika taaluma ya uanahabari huwasilisha ujumbe fulani kwa msomaji (Chukwu, 2010). Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka kwa matini za

kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* inaonyesha matumizi mbalimbali ya herufi ndogo na kubwa ili kutimiza malengo anuwai ya kimawasiliano:

154. FAO yaonya kuhusu uvamizi wa nzige (Shirika laeleza kuwa sasa wadudu hao wanaendelea kutaga mayai ambayo yataanguliwa kuunda jeshi la nzige mpakani.) (T.L 7/12/21 uk 5)
155. Urusi inatumia silaha za kemikali kuua raia-UN (T.L. 13/3/22 uk. 5)
156. KIMBUNGA: Hurricane yaporomosha majengo (New Orleans) (T.L 1/9/21 uk. 2)
157. KIANGAZI: Wachoma makaa kujikimu. (Kwale) (T.L. 15/9/21 uk. 4)
158. FOLENI NDEFU: wakazi jijini wahangaikia maji (T.L. 15/5/21 uk. 2)
159. MAAFA: mafuriko yaua 42 Ujerumani. (T.L. 16/7/21 uk. 5)

Mifano iliyotolewa hapo juu inadhihirisha kuwa matumizi ya herufi kubwa katika matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* yalikusudia kutimiza malengo mbalimbali ya kimawasiliano. Katika mifano ya 154 na 155 wanahabari wanatumia akronimu za Kiingereza ‘FAO’ na UN mtawalia. Iwapo wanahabari wangetumia lugha ya Kiswahili wangelazimika kutafsiri akronimu hizo kuwa: ‘Shirika la Kilimo na Chakula Duniani’ na ‘Umoja wa Mataifa’. Kwa kuzingatia Kiswahili, ingewalazimu kuziandika kikamilifu ili wasomaji wapate ujumbe huo bila kutatizika. Mifano ya 156, 157, 158 na 159 inaonyesha matumizi ya herufi kubwa katika neno la kwanza linalotumiwa kutanguliza kichwa cha habari. Maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa yanaonyesha msisitizo unaowekwa kwa sababu maneno hayo yanasheheni ujumbe muhimu unaowasilishwa katika kichwa cha habari.

#### 4.3.2.3 Tahajia na Sarufi

Makosa ya tahajia yalibainika katika baadhi ya matini zilizochunguzwa kwenye utafiti huu. Makosa ya tahajia na yale ya sarufi hutatiza uelewaji wa ujumbe uliokusudiwa na mwandishi wa matini (Conboy, 2010). Waandishi wanashauriwa kuhariri kazi zao

wenyewe kwa makini ili kuepuka makosa ya aina hii ambayo hupotosha ujumbe unaotolewa. Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka kwa matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* inaonyesha makosa ya kitahajia yaliyobainika katika matini hizo:

160. Waathiriwa wa kiangazi wasaidiwe kabla (**Λ**) maafa. (T.L. 6/8/21 uk. 8)
161. Burundi yakubali kupokea msaada wa chanjo **la** Covid shingo upande. (T.L. 30/7/21 uk. 6)
162. Walimu wakabili Corona shuleni **zao**. (T.L. 6/8/21 uk. 6)

Mfano wa 160 unabainisha kosa la kisarufi ambapo kuna neno lililoachwa na mwandishi wa makala. Tumetumia alama (**Λ**) katika sentensi ya mfano wa 160 kuonyesha sehemu ambayo neno lililoachwa linapaswa kuwa. Neno lililodondoshwa ni kihusishi cha a-unganifu 'ya' ili sentensi isomeke: 'waathirika wa kiangazi wasaidiwe kabla ya maafa' kwa usahihi. Mfano wa 161 unadhihirisha kosa la kisarufi linalohusu matumizi ya kihusishi cha a-unganifu 'la' ambacho hakiafikiani na nomino 'chanjo' ya ngeli ya I-ZI katika upatanisho wa kisarufi. Kihusishi cha a-unganifu kilichopaswa kutumiwa ni 'ya' kinachoafikiana kisarufi na nomino 'chanjo'. Sentensi hiyo ilipaswa kuwa: 'Burundi yakubali kupokea msaada wa chanjo **ya** Covid shingo upande' kwa usahihi. Mfano wa 162 unabainisha pia kosa la sarufi linalohusu upatanisho wa kisarufi wa kielezi cha mahali 'shuleni' na kivumishi kimilikishi 'zao'. Kimsingi, sentensi hiyo ilipaswa kuwa: 'walimu wakabili Corona shuleni mwao' au 'walimu wakabili Corona katika shule zao'. Hata hivyo, kosa hili haliathiri mawasiliano kwa njia yoyote ile kwa vile msomaji anapata ujumbe kamili uliokusudiwa na mwandishi wa makala.

#### 4.3.2.4 Uteuzi wa Hati

Uteuzi wa hati huathiriwa na mitindo mbalimbali ya mwonekano wa hati iliyotumika katika matini. Baadhi ya matini hutumia aina fulani za hati maalum, hati za italiki, zingine

hutumia hati zilizokolezwa wino na baadhi hutumia hati za kawaida. Athari ya jumla ya matumizi ya sanaa hati kwa mfano hati zilizokolezwa wino, kutumia italiki au kuchanganya hati ni kuwa inasisitiza sehemu fulani za matini zenye ujumbe maalum ambao mwandishi analenga msomaji aupate kwa kuvuta umakini wake (Gerhard, 1986). Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka kwa matini za kimazingira zilizochunguzwa kutoka katika gazeti la *Taifa Leo* inaonyesha uteuzi mbalimbali wa hati uliobainika katika matini hizo:

163. *Hofu ya ongezeko la saratani ya mapafu nchini*. (T.L. 20/8/21 uk. 15)
164. *Juhudi za kurejesha msitu katika vilima vya Maragoli*. (T.L. 8/6/21 uk. 12)
165. *Wanavyokabili janga la plastiki jijini*. (T.L. 6/7/2021 uk 6)

Katika mfano wa 163 kuna uteuzi maalum wa hati zinazotumiwa kuandika kichwa cha habari kilichoonyeshwa kwa hati za kiitaliki (tazama kielelezo cha 6). Katika matini halisi, kichwa cha habari kimeandikwa kwa kuzingatia aina za hati zinazojulikana kama 'Lucida Calligraphy' ambazo ni za italiki na zimekolezwa wino. Kifungu kilichowekwa katika mabano katika mfano wa 163 kimeandikwa kwa kuzingatia hati aina ya 'Times New Roman' za wino mwekundu uliokolezwa. Ukolezaji huu wa rangi pamoja na uteuzi wa aina tofauti ya hati unalenga kutofautisha kifungu hicho ambacho kinadokeza taarifa muhimu zilizoshehenezwa katika kichwa cha makala. Hali hiyohiyo inadhihirika katika mifano ya 164 na 165 ambayo inaweza kurejelewa kwenye vielelezo vya 2 na 3 mtawalia katika tasnifu hii. Vichwa hivi vya habari vinatumia hati aina ya 'Lucida Calligraphy' ilhali kifungu kinachofuata cha ufafanuzi kimekolezwa wino mwekundu katika matini halisi. Mtindo huu wa kimaksudi wa kutumia aina mbalimbali za hati, rangi na italiki unalenga kutofautisha sehemu mbalimbali za matini zinazosisitiza ujumbe fulani katika makala.

Uteuzi huo unakusudia pia kurahisisha mawasiliano kwa kumwezesha msomaji kukiona haraka kwenye ukurasa husika.

### 4.3.3 Sifa za Kileksia

Sifa za kileksia ni zile za kibalagha zilizotumiwa katika matini za diskosi. Baadhi ya sifa za kileksia zinazoweza kuchunguzwa katika matini za kidiskosi ni: uteuzi wa msamiati, matumizi ya tamathali za usemi na uradidi au urudiaji (Wamitila, 2007). Katika sehemu inayofuta sifa za kileksia zilizochunguzwa katika utafiti huu zimejadiliwa kwa kina na mifano kutolewa.

#### 4.3.3.1 Uteuzi wa Msamiati

Uteuzi wowote ule wa msamiati unaweza kuwa rasmi au usorasmi. Muktadha wa kijamii ambamo mawasiliano yanatendeka ndio huamua iwapo tutatumia usemi rasmi au usorasmi. Mzungumzaji huteua maneno ya kutumia katika mawasiliano kutegemea urasmi au ukawaida wa muktadha anaohitajika kuwasiliana. Ufaafu au kutokufaa kwa maneno anayotumia mzungumzaji katika mawasiliano hutegemea sifa za kimtindo za maneno hayo. Hivi ni kusema kuwa kila neno huwa na mtindo wa kiuamilifu ambao neno hilo linawakilisha au kusimamia. Mtindo wa kiuamilifu unaweza kufasiriwa kama mfumo wa kimatumizi ulio mahususi katika nyanja fulani ya mawasiliano (Van Djik, 1998). Hii ndiyo sababu ya kimsingi ya wanahabari kuteua msamiati kwa uangalifu wanapoandika matini zao.

Nyanja ya mawasiliano ni hali fulani inayoathiri mchakato mzima wa mazungumzo katika muktadha mahususi. Mifano ya miktadha hiyo ni: mazungumzo ya kitaaluma, mhadhara, barua ya kirafiki, gumzo, barua rasmi, barua ya kimapenzi au hotuba mahakamani

(Schiffrin, 1998). Hali hizo zote zinaweza kugawanywa katika makundi mawili kutegemea urasmi au ukawaida wake. Kwa mfano barua rasmi, hotuba mahakamani, utani, mhadhara na mazungumzo ya kitaaluma huhitaji mawasiliano rasmi. Kwa upande mwingine, barua ya kirafiki, gumzo na utani huhitaji mawasiliano yasiyo rasmi. Hivi ni kumaanisha kuwa mitindo ya uamilifu inaweza kuainishwa katika makundi mawili kutegemea urasmi au usorasmi wake. Katika matini zilizochunguzwa katika utafiti huu, uteuzi wa msamiati ulimulika hasa sajili ya kisayansi inayoangazia masuala ya mazingira na athari zake kwa uhai na afya ya binadamu, wanyama na mimea. Miktadha hiyo ya mawasiliano ni rasmi. Hii ina maana kuwa matini za wanahabari zilitumia lugha rasmi. Hata hivyo, kuna matukio yaliyosimuliwa majanga ya kuzuka kwa Corona na uvamizi wa nzige ambayo yalitumia lugha ya utani, kejeli, dhihaka na tashtiti ili kukashifu utepetevu, kutowajibika na ufisadi wa wahusika. Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka kwa matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* inaonyesha matumizi ya lugha rasmi yaliyotumika katika matini hizo:

166. Mabadiliko ya tabianchi yanyima watoto virutubisho tosha (...udadisi wa Kenya Market Trust, Shirika lisilo la kiserikali linalohusika na masuala ya mabadiliko ya mifumo ya ustawi wa masoko, unaonyesha kuwa viwango vya halijoto katika Kaunti ya Kajiado vitaongezeka kati ya $100^0C$ na $310^0C$ kufikia 2030.)
(T.L. 24/8/21 uk. 12)
167. Corona yasukuma maelfu kutumia kawi hatari (...Utafiti uliofanywa na hospitali ya Tenwek na Taasisi ya Kutafiti Kansa ya Amerika na Kituo cha Kudhibiti Magonjwa cha Amerika (CDC) katika Kaunti ya Bomet mwaka jana, ulibaini kuwa moshi unasababisha kansa. Watafiti hao walihusisha watu 305 ambao hawakuwa na dalili za ugonjwa wa kansa. Baadaye walipopimwa walipatikana na kansa ya umio (*esophagus cancer*), wengi wao walikuwa wanawake. Washiriki walipatikana na kemikali za *Polycyclic Aromatic Hydrocarbons* (PAHS) ambazo hupatikana kwenye moshi wa kuni. Kemikali hizo huhusika pakubwa katika kansa ya umio. (T.L. 7/12/21 uk. 15)
168. Maradhi yanayowazonga waathiriwa wengi wa mafuriko (...ugonjwa wa kipindupindu husababishwa na mtu kula chakula aua maji yaliyo na viini vinavyojulikana kama *Vibrio Cholerae*.) (T.L. 17/12/21 uk. 15)

169. Je, wajua kwa nini mende wameganda kwako? (mende hubeba bakteria hatari kama vile '*Salmonella*', '*Enterococcus*' ambao husababisha maumivu ya tumbo na kuhara, kipindupindu na hata kichocho.) (...aina nyingine za mende ambao huhangaisha watu nchini Kenya ni *Blatta Orientalis*, *Periplaneta Americana* na *Supella Longipalpa* kulingana na ICIPE.) (T.L. 30/7/21 uk. 15)

170. Uchafuzi wa mito watishia mamilioni. (Samaki, kaa na changarawe zilizochunguzwa pia zilipatikana kuwa na madini 10 hatari hasa *chromium*, *arsenic*, *cadmium*, *lead*, *selenium*, *copper*, *aluminium*, manganese, barium na chuma. (T.L. 14/8/21 uk. 2)

171. Wanavyokabili janga la plastiki jijini (..."Kwa upande wetu tunahusika na uundaji wa aina 26 za plastiki ikiwa ni pamoja na *Low-Density Polyethylene* (LDPE) *Polyethylene Teraphthalate* (PET), inayotumika kuunda chupa za maji, na *Styrofoam* aina ya plastiki inayotumika kuunda vifaa vya kupakia chakula na bidhaa za elektroniki," anaeleza Bw. Okoth.) (T.L. 6/7/2021 uk. 13)

Mifano ya 166, 167, 168, 169, 170 na 171 inadhihirisha hali ya kuchanganya lugha katika matini za kisanyansi zinazohusiana na mazingira. Hali ya kuchanganya lugha inaashiria ukosefu wa istilahi mwafaka katika lugha ya Kiswahili ambayo inarejelea dhana inayozungumziwa. Kwa mfano katika 168 na 169 kuna matumizi ya jina la Kilatini lililotumiwa kurejelea viini vinavyosababisha kipindupindu. Hali hiyo pia inajitokeza katika mfano wa 169 unaotaja aina mbalimbali za mende. Mfano wa 170 unatumia majina ya Kiingereza kutaja aina mbalimbali za madini na ule wa 171 kutaja aina mbalimbali za plastiki. Kwa kuchanganya lugha mwandishi wa makala anarahisha mawasiliano ambayo yangezua utata iwapo angedhubutu kutafsiri, kutohoa au kuswahilisha istilahi zenyewe. Kimsingi ni kuwa, matini husika ya kimazingira ilimwongoza mwanahabari aliyeitunga kujikita katika sajili fulani kwa mfano afya, misitu, magonjwa, uchafuzi na utunzaji mazingira na kadhalika. Hii ina maana kuwa msamiati alioutumia uliafiki ujumbe uliokusudiwa kutolewa na mwanahabari. Sifa mojawapo inayobainika katika sajili ya kisayansi ni matumizi ya takwimu zinazotokana na utafiti wa kisayansi uliofanywa ili kutoa ithibati ya madai yanayotolewa. Aidha, sajili hiyo huchanganya lugha na kutumia msamiati wa kitaaluma unaohusiana na taaluma inayorejelewa.

#### 4.3.3.2 Matumizi ya Tamathali za Usemi

Tamathali ni istilahi inayorejelea mbinu ambayo inahusisha maana isiyo wazi na inayomhitaji msomaji kuisimbua ili aweze kuielewa. Kwa upande mwingine, tamathali za usemi ni dhana inayotumiwa kurejelea sifa za kimtindo ambazo hutumiwa katika matini kupitia kwa matumizi ya lugha yanayolenga kuzua usemi wenye uwezo wa kushawishi (Wamitila, 2007). Tamathali za usemi huweza kuzungumziwa kama *lugha ya kitamathali* ambayo ni wenzo muhimu katika ujenzi na uimarishaji wa hisia. Lugha ya kitamathali hurembesha kile kinachozungumziwa na kukifanya kiwe na mvuto mkubwa wa kiumbuji na kisanaa. Aidha, lugha ya kitamathali hutumiwa kwa lengo la uthabitishaji yaani kukifanya kinachorejelewa kuwa na uthabiti fulani, na kwa njia hii, mkokotezo mkubwa. Wanahabari walitumia tamathali za aina mbalimbali katika utunzi wa matini za kimazingira. Baadhi ya mifano ya matumizi ya tamathali za usemi katika gazeti la *Taifa Leo* kwenye matini za kimazingira zilizochunguzwa imejadiliwa kwa kina katika sehemu inayofuata:

##### 4.3.3.2.1 Matumizi ya Misemo au Nahau

Nahau ni msemo wa kimafumbo ambapo jambo hueleweka kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja. Nahau huwa na msingi katika ulinganishi wa kiistiari (Wamitila, 2007). Kwa mfano '*pata jiko*' ni semi iliyoundwa kwa kitenzi '*pata*' na nomino '*jiko*'. Muunganiko huo wa kitenzi na nomino hubadilisha maana ya kauli iliyoundwa na kuifanya iwe ya kitamathali. Nahau huwa na msingi katika ulinganishi wa kiistiari. Kwa mfano kula njama, kuwekea kikao na kukata roho. Mifano ifuatayo ya matumizi ya misemo na nahau katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* ilikusanywa katika utafiti huu:


172. Covid-19: Kaunti za Pwani za**kaa chonjo** (T.L. 5/8/21 uk. 4)
173. Ajali: moto mkubwa wa**kata usafiri** (T.L. 6/8/21 uk 6)
174. NMS ya**piga jeki** wafanya biashara sokoni Muthurwa kwa maji safi (T.L. 11/8/21 uk 4)
175. Raia wafa njaa viongozi waki**piga domo**. (T.L 24/8/21 uk. 1)
176. Hasara maziwa 2 yaki**zamisha ardhi** (T.L. 29/9/21 uk. 4)
177. Mafuriko: wakazi wa**pata hasara** (Meru) (T.L. 30/11/21 uk. 3)
178. Corona ya**futa kazi** Wakenya 300,000 (T.L. 23/5/21 uk. 1)
179. Watu saba wa**aga dunia** mafuriko yaki**ponda nchi** (T.L. 4/5/21 uk. 4)
180. Mzee wa miaka 70 **afa maji** akijaribu ku**vuka mto** uliofurika. (Narok) (T.L. 14/7/21 uk. 4)

Mfano wa 172 unadhihirisha matumizi ya semi 'kaa chonjo' yenye maana ya 'kuwa makini au kutahadhari'. Maana inayowasilishwa ni kuwa Kaunti za Pwani ziko makini kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa Corona. Mfano wa 173 unaakisi matumizi ya semi 'kata usafiri' inayomaanisha kuzuia watu kusafiri. Hii inaonyesha kuwa moto mkubwa ulizuia watu kusafiri. Mfano wa 174 unaonyesha matumizi ya semi 'piga jeki' kuinua viwango au kuimarisha hali ya maisha ya watu. Katika muktadha huo Maisha ya wafanyabiashara wa soko la Muthurwa yaliinuliwa walipopata maji safi. Katika mifano ya 175 na 176 kuna matumizi ya semi 'piga domo' na 'zamisha ardhi' zenye maana' kujihusisha katika mazungumzo yasiyo na faida' na 'maji kufurika na kufunika ardhi' mtawalia. Mfano wa 177 unabainisha matumizi ya semi 'pata hasara' inayoonyesha athari hasi za mafuriko yaliyoharibu mali ya wakazi wa kaunti ya Meru. Mfano wa 178 unadhihirisha matumizi ya semi 'futa kazi' inayomaanisha kupoteza ajira kutokana na madhara ya Corona. Mfano wa 179 una semi 'ponda nchi' inayoashiria madhara hasi ya mafuriko yaliyosababisha vifo vya watu saba. Kwa upande mwingine, mfano wa 180 unaakisi matumizi ya semi mbili 'kufa maji' na 'vuka mto' zenye maana kifo kilisababishwa na kuzama majini na kitendo cha kusafiri kutoka ng'ambo moja ya mto hadi nyingine mtawalia. Matumizi ya misemo na nahau katika matini za kimazingira katika gazeti la Taifa Leo yalinuiwa kuipamba lugha na kuifanya iwe yenye mvuto kwa msomaji.

#### 4.3.3.2.2 Matumizi ya Sitiari

Sitiari ni tamathali ya usemi ya ulinganishi usiyotumia vilinganishi 'kama', 'mithili ya', 'ja' na 'mfano wa'. Msingi wa sitiari ni uhamishaji wa maana (Wamitila, 2007). Kwa mfano tunaposema kuwa, 'ujana ni moshi' pana uhamishi wa maana yaani 'ujana' kupewa sifa ya 'moshi'.

Sitiari hueleweka vizuri kwa kuzingatia dhana zake kuu ambazo ni: kilinganishi, kilinganishwa na msingi. *Kilinganishi* ni kile kinachotumiwa kama msingi wa kufananisha (moshi). *Kilinganishwa* ni kile kinachofananishwa (ujana). *Msingi* ni sifa yenyewe ya ulinganishi kwa mfano katika sitiari ya 'ujana ni moshi' msingi ni ile hali ya 'kupita' au 'kuwepo kwa muda mfupi'. Kielelezo kifuatacho kinaonyesha hali hiyo:




181. Taharuki baada ya *jeshi la nzige* kuvamia shamba (Nyandarua) (T.L. 3/12/21 uk. 4)
182. FAO yaonya kuhusu uvamizi wa nzige. (...Shirika hilo laeleza kuwa sasa wadudu hao wanaendelea kutaga mayai ambayo yataanguliwa na kuunda *jeshi la nzige* mpakani. (T.L. 7/12/21 uk. 14)
183. *Jeshi la nzige* lavamia ardhi maeneo ya Samburu. (T.L. 22/11/21uk. 4)
184. *Wingu la nzige* laharibu mimea Turkana, Baringo. (T.L. 7/12/21 uk. 5)
185. *Wingu la maangamizi* limetanda nchini huku aina mpya ya Corona maarufu kama 'Delta' ikiua watu kwa mamia. (T.L. 13/8/21 uk. 1)
186. *Wingu la moto* laendelea kuchoma makazi, misitu na kuibua taharuki (Clovis, Amerika, jimbo la California) (T.L. 12/9/21 uk. 5)
187. Covid: Kenya yapuuza *moto*. (T.L. 29/10/21 uk. 2)
188. Mapuuza ya wakazi tishio katika *vita* vya kukabiliana na Corona (T.L. 11/8/21 uk. 4)

189. Tujihadhari hili *zimwi* la matumizi ya pufya lisitumeze (T.L. 3/8/21 uk. 6)

Mifano ya 181, 182 na 183 inatumia sitiari kulinganisha 'nzige' na 'jeshi' linalovamia adui. Dhana 'jeshi' inatumiwa kujenga taswira ya wapiganaji wengi na pia waliojihami kwa zana za kuua au kuharibu. Hali hii inaashiria madhara ya uvamizi wa wadudu hao waharibifu. Katika mifano ya 184, 185 na 186 neno 'wingu' limetumiwa kujenga taswira ya idadi kubwa iliyotanda angani kuelekea eneo la uvamizi. Hali hii inaonyesha kuwa nzige hupaa angani kwa wingi wanapoelekea eneo wanalokusudia kuvamia. Vilevile ugonjwa wa Corona ulienea maeneo mengi nchini sawa na wingu la maangamizi lililofunika taifa zima. Kwa upande mwingine moto mkubwa unaochoma eneo kubwa unaweza kurejelewa kama wingu la moto kuashiria ukubwa wake. Kimsingi, katika mfano wa 186, moto unalinganishwa na wingu kuonyesha ukubwa wake. Moto huo mkubwa ulioteketeza msitu mkubwa ulitanda angani kama wingu. Msingi wa ulinganishi wa moto na wingu ni ukubwa wa moto huo uliosababisha uharibifu mkubwa. Katika mfano wa 187, ugonjwa wa Covid-19 unalinganishwa na moto. Sifa za moto kuteketeza kwa kasi zinakuwa msingi wa ulinganishi wa ugonjwa huo unaombukizwa na kuua kwa kasi. Hii ina maana kuwa mwanahabari anatoa tahadhari kwa serikali kuwa kupuuza Corona ni sawa na kuupuza moto unaosambaa kwa kasi. Mfano wa 188 unalinganisha juhudi za kukabiliana na ugonjwa wa Corona na vita. Katika mfano huo, madaktari wanalinganishwa na wanajeshi ilhali janga la Corona linalinganishwa na adui vitani. Msingi wa ulinganishi ni ule wa makabiliano baina ya mpiganaji vita na adui yake. Katika mfano wa 189 matumizi ya pufya au dawa za kututumua misuli miongoni mwa wanariadha yanalinganishwa na 'zimwi' linaloangamiza au kuua kuonyesha madhara yake. Matumizi ya sitiari katika matini za

kimazingira yalikusudia kujenga taswira ya kile kilichosimuliwa akilini mwa wasomaji na wakati huohuo kuifanya lugha ya masimulizi kuwa na mvuto mkubwa kwa wasomaji.

#### 4.3.3.2.3 Matumizi ya Maswali ya Balagha

Maswali ya balagha ni mbinu ya matumizi ya maswali ambayo hayajibiwi kwa kuwa majibu yake yako wazi au kwa nia ya kuchochea fikira au hisia kwa upande wa msomaji au msikilizaji. Maswali ya balagha ni mbinu muhimu katika sanaa ya usemaji au uandishi wa habari (Conboy, 2010). Katika matini za kimazingira, katika gazeti la *Taifa Leo* wanahabari walitumia maswali ya balagha kuchochea hadhira kutafakari kuhusu matukio yaliyosimuliwa. Vichwa vya habari vilitumia mtindo wa kibalagha kuvuta makini ya wasomaji kwa matini husika. Mifano ifuatayo inayohusu matumizi ya maswali ya balagha ilikusanywa kutoka kwa matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo*:

190. Wapi chakula? (T.L. 1/5/21 uk.1)
191. Je, nzige hawa ni laana iliyotoka kwa Mungu? (T.L. 3/12/21 uk. 4)
192. Je, bora mitishamba? (T.L. 22/2/22 uk. 4)
193. Tutawahi kujifunza? (T.L. 19/7/21 uk.2)
194. Tutajifunza lini? (T.L. 19/7/21 uk. 1)
195. Kafyu ya nini na ushuru juu? (T.L. 28/9/21 uk. 10)
196. Mbona kuongeza kafyu ilhali ni wanasiasa wanaopepeta Covid? (T.L. 7/10/21 uk. 10)
197. Utoaji chanjo ya HPV nchini wasuasua, kunani? (T.L. 25/1/22 uk. 15)

Mfano wa 190 unalenga kuvuta makini ya msomaji kwenye tukio la uhaba wa chakula nchini. Hili ni tatizo lililokera wakazi wengi nchini. Mwandishi anauliza msomaji swali ambalo wakazi wa Kwale, Mombasa wanauliza kuhusu kutoweka kwa chakula cha msaada kilichotolewa kwa ajili ya wahanga wa njaa. Chakula hicho pamoja na mamilioni ya pesa kiliporwa na maafisa wa serikali waliosimamia ugavi huo. Kwa kutumia swali lisilohitaji jibu la moja kwa moja, mwanahabari anafanikiwa kumchochea msomaji kutafakari kuhusu

kero hilo la njaa Kwale na kumpa ari ya kusoma makala ili apate jibu. Mfano wa 191 unaashiria matumizi ya swali la balagha linaloonyesha kinaya. Mwanahabari anamchochea msomaji kutafakari kuhusu chanzo cha janga la uvamizi wa nzige ambacho huenda asikijue. Swali hili la balagha linakusudia kuvuta makini ya msomaji kuhusu janga la uvamizi wa nzige linalokabili taifa. Swali la balagha katika mfano wa 192 linarejelea ubora wa mitishamba katika utabibu wa magonjwa. Mwanahabari anawachochea wasomaji kutafakari kuhusu matumizi ya tiba za kiasili kutibu na kuzuia ugonjwa. Mifano ya 193 na 194 inaakisi maswali ya balagha yanayochochea msomaji kutafakari kuhusu wizi hatari wa petroli kutoka kwa trela zilizopata ajali barabarani. Wizi huo husababisha maafa na uharibifu wa mazingira.

Mifano ya 195 na 196 inadadisi umuhimu wa kafyu katika kuzuia maambukizi ya Corona ilhali gharama ya maisha imepanda na wanasiasa wanendelea kukiuka masharti ya kafyu yenyewe. Kwa upande mwingine, mfano wa 197 unasaili hali ya kusuasua kwa wananchi kupata chanjo ya kuzuia maambukizi ya saratani ya HPV. Tunaweza kuhitimisha kuwa, wanahabari walitumia maswali ya balagha kuchochea hadhira kutafakari kuhusu matukio yaliyosimuliwa. Aidha, vichwa vya habari vilitumia mtindo wa kibalagha kuvuta makini ya wasomaji kwa matini husika ili asome makala nzima.

**4.3.3.2.4 Matumizi ya Methali**

Methali ni msemo wa kimapokeo unaokumbukika na wenye muundo fulani unaotambulika na wanajamii na unaoelezea uzoefu unaokubalika na wanajamii kama ukweli fulani. Methali zinaweza kutumiwa na mwandishi kama ishara muhimu katika uchanganuzi na ufafanuzi wa kazi za fasihi. Hii ina maana kuwa methali zinaweza kudokeza dhamira ya

mwandishi katika kutunga kazi ya fasihi (Wamitila, 2007). Hali hii huonekana bayana methali inapotumiwa kwenye anwani za matini zilizotungwa. Mifano ifuatayo ya matumizi ya methali katika matini za kimazingira ilikusanywa kutoka kwa gazeti la *Taifa Leo*:

198. CORONA: Mwenye macho aone... (T.L. 5/2/21 uk. 5)
199. MGENI NJOO: watalii wafurika mbuga ya Maasai Mara (T.L. 20/7/21 uk. 6)
200. Haba na haba hujaza kibaba: wahanga wa mafuriko wapata msaada (T.L 16/5/21 uk. 8)
201. PENYE NIA PANA NJIA: wakazi wafunzwa kuepuka wanyamapori (T.L 6/10/21 uk. 4)

Mfano wa 198 unaakisi methali ‘mwenye macho haambiwi tazama’ iliyodokezwa katika kichwa cha habari kumaanisha kuwa wananchi wenyewe wanaweza kujionea athari za ugonjwa wa Corona katika jamii zao hata bila kufahamishwa. Methali hii imetumika kimaksudi kutahadharisha umma kuhusu madhara ya ugonjwa wa Corona uliouwa watu wengi. Mfano wa 199 pia unatumia methali: ‘mgeni njoo mwenyeji apone’ iliyodokezwa kuonyesha hali ya afueni inayoshuhudiwa katika sekta ya utalii baada ya watalii wa kigeni kufika kwa wingi katika mbuga ya Maasai Mara. Ujio wa watalii uliinua sekta ya utalii iliyokuwa imedumazwa na ugonjwa wa Corona. Mfano wa 200 unadhihirisha matumizi ya methali ‘haba na haba hujaza kibaba’ inayomaanisha kuwa kitu kikiongezwa kidogo kidogo hatimaye hufanyika kuwa kingi. Hali hii inamaanisha kwamba waathiriwa wa mafuriko wanaendelea kupata msaada polepole kwa wahisani ambao unaimarisha hali yao ya maisha.

Mfano wa 201 unabainisha matumizi ya methali ‘penye nia pana njia’ inayotumika kuonyesha juhudi za wenyeji wanaoishi karibu na mbuga za wanyama. Haya yanatokea baada ya wenyeji kufundishwa mbinu mpya za kuishi bila uhasama na wanyama hao baada ya kupokea mafunzo kutoka kwa Shirika la Wanyamapori. Kimsingi, tunaweza

kuhitimisha kuwa matumizi ya methali katika vichwa vya habari katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* ni ishara muhimu inayotumiwa na wanahabari. Methali hizo huwadokezea wasomaji wao ujumbe muhimu ulio katika matini bila kuwafichulia wazi bali kwa kuwachochea kusoma zaidi ili kupata ujumbe huo.

#### 4.3.3.2.5 Matumizi ya Tashhisi

Tashhisi ni mbinu ya kisanaa ya kuvipa vitu visivyo na uhai sifa za kiuhai yaani vitu hivyo vinaweza kuwa hai na kutenda anavyofanya binadamu (Wamitila, 2007). Katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo*, tashhisi ilitumiwa kuyafanya majanga ya kimazingira yaonekane kama binadamu aliye na uwezo wa kudhulumu, kuharibu au hata kuangamiza kabisa. Kwa njia hiyo wanahabari walifanikiwa kutoa athari ya kihisia iliyokusudiwa kwa hadhira kama vile huzuni, kichomi au huruma. Mifano ifuatayo ya matumizi ya tashhisi ilikusanywa kutoka katika matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo*:

202. Tetemeko la ardhi *limeiporomosha* Haiti kiuchumi, Waziri Mkuu asema. (T.L. 20/8/21 uk. 5)
203. Tetemeko kubwa *lapiga* Haiti na kuua 700 maelfu wakijeruhiwa. (T.L. 16/8/21 uk. 8)
204. Tetemeko *latikisa* Uturuki na Ugiriki na kuzua maafa. (T.L. 1/11/21 uk. 5)
205. Mafuriko *yaua* 7 *yaacha* mamia kwenye kibaridi. (T.L 4/5/21 uk 4)
206. Watu saba waaga dunia mafuriko *yakiponda* nchi. (T.L. 4/5/21 uk. 1)
207. Shule 10 *zamezwa* na mafuriko (T.L. 24/7/21 uk.2)
208. Corona *yafagia* asilimia 35 ya biashara ndogo. (T.L. 3/12/21 uk. 3)
209. Corona *yaponda* miji na vijiji. (T.L. 25/7/21 uk. 4)
210. Mlipuko 2020 *waletea raia* umaskini (Beirut, Lebanon) (T.L. 30/7/21 uk. 6)
211. Umasikini *wasukuma* wavuvi katika bahari hatari (T.L. 26/8/21 uk. 4)

Mifano ya 202, 203 na 204 inahuisha janga la kimazingira la tetemeko la ardhi ambalo linaelekewa kuwa lilitiksa mataifa ya Uturuki, Ugiriki na Haiti. Taswira inayoibuliwa

kupitia kwa matumizi ya vitenzi 'tikisa', 'poromosha' na 'piga' ni ile ya kitu kinachosukumwa upandeupande kwa nguvu hadi kikavunjika vipandevipande. Kwa njia hii mwanahabari anafanikiwa kutoa picha ya uharibifu na madhara ya tetemeko la ardhi. Mfano wa 205 unaakisi matumizi ya kitenzi 'ua' kinachoonyesha uharibifu wa mafuriko yaliyosababisha vifo vya watu saba na kuwaacha mamia bila makao. Mfano wa 206 unatoa picha ya uharibifu unaosababishwa na mafuriko kupitia kwa matumizi ya kitenzi 'ponda'. Msomaji anapata taswira ya kitu kilichowekwa kwenye kinu na kugongwa kwa nguvu kwa kutumia mchi. Madhara ya mafuriko yanalinganishwa na hali ya kuponda kitu kwenye kinu. Mfano wa 207 unatoa madhara ya mafuriko kwa kuyalinganisha na mtu anayemeza kitu. Kupitia kwa matumizi ya kitenzi 'meza' uwezo wa mafuriko wa kuharibu shule 10 unaonyeshwa na mwandishi wa matini. Mfano wa 208 unasawiri ugonjwa wa Corona kama ulio na uwezo wa 'kufagia' biashara. Hali hii inaonyesha madhara ya Corona katika sekta ya uchumi.

Mfano wa 209 unabainisha taswira ya mtu mkatili anayedhulumu wengine akitumia hali zinazosababisha uchungu mwilini. Ugonjwa wa Corona unasawiriwa kama ulio na uwezo wa kutesa. Uwezo wa Corona wa kudhuru binadamu kwa kumsababishia machungu kiafya unabainika wazi kupitia kwa matumizi ya kitenzi 'ponda'. Mfano wa 209 unatoa taswira ya madhara ya ugonjwa wa Corona ambao unaonyeshwa kuwa na uwezo wa 'kuponda' mtu. Kuambukizwa, kuugua na hata kufa kwa Corona kunaakisiwa kama 'pigo' linalotokana na kupondwa na ugonjwa wenyewe. Katika mifano ya 210 na 211 majanga ya mlipuko na umaskini yanahuishwa ili kuonyesha athari zake katika maisha ya binadamu. Matumizi ya tashhisi katika matini hizo za kimazingira zinazoonyesha madhara ya majanga ya kimazingara yanakusudiwa kuathiri hadhira kwa njia inayokusudiwa na mwandishi.

Katika matini husika majanga hayo yanasawiriwa kuwa na uwezo wa kutikisa, kutesa, kugonga, kuponda na kuua. Vitenzi hivi vinavyoelezea vitendo vya kidhalimu vinalenga kuibua hisia za huzuni na huruma.

#### 4.3.3.2.6 Matumizi ya Kinaya

Kinaya ni mbinu ya kisanaa inayotokea katika kazi ya matini pale ambapo maneno yanayotumiwa yanaelekea kukinzana na fahiwa au maana inayohitajika katika muktadha maalum na ile inayokusudiwa na msomaji au mtumiaji lugha (Wamitila, 2007). Kinachozungumziwa katika matini yenye kinaya huwa kinakinzana kimaana na matarajio ya wasomaji wa makala. Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka kwa matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* inaonyesha matumizi ya kinaya:

212. Kinaya Naibu wa Rais akishtushwa na njaa (T.L. 19/10/21 uk. 4)
213. Serikali na wajitia hamnazo njaa ikiua wakazi Marsabit. (T.L. 24/1/22 uk. 13)
214. Kaunti ya Kwale inayokabiliwa na njaa yaonya wanaoiba chakula cha msaada. (T.L. 4/5/21 uk 4)
215. Wapi chakula? (...raia maskini wapika mawe na kutafuna mizizi licha ya wahisani kutoa chakula na mamilioni ya pesa.) Mombasa(T.L. 1/5/21 uk. 1)
216. Chakula tele mamilioni wakifa njaa (T.L. 15/9/21 uk. 2)
217. Walafi wauza chakula cha msaada njaa ikikeketa raia. (T.L. 15/10/21 uk. 3)
218. Hofu ya maambukizi mapya ya Covid-19 barakoa feki zikifurika nchini. (T.L. 24/2/21 uk. 2)
219. Mradi wa kurembesha jiji wageuka jaa la taka. (T.L. 15/2/21 uk. 3)

Mifano ya 212, 213, 214, 215, 216 na 217 inaonyesha kinaya kwa sababu maeneo mengi nchini yanayokabiliwa na janga la njaa yalipokea msaada wa pesa na chakula kwa ajili ya kuwagawia wahanga wa janga hilo lakini fedha na chakula hicho kikaporwa na maafisa wa serikali. Waandishi wa makala wanatumia kinaya kuwakejeli viongozi wa kisiasa pamoja na maafisa wa serikali waliopewa majukumu ya kutoa msaada na kugawa chakula hicho

lakini badala yake wanazembea na kupora msaada wenyewe. Kwa kuwakejeli maafisa hao, waandishi wa makala wanahimiza uwazi na uwajibikaji miongoni mwa wale wanaotwikwa jukumu la kuwawajibikia wahanga wa janga la njaa. Mfano wa 218 unaonyesha matumizi ya kinaya kukashifu uuzaji wa barakoa bandia uliofanywa na wafanyabiashara wenye tamaa ya kupata faida kubwa ambao walihatarisha maisha ya wananchi waliotishiwa kuambukizwa Corona. Ni kinaya kuwa binadamu anaweza kuthamini pesa kuliko maisha ya binadamu mwenzake. Mfano wa 219 unatumia kinaya kukashifu miradi ya serikali isiyo endelevu na ambayo hukwama kutokana na uhaba wa fedha za kuikamilisha. Kitika mifano iliyotolewa, kinaya kinatumika kama njia inyotumiwa na wanahabari kukashifu vitendo vinavyohujumu mzingira na wakati huohuo kuelimisha jamii kuhusu maadili.

**4.3.3.3 2.7 Uradidi**

Hii ni mbinu inayorejelea urudiaji wa maneno au sauti fulani kwa lengo la kusisitiza jambo linalozungumziwa katika matini. Urudiaji unaojitokeza katika matini za taarifa za habari ni ule ulio rahisi kutambulika. Urudiaji sahili unahusu neno au msamiati fulani kwa lengo la kusisitiza ujumbe husika. Urudiaji wa neno au msamiati unaohusiana na sajili fulani unaweza kuangaliwa kwa namna mbili (Wamitila, 2007). Namna ya kwanza ni pale ambapo neno fulani lenye dhima maalum hurudiwarudiwa katika matini husika. Mfano mzuri ni maneno **Corona**, **mafuriko** na **nzige** ambayo yanapatikana kwa wingi na kurudiwarudiwa katika magazeti ya *Taifa Leo* yaliyochapishwa mwaka wa 2021. Majanga hayo ya kimazingira yaliripotiwa kila siku katika gazeti la *Taifa Leo*. Namna ya pili ya urudiaji sahili ni pale ambapo neno linarudiwa kwa kuzingatia kisawe chake katika matini hiyohiyo kwa mfano matumizi ya neno ‘Corona’ na ‘Covid-19’ katika matini za

kimazingira kusisitiza janga hilo. Kuna urudiaji ambao unahusu neno moja kurudiwa katika sentensi ili kusisitiza ujumbe fulani kwa mfano:

220. Raia njaa *tu*, vigogo nao siasa *tu*! (T.L. 3/2/21 uk. 2)
221. *Hali* si *hali*: maziwa yazidi kufurika Rift Valley. (T.L. 31/10/21 uk. 1)
222. *Haba* na *haba* hujaza kibaba: wahanga wa mafuriko wapata msaada (T.L 16/5/21 uk. 8)
223. Corona: Siku*kuu* kuwa tishio *kuu* (T.L. 22/12/21 uk. 8)

Katika mfano wa 220 kihisishi '*tu*' kinarudiwa ili kusisitiza hali zinazoendelea kwa muda. Kinachobainika hapa ni kuwa, mwanahabari anashangazwa na hali ya raia kuendelea kuteseka kwa njaa huku viongozi wao wakiendelea kupiga siasa. Mfano wa 221 unabainisha marudio ya neno 'hali' katika kauli '*hali si hali*' inayoashiria ugumu wa maisha unaotokana na kufurika kwa maziwa Baringo na Bogoria. Kauli 'hali si hali' hutumiwa katika mazungumzo ya kawaida kuonyesha kudhoofika kwa mambo kutoka kwa 'hali mbaya' hadi kuwa 'mbaya zaidi'. Kinachosisitizwa ni kuongezeka kwa mafuriko yanayoathiri maisha ya wakazi wa maeneo ya maziwa hayo. Mfano wa 222 unabainisha kurudiwa kwa neno 'haba' katika methali 'haba na haba hujaza kibaba' kumaanisha kuwa wahanga wa mafuriko wanapata msaada kidogo kidogo unaoimarisha hali yao ya maisha. Mfano wa 223 unaakisi marudio ya neno 'kuu' kuonyesha jinsi mwanahabari anavyotumia lugha kisanaa kupitia kwa mchezo wa maneno. Lengo la mchezo huo wa maneno ni kuonyesha ukinzani uliopo kati ya kusherehekea sikukuu ya Krismasi na hofu ya maambukizi ya Corona kuzidi msimu huo wa Krismasi.

Kimsingi, urudiaji katika matini za kimazingira ulitumiwa na wanahabari kwa nia ya kushadidi au kusisitiza kinachozungumziwa. Katika hali hiyo, maneno fulani yalirudiwa katika matini ili kutoa ujumbe fulani kwa mfano kuhusu utunzaji wa mazingira. Aidha, maneno yenye umuhimu wa kimawasiliano yalirudiwa ili kutoa athari ya kihisia katika

hadhira. Kwa mfano urudiaji wa neno 'mafuriko' uliibua hisia za huzuni kwa wahanga walioathiriwa na janga hilo. Urudiaji huo ulinuiwa kueleza hisia za mwanahabari kuhusu janga la kimazingira lililowasibu wanajamii. Aidha, urudiaji ulikusudiwa kuibua hisia za huzuni, ghadhabu, chukizo au furaha miongoni mwa wasomaji kutegemea ujumbe uliowasilishwa na waandishi wa makala.

### 4.3.4 Sifa za Kiusemi

Hizi ni sifa za kidiskosi zinazotumiwa katika uchunguzi wa kiisimumatini kueleza jinsi mshikamano na muwala unavyobainika katika matini. Isimumatini huchunguza matini andishi kwa lengo kutathmini jinsi matini hizo zinavyotoa maana pamoja na zana za kiisimu zilizotumiwa na waandishi ili kuwasilisha maana wanazokusudia katika matini zao (Halliday & Hasan, 1976). Katika utafiti huu sifa za kiusemi zilizochunguzwa katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* ni zile za mshikamano na muwala. Sifa hizo zimefafanuliwa kwa kina katika sehemu inayofuata.

#### 4.3.4.1 Mshikamano

Mshikamano ni istilahi inayotumiwa kueleza uhusiano wa maana uliopo katika matini. Kwa mujibu wa maelezo ya Halliday na Hasan (1976) ushikamano katika matini huwepo iwapo ufasiri wa baadhi ya vipengele vya usemi unategemea vipengele vingine katika matini hiyo. Halliday na Hasan ( *wametajwa* ) wanaendelea kufasiri mshikamano kuwa ile hali ya uwezekano iliyopo katika lugha kwa ajili ya kufanya matini kuungana pamoja: yaani uwezo alio nao msemaji au mwandishi ili autumie katika mawasiliano yake. Hivyo, mshikamano kama mchakato daima unahusisha kipengele kimoja kuzungumzia kingine,

ambapo, sifa kuu ya uhusiano wa kiushikamano ni ukweli kwamba kipengele kimoja huwa chanzo cha kufasiri kipengele kingine.

Mshikamano hutokea katika hali inayoonyesha kwamba udhihirikaji wa kipengele kimoja ni dhanaawali ya kipengele kingine. Hii ina maana kuwa kipengele kimoja hakiwezi kueleweka au kufasiliwa vyema bila ya kuwa na ufahamu mzuri kuhusu kipengele kingine kilichotangulia. Mshikamano katika matini huonyeshwa kwa njia ya mahusiano ya urejelezi (Flowerdew & Mahlberg, 2009). Hili linamaanisha kuwa vipengele vinavyorejelea vipengele vingine hutumiwa ili kuashiria mshikamano katika matini. Mshikamano huashiriwa kupitia kwa matumizi ya vipashio vya kisarufi na vile vya kileksia katika matini. Katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* kuna maneno, vishazi na vifungu vya maneno kurejelea maneno na vifungu vingine katika matini moja iliyokuwa inasimuliwa. Utafiti huu ulitumia mifano ifuatayo kuonyesha jinsi hali ya mshikamano inavyojitokeza katika matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo*:


MAKALA MAALUM

# Ukataji wa miti asili unavyotishia kupotea kwa dawa za mitishamba

*Kilelezo 7*: Makala kutoka safu ya ‘Makala Maalum’, *Taifa Leo,* Machi 23, 2022 uk. 10

Mshikamano wa kiusimulizi au kimatukio hutokea katika matini pale ambapo tukio fulani linafuatwa na jingine kwa namna ambayo ina mantiki na inakubalika kwa msomaji wa matini (Halliday & Hasan, 1976). Katika makala inayorejelewa katika kielelezo cha 7 mwanahabari anaanza kwa kutaja matumizi ya tiba za asili tangu zamani kisha anaelekea jinsi yanavyobainika katika Kaunti ya Nandi. Kuna mshikamano wa kiusimulizi mwanahabari anapoeleza changamoto zinazokabili matumizi ya tiba za kiasili kwa mfano kuharibiwa kwa misitu ya kiasili pamoja na upanzi wa miti ya *bluegum* na *cypress*. Baadaye anasimulia kuhusu maeneo katika Kaunti ya Nandi ambako misitu ya kiasili iliyo na mitishamba inapatikana. Maeneo hayo ni Kipkurere, Serongonik, Ng’atibkong, Kipsamoite na King’wal.

Mshikamano wa kimantiki hudhihirika katika matumizi ya lugha yanayoonyesha mfuatano wa sentensi wenye mantiki. Aidha, hali hii hutokea tunapochunguza usimulizi wa matini na jinsi unavyotekelezwa katika makala inayochunguzwa (Halliday & Hasan, 1976; Flowerdew & Mahlberg, 2009). Kuna mantiki katika mfuatano wa masimulizi yanayohusu utunzaji wa miti ya kiasili inayotumiwa kama mitishamba kutibu magonjwa. Mwanahabari anafafaunua matukio yanayohusu maeneo yaliyo na misitu ya kiasili inayohifadhiwa na serikali ili kutunza miti ya kiasili. Masimulizi yake yanaelekea kwenye changamoto zinazowakabili matabibu wanaotegemea miti ya kiasili kutibu magonjwa katika Kaunti ya Nandi. Miongoni mwa changamoto hizo ni kutoweka kwa miti ya tiba za kiasili kwa mfano *Murguiyet* (Anacanthecea) ambao majani yake hutumiwa kutibu kikohozi na magonjwa ya ngozi. Hatimaye masimulizi yanaelekea kwenye juhudi zinazofanywa na serikali kutunza misitu yenye miti ya kiasili dhidi ya ukataji ovyo. Kuna mshikamano wenye mantiki katika usimulizi wa matukio ya utunzaji wa misitu ya kiasili katika Kaunti ya Nandi.

Mshikamano wa kiusemi hujengwa kwenye kaida ya mfuatano wa matukio katika matini, yaani baada ya tukio hili linafuta lile. Mfuatano huo huelezeka kwenye mada fulani bayana au dhamira inayokuzwa na kazi husika (Halliday & Hasan, 1976; Flowerdew & Mahlberg, 2009). Lugha inayotumiwa katika matini ina mpangilio mahususi wa sentensi na vipashio vyake. Mpangilio huo ndio unaojenga mshikamano wa kisintaksia katika matini. Katika matini inayorejelewa katika kielelezo cha saba sentensi zinazotumika zina uhusiano wa karibu unaoonyesha jinsi zinavyopangwa kimuundo kwa utaratibu utakaomwezesha mwanahabari kusimulia matukio yanayohusu matumizi ya dawa za asili katika tiba, changamoto za utowekaji wa dawa hizo, maeneo yenye misitu ya asili ambayo ndicho

chanzo cha dawa zenyewe na hatimaye juhudi zinazofanywa na serikali kutunza na kuhifadhi misitu hiyo. Matini imegawika katika sehemu hizo mahususi.

Mshikamano wa kirejelezi hubainika katika matini yoyote inayounda taswira fulani ya ulimwengu wa kibunifu ambao unaweza kuwa umejengwa au kuundwa kwenye ulimwengu halisi. Ulimwengu huo huathiri usimulizi, uteuzi wa msamiati na ishara zinazohusika na uteuzi wa lugha. Kwa upande mwingine, mshikamano wa kisemantiki hubainikana kutokana na kuwepo kwa mfuatano mzuri wa sajili zinazotumiwa (Halliday & Hasan, 1976; Flowerdew & Mahlberg, 2009). Kwa mfano mwandishi anaanza makala kwa kuzingatia sajili ya kihistoria kusimulia asili ya matumizi ya tiba za kiasili. Anarejelea changamoto za kutoweka kwa miti ya kiasili katika kaunti ya Nandi kwa kutaja baadhi ya miti inayotishia hiyo ya kiasili kwa mfano *bluegum* na *cypress* kwa kutumia msamiati wa Kiingereza. Sajili ya kijografia inatumiwa kutaja majina ya misitu ya kiasili katika Kaunti ya Nandi. Majina haya yanatumia lugha ya Kinandi ambayo msomaji huenda asiyajue vyema. Sehemu inayofuata inazingatia sajili ya kisayansi. Baadhi ya istilahi anazotumia mwandishi wa matini husika zimekopwa kutoka kwa Kilatini na Kinandi. Majina ya miti ya kiasili iliyotoweka yanatolewa kwa lugha ya Kinandi '*murguiyet*' na Kilatini '*anacanthecea*'. Majina haya yametumika ili kurahisisha mawasiliano kwa kuepuka kutohoa au kutumia maelezo marefu. Maelezo yanayotolewa ni ya kitaaluma na yanayokusudia kumhamasisha msomaji jinsi mitishamba inavyotumika kutibu maradhi.

Mshikamano wa kimtindo hudhihirika kupitia kwa uteuzi na matumizi ya lugha na usarifu wa mbinu tofauti za lugha zinazotumiwa na mwandishi wa matini katika ujenzi na udumishaji wa maana katika matini (Halliday & Hasan, 1976; Flowerdew & Mahlberg, 2009). Mwanahabari ametumia lugha kavu, nyepesi na ya kitaaluma kumhamasisha

msomaji jinsi miti ya kiasili ilivyo muhimu katika kutibu maradhi na jinsi uharibifu wa misitu unavyotishia kuangamiza miti yenyewe.

### 4.3.4.2 Muwala

Muwala hufanya kazi pamoja na mshikamano katika matini. Muwala ni istilahi inayorejelea ule mwendelezo wa mawazo katika matini na mahusiano yaliyopo kati ya mawazo hayo (Halliday & Hasan, 1976). Wasomaji huelewa ujumbe kwenye matini endapo sentensi, mawazo, na maelezo yanayotolewa yanaingiliana pamoja kwa njia iliyo wazi. Hii ina maana kuwa wasomaji wanaweza kufuata kinachoelezwa kwa urahisi. Matini andishi huwa na muwala madhubuti iwapo mawazo yanafungamana pamoja vizuri na kwa uwazi. Isitoshe, matini huwa na muwala iwapo mawazo yake yataonekana kutegemeana kiasi cha kwamba matini nzima kwa ujumla itawasilishwa kama kitu kimoja kikamilifu. Muwala ni zaidi ya muungano wa sentensi; yaani, ni ukamilifu wa wazo zima kwenye matini. Mshikamano na muwala, ndizo njia za msingi zinazoashiria kuwepo kwa umatini. Utafiti huu ulitumia matini inayorejelewa katika kielelezo cha 8 kuchunguza kuwepo kwa muwala katika matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo*:


MAKALA MAALUM

Eneo la kutupia taka lililo hatari kwa wakazi wa Kisii

*Kilelezo 8*: Makala kutoka safu ya 'Makala Maalum', *Taifa Leo*, Machi 28, 2022 uk. 10

Matini katika kielelezo cha 8 inadhihirisha kuwa na muwala madhubuti kutokana na mawazo yanaliyofungamana pamoja vizuri na kwa uwazi. Matini inatumia lugha nyepesi, sahili na yenye mtiririko wa moja kwa moja. Kiini cha matini ni madhara ya kimazingira yanayotokana na jaa la taka la Nyambera lililoko katika kaunti ya Kisii. Makala yanaanza kusimulia kuhusu jaa lenyewe lililopo mjini Kisii, kero zinazotokana na kuwepo kwake pamoja na shughuli za uchimbaji mawe ya kokoto karibu na jaa lenyewe. Masimulizi yanatolewa kwa kurejelea ripoti ya utafiti uliofanywa na watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kisii na kuchapishwa katika jarida la kimataifa kuhusu madhara ya jaa hilo kwa mazingira.

Isitoshe, matini ya kielelezo cha 8 ina muwala kutokana na mawazo yake kuonekana kutegemeana kiasi cha kwamba matini nzima kwa ujumla inawasilishwa kama kitu kimoja kikamilifu. Matini tunayoichunguza ilizingatia wazo moja ambalo ni athari za uchafuzi wa mazingira unaookana na jaa la taka la Nyambera. Athari tatu ambazo ni uchafuzi wa mto Nyakomisana, uchafuzi wa mfumo wa ikolojia pamoja na kero za jumla kwa wakazi zinazotokana na jaa hilo kuwa hatari kwa afya na maisha yao zinasimuliwa kwenye matini. Matini inaanza kwa kusimulia kuhusu jaa lenyewe lililopo na jinsi lilivyo kero na hatari kwa maisha ya wakazi wa Kisii mjini. Matini inasimulia athari za jaa hilo katika uchafuzi wa mto ulio karibu kwa madini hatari ya *zinc*, c*oppe*r na *cadmium*. Masimulizi yanarejelea makala ya kitaaluma ya watafiti kutoka chuo Kikuu cha Kisii. Kuna masimulizi kuhusu ukosefu wa sera madhubuti za kuzuia uchafuzi wa mazingira katika Kaunti ya Kisii. Matini inahitimisha kwa kuzungumzia juhudi zinazofanywa na serikali pamoja na Kaunti ya Kisii katika kupambana na janga la utupaji taka na uhifadhi wa mazingira mjini. Wito unatolewa kwa serikali pamoja na uongozi wa Kaunti kuliondoa jaa hilo na kulihamisha kabisa ili

kuwaondolea wakazi kero hizo. Hali hii inadhihirisha kuwa muwala ni zaidi ya muungano wa sentensi; yaani, ni ukamilifu wa wazo zima kwenye matini. .

### 4.4 Ujumbe Ulioibuliwa Kutokana na Matumizi ya Lugha katika Kuwasilisha Habari za Mazingira katika Gazeti la *Taifa Leo*.

Sehemu hii inafafanua aina za jumbe ambazo ziliibuliwa kutokana na matumizi ya lugha katika kuripoti habari za mazingira kwa kuzingatia mitindo mbalimbali. Aidha, dhima inayotekelezwa na ujumbe wa kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* imeelezwa.

#### 4.4 1 Aina ya Ujumbe Ulioibuliwa Kutokana na Matumizi ya Lugha katika Kuwasilisha Habari za Mazingira katika Gazeti la *Taifa Leo*.

Utafiti huu ulibainisha kwamba kuna aina tofauti za jumbe ambazo ziliibuliwa wanahabari walipoteua lugha ili kueleza habari za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Baadhi ya jumbe za kimazingira zilizojitokeza katika matini zilizochambuliwa ni:

i) Ujumbe wa kimazingira wenye maana dhamirifu

ii) Ujumbe wa kimazingira wenye maana akisifu

iii) Ujumbe wa kimazingira wenye maana athirifu

iv) Ujumbe wa kimazingira wenye maana kimtindo

v) Ujumbe wa kimazingira wenye maana halisi

vi) Ujumbe wa kimazingira wenye maana ashirifu.

#### 4.4.1.1 Ujumbe wa Kimazingira wenye Maana Dhamirifu

Maana dhamirifu hujulikana pia kama maana ya kimatini. Maana dhamirifu hudhihirika kutegemea jinsi ujumbe unaowasilishwa katika lugha ulivyopangwa au kuratibiwa. Kimsingi ni kwamba maana dhamirifu inahusu upangaji wa vipengele vya kimawasiliano ambavyo huamua maeneo yanayosisitizwa. Upangaji huo hutegemea umuhimu wa mada, kiini na msisitizo (Cruse, 2010). Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka gazeti la *Taifa Leo* inabainisha matini zenye kuwasilisha maana dhamirifu za kimazingira:

| | | |
|---|---|---|
| 224. | *Njaa* yazuia mamia ya watoto kufika shuleni | (T.L. 18/8/21 uk. 4) |
| 225. | *Asilimia 10* huenda choo vichakani. (Homabay) | (T.L. 12/8/21 uk. 4) |
| 226. | *Hofu tele* nzige wakirejea Taita | (T.L 22/11/21 uk. 4) |
| 227. | *Jeshi la nzige* lavamia ardhi meneo ya Samburu | (T.L 22/11/21 uk. 4) |
| 228. | *Wafugaji wa msitu Boni* walalamikia kusumbuliwa na mbung'o wanaoleta maradhi (Lamu) | (T.L. 12/8/21 uk. 5) |
| 229. | *Wanafunzi* wazimia shuleni kwa njaa | (T.L. 27/8/21 uk. 3) |
| 230. | *Hofu* vimbunga vikiua watu 100 (New Yolk) | (T.L. 13/12/21 uk. 8) |

Kimsingi mada za mifano ya hapo juu zinadhihirisha ujumbe unaohusiana na masuala ya kimazingira na ambao unakusudiwa kutimiza dhamira fulani. Hata hivyo, kiundani kuna tofauti ya maana kutegemea mpangilio wa mada na kiini. Katika mfano wa 224 msisitizo upo kwenye njaa inayowazuia wanafunzi kwenda shuleni. Mwandishi wa makala angekuwa na dhamira tofauti huenda angesisitiza kitendo cha wanafunzi kutoenda shuleni. Katika mfano wa 225 msisitizo upo kwenye idadi ya watu wala sio kwenye kitendo cha uharibifu wa mazingira cha kwenda haja vichakani. Katika sentensi ya mfano wa 226 msisitizo unatiliwa kwa *Hofu tele* ilhali katika sentensi ya mfano wa 227 msisitizo upo kwenye wingi wa nzige waliovamia ardhi ambao wanarejelewa kama *jeshi la nzige*. Katika mifano yote ya 228, 229 na 230 msisitizo upo kwenye wafugaji kwenye msitu wa Boni, wanafunzi na hofu ya kimbunga mtawalia; hata hivyo, mada inayorejelewa ni ileile moja

kuhusu suala ya kimazingira. Licha ya tofauti ya msisitizo, kiini cha maana inayodhamiriwa kutimiza lengo la maana inayojitokeza katika matini. Kwa ujumla, lugha huteua na kupanga maneno kutegemea nini hasa kinachosisitizwa (Griffiths, 2006). Katika matini za kimazingira kilichosisitizwa ni majanga yaliyohusika, athari za majenga yenyewe au ujumbe muhimu uliotolewa na mwanahabari. Katika matini hizo, msisitizo wa taarifa za kimazingira unadhihirika kupitia sifa mbalimbali za kigrafolojia kama vile matumizi ya herufi kubwa, hati za mlazo au kupigia mstari maneno pamoja na matumizi ya wino uliokolezwa rangi nyekundu.

#### 4.4.1.2 Ujumbe wa Kimazingira wenye Maana Akisifu

Maana akisifu hujulikana pia kama maana zalishi au maana fumano. Kimsingi, maana akisifu inahusiana na kauli ambazo zina maana nyingi au mseto wa maana. Maneno yenye maana nyingi au maneno ya kipolisemi huwa na maana akisifu (Cruse, 2010). Hata hivyo, huwa kuna maana kuu miongoni mwa maana mbalimbali zinazojitokeza. Hii ina maana kuwa kuna fahiwa fulani ya neno inayotamalaki ambayo hutawala fahiwa nyingine za neno hilo. Fahiwa zinazotawaliwa hufifia muda unapoendelea kuyoyoma na hatimaye hutoweka kabisa (Saeed, 2009). Kwa mfano neno ‘posho’ lilimaanisha chakula chochote kile lakini sasa linamaanisha marupurupu anayopewa mtu kwa ajili ya majukumu, takrima au usumbufu. Maana ya pili ndiyo inayotawala na kutamalaki ile ya awali. Maana akisifu hutokana na maana mbili au zaidi zilizobwiwa. Fahiwa moja ya neno hutuelekeza katika fahiwa nyingine (Cruse, 2010). Kwa kawaida maana moja huwa imeshika kani kimatumizi kiasi cha kwamba imehusishwa na kuzua maana zingine za ziada. Katika zama hizi za mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha magonjwa hatari kama Corona kuna istilahi za

zamani ambazo zilipata maana akisifu na maana halisia imefifia kimatumizi. Mifano ifuatayo iliyokusanywa kutoka katika gazeti la *Taifa Leo* inabainisha hali hiyo:

231. Kuzima *barakoa* kwa waacha na njaa. (T.L. 15/3/22 uk. 4)
232. *Kafyu* haisadii kudhibiti usambazi wa covid-19. (T.L. 15/5/21 uk. 8)
233. *Kafyu* inafinya ila tutadhibiti tu hili janga kila mhusika akipokea chanjo. (T.L. 8/10/21 uk. 10)
234. Covid: Waziri azima hofu ya '*lockdown*' (T.L. 16/12/21 uk. 1)
235. Walevi sugu wanya *sanitaiza* kuzima kiu. (T.L. 18/2/21 uk. 2)
236. Ufuo wa umma sasa himaya ya '*masonko*' (T.L 13/10/21 uk. 5)

Mfano wa 231 unabainisha matumizi ya istilahi '**barakoa**' ambapo zamani ilirejelea vazi la kufunika uso lililovaliwa na waigizaji ili kuafiki jukumu walilokuwa wakiigiza. Neno hili liliwanda kimaana katika zama za kuzuka kwa Corona ambapo lilitumika kwa maana ya vazi la kufunika mdomo na mapua ili kujikinga na maambukizi ya Covid-19 kutoka kwa watu walio karibu kupitia upumuaji hewa. Maana hii inatokana na kuhusisha matumizi ya vazi la uigizaji na vazi la kiafya kutokana na dhana ya Kiingereza '*mask*'. Mifano ya 232 na 233 inaakisi istilahi ya pili '**kafyu**' iliyotoholewa kutoka kwa Kiingereza yaani '*curfew*'. Zamani, neno kafyu lilimaanisha kutangazwa kwa hali ya hatari ambako kulidhibiti muda na wakati wa kutoka na kurudi nyumbani kwa ajili ya usalama. Kafyu ilitumiwa kudhibiti shughuli za watu katika eneo fulani kutokana na sababu za kiusalama. Katika zama za kuzuka kwa Corona, neno kafyu lilipata maana mpya na kurejelea hali ya serikali kuzuia watu kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine na kutangamana na watu wa maeneo mengine ili kudhibiti kuenea kwa ugonjwa wa C orona ulioambukizwa kwa kasi. Sababu kuu za kuwepo kwa kafyu katika hali hii sio za kiusalama bali za kiafya. Mfano wa 234 unaonyesha istilahi '**sanitaiza**' iliyopata maana mpya zama za maambukizi ya Corona. Awali neno hili halikutumika sana katika jamii lakini lilitumiwa katika sajili ya hospitali kurejelea dawa ya kuua viini vinavyosababisha ugonjwa ambayo ni '*sanitiser*' katika

Kiingereza. Katika muktadha wa maambukizi ya kasi ya Corona neno hilo lilitumika kwa maana hiyohiyo ya awali lakini pia kukabuniwa kitenzi 'kusanitaizi' au kutakasa mikono kwa kutumia dawa ya kuua viini vinavyosababisha Covid-19. Katika mfano wa 236 neno '**masonko**' limetumiwa kurejelea mabwenyenye wanaomiliki mali nyingi. Neno hili la msimu linatokana na jina kilakabu alilojipa aliyekuwa gavana wa jiji la Nairobi bwana Mike Mbuvi 'Sonko'.

#### 4.4.1.3 Ujumbe wa Kimazingira wenye Maana Athirifu

Maana athirifu hujulikana pia kama maana shawishi. Maana athirifu huhusiana na hisia au mielekeo ya mzungumzaji kuhusu hadhira yake au mada anayoizingatia katika mawasiliano. Maana athirifu hubainika kupitia kwa uteuzi wa maneno (Saeed, 2009). Kuna baadhi ya maneno ambayo huashiria hisia chanya kwa mfano: upendo, uzuri, furaha na bashasha. Kwa upande mwingine kuna maneno yanayoibua hisia hasi kwa mfano kero, ghadhabu, chuki na bughudha (Cruse, 2010). Vihisishi hudokeza hisia za kiakili za mzungumzaji kwa mfano: hisia za furaha: oyee, oyaa; hisia za huzuni: pole, hamadi; hisia za mshtuko: afanalek, la, lo, alaa, amaa, aisee; hisia za mshangao: aa, eti, ati, salale, ajabu, kumbe, lahaula; hisia za bezo: aka, zii, sasa.

Kuna wakati ambapo lugha hudokeza hisia na mielekeo na watumiaji kuhusu maana ya kuzungumzia. Aina hiyo ya lugha hudokeza na kutoa fununu kumhusu mshiriki. Kupitia lugha ni rahisi kubainisha mitazamo kuhusu washirika (Kearns, 2000). Lugha aidha inaweza kuonesha dharau, furaha, mshangao au hata huzuni. Hali hizi ndizo ambazo hutuelekeza katika hisia za wahusika. Aghalabu maana ya kihisia hutegemea aina nyingine za kimaana kama vile maana bwiwa, maana ziada na maana kimtindo. Mara nyingi maana

kiuathirifu hubainishwa kupitia matumizi ya viingizi au vihusishi ambavyo hutokea katika mawasiliano. Viingizi ni maneno ambayo hayana jukumu lingine lolote ila tu huibua hisi na kuathiri maana

| | | |
|---|---|---|
| 237. | Njaa yatesa licha ya serikali kutoa sh 2B! | (T.L. 30/9/21 uk. 2) |
| 238. | Corona: Nairobi kiazimoto! | (T.L. 31/3/21 uk. 1) |
| 239. | Corona yatimua watu ofisini! | (T.L. 25/3/21 uk. 3) |
| 240. | Kafyu yaanza kwa machozi! | (T.L. 8/10/21 uk. 1) |
| 241. | Raia njaa tu vigogo siasa tu! | (T.L. 3/2/21 uk. 2) |
| 242. | JOTO: Jua lawaka Mombasa! | (T.L. 10/12/21 uk 6) |

Mfano wa 327 unakusudia kuwasilisha hisia za mshangao unaoonyesha kinaya. Kwamba serikali imetoa kima cha shilingi bilioni mbili kuzuia njaa nchini lakini raia bado wanahangaishwa na janga hilo. Mfano wa 328 unadhihirisha matumizi ya neno ‘kiazimoto’ ambayo ni ya kiistiari. Jiji la Nairobi linalilanganishwa na kiazimoto ambacho kinaweza kumchoma mlaji kinywani kikiwa kingali moto. Hali hii inaonyesha kuwa jiji la Nairobi lilikuwa kitovu cha maambukizi ya Corona. Hii ndio sababu ya kutangazwa kwa kafyu katika jiji hilo na viunga vyake. Kwa kutumia kihisishi, mwandishi wa matini anatoa tahadhari kwa wasomaji wawe makini. Hisia zinazotolewa katika kauli hiyo ni zile za kutahadharisha. Mfano wa 239 unabainisha matumizi ya tashihisi ambapo Corona inapewa sifa za kibinadamu yaani uwezo wa kutimua watu kutoka ofisini. Kauli hiyo inakusudia kutoa hisia za kutamauka zinazoonyesha kuwa licha ya watu hao kutaka kubaki maeneo yao ya kazi kujikimu, haingewezekana kutokana na maambukizi ya kasi ya Corona.

Mfano wa 240 unatumia neno ‘machozi’ kitaashira kurejelea majonzi au mateso ambayo wananchi walikumbana nayo mikononi mwa polisi siku ya kwanza wakitekeleza amri ya kafyu. Watu wengi waliokaidi amri hiyo walidhulumiwa kwa kupigwa, kutiwa mbaroni na kuwekwa katika vituo vya kuzuilia walioshukiwa kuwa wameambukizwa Corona. Hisia

zinazowasilishwa ni zile za huzuni na kilio. Mfano wa 241 unakusudia kuwasilisha hisia za chukizo na kukereka kwa raia wanaoangamizwa na njaa huku wanasiasa wakiendelea na shughuli za siasa. Kwa upande mwingine, mfano wa 242 unaakisi hisia za mshangao kuhusu jua linalowaka kwa namna isiyokuwa ya kawaida na kusababisha joto jingi.

#### 4.4.1.4 Ujumbe wa Kimazingira wenye Maana Kimtindo

Maana ya kimtindo hujulikana pia kama maana ya kijamii. Maana ya kimtindo au ya kijamii hudhihirika wakati ambapo ruwaza fulani ya unenaji, aina fulani ya lugha au aina fulani ya uneni inahusishwa na muktadha mahususi wa kijamii. Ni jambo la kawaida kwamba uteuzi wa maneno na miundo ya sentensi wa mzungumzaji hudhihirisha usuli wake wa kijamii, kieneo, kijiografia na hata kiuchumi (Griffiths, 2006). Uteuzi huo unaweza pia kuthibitisha kiwango cha kufahamiana kilichopo baina ya mzungumzaji na mpokezi wa ujumbe. Msisitizo huwa kwenye mitindo mbalimbali inayotofautiana ambayo inaweza kutumiwa na mwandishi wa makala (Cruse, 2010). Mifano ifuatayo inaonyesha matini za kimazingira zenye maana za kimtindo iliyokusanywa kutoka kwa gazeti la *Taifa Leo*:

243. Wakenya njaa viongozo *wakipiga domo* (T.L 3/2/21 uk 1)
244. Kuku wa kienyeji bado *simaku* sokoni (T.L. 26/1/22 uk 17)
245. Serikali na wanasiasa *wajitia hamnazo* njaa ikiua wakazi Marsabit (T.L. 24/1/22 uk. 4)
246. Wafugaji sasa *walia kupunjwa* na serikali (T.L. 5/11/21 uk. 4)
247. Janga la njaa *njiani* kutokana na tishio la Corona duniani. (T.L. 27/3/21 uk. 3)
248. Uuaji nzige *kutoka angani* wasitishwa (Garissa) (T.L. 9/2/21 uk. 4)
249. *Njaa ya nzige* yaanza kuuma Tana River (T.L. 28/3/21 uk. 6)
250. Baadhi ya wakazi katika maeneo yaliyoathiriwa na njaa *wasubiri kifo* tu. (T.L. 30/9/21 uk. 2)
251. Covid: Kifo cha polisi *chaanika* mahangaiko (T.L. 2/9/21 uk. 4)
252. Biashara haramu *kuzimwa* Ziwani Victoria (T.L. 9/2/21 uk. 4)

Mfano wa 243 unabainisha matumizi ya nahau kuonyesha utepetevu wa viongozi wanaopuuza raia kwa kujihusisha na siasa huku raia wakikumbwa na njaa. Mfano wa 244 unabainisha matumizi ya lugha ya kiistiari, kuku wa kienyeji wanalinganishwa na simaku ambayo *huvuta* vitu karibu. Hii ina maana kuwa kuku hao huwavutia sana wateja sokoni. Katika mfano wa 246 kauli 'walia kupunjwa' inaonyesha masikitiko ya jamii za wafugaji zilizohujumiwa na serikali. Katika mfano wa 247 matumizi ya neno '*njia*' ni ya kitaashira kuonyesha hali ya kuja. Hii inamaana kuwa kuna kufuatana kwa majanga mawili yanayozungumiwa. Janga linalotangulia ni Corona inayoathiri shughuli za kilimo na kusababisha njaa. Mfano wa 248 unaakisi kauli '*njaa ya nzige*' inayorejelea njaa iliyosababishwa na uharibifu wa mazao na mimea ulifanywa na nzige. Hii inamaanisha kuwa janga la nzige lilitangulia kisha likasababisha janga la njaa Tana River. Matumizi ya kauli ya kitamathali 'kusubiri kifo' katika mfano wa 250 yanaashiria kutamauka kwa wakazi wa Tana River kwa kukosa la kufanya kukabili janga la njaa. Kwa upande mwingine, matumizi ya kitenzi '*anika*' katika mfano wa 251 yanaonyesha hali ya kufichua shida zinazokabili wafanyakazi katika idara ya polisi. Matumizi ya kitenzi '*zima*' katika mfano wa 252 yanaashiria hali ya kumaliza jambo kabisa.

#### 4.4.1.5 Ujumbe wa Kimazingira wenye Maana Halisi

Ujumbe wenye maana halisi ni ule unaoakisi maana ya kimsingi au maana ya kimantiki ya matini. Hii ndiyo maana ya kwanza na ya kawaida ya matini ambayo hufafanuliwa kwa hali ya kawaida bila kufumbata ujumbe fiche (Saeed, 2009). Hii ina maana kuwa matini huwa na ujumbe wenye maana ambayo haijaathiriwa kwa njia yoyote ile na muktadha wala hisia zinazohusiana na tukio la mawasiliano (Griffiths, 2006). Kimsingi, kuna maana halisi ya kila neno ambayo huchukuliwa kuwa inajulikana miongoni mwa wanajamii

wanaozungumza lugha fulani wanaokusudiwa kuupokea ujumbe unaowasilishwa (Kearns, 2000). Kutokana na hali kuwa matini za kimazingira hutumia lugha ya kisayansi ambayo ni rasmi, matumizi ya lugha ya kitamathali ni machache; badala yake kuna matumizi ya lugha ya kawaida inayowasilisha maana halisi.

Maana halisi katika matini za kimazingira ilibainishwa kutokana na maneno yaliyotumiwa na wanahabari katika sentensi. Kimsingi ni kuwa wasomaji wanatarajiwa kuipata aina hii ya maana kwa njia ya moja kwa moja bila utata wowote. Maana halisi katika matini za kimazingira ilikuwa msingi wa mawazo waliyonayo wanajamii kuhusu dhana, vitu na hali mbalimbali za kimazingira katika jumuia-lugha wanamoishi. Kwa mfano matini zilizozungumza kuhusu uharibifu wa msitu Mau, ugonjwa wa Corona na kubadilika kwa tabianchi ulitolewa kwa njia ya moja kwa moja ili kueleweka kwa urahisi na hadhira.

253. Ukame: Viwanda vyafungwa mahindi yakisosekana (T.L. 22/1/22 uk. 3)
254. Ni kuni na makaa baada ya bei ya gesi kupanda (T.L. 1/3/22 uk. 4)
255. Uvamizi wa mbung'o Kwale unaibua hofu (T.L. 26/3/22 uk. 7)
256. Ukame watisha wafugaji Mwingi kwa kukosa lishe (T.L. 13/1/22 uk. 5)
257. Mafuriko yasababisha vifo na uharibifu wa mali (T.L. 22/7/21 uk. 6)
258. Watu 21 wafa kwenye mkasa wa barafu (T.L. 10/1/22 uk. 8)
259. Pwani: Kiangazi chaleta maafa (T.L. 16/9/21 uk. 4)
260. Utafiti kuhusu hatari ya ziwa Victoria usipuuzwe (T.L. 26/10/21 uk. 8)
261. Serikali imeshindwa kutulizamakali ya njaa (T.L. 18/11/21 uk. 7)

Mifano ya 253 hadi 261 inaakisi matumizi ya maana halisi inayotokana na matumizi ya kawaida ya lugha. Mada za mifano hiyo zinazungumzia matukio ya kimazingira kuhusu ukame, kawi, uvamizi wa wadudu waharibifu, mafuriko, majanga ya kiasili, kiangazi, na njaa kwa kutumia lugha ya kawaida. Maana halisi hudhihirika kwa wasomaji kwa njia ya moja kwa moja bila utata wa aina yoyote. Maana halisi ndiyo msingi wa mawasiliano wa habari za mazingira zinazowalenga wasomaji wa kawaida katika jamii. Isitoshe, maana

halisi hutokana na mfumo wa kimofolojia na kisintaksia; kwa pamoja mifumo hii humwezesha mtumiaji wa lugha kutambua sifa bainifu za kila neno na dhana inayorejelewa katika matini ya kimazingira. Matini zote za kimazingira zilizochunguzwa katika utafiti huu kutoka gazeti la *Taifa Leo* ziliakisi ujumbe uliosheheni maana halisi. Hata hivyo, wanahabari walichanganya lugha ya kawaida na lugha ya kitamathali pamoja na lugha ya kitaaluma ili kutimiza malengo fulani ya kimawasiliano.

#### 4.4.1.6 Ujumbe wa Kimazingira wenye Maana Ashirifu

Matini za kimazingira zilizochunguzwa katika utafiti huu zilisheni ujumbe wenye maana ashirifu. Ujumbe wenye maana ashirifu ni ule ulio na maana matlaba au maana ya ziada. Hii ina maana kuwa kuna maana ya ziada iliyoshehenezwa katika matini ya kimazingira ambayo inahitaji jicho la kimakini ili kupata maana hiyo iliyoghubikwa (Saeed, 2009). Kimsingi, maana ashirifu hujumuisha vipengele vya maana halisi ya matini pamoja na ufasiri wa kibinafsi wa mtu wa kile ambacho kinawasilishwa kimawasiliano na mtunzi wa matini (Cruse, 2010). Hali hii inamaanisha kuwa wanahabari walioumba matini za kimazingira zenye ujumbe wa maana ashirifu hawakumlenga msomaji wa kawaida katika jamii bali sehemu fulani ya wasomaji wenye tajriba na uzoefu wa kufasiri na kuelewa ujumbe uliokusudiwa. Ufasiri huo hutegemea tajriba ya kibinafsi ya mpokezi wa ujumbe. Hii ina maana kuwa maana ashirifu hutofautiana kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kutegemea tajriba ya mtu katika mawasiliano yanayotendeka (Cruse, 2010). Hali hii, ilibainika katika matini za kimazingira katika gazeti la Taifa Leo wakati ambapo ujumbe, kwa mfano, uliowalenga wataalam wa mazingira, wataalam wa afya, wanazuoni, watu wazima na aina nyingine za hadhira zenye tajriba fulani ulitofautiana. Safu za kisayansi kama vile Shina la Uhai, Afya ya Jamii, Kilimo, Sayansi na Mazingira na Akilimali

zililenga hadhira ya aina hiyo Maana ashirifu inaweza pia hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine (Kearns, 2000).

Utafiti huu ulibainisha kuwa matumizi ya istiari, methali, nahau na tamathali nyingine za usemi katika matini za kimazingira zilinuiwa kuibua sifa za ziada za kisemantiki ambazo zilihusiana na maana ashirifu. Kwa mfano maana ya methali na tamathali za usemi inatokana na uashirifu. Katika matini za aina mbalimbali huwa kuna taashira ambazo huwa na maana ashirifu inayotofautiana kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine. Kwa mfano katika jamii ya Waswahili 'sungura' huchukuliwa kama ishara ya ujanja naye 'kobe' akasimamia hekima. Kwenye jamii za kimagharibi 'mbweha' ndiye ishara ya ujanja. Mifano ifuatayo ya matini zenye maana ashirifu ilikusanywa kutoka katika gazeti la *Taifa Leo*:

262. Covid, joto kali *zatumbukiza* Olimpiki katika hali ya *mshikemshike* (T.L. 21/7/21 uk. 1)
263. Desturi ya aina yake kisiwani Lamu inayozipatia mashua '*uhai*' baharini. (T.L. 22/7/21 uk. 7)
264. *Nia njema* inahitajika kukabiliana na janga la ukame. (T.L. 29/9/21 uk. 8)
265. Kongoni wafurika Kenya '*kujaza dunia*' (T.L. 7/7/21 uk. 2)
266. Radi yaua 60 wakiwemo 11 waliokuwa *wakipiga* '*selfie*' (T.L. 13/7/21 uk. 5)
267. Chombo *chapiga jeki* unyunyiziaji maji (T.L. 5/1/22 uk. 16)
268. Stima: Uhuru *aenjoi* Wakenya. (Rais Kenyatta ametoa ahadi ya kupunguza gharama kubwa ya nguvu za umeme tangu mwaka wa 2018. (T.L. 5/1/22 uk. 1)
269. Ndovu wenye *kiu* watatiza amani vijijini (T.L. 20/7/21 uk. 2)
270. Corona bado *yatesa* (T.L. 6/1/22 uk. 8)

Katika mfano wa 262 kitenzi 'tumbukiza' kina maana ya ziada inayoashiria kuweka kitu katika hali tatanifu. Neno 'uhai' katika mfano wa 263 linaashiria kufanya kitu kiwe kipya. Kwa upande wake, kauli 'kuwa na nia njema' iliyotumika katika mfano wa 264 inaashiria kubadili mawazo kuhusu kusudi la kufanya jambo. Katika mfano wa 265, kauli 'kujaza

dunia' inaashiria kuongezeka idadi kwa kuzaana. Kauli 'kupiga selfie' katika mfano wa 266 inarejelea kitendo cha kujipigia simu kwa kutumia kamera ya simu. Matumizi ya maneno 'piga jeki', 'enjoi', 'kiu' na 'tesa' katika mifano ya 268, 269 na 270 mtawalia yaashiria maana ya ziada ya maneno hayo. 'Kupiga jeki' ni kuinua hali ya kitu fulani. 'Kuenjoi mtu' ni kauli ya sheng inayomaanisha kudanganya au kuhadaa mtu. 'kuwa na kiu' kunamaanisha kuwa na haja ya kunywa maji nalo neno 'kutesa' ni msimu unaomaanisha kusababisha kero au bughudha. Kimsingi, maana ziada ni jumla ya maana zote ambazo hurejelewa au huhusishwa na neno fulani. Maana ziada ni maana ambayo hujengwa kutokana na maana bwiwa na kuongezewa sifa zaidi ambazo kirejeleo kinatarajiwa kuwa nazo. Ni maana iliyo pevu zaidi kuliko ya maana halisi. Maana ashirifu au sifa zaidi hutokana na matarajio ya kisaikolojia na kijamii kuhusiana na kirejelewa.

Sehemu hii imefafanua aina ya ujumbe ulioibuliwa kutokana na matumizi ya lugha na mtindo wa uwasilishaji wa taarifa za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Sehemu inayofuata inalenga kueleza dhima ya ujumbe wa habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo.*

### 4.4.2 Dhima ya Ujumbe Ulioibuliwa Kutokana na Matumizi ya Lugha katika Kuwasilisha Habari za Mazingira katika Gazeti la *Taifa Leo.*

Waandishi wa matini huumba kazi zao kiupekee kwa kufinyanga lugha kiufundi na kutumia mitindo teule ya kutoa ujumbe wanaowasilisha ili kutimiza malengo fulani ya kimawasiliano (Saeed, 2009). Malengo hayo yanaweza kubainishwa kwa kuchunguza dhima za kimawasiliano za ujumbe unaotolewa katika matini husika ( Cruse, 2010 ). Kwa kuzingatia kigezo hiki, utafiti huu uligawa ujumbe uliowasilishwa na wanahabari katika

makundi mbalimbali kutegemea dhima zake za kimawasiliano. Makundi hayo yamefafanuliwa na mifano kutolewa katika sehemu inayofuata:

#### 4.4.2.1 Kushawishi Wasomaji

Sifa kuu isiyo ya kiisimu katika mtindo wa kushawishi ni ule mwelekeo wa kutoa taarifa kwa kumwelekeza msomaji akubali msimamo, mtazamo au upande fulani wa mawazo. Hii ina maana kwamba mwandishi wakati wote hujitahidi sio tu kutoa habari au taarifa fulani, bali pia kuonyesha msimamo wake na uhusiano wake kwa hayo anayoyaandika na kuibua uhusiano maaluma wa wasomaji kwa yale wanayoyasoma (Grundy, 2008). Ili mawasiliano ya namna hii yaweze kutekelezwa vizuri zaidi na kwa ufanisi wa juu ni lazima lugha mguso itumike. Jambo hili huathiri sana mfumo wa matumizi ya zana za kiisimu katika mtindo wa mawasiliano ya magazetini na shughuli za kimazingira, kwani zana zote za kiisimu zinajitokeza katika hali hii ya kutaka kuleta mguso mkubwa katika lugha, na hivyo kuwasisimua na kuwapendeza wasomaji na kwa hali hiyo kuwashawishi kukubali taarifa zinazotolewa. Kielelezo cha 9 kinabainisha matumizi ya lugha ya mvuto wa kushawishi uliokusanywa na utafiti huu kutoka kwa matini za kimazingira kutoka katika gazeti la *Taifa Leo*:


Shina la uhai

Afya Jamii

# Mabadiliko ya tabianchi yanyima watoto virutubisho tosha

NA PAULINE ONGAJI

C

*Kilelezo 9*: Makala kutoka safu ya 'Shina la Uhai', *Taifa Leo*, Agosti 24, 2021 uk. 12

Katika matini iliyo kwenye kielelezo cha 9 kichwa cha habari kina mvuto wa kumshawishi msomaji kuwa mabadiliko ya tabianchi huwanyima watoto virutubisho tosha. Mwanahabari analenga kubadilisha imani na mielekeo potovu katika jamii kuhusu magonjwa ya utapia mlo yanayowaathiri watoto. Kupitia kwa lugha ya kushawishi yenye mvuto na ushahidi wa kisayansi mwanahabari analenga kubadilisha imani na mwelekeo wa jamii kuhusu magonjwa yanayatokana na lishe bora au lishe duni kwa kuhusisha chanzo chake na mabadiliko katika hali ya tabianchi.

### 4.4.2.2 Kukashifu Matukio Anuwai

Matini ya habari inayolenga kukashifu shughuli, tabia au matendo fulani ya binadamu itatumia lugha ya kushutumu, kukashifu na kuonyesha madhara ya vitendo hivyo (Verschueren, 1999). Wanahabari wa matini za kimazingira waliolenga kukashifu shughuli na vitendo vya binadamu vilivyoathiri mazingira walitumia lugha ya kukemea na kukashifu vitendo hivyo. Mfano wa kielelezo cha 10 unaonyesha matini ya kimazingira inayoshutumu shughuli za binadamu zinazoathiri mazingira zilizokusanywa kutoka kwa gaezeti la *Taifa Leo*:




*Kilelezo 10*: Makala kutoka safu ya 'Shina la Uhai', *Taifa Leo*, Disemba 7, 2021 uk. 14-15

Katika mfano huu mwandishi anashutumu na kukashifu vitendo vya kutumia kawi hatari kutoka kwa kuni na makaa ambayo husababisha ukataji kiholela wa miti na pia hutoa moshi mkali unaoathiri afya ya mtumiaji. Lugha inayotumiwa ni ile ya kutoa tahadhari na kushutumu kwa kutoa ushahidi wa kisayansi.

### 4.4.2.3 Kutahadharisha Hadhira

Matini zinazolenga kutahadharisha hadhira hutumia lugha ya kuonya na kuhimiza jamii kuwa makini kutokana na uwezekano wa kuzuka kwa majanga au hali hatari. Lugha hiyo hukusudia kuwafanya wanajamii kuchukua tahadhari ili kujiepusha na majanga hayo (Grundy, 2008). Mfano wa matini katika kielelezo cha 11 uliokusanywa kutoka kwa gazeti la *Taifa Leo* unaonyesha makala inayolenga kutahadharisha hadhira:


HABARI ZA KAUNTI

Serikali yapiga jeki kiwanda cha maziwa kwa Sh350 milioni

Kaunti yahamishia huduma zake kwa mfumo wa dijitali

NACADA yataka serikali ijenge vituo vya kurekebisha waraibu wa dawa za kulevya

Huenda wakazi wa kusini na kaskazini nchini wakapoteza mifugo yao

Jiandae kwa ukame, wafugaji waonywa

Gavana Ongwae na Maangi wapatana

Shirika lawafaa wafugaji Pokot

Kinyozi aliyemuua mwanafunzi asakwa

Korti yazuia kwa muda marufuku kwa Spika

*Kilelezo 11*: Makala kutoka safu ya 'Habari za Kaunti', *Taifa Leo*, Septemba 4, 2021 uk. 4

Matini ya kimazingira katika kielelezo cha 11 inawatahadharisha wafugaji katika maeneo ya kusini na kaskazini mwa nchi kuhusu kuzuka kwa ukame utakaoathiri mifugo. Matini inatumia data ya kisayansi kuthibitisha uhalali wa madai yanayotolewa. Mwelekeo wa

makala ni wa kitabiri na lugha inayotumiwa ni ile ya kuonya na kushawishi kuchukua tahadhari.

#### 4.4.2.4 Kuhamasisha Hadhira

Matini zenye mwelekeo wa kuhamasisha hutumia lugha ya kitaaluma inayoelimisha na kufundisha jamii kuhusu mambo yanayopuuzwa kwa kutoeleweka vyema ambayo yanaweza kuwa na madhara au pengine kuhusu faida za mambo fulani (Huang, 2007). Mfano wa matini katika kielelezo cha 12 unabainisha matini ya kimazingira iliyokusanywa katika gazeti la *Taifa Leo* inayolenga kuhamasisha wasomaji:



AKILI MALI

# Mabadiliko ya tabianchi yanavyoathiri kilimo cha plamu nchini

Ujasiriamali

Ufugaji

Uk

Mitambo

*Kilelezo 12*: Makala kutoka safu ya 'Akili Mali', *Taifa Leo*, Januari 12, 2021 uk. 13

Matini ya kimazingira katika kielelezo cha 12 inatumia mada yenye lugha yenye mwelekeo wa kuhamasisha na kufundisha wasomaji kuhusu uwezekano mkubwa wa mabadiliko ya tabianchi kuathiri kilimo cha plamu nchini Kenya. Mwandishi anahamasisha na kufundisha wasomaji kuhusu jinsi mabadiliko katika tabianchi yanavyohujumu shughuli za kilimo cha matunda na mboga nchini na namna ya kukabili mabadiliko hayo.

#### 4.4.2.5 Kutamausha Hadhira

Matini yenye mwelekeo wa kutamausha hutumia lugha inayokatisha tamaa kwa kuonyesha ukosefu wa matumaini (Huang, 2009). Lengo la kutumia lugha ya aina hii ni kuonyesha mateso, dhiki na mashaka yanayowakabili wahanga wa majanga ya kimazingira. Mfano wa matini iliyo katika kielelezo cha 13 ambayo ilikusanywa kutoka gazeti la *Taifa Leo* unaonyesha makala inayolenga kutamausha msomaji:




*Kilelezo 13*: Makala kutoka safu ya 'Shina la Uhai', *Taifa Leo*, Juni 29, 2021 uk. 12

Matini ya kimazingira katika kielelezo cha 13 inazungumzia ugonjwa wa pumu ( nimonia ) ambao unasababishwa na mabadiliko ya tabianchi na kuwaangamiza watoto kila uchao. Mwandishi anazungumzia chanzo, athari, tiba, viwango vya maafa na jinsi ya kujiepusha na ugonjwa wa nimonia. Lengo la kusawiri viwango vya maafa ya watoto yanayotokana na ugonjwa wa nimonia lilikuwa kuwatamausha wanajamii ili wachukue hatua za dharura

kujiepusha na ugonjwa huo. Makala haya yanatoa hisia za huruma, huzuni na simanzi kwa wasomaji waliokumbwa na athari za nimonia.

### 4.4.2.6 Kuchochea Ari ya Pamoja ya Hadhira

Matini zinazolenga kuchochea ari ya pamoja hutumia lugha ya kutia hamasa na kuchochea ghadhabu kwa watu kuchukua hatua za pamaoja kuauni hali fulani inayowakabili. Lugha ya aina hii inalenga kuamsha hisia za pamoja ili kufanya uamuzi utakaowanufaisha watu wote wanaokabiliwa na tatizo fulani (Huang, 2007). Mfano wa matini ulio katika kielelezo cha 14 uliokusanywa kutoka gazeti la *Taifa Leo* unabainisha makala yanayolenga kuchochea ari ya pamoja ya wasomaji:




*Kilelezo 14*: Makala kutoka safu ya 'Akili Mali', *Taifa Leo*, Februari 23, 2022 uk. 13

Matini ya kimazingira katika kielelezo cha 14 inaonyesha matumizi ya lugha inayolenga kuwachochea wakulima wa zao la kahawa kudai bei nafuu na fidia kutoka kwa serikali. Mwelekeo wa mwandishi ni ule wa kuwahamasisha na kuwachochea wakulima ambao

wamepata hasara kutokana na bei duni ya zao la kahawa wanayolipwa na serikali. Hii ni njia ya kuwahamasisha kuwa wanafaa kudai fidia ya hasara waliopata kutoka kwa serikali.

### 4.5 Hitimisho

Sura hii ilizingatia uchanganuzi wa data na ufasiri wa matokeo ya utafiti. Ilianza kwa kutoa ripoti za habari kuhusu mazingira. Aidha, ilitoa maelezo kuhusu jinsi data iliyokusanya ilivyochanganuliwa hatua kwa hatua na kutoa ufasiri wa matokeo ya utafiti kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Sehemu inayofuata inahusu mahtasari, mahitimisho na mapendekezo yanayochochewa na utafiti huu.

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 Utangulizi

Sura hii ina muhtasari wa utafiti, hitimisho la matokeo muhimu ya utafiti, mapendekezo ya utafiti na hatimaye mapendekezo ya utafiti zaidi unaoweza kufanywa na watafiti wengine.

### 5.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulihusu tathmini ya matumizi ya lugha katika uwasilishaji wa habari za mazingira katika gazeti la Taifa Leo la Kenya. Utafiti uliongozwa na malengo matatu: uchanganuzi vipengele vya lugha vilivyoteuliwa katika kuripoti taarifa za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*, kutathmini mtindo uliotumiwa na waandishi katika kuripoti habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* na kubainisha aina na dhima za ujumbe ulioibuliwa kupitia uteuzi wa lugha na mtindo wa kuwasilisha habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*.

Sura ya pili ya utafiti huu ilihusu mwauo wa maandishi yanayohusiana na matumizi ya lugha na mtindo wa uwasilishaji wa habari katika gazeti la Taifa Leo la Kenya. Maandishi yanayohusiana na utafiti huu yaligawanywa katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza ilifafanua tafiti ambazo zimewahi kufanywa na ambazo zinalenga matumizi ya lugha katika vyombo vya habari ili kubaini pengo ambalo matokeo ya utafiti huu yangeziba. Ili kubainisha lengo kuu la utafiti huu mtafiti alisoma maandishi yanayofafanua matumizi ya lugha katika gazeti la *Taifa Leo* kwa nia ya kuonyesha mfanano na tofauti kati ya utafiti huu na tafiti zilizofanywa kwa kutumia data inayopatikana katika gazeti la *Taifa Leo* katika sehemu ya pili. Sehemu ya tatu ilifafanua tafiti ambazo zilichunguza mtindo kwa kuhusisha

data tofauti tofauti na jinsi tafiti hizo zinafanana na kutofautiana na utafiti huu. Data ya utafiti huu ilihusu habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Ili kuutenga utafiti huu na tafiti nyingine, mtafiti alisoma na kuchanganua tafiti mbalimbali ambazo zilitumia data za mazingira.

Sehemu ya mwisho ya sura ya pili ilichanganua nadharia ambazo ziliongoza ufafanuzi wa data katika utafiti huu .Uchunguzi huu ulielekezwa na mihimili ya Nadharia ya Uchangunuzi Usemi na Nadharia ya Umtindo. Mwauo wa maandishi mbalimbali umeonyesha kwamba matumizi ya lugha kulingana na mada ni muhimu katika mawasiliano kwa kuwa hili huchangia uwasilishaji wa ujumbe uliokusudiwa. Aidha, mtindo wa kuwasilisha ujumbe huamua upokezi wa ujumbe husika kwa kiwango kikubwa. Utafiti huu ulichunguza mitindo iliyotumiwa na wanahabari kuandika habari za kimazingira ambayo inaakisi matumizi ya lugha teule au yenye upekee wa aina fulani. Ujumbe huu kwa ujumla unaonyesha kuwa ikiwa msomaji atazipokea taarifa hizi ipasavyo, pana uwezekano mkuu wa asasi husika kuyatunza mazingira.

## 5.2 Mahitimisho ya Matokeo Muhimu ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza matumizi ya lugha na mitindo iliyotumiwa na wanahabari kuandika habari za kimazingira ambayo inaakisi matumizi ya lugha teule au yenye upekee wa aina fulani. Matokeo ya utafiti yalitolewa kulingana na malengo ya utafiti:

### 5.2.1 Lengo la Kwanza Lilikuwa Uchanganuzi wa Vipengele vya lugha vilivyoteuliwa katika uwasilishaji wa habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*.

Taarifa za mazingira katika gazeti la Taifa Leo zilibainisha matumizi ya lugha inayoonyesha udhamiriaji, matumizi ya nafsi katika masimulizi, matumizi ya toni, miundo

ya sentensi pamoja na uteuzi wa mada. Utafiti huu ulibainisha kwamba waandishi wa habari walizingatia aina mbalimbali za udhamiriaji kama vile udhamiriaji wa ulazima, mazoea, unaobainisha nia ya uwezekano na unuiaji.

Uchunguzi huu ulibainisha kuwa lengo kuu la udhamiriaji wa ulazima katika matini za kimazingira ni kuonyesha udharura uliopo katika kutunza mazingira. Kutotunza mazingira kutasababisha mabadiliko ya tabianchi na maangamizi ya binadamu na viumbe wengine duniani. Ujumbe huu kwa ujumla unaonyesha kuwa ikiwa msomaji atazipokea taarifa hizi ipasavyo, pana uwezekano mkuu wa asasi husika kuyatunza mazingira.

Udhamiriaji unaobainisha nia ya uwezekano unatumiwa katika matini za kimazingira na wanahabari kwa lengo la kuonya, kutahadharisha na kuwatia umakini wasomaji ili waepukane na madhara au athari fulani zinazotarajiwa. Kwa mfano iwapo mazingira hayatatunzwa vizuri, kuna athari ya maafa yatakayotokea kutokana na uharibifu huo. Katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo*, wanahabari walitumia udhamiriaji unaoonyesha unuiaji kuripoti matukio yaliyotarajiwa kutendeka ambayo hayakuwa yametendeka tayari. Udhamiriaji wa mazoea katika matini za kimazingira unalenga kuwatanabahisha wasomaji kuhusu matukio yanayotendeka kila mara ambayo huenda wakayapuuza lakini yana madhara makubwa kwa afya na mazingira. Kwa kuchukua hatua mwafaka huenda umma ukaepukana na madhara au athari hizo. Udhamiriaji huu pia unatumika kuelimisha na kuhimiza jamii kuhusu vitendo chanya ambavyo huenda vikainua na kudumisha viwango bora vya afya na mazingira.

Matini za kimazingira ziliwasilishwa katika gazeti la *Taifa Leo* kwa kutumia mbinu ya usimulizi unaozingatia nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu.Usimulizi wa nafsi ya kwanza

hujenga ukaribu mkubwa baina ya mwanahabari msimulizi au mhusika anayesimulia habari za kimazingira na msomaji. Sauti inayosikika katika taarifa inayowasilishwa kwa nafsi ya kwanza ni ile ya mhusika aliyeshuhudia au kuathiriwa na matukio yanayosimuliwa na mwanahabari. Kwa kufanya hivyo mwanahabari anayafanya matukio yanayosimuliwa yawe ya kusadikiwa na kuaminika kwa urahisi. Matukio hayo yanafanywa kuwa halisi kabisa kwa msomaji. Vilevile, mwanahabari anafanikiwa kukuza athari anayolenga kuibua kwa msomaji. Mwanahabari anapoipa nafsi ya kwanza kusimulia matukio yaliyotendeka, msomaji anaathiriwa kihisia kutokana na usimulizi huo. Kwa njia hii mwanahabari anafanikiwa kumshawishi, kumwelekeza kifikra na kumbadilisha kimawazo msomaji wake kuhusu matukio ya kimazingira yanayosimuliwa.

Usimulizi wa nafsi ya pili hutambulika kupitia kwa matumizi ya kiambishi **–u-** cha nafsi. Kwa kutumia nafsi ya pili, msimulizi hurejelea ulimwengu wa msomaji au mlengwa wa taarifa. Hali hii inamaanisha kuwa mwandishi huvunja mpaka uliopo kati ya ulimwengu wa uandishi na ulimwengu halisi au ulimwengu wa nje ya matini. Kwenye matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo,* wanahabari walitumia nafsi ya pili kumshirikisha msomaji katika matukio yaliyosimuliwa. Mwanahabari anamshirikisha msomaji wa habari katika muktadha wa mazingira anayoyasimulia. Taswira inayojitokeza ni ile inayonuiwa kuathiri hisia za msomaji. Matumizi ya nafsi ya pili kwenye matini za habari ya mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* yanakusudiwa kumshirikisha msomaji katika matukio yanayosimuliwa ili kumwathiri kwa njia inayokusudiwa na mwandishi wa makala.

Usimulizi wa nafsi ya tatu hutambulika kupitia kwa matumizi ya kiambishi **–a-** cha nafsi ya tatu umoja. Usimulizi huu unawawezesha waandishi wa matini husika kuwa na mtazamo mpana wa matukio yanayopatikana katika ulimwengu halisi au wa kiubunifu

wanaoutungia. Kiambishi **–wa-** cha nafsi ya tatu katika wingi kikitumiwa katika matini kinarejelea nafsi ya kijamii. Nafsi ya kijamii inaweza pia kutumiwa na wanahabari kama njia ya kumshirikisha msomaji kwenye masimulizi na kumfanya ashirikiane na mtunzi wa matini husika.

Lugha andishi inayotumika katika matini za kimaandishi huakisi toni fulani. Kimsingi, toni hurejelea suala linalozungumziwa katika matini husika ambalo huibua hisia fulani kupitia kwa maneno yaliyoteuliwa na mtunzi wa matini. Hili linamaanisha kuwa, mtunzi wa matini huteua maneno ili kuibua maana maalum kutegemea muktadha wa matumizi ya maneno hayo. Maana inayowasilisha katika matini huibua hisia fulani ambazo zinaweza kuwa, kwa mfano, dhihaka, kicheko, kashfa au huzuni. Uteuzi wa maneno au visawe vyake haudhibitiwi tu na maana ya maneno hayo pekee bali pia na athari inayoibuliwa na maneno yenyewe. Hali hii ina umuhimu katika ujenzi wa toni ya matini ya kimazingira ili kuathiri hadhira ya wasomaji kwa njia inayokusudiwa na mwanahabari. Kwa mfano mwandishi wa makala atatumia maneno ya kashfa anapokusudia kukashifu uharibifu wa mazingira. Kwa upande mwingine, atatumia maneno ya kusifu, kupongeza na kuhimizi akitaka kukuza tabia ya kutunza na kujali mazingira. Kimsingi, kwenye matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* utafiti huu ulibainisha matumizi ya toni ya kichomi, huzuni, kukashifu, kutamauka au kukata tamaa, kusononeka, kusikitisha, kutumaini, na kupongeza.

Utafiti umebainisha kuwa baadhi ya matini za kimazingira zilikusudiwa kuibua hisia fulani kwa msomaji. Suala la hisia katika matini hizo lilifungamana kwa kiasi kikubwa na dhana za toni. Toni ya huzuni inakusudiwa kuibua hisia za huzuni kwa wasomaji. Toni ya huzuni inaweza kudhihirika katika matini inayochunguzwa kupitia kwa uteuzi wa maneno ambayo mwandishi wa matini ya kimazingira anayatumia kutoa ujumbe anaokusudia. Athari

inayotokana na usomaji wa maneno yaliyotumika ni ile ya kuhuzunisha inayoibuliwa na hisia za huzuni.

Toni ya kukashifu ni ile inayohusu uteuzi wa maneno yanayokusudia kufichua jambo lisililojulikana lenye uovu au la kuzua aibu na kulifanya lijulikane kwa kuibua hisia za kushtumu.Toni ya kukashifu ilidhihirika kupitia kwa maneno ya kushtumu au kukashifu yaliyoteuliwa na waandishi wa matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Maneno hayo yalinuiwa kuibua hisia za chukizo na kukereka dhidi ya vitendo vya kuharibu au kuchafua mazingira vya baadhi ya wanajamii.

Toni ya kutamauka hudhihirika wakati ambapo waandishi wa matini hutumia maneno yanayolenga kuibua hisia za kukatisha tamaa. Toni ya kutamauka ilibanika katika matini zilizokusanywa zilizosimulia kuhusu mazingira zilizoonyesha kuwepo kwa fadhaa, pekecho, wasiwasi na kukithiri kwa viwango hasi ambavyo havikutoa matumaini yoyote. Waandishi walitumia toni hii kuibua hisia za ghadhabu ili wanajamii wabadili mielekeo na vitendo hasi dhidi ya mazingira. Kimsingi ni kuwa wanahabari walipotumia toni ya kutamausha katika habari walizotoa walilenga kuangazia kero za wananchi na wakati huohuo kutoa wito wa dharura kwa serikali ishughulikie majanga ya kimazingira yaliyotishia kuwaangamiza raia.

Toni ya masikitiko hubainika katika matini za kifasihi kupitia kwa matumizi ya maneno yanayoonyesha masikitiko kutokana na hali zinazosimuliwa na waandishi. Toni ya kusikitisha ilibainika katika matini za kimazingira zilizochunguzwa katika utafiti huu. Kwa mfano, wanahabari waliporipoti taarifa zilizohusu majanga ya kiasili kama vile: uvamizi

wa nzige, njaa, mafuriko na mikurupuko ya maradhi, walitumia maneno ya kuonyesha kusikitika kutokana na utepetevu wa serikali katika kuyashughulikia majanga haya.

Toni ya matumaini ni ile iliyo kinyume cha toni ya kutamausha. Toni hii huonyesha faraja, matumaini au imani kuwa hali hasi itabadilika na kuwa chanya. Maneno yanayotumiwa katika matini huonyesha matumaini au kuimarika kwa hali ambazo awali zilionekana kuwa hasi kabisa. Toni ya matumaini inatumiwa na wanahabari kuonyesha kuwa, licha ya kuwa na uharibifu mkubwa wa mazingira unaotokana na vitendo vya wanadamu pamoja na majanga; lakini pia kuna afueni na matumaini ya kunusuru uharibifu huo.

Toni ya kupongeza ni ile inayotumiwa kuhimiza matendo mema yanayofanywa na watu mbalimbali katika jamii. Toni hii inatumiwa kusifia vitendo vya hisani na utu vinavyofanywa na watu binafsi, mashirika au taasisi mbalimbali. Katika matini za kimazingira zilizokusanywa na utafiti huu, wanahabari walitumia maneno yaliyokusudiwa kuibua toni ya kupongeza ili kusifu vitendo bora vya kutunza au kujali mazingira vilivyofanywa na watu au mashirika katika jamii. Katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo*, wanahabari walitumia toni ya kupongeza kusifu juhudi zilizofanywa na watu binafsi, viongozi na mashirika katika kukabiliana na majanga au kuwasaidia waathiriwa wa majanga hayo.

Nyenzo kuu inayotumiwa na wanahabari kuumba matini zao ni lugha. Matumizi ya lugha huonekana kupitia kwa namna wanavyounda sentensi zinazojenga matini husika. Kuna miundo mikuu mitatu ya sentensi ambayo ni muundo sahili, muundo changamani na muundo ambatani. Maelezo yaliyotolewa katika matini za mazingira yalichanganya sentensi sahili, changamani na ambatani kutegemea ujumbe. Sentensi sahili ni ile ambayo

ina kitenzi kimoja, ambacho maana yake ni kamilifu. Sentensi sahili huwa na kitenzi kikuu kimoja. Hata hivyo, si lazima sentensi sahili iwe rahisi kueleweka kimaana wala iwe fupi katika muundo wake. Sentensi sahili hueleza wazo moja tu ambalo hubebwa na kishazi kikuu kimoja. Sentensi sahili zilitumiwa na wanahabari walioripoti matukio ya kimazingira kutoka taarifa kamilifu wakitumia maneno machache. Hali hii ilibainika kwenye vichwa vya habari vilivyofinyangwa kwa mitindo ya kiiktisadi ili kutoa taarifa za kuvuta nadhiri ya wasomaji kwa kutumia maneno machache. Baadhi ya vichwa hivyo vilidokeza tu taarifa zenyewe na vingine vikatumia lugha ya mkato kupitia kwa matumizi ya sentensi sahili.

Matumizi ya sentensi changamani katika matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* yalibainika katika maelezo yaliyotolewa kufafanua matukio yaliyokuwa yanasimuliwa na wanahabari. Sentensi changamani zilizotumika zilikuwa na vishazi huru na vishazi tegemezi. Vishazi huru vilitoa taarifa kamili kuhusu matukio yaliyosimuliwa na wanahabari. Kwa upande mwingine, vishazi tegemezi vilitoa habari za ziada kuhusu matukio yaliyotolewa katika vishazi huru. Kwa ujumla, vishazi tegemezi katika sentensi changamani zilizobainishwa kwenye mifano iliyoteuliwa zinatoa taarifa za ziada zinazofafanua matukio ya kimazingira yanayosimuliwa katika vishazi huru ili kumwondolea msomaji tashwishi kuhusu matukio hayo. Kwa njia hii ujumbe mkamilifu unatolewa kwa msomaji na mwandishi wa matini.

Sentensi ambatani huitwa hivi kwa sababu kuna tungo nyingi na sentensi nyingi zilizoambatanishwa. Muundo wa sentensi ambatani ni kwamba inaundwa na sentensi sahili na sentensi sahili nyingine au sentensi sahili tatu. Sentensi ambatani huwa na vishazi huru viwili au zaidi ndani yake. Vishazi huru ambavyo vyenyewe huwa sentensi sahili huambatana kwa kutumia viunganishi. Sentensi ambatani zilizotumika katika matini za

kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* ziliwawezesha wanahabari kutumia sentensi moja kutoa ujumbe wenye maelezo yaliyokamilika kabisa. Hali hii iliwaondolea uwezekano wa kuligawa wazo moja linaloweza kuelezeka kikamilifu katika sentensi mbili au zaidi. Hali hii iliondoa uradidi na uziada ambao ungepotosha maana ya matini. Sentensi ambatani zilizotumiwa katika matini za kimazingira zilizokusanywa katika utafiti huu zilikuwa na vishazi viwili au zaidi vilivyounganishwa pamoja.

Matumizi ya takwimu katika matini za habari yalibainika wakati wa kunukuu kutoka kwa wanaohusika ili kujenga taswira ya uhalisia wa matukio yanayoripotiwa. Katika hali hiyo, matukio yaliyoshuhudiwa moja kwa moja, mahojiano kutoka kwa walioshuhudia na kutoka kwa ripoti rasmi zilizopokelewa kutoka kwa watu na taasisi zilizo na nguvu na hadhi ya juu hufafanuliwa yakiambatana na takwimu zinatoa idadi au kiasi kamili ya kile kinachoripotiwa. Matumizi ya takwimu hudhihirisha usahihi wa ujumbe unaotolewa na huonyesha umuhimu wa ujumbe wenyewe. Kwa hivyo, takwimu ni mbinu muhimu inayotumiwa katika uandishi wa habari kudumisha uhalisia, uhalali na utegemeo wa habari zinazotolewa. Utafiti huu uliainisha matumizi ya takwimu katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* katika makundi mbalimbali.

Takwimu za kiidadi zilitolewa kwa kuzingatia vivumishi vya idadi. Vivumishi vya idadi ni vile vinavyotaja idadi ya nomino husika. Kuna aina mbili za vivumishi vya idadi yaani, vivumishi vya idadi mahususi na vivumishi vya idadi isiyo mahususi. Vivumishi vya idadi mahususi hudhihirika kupitia kwa maneno yanayotaja idadi kamili ya vitu kwa mfano *kimoja, viwili, vitatu* au *tisa*. Kimofolojia vivumishi vya idadi mahususi huundwa kwa kuambatisha kiambishi patanishi cha msingi kwenye mizizi ya vivumishi vinavyotaja idadi

mahususi. Sajili ya sayansi hutegemea data inayotokana na utafiti wa kina ili kuonyesha uhalali, uhalisi na kutegemewa kwa taarifa inayotolewa.

Takwimu zinazohusu kiwango zilionyeshwa kwa kutumia vivumishi vya idadi isiyo dhahiri yaani uchache au wingi. Vivumishi vya idadi isiyo dhahiri hudhihirika kupitia kwa maneno yasiyotaja idadi kamili ya vitu, kwa mfano, –chache au -ingi. Kimofolojia vivumishi vya idadi isiyo dhahiri huundwa kwa kuambatisha kiambishi patanishi cha msingi kwenye mizizi ya vivumishi visivyotaja idadi dhahiri au mahususi. Kwa kutumia kauli '*wengi*', '*nyingi*' na '*mkubwa*' mwanahabari anatumia taswira kama ya idadi ya jumla ya vitu au viwango vya hali zinazozungumziwa. Kupitia kwa taswira hizi, wanahabari wanafanikiwa kutoa picha ya uharibifu mkubwa na madhara ya kimazingira yaliyofanywa na shughuli za binadamu zinazozungumziwa

Uteuzi wa mada za habari au vichwa vya habari ni muhtasari au ufupisho wa taarifa zinazotolewa ambao huandikwa juu ya makala husika katika gazeti. Mara nyingi mada za habari haziandikwi kama sentensi kamili.Mtafiti alibainisha kuwa vichwa hivi viliweza kukosa nomino au vitenzi fulani. Sababu ya kuacha maneno hayo inaweza kuwa ni kufanya mada hiyo kuvutia zaidi na isiwe na maneno mengi. Utafiti huu ulibainisha kuwa wanahabari walitumia mitindo tofauti tofauti katika kuteua mada za matini walizotunga na umegawa vichwa vya habari vilivyochunguzwa katika makundi mbalimbali:

Mada za kimdokezo au kimkato huwa na maneno yaliyoachwa ambayo yanabeba ujumbe ulio muhimu au mzito. Aghalabu maneno huachwa kimaksudi ili kusababisha taharuki na hivyo kuchochea msomaji kuendelea kusoma ili apate ujumbe kamili. Maneno ambayo huachwa kwenye mada ni vihusishi, vitenzi visaidizi, vivumishi, vimilikishi na

viunganishi. Matumizi ya vichwa vya habari vya kimdokezo katika matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* yalilenga kujenga taharuki na hivyo kuchochea msomaji kuendelea kusoma ili apate ujumbe kamili kuhusu matukio yaliyosimuliwa. Kwa njia hii wasomaji watapata ari ya kutaka kujua ujumbe uliotolewa kwa njia ya mkato. Vyombo vya habari hukusudia kujiuza kwa wasomaji. Njia mojawapo ya kuhakikisha lengo hili limetimia ni kutumia vichwa vya kimkato vinavyovutia macho ya wasomaji.

Mada za kibalagha huchukua muundo wa swali ambalo halihitaji jibu. Swali linalotolewa katika kichwa cha habari hulenga kuchochea hadhira ya wasomaji kutafakari kwa kina kuhusu ujumbe unaotolewa na kwa njia hiyo huathiriwa kwa njia inayokusudiwa na mwandishi. Aidha, swali la balagha linaweza kuwa na dhamira ya kuchochea hisia fulani kwa wasomaji kwa mfano kusikitika, kukereka au kustaajabu. Tunaweza kufikia hitimisho kuwa vichwa vya habari vya kibalagha katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* vilikusudiwa na wanahabari kuchochea hisia fulani kwa wasomaji kwa mfano kusikitika, kukereka au kustaajabu kuhusu matukio yaliyosimuliwa.

Mada za kitakwimu ni zile zinazotaja idadi au kiwango cha vitu na hali zinazozungumziwa katika kichwa cha habari. Takwimu hizi zinaweza kuwa kiasi mahususi cha fedha, umaratokezi wa tukio fulani au kiwango cha athari ya jambo fulani. Vichwa vya habari vyenye mada za kitakwimu hutaja idadi hiyo kwa hali mahususi au ujumla wake. Lengo la kutumia takwimu mahususi ni kuonyesha uhalisia wa jambo. Aidha, taarifa za kitakwimu hutoa ithibati inayoonyesha kuwa matukio yanayoripotiwa yanasadifu ukweli usiopingika. Tunaweza kufikia hitimisho kuwa vichwa vya habari vya kitakwimu vilivyotumiwa katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* vililenga kutoa ithibati iliyoonyesha kuwa matukio yaliyoripotiwa yalisadifu ukweli na uhalisia wa mambo.

Mada za kitaharuki ni zile zinazoamsha ari ya msomaji kutaka kujua kinachojiri katika matini. Mada hizi hufinyangwa kwa uteuzi teule wa maneno yanayonuiwa kuteka makini ya msomaji ili asome zaidi kilicho katika matini. Mada za aina hii huzua taharuki kwa kumchochea msomaji kusoma matini nzima ili kujua kinachosimuliwa. Mada hudokeza tu jambo ambalo linamsisimua msomaji na inamlazimu asome makala nzima ili kujijazia mianya ya kiusimulizi iliyodokezwa katika kichwa cha habari. Hata hivyo, huenda kilichodokezwa katika kichwa cha habari kikasimuliwa kwa njia tofauti kabisa na matarajio ya msomaji. Lengo la taharuki ni kuchochea ari ya msomaji na kuvuta umakini wake kwenye matini husika. Tunaweza kuhitimisha kuwa matumizi ya vichwa vya habari vya kitaharuki katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* yanalenga kuchochea ari ya msomaji na kuvuta umakini wake kwenye matini husika na kwa njia hii akapata ujumbe unaotolewa kwa urahisi.

Mada za kimaelekezo ni zile zinazomwongoza msomaji kupata habari fulani ambazo huenda angezipuuza katika chombo cha habari. Msamiati unaoteuliwa na vilevile lugha inayotumiwa hulenga kumwelekeza msomaji kupata habari fulani ambazo huenda hangezitilia maanani iwapo zingewasilishwa kwa njia tofauti. Katika gazeti la *Taifa Leo* kwa mfano, habari zinazohusu utunzaji na uharibifu wa mazingira zilitangulizwa kwa vichwa vya habari vilivyowaelekeza wasomaji kutahadhari, kubadili mielekeo na kuwa makini ili kutunza mazingira.

Mada za kiistiari ni zile zilizotumia tamathali za ulinganishi bila kutumia maneno yanayoashiria ulinganishi huo kama vile‘kama, mfano wa, na mithili ya’. Msingi wa sitiari ni uhamishaji wa maana. Msingi mkuu wa istiari ni uhamishaji maana kutoka kwa kitu kimoja hadi kitu kingine kwa kuvilinganisha.

### 5.2.2 Lengo la Pili Lilikuwa Kutathmini Mitindo iliyotumiwa na Waandishi wa Habari za Mazingira katika Gazeti la *Taifa Leo*

Wanahabari hutumia mitindo mbalimbali kuwasilisha ujumbe wao kwa hadhira wanayoikusudia. Mitindo inayotumiwa inaweza kuchunguzwa kwa mujibu wa Nadharia ya Umtindo. Utafiti huu ulitumia Nadharia ya Umtindo kwa sababu inajikita kwenye uchunguzi wa lugha kwa kiasi kikubwa. Uchunguzi huo wa lugha unabainisha ubunifu uliopo kwenye lugha hiyo na kwa kuuchunguza kwa undani unasaidia uelewekaji wa matini husika. Nadharia ya Umtindo hudhamiria kuchunguza na kuchanganua matini kwa kuzingatia taratibu za kisayansi pamoja na zile za kitaaluma.

Watafiti wanaochunguza mitindo wanaweza kutumia mikabala miwili kufanikisha uchunguzi wao. Mkabala wa kwanza ni ule wa jadi ambao hutenganisha maudhui au yaliyomo kwenye matini ili kubainisha ujumbe au maana inayojitokeza pamoja na fani iliyotumiwa na mtunzi wa matini. Kupitia kwa mkabala huu, mtindo huchunguza jinsi ujumbe au maana hiyo inawasilishwa kwa matumizi ya mbinu tofauti ambazo zinadhamiriwa na mtunzi kuibua athari fulani ya kiujumi kwa mlengwa au msomaji wa matini. Mkabala wa pili ni ule wa kiisimu. Kwa kuzingatia mkabala huu, maarifa ya kiisimu hutumiwa kubainisha sifa za kimtindo za matini. Sifa hizo zinaweza kuwa za kifonolojia kwa mfano; ruwaza za sauti, vina na mizani pamoja na zile za grafolojia.

Aidha, sifa za kisintaksia kwa mfano, miundo ya sentensi, virai, vishazi na aina za sentensi zilizotumiwa zinaweza kuchunguzwa. Mtafiti anaweza kuchunguza sifa za kimsamiati kwa mfano uteuzi wa maneno na kategoria za maneno yaliyotumiwa katika matini. Isitoshe, mtafiti anaweza kuchunguza sifa za kisemantiki, sifa za kiusemi au diskosi na zile za

kimuktadha au kipragmatiki. Utafiti huu ulitumia mkabala wa kiisimu kuchunguza sifa zifuatazo za kimtindo kwenye matini za kimazingira zilizochunguzwa:

Uchunguzi wa kimtindo unaolenga grafolojia huchunguza mwonekano wa matini yaani abjadi au hati zilizotumiwa pamoja na upangaji wa taarifa kwenye safu za matini. Matini inaweza kuwa na sifa maalum za kimaandishi ambazo zinachimuzwa na kwa njia hii kukifanya kiwango hiki kuwa muhimu katika uchunguzi wa kimtindo wa matini. Sifa za kigrafolojia zinahusisha mpangilio wa aya, mpangilio wa kurasa, nafasi baina ya sentensi, matumizi ya picha na michoro, rangi mbalimbali, utaratibu uliotumiwa katika vichwa vya habari pamoja na upangaji wa safu za maneno zilizochunguzwa katika matini za habari katika gazeti la *Taifa Leo*. Uchunguzi wa mpangilio wa aya za matini kwenye gazeti la *Taifa Leo* zilizohusu habari za kimazingira unadhihirisha umakini uliotumiwa katika ujenzi wa matini zenyewe na wanahabari.

Taarifa za habari katika gazeti la *Taifa Leo* zimepangwa kwa uangalifu, umakini na utaratibu mwafaka katika gazeti lililochapishwa. Gazeti la *Taifa Leo* limezingatia mpango mahususi wa safu zenye aya zilizoratibiwa vyema. Gazeti la *Taifa Leo* limezingatia taarifa za habari kuhusu mazingira zilizopangwa katika aya maalum.

Aya ya kwanza ina taarifa zilizokolezwa wino kusisitiza kiini cha habari kwenye matini. Baadhi ya taarifa ziliandikwa katika hati za kiitaliki kusisitiza ujumbe fulani uliotolewa na mwanahabari. Hata hivyo, uchunguzi wa kina wa habari katika aya zenyewe ulibainisha kuwa taarifa za habari kwenye matini zote zilizochunguzwa zilipangwa kwa aya fupi na kwa kuzingatia utondoti kutokana na ubanifu wa matini. Kwa hali hii, msomaji anaelekezwa kwa kudokezewa kilichojiri badala ya kufafanuliwa na kufahamishwa

kilichotendeka. Mwandishi anamwelekeza msomaji kujijazia mianya ya kimawasiliano katika matini bila kumweleza kwa kina kinachosimuliwa. Kwa njia hii mwandishi anaweza kumshawishi, kumchochea au kumwongoza msomaji kifikra pasipo msomaji mwenyewe kujua.

Matokeo ya utafiti yanaonyesha mpangilio wa kurasa za safu kuhusu mazingira kwa utaratibu mahususi katika gazeti la *Taifa Leo*. Kila ukurasa unaonyesha taarifa za habari za matukio ya aina mbalimbali. Kila ukurasa unaonyesha safu ya habari, mwandishi wa habari zenyewe, tarehe ya kuchapishwa kwa taarifa zenyewe na ukurasa husika.

Matini zilizochapishwa huzingatia utaratibu maalum wa kuacha nafasi baina ya maneno na vilevile kutoka sentensi moja hadi nyingine au safu moja na nyingine. Sifa hii inazifanya zionekane nadhifu na zenye mvuto kwa msomaji. Kwa upande mwingine, matini zinazohusu habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* zinaacha nafasi baina ya sentensi kwa utaratibu wa kawaida unaozingatiwa katika matini zilizopigwa chapa katika vitabu. Mwonekano huu unazifanya matini hizi zionekane kwa unadhifu unaorahisisha usomaji wake.

Picha za rangi zilizingatiwa ili kutimiza malengo mbalimbali ya kimawasiliano. Taarifa zinazotolewa huambatishwa na picha za matukio yanayosimuliwa. Sifa hii inaongeza uhalisia wa habari za kimazingira zinazotolewa kwenye gazeti la *Taifa Leo*. Kurasa na safu zinazotoa habari za matukio ya kimazingira zinatumia rangi mbalimbali kuvuta jicho la msomaji. Mbali na kuvuta umakini wa msomaji kwenye habari zinazotolewa, matumizi ya picha na michoro yanaimarisha uelewekaji wa habari za kimazingira zinazotolewa. Aidha, hali hii inajenga uhalisia kwa vile msomaji anajionea kile kinachofafanuliwa. Isitoshe,

matumizi ya picha na michoro yanafanya matini kutoa taarifa za habari kwa muhtasari kwa msomaji.

Matumizi ya picha za rangi yanazingatiwa katika matini za habari za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Taarifa zinazotolewa zinaambatishwa na picha za rangi za matukio yanayosimuliwa. Aidha, kurasa zenyewe zina rangi mbalimbali zinazojenga taswira inayokusudiwa na mwandishi wa matini. Sifa hii inaongeza uhalisia wa habari zinazotolewa kwenye matini husika. Aidha, matini hizi zinatumia rangi mbalimbali kuvuta jicho la msomaji. Rangi ni taashira au ishara mbalimbali zinazotoa ujumbe na maana fulani kwa msomaji. Rangi nyekundu inaweza kuashiria hali hatari. Kwa upande mwingine rangi ya bluu ikaashiria kuwepo kwa matumaini.

Upangaji wa safu za maneno kwenye ukurasa unaokusudiwa kupigwa chapa huzingatia utaratibu maalum. Mpangilio huo wa mikururo ya safu kwenye ukurasa uliochapishwa hukusudia kuvuta jicho la msomaji kwenye matini husika. Katika gazeti la *Taifa Leo*, kichwa cha habari kinachotangulia makala yenyewe kikifuatwa na picha pamoja na jina la mwandishi wa makala. Herufi ya kwanza ya neno la kwanza katika aya ya kwanza ni kubwa ikilinganishwa na herufi zingine za neno hilo. Taarifa muhimu kwenye aya za safu zinasisitizwa kwa kutumia hati za kiitaliki, zilizokolezwa wino au zinazotumia wino wa rangi. Sifa za kigrafolojia za kimtindo kwenye matini za taarifa za kimazingira katika gazeti la Taifa Leo zinakusudia kutimiza malengo fulani ya kimawasiliano. Ukurasa umepangwa kwa utaratibu maalum unaogawa safu, aya na mikururo ya maneno katika utaratibu mahususi unaokusudiwa kuteka jicho na umakini wa msomaji kwa haraka. Kuna matumizi ya picha, michoro na vielelezo vinavyomsaidia msomaji kupata habari kwa

urahisi na kwa njia ya kasi. Uteuzi wa rangi zinazotumiwa na hata mpangilio wake katika matini unatimiza malengo ya kimawasiliano ya mwandishi wa makala.

Sifa za kiothografia zinahusisha suala la uakifishaji, matumizi ya herufi ndogo na kubwa, tahajia sarufi na uteuzi wa hati. Uakifishaji huathiri uwasilishaji wa ujumbe kwa msomaji. Kwa hivyo, ni wenzo muhimu katika uandishi wa matini za habari kwenye gazeti la *Taifa Leo*. Uakifishaji kwa msingi huu unaweza kutumiwa kama mkakati wa kudengua matini na kuchochea mtazamo mwingine wa msomaji. Udenguzi ni mtazamo wa kifalsafa na kitaaluma wa kudadisi, kuchunguza na kuonyesha kuwepo kwa ukinzani, uchangamano au utata katika hali zinazoonekana kuwa za kawaida. Viakifishi kama alama za dukuduku, koloni, vihisishi na alama ya kuuliza ni nyenzo muhimu zinazoweza kudenguliwa ili kuonyesha hisia za mwandishi.Tunaweza kuhitimisha kuwa matumizi ya viakifishi kama alama za dukuduku, koloni, vihisishi na alama ya kuuliza ni nyenzo muhimu zinazoonyesha hisia za mwandishi wa makala. Aidha, viakifishi hivyo vinatumiwa kwa njia maalum ili kutimiza malengo fulani ya kimawasiliano jinsi tulivyobainisha katika maelezo yaliyotolewa.

Matumizi ya herufi kubwa na ndogo huathiri ujumbe unaowasilishwa kwa msomaji. Herufi kubwa zinaweza kuashiria msisitizo wa ujumbe fulani. Hii ina maana kuwa matumizi ya herufi kubwa na ndogo katika taaluma ya Uanahabari huwasilisha ujumbe fulani kwa msomaji. Maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa yanaonyesha msisitizo unaowekwa kwa sababu maneno hayo yanasheheni ujumbe muhimu unaowasilishwa katika kichwa cha habari.

Uteuzi wa hati huathiriwa na mitindo mbalimbali ya mwonekano wa hati iliyotumika katika matini. Baadhi ya matini hutumia aina fulani za hati maalum, hati za italiki, zingine hutumia hati zilizokolezwa wino na baadhi hutumia hati za kawaida. Athari ya jumla ya matumizi ya sanaa hati kwa mfano hati zilizokolezwa wino, kutumia italiki au kuchanganya hati ni kuwa inasisitiza sehemu fulani za matini zenye ujumbe maalum ambao mwandishi analenga msomaji aupate kwa kuvuta umakini wake. Pia uteuzi huo unakusudia pia kurahisisha mawasiliano kwa kumwezesha msomaji kukiona kwa haraka kwenye ukurasa husika.

Sifa za kileksia ni zile za kibalagha zilizotumiwa katika matini za diskosi. Baadhi ya sifa za kileksia zinazoweza kuchunguzwa katika matini za kidiskosi ni: uteuzi wa msamiati, matumizi ya tamathali za usemi na uradidi au urudiaji.

Uteuzi wowote ule wa msamiati unaweza kuwa rasmi au usorasmi. Muktadha wa kijamii ambamo mawasiliano yanatendeka ndio huamua iwapo tutatumia usemi rasmi au usorasmi. Mzungumzaji huteua maneno ya kutumia katika mawasiliano kutegemea urasmi au ukawaida wa muktadha anaohitajika kuwasiliana. Ufaafu au kutokufaa kwa maneno anayotumia mzungumzaji katika mawasiliano hutegemea sifa za kimtindo za maneno hayo. Hivi ni kusema kuwa kila neno huwa na mtindo wa kiuamilifu ambao neno hilo linawakilisha au kusimamia. Mtindo wa kiuamilifu unaweza kufasiriwa kama mfumo wa kimatumizi ulio mahususi katika nyanja fulani ya mawasiliano. Hii ndiyo sababu ya kimsingi ya wanahabari kuteua msamiati kwa uangalifu wanapoandika matini zao.

Nyanja ya mawasiliano ni hali fulani inayoathiri mchakato mzima wa mazungumzo katika muktadha mahususi. Mifano ya miktadha hiyo ni: mazungumzo ya kitaaluma, mhadhara,

barua ya kirafiki, gumzo, barua rasmi, barua ya kimapenzi au hotuba mahakamani. Hali hizo zote zinaweza kugawanywa katika makundi mawili kutegemea urasmi au ukawaida wake. Kwa mfano barua rasmi, hotuba mahakamani, utani, mhadhara na mazungumzo ya kitaaluma huhitaji mawasiliano rasmi. Kwa upande mwingine, barua ya kirafiki, gumzo na utani huhitaji mawasiliano yasiyo rasmi. Hivi ni kumaanisha kuwa mitindo ya uamilifu inaweza kuainishwa katika makundi mawili kutegemea urasmi au usorasmi wake. Katika matini zilizochunguzwa katika utafiti huu, uteuzi wa msamiati ulimulika hasa sajili ya kisayansi inayoangazia masuala ya mazingira na athari zake kwa uhai na afya ya binadamu, wanyama na mimea. Miktadha hiyo ya mawasiliano ni rasmi. Hii ina maana kuwa matini za wanahabari zilitumia lugha rasmi. Hata hivyo, kuna matukio yaliyosimuliwa majanga ya kuzuka kwa Corona na uvamizi wa nzige ambayo yalitumia lugha ya utani, kejeli, dhihaka na tashtiti ili kukashifu utepetevu, kutowajibika na ufisadi wa wahusika.

Tamathali ni istilahi inayorejelea mbinu ambayo inahusisha maana isiyo wazi na inayomhitaji msomaji kuisimbua ili aweze kuielewa. Kwa upande mwingine, tamathali za usemi ni dhana inayotumiwa kurejelea sifa za kimtindo ambazo hutumiwa katika matini kupitia kwa matumizi ya lugha yanayolenga kuzua usemi wenye uwezo wa kushawishi. Tamathali za usemi huweza kuzungumziwa kama *lugha ya kitamathali* ambayo ni nyenzo muhimu katika ujenzi na uimarishaji wa hisia. Lugha ya kitamathali hurembesha kile kinachozungumziwa na kukifanya kiwe na mvuto mkubwa wa kiumbuji na kisanaa. Aidha, lugha ya kitamathali hutumiwa kwa lengo la uthabitishaji yaani kukifanya kinachorejelewa kuwa na uthabiti fulani, na kwa njia hii, mkokotezo mkubwa. Wanahabari walitumia tamathali za aina mbalimbali katika utunzi wa matini za kimazingira. Baadhi ya mifano ya

matumizi ya tamathali za usemi katika gazeti la *Taifa Leo* kwenye matini za kimazingira zilizochunguzwa imejadiliwa kwa kina katika sehemu inayofuata:

Nahau ni msemo wa kimafumbo ambapo jambo hueleweka kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja. Nahau huwa na msingi katika ulinganishi wa kiistiari. Matumizi ya semi na nahau katika matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* yalinuiwa kuipamba lugha na kuifanya iwe yenye mvuto kwa msomaji. Kwa upande mwingine, sitiari ni tamathali ya usemi ya ulinganishi usiotumia vilinganishi 'kama', 'mithili ya', 'ja' na 'mfano wa'. Msingi wa sitiari ni uhamishaji wa maana. Kwa mfano tunaposema kuwa, 'ujana ni moshi' pana uhamishi wa maana yaani 'ujana' kupewa sifa ya 'moshi'.

Sitiari hueleweka vizuri kwa kuzingatia dhana zake kuu ambazo ni: kilinganishi, kilinganishwa na msingi. *Kilinganishi* ni kile kinachotumiwa kama msingi wa kufananisha (moshi). *Kilinganishwa* kwa mfano, ni kile kinachofananishwa (ujana). *Msingi* ni sifa yenyewe ya ulinganishi kwa mfano katika sitiari ya 'ujana ni moshi' msingi ni ile hali ya 'kupita' au 'kuwepo kwa muda mfupi'. Matumizi ya sitiari katika matini za kimazingira yalikusudia kujenga taswira ya kile kilichosimuliwa akilini mwa wasomaji na wakati huohuo kuifanya lugha ya masimulizi kuwa na mvuto mkubwa kwa wasomaji.

Maswali ya balagha ni mbinu ya matumizi ya maswali ambayo hayajibiwi kwa kuwa majibu yake yako wazi au kwa nia ya kuchochea fikira au hisia kwa upande wa msomaji au msikilizaji. Maswali ya balagha ni mbinu muhimu katika sanaa ya usemaji au uandishi wa habari. Katika matini za kimazingira, katika gazeti la *Taifa Leo* wanahabari walitumia maswali ya balagha kuchochea hadhira kutafakari kuhusu matukio yaliyosimuliwa. Vichwa vya habari vilitumia mtindo wa kibalagha kuvuta makini ya wasomaji kwa matini

husika.Tunaweza kuhitimisha kuwa, wanahabari walitumia maswali ya balagha kuchochea hadhira kutafakari kuhusu matukio yaliyosimuliwa. Aidha, vichwa vya habari vilitumia mtindo wa kibalagha kuvuta umakini wa wasomaji kwa matini husika ili wasome makala nzima.

Methali ni msemo wa kimapokeo unaokumbukika na wenye muundo fulani unaotambulika na wanajamii na unaoelezea uzoefu unaokubalika na wanajamii kama ukweli fulani. Methali zinaweza kutumiwa na mwandishi kama ishara muhimu katika uchanganuzi na ufafanuzi wa kazi za fasihi. Hii ina maana kuwa methali zinaweza kudokeza dhamira ya mwandishi katika kutunga kazi ya fasihi. Hali hii huonekana bayana methali inapotumiwa kwenye anwani za matini zilizotungwa. Kimsingi, tunaweza kuhitimisha kuwa matumizi ya methali katika vichwa vya habari katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* ni ishara muhimu inayotumiwa na wanahabari kuwadokezea wasomaji wao ujumbe muhimu ulio katika matini bila kuwafichulia wazi bali kwa kuwachochea kusoma zaidi ili kupata ujumbe huo.

Tashihisi ni mbinu ya kisanaa ya kuvipa vitu visivyo na uhai sifa za kiuhai yaani vitu hivyo vinaweza kuwa hai na kutenda anavyofanya binadamu. Katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo*, tashhisi ilitumiwa kuyafanya majanga ya kimazingira yaonekane kama binadamu aliye na uwezo wa kudhulumu, kuharibu au hata kuangamiza kabisa. Kwa njia hiyo wanahabari walifanikiwa kutoa athari ya kihisia iliyokusudiwa kwa hadhira kama vile huzuni, kichomi au huruma.

Uradidi ni mbinu inayorejelea urudiaji wa maneno au sauti fulani kwa lengo la kusisitiza jambo linalozungumziwa katika matini. Urudiaji unaojitokeza katika matini za taarifa za

habari ni ule ulio sahili ambao ni rahisi kutambulika. Urudiaji sahili unahusu neno au msamiati fulani kwa lengo la kusisitiza ujumbe husika. Urudiaji wa neno au msamiati unaohusiana na sajili fulani unaweza kuangaliwa kwa namna mbili. Namna ya kwanza ni pale ambapo neno fulani lenye dhima maalum hurudiwarudiwa katika matini husika. Kimsingi, urudiaji katika matini za kimazingira ulitumiwa na wanahabari kwa nia ya kushadidi au kusisitiza kinachozungumziwa. Katika hali hiyo, maneno fulani yalirudiwa katika matini ili kutoa ujumbe fulani kwa mfano kuhusu utunzaji wa mazingira. Aidha, maneno yenye umuhimu wa kimawasiliano yalirudiwa ili kutoa athari ya kihisia katika hadhira. Kwa mfano urudiaji wa neno 'mafuriko' uliibua hisia za huzuni kwa wahanga walioathiriwa na janga hilo. Urudiaji huo ulinuiwa kueleza hisia za mwanahabari huhusu janga la kimazingira lililowasibu wanajamii. Aidha, urudiaji ulikusudiwa kuibua hisia za huzuni, ghadhabu, chukizo au furaha miongoni mwa wasomaji kutegemea ujumbe uliowasilishwa na waandishi wa makala.

Sifa za kiusemi ni sifa za kidiskosi zinazotumiwa katika uchunguzi wa kiisimumatini kueleza jinsi mshikamano na muwala unavyobainika katika matini. Isimumatini huchunguza matini andishi kwa lengo la kutathmini jinsi matini hizo zinavyotoa maana pamoja na zana za kiisimu zilizotumiwa na waandishi ili kuwasilisha maana wanazokusudia katika matini zao. Katika utafiti huu sifa za kiusemi zilizochunguzwa katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* ni zile za mshikamano na muwala.

Mshikamano ni istilahi inayotumiwa kueleza uhusiano wa maana uliopo katika matini. Kwa mujibu wa maelezo ya mshikamano katika matini huwepo iwapo ufasiri wa baadhi ya vipengele vya usemi unategemea vipengele vingine katika matini hiyo. Kufasiri mshikamano ni ile hali ya uwezekano iliyopo katika lugha kwa ajili ya kufanya matini

kuungana pamoja: yaani uwezo alio nao msemaji au mwandishi ili autumie katika mawasiliano yake. Hivyo, mshikamano kama mchakato daima unahusisha kipengele kimoja kuzungumzia kingine, ambapo, sifa kuu ya uhusiano wa kiushikamano ni ukweli kwamba kipengele kimoja huwa chanzo cha kufasiri kipengele kingine. Mshikamano hutokea katika hali inayoonyesha kwamba udhihirikaji wa kipengele kimoja ni dhanaawali ya kipengele kingine. Hii ina maana kuwa kipengele kimoja hakiwezi kueleweka au kufasiliwa vyema bila ya kuwa na ufahamu mzuri kuhusu kipengele kingine kilichotangulia. Mshikamano katika matini huonyeshwa kwa njia ya mahusiano ya urejelezi. Hili linamaanisha kuwa vipengele vinavyorejelea vipengele vingine hutumiwa ili kuashiria mshikamano katika matini. Mshikamano huashiriwa kupitia kwa matumizi ya vipashio vya kisarufi na vile vya kileksia/kimsamiati katika matini. Katika matini za kimazingira kwenye gazeti la *Taifa Leo* kuna maneno, vishazi na vifungu vya maneno kurejelea maneno na vifungu vingine katika matini moja iliyokuwa inasimuliwa.

Mshikamano wa kiusimulizi au kimatukio hutokea katika matini pale ambapo tukio fulani linafuatwa na jingine kwa namna ambayo lina mantiki na inakubalika kwa msomaji wa matini. Mshikamano wa kimantiki hudhihirika katika matumizi ya lugha yanayoonyesha mfuatano wa sentensi wenye mantiki. Aidha, hali hii hutokea tunapochunguza usimulizi wa matini na jinsi unavyotekelezwa katika makala inayochunguzwa. Mshikamano wa kiusemi hujengwa kwenye kaida ya mfuatano wa matukio katika matini, yaani baada ya tukio hili linafuata lile. Mfuatano huo huelezeka kwenye mada fulani bayana au dhamira inayokuzwa na kazi husika. Lugha inayotumiwa katika matini ina mpangilio mahususi wa sentensi na vipashio vyake. Mpangilio huo ndio unaojenga mshikamano wa kisintaksia katika matini. Mshikamano wa kirejelezi hubainika katika matini yoyote inayounda taswira

fulani ya ulimwengu wa kibunifu ambao unaweza kuwa umejengwa au kuundwa kwenye ulimwengu halisi. Ulimwengu huo huathiri usimulizi, uteuzi wa msamiati na ishara zinazohusika na uteuzi wa lugha. Kwa upande mwingine, mshikamano wa kisemantiki hubainikana kutokana na kuwepo kwa mfuatano mzuri wa sajili zinazotumiwa. Mshikamano wa kimtindo hudhihirika kupitia kwa uteuzi na matumizi ya lugha na usarifu wa mbinu tofauti za lugha zinazotumiwa na mwandishi wa matini katika ujenzi na udumishaji wa maana katika matini.

Muwala hufanya kazi na mshikamano. Muwala ni ule mwendelezo wa mawazo katika matini na mahusiano yaliyopo kati ya mawazo hayo. Wasomaji huelewa ujumbe kwenye matini endapo sentensi, mawazo, na maelezo yanayotolewa yanaingiliana pamoja kwa njia iliyo wazi. Utafiti huu ulichanganua matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* na kuthibitisha kuwa matini hizi zina muwala madhubuti kutokana na mawazo yaliyofungamana pamoja vizuri na kwa uwazi. Matini husika zinatumia lugha nyepesi, sahili na yenye mtiririko wa moja kwa moja. Hali hii inadhihirisha kuwa muwala ni zaidi ya muungano wa sentensi; yaani, ni ukamilifu wa wazo zima kwenye matini.

### 5.2.3 Lengo la Tatu Lilikuwa Kubainisha Ujumbe Ulioibuliwa Kutokana na Uteuzi wa Lugha na Mtindo wa Kuwasilisha Habari za Mazingira katika Gazeti la *Taifa Leo*

Sehemu hii inabainisha aina za ujumbe ulioibuliwa kupitia matumizi ya lugha na mtindo wa kuwasilisha habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Aidha, dhima zilizokusudiwa na jumbe hizo zimeelezwa.

#### 5.2.3.1 Aina za Jumbe Zilizoibuliwa Kutokana na Matumizi ya Lugha na Mtindo wa Uwasilishaji wa Habari za Mazingira katika Gazeti la *Taifa Leo*

Waandishi wa matini huumba kazi zao kiupekee kwa kufinyanga lugha kiufundi na kutumia mitindo teule ya kutoa ujumbe wanaowasilisha ili kutimiza malengo fulani ya kimawasiliano. Malengo hayo yanaweza kubainishwa kwa kuchunguza athari za kimawasiliano za ujumbe unaotolewa katika matini husika.

Utafiti huu ulibainisha aina mbalimbali za maana zilizoibuliwa kutokana na matumizi ya lugha na mtindo wa uwasilishaji wa habari za mazingira katika gazeti la *taifa leo*:

Maana dhamirifu hujulikana pia kama maana ya kimatini. Maana dhamirifu hudhihirika kutegemea jinsi ujumbe unaowasilishwa katika lugha ulivyopangwa au kuratibiwa. Kimsingi ni kwamba maana dhamirifu inahusu upangaji wa vipengele vya kimawasiliano ambavyo huamua maeneo yanayosisitizwa. Upangaji huo hutegemea umuhimu wa mada, kiini na msisitizo. Kwa ujumla, lugha huteua na kupanga maneno kutegemea nini hasa kinachosisitizwa. Katika matini za kimazingira kilichosisitizwa ni majanga yaliyohusika, athari za majanga yenyewe au ujumbe muhimu uliotolewa na mwanahabari. Katika matini hizo, msisitizo wa taarifa za kimazingira unadhihirika kupitia sifa mbalimbali za kigrafolojia kama vile matumizi ya herufi kubwa, hati za mlazo, maandishi yaliyopoza au kupigia mstari maneno pamoja na matumizi ya wino uliokolezwa wa rangi nyekundu.

Maana akisifu hujulikana pia kama maana zalishi au maana fumano. Maana akisifu inahusiana na kauli ambazo zina maana nyingi au mseto wa maana. Maneno yenye maana nyingi au maneno ya kipolisemi huwa na maana akisifu. Hata hivyo, huwa kuna maana kuu miongoni mwa maana mbalimbali zinazojitokeza. Hii ina maana kuwa kuna fahiwa fulani ya neno inayotamalaki ambayo hutawala fahiwa nyingine za neno hilo. Fahiwa zinazotawaliwa hufifia muda unapoendelea kuyoyoma na hatimaye hutoweka kabisa. Kwa

mfano neno ‘posho’ lilimaanisha chakula chochote kile lakini sasa linamaanisha marupurupu anayopewa mtu kwa ajili ya majukumu, takrima au usumbufu. Maana ya pili ndiyo inayotawala na kutamalaki ile ya awali. Maana akisifu hutokana na maana mbili au zaidi zilizobwiwa. Fahiwa moja ya neno hutuelekeza katika fahiwa nyingine. Kwa kawaida maana moja huwa imeshika kani kimatumizi kiasi cha kwamba imehusishwa na kuzua maana zingine za ziada. Katika zama hizi za mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha magonjwa hatari kama Corona kuna istilahi za zamani ambazo zilipata maana akisifu na maana halisia imefifia kimatumizi.

Maana athirifu hujulikana pia kama maana shawishi. Maana athirifu huhusiana na hisia au mielekeo ya mzungumzaji kuhusu hadhira yake au mada anayoizingatia katika mawasiliano. Maana athirifu hubainika kupitia kwa uteuzi wa maneno (Saeed, 2009). Kuna baadhi ya maneno ambayo huashiria hisia chanya kwa mfano: upendo, uzuri, furaha na bashasha. Kwa upande mwingine kuna maneno yanayoibua hisia hasi kwa mfano kero, ghadhabu, chuki na bughudha. Vihisishi hudokeza hisia za kiakili za mzungumzaji kwa mfano: hisia za furaha: oyee, oyaa; hisia za huzuni: pole, hamadi; hisia za mshtuko: afanalek, la, lo, alaa, amaa, aisee; hisia za mshangao: aa, eti, ati, salale, ajabu, kumbe, lahaula; hisia za bezo: aka, zii, sasa.

Kuna wakati ambapo lugha hudokeza hisia na mielekeo ya watumiaji kuhusu maana ya kuzungumzia. Aina hiyo ya lugha hudokeza na kutoa fununu kumhusu mshiriki. Kupitia lugha ni rahisi kubainisha mitazamo kuhusu washirika. Aidha, lugha inaweza kuonyesha dharau, furaha, mshangao au hata huzuni. Hali hizi ndizo ambazo hutuelekeza katika hisia za wahusika. Aghalabu maana ya kihisia hutegemea aina nyingine za kimaana kama vile maana bwiwa, maana ziada na maana kimtindo. Mara nyingi maana kiuathirifu

hubainishwa kupitia matumizi ya viingizi au vihusishi ambavyo hutokea katika mawasiliano. Viingizi ni maneno ambayo hayana jukumu lingine lolote ila tu kuibua hisi na kuathiri maana.

Maana ya kimtindo hujulikana pia kama maana ya kijamii. Maana ya kimtindo au ya kijamii hudhihirika wakati ambapo ruwaza fulani ya unenaji, aina fulani ya lugha au aina fulani ya uneni inahusishwa na muktadha mahususi wa kijamii. Ni jambo la kawaida kwamba uteuzi wa maneno na miundo ya mzungumzaji hudhihirisha usuli wake wa kijamii, kieneo, kijografia na hata kiuchumi. Uteuzi huo unaweza pia kuthibitisha kiwango cha kufahamiana kilichopo baina ya mzungumzaji na mpokezi wa ujumbe. Msisitizo huwa kwenye mitindo mbalimbali inayotofautiana ambayo inaweza kutumiwa na mwandishi wa makala.

Ujumbe wenye maana halisi ni ule unaoakisi maana ya kimsingi maana au maana ya kimantiki ya matini. Hii ndiyo maana ya kwanza na ya kawaida ya matini ambayo hufafanuliwa kwa hali ya kawaida bila kufumbata ujumbe fiche. Hii ina maana kuwa matini huwa na ujumbe wenye maana ambayo haijaathiriwa kwa njia yoyote ile na muktadha wala hisia zinazohusiana na tukio la mawasiliano. Kimsingi, kuna maana halisi ya kila neno ambayo huchukuliwa kuwa inajulikana miongoni mwa wanajamii wanaozungumza lugha fulani wanaokusudiwa kuupokea ujumbe unaowasilishwa.

Kutokana na hali kuwa matini za kimazingira hutumia lugha ya kisayansi ambayo ni rasmi, matumizi ya lugha ya kitamathali ni machache; badala yake kuna matumizi ya lugha ya kawida inayowasilisha maana halisi. Maana halisi katika matini za kimazingira ilibainishwa kutokana na maneno yaliyotumiwa na wanahabari katika sentensi. Kimsingi

ni kuwa wasomaji wanatarajiwa kuipata aina hii ya maana kwa njia ya moja kwa moja bila utata wowote. Maana halisi katika matini za kimazingira ilikuwa msingi wa mawazo waliyo nayo wanajamii kuhusu dhana, vitu na hali mbalimbali za kimazingira katika jumuia-lugha wanamoishi. Kwa mfano matini zilizozungumza kuhusu uharibifu wa misitu Mau, ugonjwa wa Corona na kubadilika kwa tabianchi ulitolewa kwa njia ya moja kwa moja ili kueleweka kwa urahisi na hadhira.

Maana halisi hudhihirika kwa wasomaji kwa njia ya moja kwa moja bila utata wa aina yoyote. Maana halisi ndiyo msingi wa mawasiliano wa habari za mazingira zinazowalenga wasomaji wa kawaida katika jamii. Isitoshe, maana halisi hutokana na mfumo wa kimofolojia na kisintaksia; kwa pamoja mifumo hii humwezesha mtumiaji wa lugha kutambua sifa bainifu za kila neno na dhana inayorejelewa katika matini ya kimazingira. Matini zote za kimazingira zilizochunguzwa katika utafiti huu kutoka katika gazeti la *Taifa Leo* ziliakisi ujumbe uliosheheni maana halisi. Hata hivyo, wanahabari walichanganya lugha ya kawaida na lugha ya kitamathali pamoja na lugha ya kitaaluma ili kutimiza malengo fulani ya kimawasiliano.

Matini za kimazingira zilizochunguzwa katika utafiti huu zilisheni ujumbe wenye maana ashirifu. Ujumbe wenye maana ashirifu ni ule ulio na maana matlaba au maana ya ziada. Hii ina maana kuwa kuna maana ya ziada iliyoshehenezwa katika matini ya kimazingira ambayo inahitaji jicho la kimakini ili kupata maana hiyo iliyoghubikwa. Kimsingi, maana ashirifu hujumuisha vipengele vya maana halisi ya matini pamoja na ufasiri wa kibinafsi wa mtu wa kile ambacho kinawasilishwa katika mawasiliano na mtunzi wa matini.

Hali hii inamaanisha kuwa wanahabari walioumba matini za kimazingira zenye ujumbe wa maana ashirifu hawakumlenga msomaji wa kawaida katika jamii bali sehemu fulani ya wasomaji wenye tajriba na uzoefu wa kufasiri na kuelewa ujumbe uliokusudiwa. Ufasiri huo hutegemea tajriba ya kibinafsi ya mpokezi wa ujumbe. Hii ina maana kuwa maana ashirifu hutofautiana kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kutegemea tajriba ya mtu katika mawasiliano yanayotendeka. Hali hii ilibainika katika matini za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* wakati ambapo ujumbe, kwa mfano, uliwalenga wataalam wa mazingira, wataalam wa afya, wanazuoni, watu wazima na aina nyingine za hadhira zenye tajriba fulani. Safu za kisayansi kama vile Shina la Uhai, Afya ya Jamii, Kilimo, Sayansi na Mazingira na Akilimali zililenga hadhira ya aina hiyo. Maana ashirifu inaweza pia kutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine.

Utafiti huu ulibainisha kuwa matumizi ya istiari, methali, nahau na tamathali nyingine za usemi katika matini za kimazingira zilinuiwa kuibua sifa za ziada za kisemantiki ambazo zilihusiana na maana ashirifu. Kwa mfano, maana ya methali na tamathali za usemi inatokana na uashirifu. Katika matini za aina mbalimbali huwa kuna taashira ambazo huwa na maana ashirifu inayotofautiana kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine. Kwa mfano, katika jamii ya Waswahili 'sungura' huchukuliwa kama ishara ya ujanja naye 'kobe' akasimamia hekima. Kwenye jamii za kimagharibi 'mbweha' ndiye ishara ya ujanja. Kimsingi, maana ziada ni jumla ya maana zote ambazo hurejelewa au huhusishwa na neno fulani. Maana ziada ni maana ambayo hujengwa kutokana na maana bwiwa na kuongezewa sifa zaidi ambazo kirejeleo kinatarajiwa kuwa nazo. Ni maana iliyo pevu zaidi kuliko ya maana halisi. Maana ashirifu au sifa zaidi hutokana na matarajio ya kisaikolojia na kijamii kuhusiana na kirejelewa.

#### 5.2.3.2 Hitimisho Kuhusu Dhima ya Ujumbe Ulioibuliwa Kutokana na Matumizi ya Lugha na Mtindo wa Uwasilishaji wa Habari za Mazingira katika Gazeti la *Taifa Leo*

Utafiti huu ulichunguza uteuzi wa lugha na mtindo uliotumiwa na wanahabari katika kuwasilisha habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa ujumbe ulioibuliwa ulikusudiwa kutimiza dhima mbalimbali kama zinavyofafanuliwa katika sehemu hii:

i) Kushawishi wasomaji.

Sifa kuu isiyo ya kiisimu katika mtindo wa kushawishi ni ule mwelekeo wa kutoa taarifa kwa kumwelekeza msomaji akubali msimamo, mtazamo au upande fulani wa mawazo. Hii ina maana kwamba mwandishi wakati wote hujitahidi sio tu kutoa habari au taarifa fulani, bali pia kuonyesha msimamo wake na uhusiano wake kwa hayo anayoyaandika na kuibua uhusiano maalumu wa wasomaji kwa yale wanayoyasoma. Ili mawasiliano ya namna hii yaweze kutekelezwa vizuri zaidi na kwa ufanisi wa juu ni lazima lugha mguso itumike. Jambo hili huathiri sana mfumo wa matumizi ya zana za kiisimu katika mtindo wa mawasiliano ya magazetini na shughuli za kimazingira, kwani zana zote za kiisimu zinajitokeza katika hali hii ya kutaka kuleta mguso mkubwa katika lugha, na hivyo kuwasisimua na kuwapendeza wasomaji na kwa hali hiyo kuwashawishi kukubali taarifa zinazotolewa.

ii) Kukashifu matukio anuwai.

Matini ya habari inayolenga kukashifu shughuli, tabia au matendo fulani ya binadamu itatumia lugha ya kushutumu, kukashifu na kuonyesha madhara ya vitendo hivyo. Wanahabari wa matini za kimazingira waliolenga kukashifu

shughuli na vitendo vya binadamu vilivyoathiri mazingira walitumia lugha ya kukemea na kukashifu vitendo hivyo.

iii) Kutahadharisha hadhira.

Matini zinazolenga kutahadharisha hadhira hutumia lugha ya kuonya na kuhimiza jamii kuwa makini kutokana na uwezekano wa kuzuka kwa majanga au hali hatari. Lugha hiyo hukusudia kuwafanya wanajamii kuchukua tahadhari ili kujiepusha na majanga hayo.

iv) Kuhamasisha hadhira. Matini zenye mwelekeo wa kuhamasisha hutumia lugha ya

kitaaluma inayoelimisha na kufundisha jamii kuhusu mambo yanayopuuzwa kwa kutoeleweka vyema ambayo yanaweza kuwa na madhara au pengine kuhusu faida za mambo fulani.

v) Kutamausha Hadhira

Matini yenye mwelekeo wa kutamausha hutumia lugha inayokatisha tamaa kwa kuonyesha ukosefu wa matumaini. Lengo la kutumia lugha ya aina hii ni kuonyesha mateso, dhiki na mashaka yanayowakabili wahanga wa majanga ya kimazingira

vi) Kuchochea ari ya pamoja ya hadhira.

Matini zinazolenga kuchochea ari ya pamoja hutumia lugha ya kutia hamasa na kuchochea ghadhabu kwa watu kuchukua hatua za pamaoja kuauni hali fulani inayowakabili. Lugha ya aina hii inalenga kuamsha hisia za pamoja ili kufanya uamuzi utakaowanufaisha watu wote wanaokabiliwa na tatizo fulani.

Sehemu hii ilizingatia ufafanuzi wa hitimisho la matokeo muhimu ya utafiti. Ilianza kwa kutoa madhumuni ya utafiti ambayo yalikuwa uchanganuzi vipengele vya lugha

vilivyoteuliwa katika kuripoti taarifa za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*, kutathmini mtindo uliotumiwa na waandishi katika kuripoti habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* na kubainisha aina na dhima za ujumbe ulioibuliwa kupitia uteuzi wa lugha na mtindo wa kuwasilisha habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*.

Aidha, ilitoa upambanuzi wa hitimisho la matokeo kwa kuonyesha jinsi unalandana na malengo ya utafiti. Sehemu inayofuata inahusu mapendekezo ya utafiti huu.

## 5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu unapendekeza na kutoa ushauri kuhusu mambo mbalimbali yanayostahili kutiliwa maanani ili yawe suluhu kwa tatizo ambalo limetafitiwa. Utafiti wetu umebainisha kwamba wanahabari katika gazeti la *Taifa Leo* katika kipindi kilicholengwa walifaulu kuwasilisha habari za mazingira kwa kuteua vipengele vya lugha kama vile mbinu ya udhamiriaji, usimulizi wa nafsi, matumizi ya toni, uteuzi ya miundo ya sentensi maalum, matumizi ya takwimu, na vile vile uteuzi maalumu wa mada. Hii ni habari njema kuhusu taaluma ya uanahabari kwa kuwa jambo hili linadhihirisha kwamba wanahabari husika wana umilisi wa kiisimu wa kuweza kutoa taswira halisi ya hali ilivyo kuhusu suala nyeti la mazingira na kuiwasilisha kwa jamii kupitia lugha ya Kiswahili. Jambo hili pia linaonyesha kwamba lugha ya Kiswahili ina uwezo wa kukidhi mahitaji ya watumiaji wake, hasa ile haja ya kupata kujua hali ya mazingira yao.

Lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi na pia ya taifa kikatiba nchini Kenya, jambo linaloonyesha kuwa inaweza kutumika katika mijadala muhimu ya kitaifa kutokana na huo uwezo wa kueleza masuala ambayo kwa sasa ni nyeti na pia changamoto kwa kila taifa duniani kwa ujumla. Ufahamu kamili wa mazingira miongoni mwa jamii ni muhimu kwa

kuwa ufahamu huu ndio huiwezesha kutangamana na mazingira yao kwa njia ifaayo. Mabadiliko ya tabianchi ni suala ambalo linahangaisha ulimwengu wote na kutokana na hili ni busara kwa kila mtu kuelewa hali ilivyo ili ashiriki au atoe mchango wake katika harakati ya kuuokoa ulimwengu .

Uelewaji wa habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* pia ulichangiwa na uzingatiaji wa mitindo mwafaka.kwa upande wa wanahabari. Waandishi wa habari walihusisha sifa za grafolojia, kiothografia, kileksia na kiusemi na hili ni jambo muhimu. Hata hivyo, ili umilisi huu uweze kusaidia wengine unahitaji kufungamanishwa na utendaji wa hali na kiwango sawa. Uchunguzi wa mpangilio wa matini kwenye gazeti la *Taifa Leo* zilizohusu habari za kimazingira unadhihirisha umakini uliotumiwa katika ujenzi wa matini zenyewe na wanahabari. Taarifa za habari katika gazeti la *Taifa Leo* zimepangwa kwa uangalifu, umakini na utaratibu mwafaka katika gazeti lililochapishwa. Jambo hili lilisaidia uelewekaji wa habari na msomaji.

Waandishi wa matini waliumba kazi zao kiupekee kwa kufinyanga lugha kiufundi na kutumia mitindo teule ya kutoa ujumbe wanaowasilisha ili kutimiza malengo fulani ya kimawasiliano. Malengo hayo yanaweza kubainishwa kwa kuchunguza aina na dhima za ujumbe unaotolewa katika matini husika. Kwa kuzingatia kigezo hiki, utafiti huu uligawa ujumbe uliowasilishwa na wanahabari katika aina mbalimbali kutegemea athari zake za kimawasiliano. Aina za ujumbe zilizodhihirika kutokana na uchanganuzi wa mtafiti ni kama vile ujumbe wa kimazingira wenye maana dhamirifu, maana akisifu, maana athirifu, maana kimtindo, maana halisi na maana ashirifu. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, maana zote zilikuwa na mwelekeo chanya. Hili lina maana kuwa ujumbe alioupata msomaji wa gazeti la *Taifa Leo* ulikusudiwa kumfanya ayafahamu masuala ya mazingira

kwa undani na pia aweze kutangamana na mazingira yake kwa njia inayomfaidi kama msomaji na pia kuyafaidi mazingira yake.

Pamoja na ufanisi wa kimawasiliano baina ya mwandishi wa habari na msomaji wa taarifa za mazingira katika gazeti la T*aifa Leo* uliobainishwa na utafiti huu, mtafiti aligundua kwamba katika juhudi za kueleza matukio ya kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* wanahabari walikosa kuzingatia mambo ambayo ni ya kimsingi katika utoaji wa habari. Kwanza kabisa, baadhi ya matini zilizohusu taarifa za kimazingira katika gazeti la *Taifa Leo* katika kipindi teule yalikuwa na makosa ya tahajia na kisarufi. Makosa ya aina hii yana uwezo wa kutatiza mawasiliano kwani hayaangazii maana iliyokusudiwa na mwandishi. Hili linaashiria kuwa msomaji wa matini zenye makosa ya tahajia na kisarufi hataelewa ujumbe na hivyo hatakuwa na ufahamu utakaomwezesha kutangamana na mazingira yake ipasavyo. Kutokana na haya, waandishi wanashauriwa kuhariri kazi zao wenyewe kwa makini ili kuepuka makosa ya aina hii ambayo hupotosha ujumbe unaotolewa. Isitoshe,wahariri wa habari katika gazeti la T*aifa Leo* wanashauriwa kupitia taarifa za mazingira na kuchuja habari kabla ya kuchapishwa habari hizo.

Aidha, utafiti huu ulibainisha kwamba baadhi ya matini kuhusu habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* zilisheheni utohozi wa dhana na maneno ambao hauambatani na kanuni za lugha ya Kiswahili. Utohozi wa aina hii ni kikwazo kwa mawasiliano kwa sababu msomaji hatapata ujumbe uliodhamiriwa na mwandishi. Vilevile, msomaji huenda akakosa kutilia maana kilichoandikwa ikiwa msamiati uliotumika hajafahamiana nao. Ni muhimu kutaja kwamba utohozi huu pia una uwezo mkubwa wa kudunisha lugha ya Kiswahili kwa kuwa hali hii inapalilia mtazamo kuwa kila mtu anaweza kuunda msamiati apendavyo na kuutumia apendavyo. Mtafiti anatoa ushauri kwa waandishi wa habari kwamba

wanatakiwa kujikita kwenye matumizi ya msamiati na istilahi ambazo zimeidhinishwa na vyombo ambavyo kirasmi vimetwikwa jukumu la uundaji wa msamiati na istilahi.

Hali kadhalika, utafiti huu ulibainisha kwamba waandishi wa habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* walitumia mtindo wa lugha usio rasmi. Katika baadhi ya matini za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* kulikuwa na matumizi ya maneno ya *Sheng'*. Matumizi hayo yana uwezo mkubwa wa kufanya msomaji akose kuelewa ujumbe unaotolewa, na zaidi mno, ikiwa msomaji husika hana ufahamu wa *Sheng'*. Ni hekima kusema kwamba mtafiti anafahamu fika kwamba kuna kundi miongoni mwa hadhira ya mwandishi wa gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya ambalo hutumia *Sheng'* kama lugha yao ya mawasiliano na kwamba kundi hili halina tatizo la kuelewa *Sheng*`. Hata hivyo, lugha rasmi iliyoteuliwa ili itumike katika muktadha uliolengwa na utafiti huu ni Kiswahili. Matumizi ya lugha nyingine tofauti na Kiswahili katika kuwasilisha habari za mazingira yalichukuliwa kuwa mtindo usio rasmi. Ifahamike kwamba umuhimu wa lugha hutegemea majukumu yaliyotwikwa lugha hiyo katika jamii. Matumizi ya Sheng` katika kuwasilisha habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* au kuchanganya ndimi kwa mujibu huu ni ukiushi wa matumizi rasmi ya lugha. Isitoshe, kuchanganya matumizi ya Kiswahili na *Sheng'* ni kudunisha hadhi yake, bila kutaja kwamba inapotosha hadhira ambayo inang`ang`ana kudumisha matumizi sanifu ya lugha ya Kiswahili. Kutokana na haya, waandishi wa habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* wanashauriwa kuzingatia matumizi ya Kiswahili sanifu hasa inapozingatiwa kwamba lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi kikatiba na kwamba imetwikwa jukumu la kuwasilisha habari rasmi nchini Kenya. Njia moja ya kuhakikisha kwamba wanahabari ambao wanatumia lugha ya Kiswahili katika utoaji wa habari wana ufasaha wa kutosha ni kuwafundisha kozi za taaluma ya

uanahabari kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, wataalamu katika nyanja mbalimbali wanashauriwa kukionea fahari Kiswahili ili kuwa vielelezo mwafaka kwa kizazi cha leo na kesho.

Kulingana na matokeo ya utafiti huu, ilibainika kwamba ukosefu wa ufasaha katika matumizi lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa udhaifu unaodhihirishwa na waandishi wa habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Suala hili linahusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa ujumla hasa umantiki katika mijadala inayofafanua habari za mazingira. Tatizo la ukosefu wa ufasaha katika lugha hutokana na uduni wa umilisi wa lugha yenyewe. Waandishi wa habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* wanashauriwa kumakinikia wenzo wanaotumia katika kazi yao ya kila siku na hasa kule kutathmini ufaafu wa maneno katika muktadha husika. Isitoshe, wahariri wa habari katika gazeti la T*aifa Leo* wanashauriwa kupitia taarifa za mazingira na kuchuja habari kabla ya kuchapishwa habari hizo. Aidha, wanaohusika na upangaji lugha nchini wanahimizwa kwamba labda huu ndio wakati ufaao wa kuweka mipango mwafaka kuhusiana na matumizi ya lugha mbalimbali nchini Kenya. Vilevile ni jambo la busara kukifanya Kiswahili somo la lazima katika viwango mbalimbali vya elimu kama njia mojawapo ya kuhakikisha kuwa wanaotumia lugha hii wanafanya hivyo kwa ufasaha unaofaa.

### 5.4 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Utafiti huu ulichunguza uteuzi wa lugha na mtindo katika uwasilishaji wa habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya. Hata hivyo, haiwezekani kuchunguza vipengele vyote vya lugha na mtindo wa kuwasilisha habari za mazingira katika utafiti

mmoja. Utafiti huu ulichunguza uteuzi wa vipengele vya lugha katika kuripoti habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* kuanzia Januari 2021 hadi machi 2022.

Utafiti huu ulichanganua data kuhusu matumizi ya lugha katika kuwasilisha habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* ukiongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Usemi. Hata hivyo, pana haja ya utafiti mwingine kufanywa na watafiti wengine kuhusu matumizi ya lugha katika kuripoti taarifa za mazingira kwa kutumia Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ambayo inaegemea muktadha wa jamii, uongozi na utabaka katika jamii ili suala la mazingira lifahamike zaidi kwa mkondo huo.

Utafiti huu ulichunguza uteuzi wa vipengele vya lugha katika kuripoti habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo* kuanzia Januari 2021 hadi machi 2022. Utafiti huu unapendekeza utafiti mwingine ufanywe na watafiti wengine ili suala la mielekeo ya wanahabari kuhusu matumizi ya lugha katika kuwasilisha habari za mazingira libainishwe.

Utafiti huu ulichunguza uteuzi wa vipengele vya lugha ya Kiswahili katika kuripoti habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Utafiti huu unapendekeza utafiti mwingine ufanywe na watafiti wengine ili suala la matumizi ya lugha tofauti na Kiswahili katika kuwasilisha habari za mazingira katika gazeti tofauti na gazeti la *Taifa Leo* lifahamike zaidi. Habari katika gazeti la *Taifa Leo* mara nyingi hufanana na habari katika gazeti la *The Daily Nation*. Uchunguzi linganishi wa uteuzi wa vipengele vya lugha ya Kiingereza katika kuripoti habari za mazingira katika gazeti la *The Daily Nation* huenda ukatoa mwanga zaidi kuhusu habari za mazingira.

Mazingira ni suala mtambuko na nyeti kitaifa na kimataifa. Mazingira yanaathiri maisha ya kila kiumbe kila siku kwa njia moja au nyingine. Kutokana na haya, pendekezo

linatolewa kwamba utafiti mwingine ufanywe na watafiti wengine kuhusu Isimu Ikolojia ili kubainisha jinsi lugha zinavyofanya kazi, kuingiliana na jinsi zinavyoathiri mazingira na ikolojia zinamotumika. Utafiti unaopendekezwa hapa ni ule utakaohusisha lugha zinazozungumzwa nchini Kenya.

Utafiti huu ulichunguza uteuzi wa vipengele vya lugha andishi katika kuripoti habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Utafiti huu unapendekeza utafiti mwingine ufanywe na watafiti wengine ili suala la matumizi ya lugha semwa katika vyombo vya habari kama vile runinga na redio katika kuwasilisha habari za mazingira lieleweke zaidi katika muktadha wa mazungumzo.

Utafiti huu ulichunguza uteuzi wa vipengele vya lugha andishi katika kuripoti habari za mazingira katika gazeti la *Taifa Leo*. Utafiti huu unapendekeza utafiti mwingine ufanywe na watafiti wengine ili suala la mazingira katika sanaa bunifu na sanaa tendaji lipewe mwanga .

## MAREJELEO


Adegoju, A. (2008). *Graphology as a Signifying System*. In Ateyo, R.O. (ed.) University of Ibadan Official Bulletin. *Papers in English and Linguistics*, Vol. 9

Ahuja, B.K. (2014). *Mass Media Communication:Theory and Practice*. New Delhi: Saurabh Publishing House.

Ansdabehere, S. *et al* (2005).*Unrepresentative information:the case of newspaper reporting on campaign finance*.htttp://www.fec.gov//finance/ftpsum.htm

Alexander, R. (2008). *Framing Discourse on the Environment: a Critical Discourse Approach*. New York: Routledge.

Armando, J .*et al* (2017). *The Effects of Strategic News Sources on Media Coverage*. Centre for Applied Research at NHH, Helleeien 30, 5045 Berger, Norway. https://doi.org/10.1016/s.infoecop 01.2017.10.002.

Barasa, S.N. (2010). *Language, Mobile Phones and Internet: a Study of SMS Texting, Email, im and SNS Chats in Computer Mediated Communication (CMC) in Kenya*. LOT Janskerkhof 13 :The Netherlands.

Buffon, G.(1930). *Buffon`s Discourse on Style*. Paris: Librairie Hatier Publishers

Capella, J.N, & Jamieson, K.H. (1997.) *The Spiral Cynicism: the Press and the Public Good*. New York: Oxford: Oxford University Press.

Chepkorir, F. (2016).*Uchanganuzi wa Mtindo katika Tahakiki ya Gazeti la Taifa Leo*.Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu, UON. (Haijachapishwa).

Chukwu, E. (2010). Graphological Elegance of English Punctuation Notations. *Journal of Religion and Human Relations*, Vol., 1 (3)

Conboy, M. (2010).*The language of newspapers*. Continuum International Publishing Group. New York.

Cruse, D.A. (2010). *Meaning in Language: an Introduction to Semantics and Pragmatics*. Oxford: Oxford University Press.

Dorroh, J. (2015). *Environmental Reporting and Media Development: Equiping Journalists with the Training and Tools to Cover a Critical Beat*. Washington DC: CIMA.

Fairclough, N. & Wodak, R. (1997). Critical discourse analysis. In Van Dijk (ed.) *Discourse as social interaction*. London:SAGE Publications.

Fairclough, N. (2003). *Analysing Discourse: Textual Analysis for Social Research*. London: Routledge Publishers.

Florin B. (2016).*Explaining media-centred reporting styles :an internationally comparative typology and explication of election campaign in TV evening news*. Zuric Open Repository and Archive.University of of Zuric Main Library.www.zora.uzh.ch

Flowerdew, J. & Mahlberg, M. (2009). *Lexical cohesion and corpus linguistics*. Amsterdam: John Benjamins Publishing Company.

Fowler, R. (1975). *Style and structure in literature :essays in the new stylistics*. Oxford: Blackwell.

Freeman, D. (1996). *Styles of News Reporting:Political News and Ideology*

Gathenya, E.W. (2018). *Mielekeo na mtindo wa shafi adam shafi katika riwaya za kuli na haini*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

Gerhard, A. (1986). *New trends in graphemics and orthography*. Berlin: De Gruyter

Gillian, B. & Yule, G. (1983). *Discourse analysis*. New York:Cambridge University Press.

Gitau, R.W. (2015). *Sajili ya matangazo ya biashara:mtazamo wa kipragmatiki*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi .Haijachapishwa.

Gomez-Jimenez, E. (2015). An introduction to graphology: definition, theoretical background and levels of analysis. In *Miscelanea: a journal of English and American studies*, 5(1):17-85

Griffiths, P. (2006). *English semantics and pragmatics*. Edinburgh: Edinburgh University Press.

Grundy, P. (2008). *Doing pragmatics*. London: Anold Hodder Publishers.

Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya sarufi ya kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers

Haynes, J. (1995). *Style*. London and New York:Routledge.

Hoffman, J. & Hawkins, V. eds (2015). *Communication and peace: mapping an emerging field*. London and New York: Routledge

Hojjati, N. & Muniandy, B. (2014). The Effects of Font Type and Spacing of Text for Online Readability and Performance. Universiti Sains Malaysia, Malaysia. *Contemporary educational technology*, 2014, 5(2), 161-174

Huang, Y. (2007). *Pragmatics*. Oxford: Oxford University Press

Ingram, D. (2012). *The news manual: language and style basics*. Retrieved from: https://www/the news manual.net/

Ireri, K. (2017). *Exploring journalism and mass communication training in Kenya:A national survey*. Sagepub.com/journalspermissions.nav, D01:10.1177/1077695817720678 jmce.sagepub.com

Ireri, K. (2012). *Kenyan journalists:A study of demographics, job satisfaction, news values and perceived autonomy*. School of Journalism, Indiana University-Blooomington 2012 AEJMC conference, Chicago, Illinois Aug 9-12

Jamah, A. (2015). *Kenya`s print media coverage of religious communities in the Mandera and Garissa terrorist attacks*. M.A Thesis, UON. Unpublished

Jagero, J.A (2015). *Uchanganuzi wa usemi wa kisiasa kuhusu nchi ya Kenya katika blogu teule zilizoandikwa katika Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Maseno, https://repository.maseno.ac.ke/handle/123456789/990

Jagero, A.J., Mohochi, E.S. & Indede, F. (2013). The Use of Kiswahili in blog discourse and the effect on its development. In *International Journal of Humanities and Social Science*,Vol. 3 No.14, pp.192-199

Jamieson, K.H. & Waldman, P. (2003). *The press effect*. Oxford: Oxford University Press.

Kairu, W.M .(2005). *Uhalisia na mtindo wa Ken Walibora katika fasihi ya watoto*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

Kamenchu, F.M. (2015). *A Study of how social media have changed newsroom operations in kenya:a case of the Standard Group and Nation Media Group*. MA Thesis, UON, Unpublished.

Kariuki, M. (2017). *Nurturing our environment for sustainable development*. Nairobi: Glenwood Publishers

Kearns, K. (2000). *Semantics: modern linguistics series*. London: Palgrave Macmillan (UK)

Kevogo, A.U. & Kevogo, S.A. (2014). *Matumizi ya lugha katika mitandao ya kijamii: mfano wa Kiswahili katika blogu za kikristo* ( Mswada haujachapishwa)

Kibuga, K.F (2009). *Elimu ya mazingira kwa shule za msingi: toleo la milima ya TAO la mashariki: kiongozi cha mwalimu*. Desk Top Productions Ltd

Kisang, A. (2014). Reporting terrorism among kenyan media: should journalists be cautious? *Journal of Media and Communication Studies*, Vol.6(5),82-82

Kovach, B.et al (2001). *The Elements of Journalism*. New York: Three Rivers Press.

Korir, G. & Nabushawo, C.N. (2021). Print media and global pandemics:a look at the news report in the kenyan press during the COVID-19 pandemic. *Global Media Journal* Vol.19 No. 37:230. ISSN 1550-7521

Leech, G.H. & Short, M.H. (1981). *Style in fiction: A linguistic introduction to english fiction prose*. England:Longman Group Ltd.

Leech, G. (1969). *A linguistic guide to English poetry*. London: Longman.

Lodge, D. (1972). *20th century literary criticism*. London:Longman.

Loughran, G.(2010). *Birth of a Nation*. London:I.B.Taurus & CO Ltd

Lusekelo, A. (2017). Language Usage, Style and Content of Mass Media Outlets in Tanzania: the Case of "Hardcore" and "Tabloid" Kiswahili Newspapers. In *Lugha na Fasihi katika Karne ya Ishirini na Moja*. Wah: Kandagor M. na Ogechi, N.,Vierke,C. Uk, 375.

Lynch, S. *et al* (2002). *Analysing Newspaper Content: A How–to Guide*. Readership Institute: Northwestern University.

Macharia, H.N. (2015). *Examining Lexical Style in Youth Magazines in Kenya:A Case Study of Zuqka and Pulse Magazines*. Unpublished M.A Project, UON.

Maina, R.W. (2011). *Mbinu za Mawasiliano katika Matangazo ya Runinga nchini Kenya*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

Maxwell T. B. (2009). *We Speak for the trees: media reporting on the envirnment*. Ann. Rev.Environ.Resour.2009.34;431-57 www.annualreviews.org

Media Council of Kenya (2014). *Deconstructing Terror: Assessing Media`s Role in Religious intolerance and radicalization*.

Mbugua A. M. ( ) .*Competetive Strategies Adopted by Mainstream Daily Print Media Firms in Kenya*. MBA Thesis, UON.Unpublished

Mieke, B. (1985). *Narratology: Introduction to the Theory of Narrative*. Toronto: University of Toronto Press

Mohamed, A.M. (1986). *Sarufi Mpya*. Nairobi: Foundation Publishers

Motanya, M.M, Kisurulia, E. & Sawe, S. (2021). Ukiushi kama Elementi ya Kimtindo katika Baadhi ya Riwaya Ken Walibora. *International Academic Journal of Social Sciences and Education.* 2 (2);340-353 https://iajournals.org/articles/iajsse_V2_i2_340-353.pdf ISSN 2518-2412

Mukuthuria M. (2006). Kiswahili and it`s expanding roles of development in east african cooperation: a case of Uganda. *Nordic Journal of African Studies* 15(2):154-165 (2006).

Murumba, J.B. (2013). *Mtindo katika watu wa Gehenna* (Olali, 2012). Unpublished MA Thesis,UoN.

Musembi N.N. (2008).*Matumizi ya taswira na ukinzano kama kichocheo cha zinduko katika riwaya za G.K. Mkangi Mafuta (1984) na Walenisi(1995).*Tasnifu ya Shahada ya Uzamili,Chuo Kikuu cha Kenyatta.Haijachapishwa.

Musotsi, E.L. (2017). *Grafolojia katika uchapishaji wa riwaya ya Mkamandume.* Tasnifu isiyochapishwa ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili. Chuo kikuu cha Kenyatta.

Musotsi, E., Miruka, F., & Okal, B. (2021). Aspects of graphology in the construction of selected Kiswahili children's novels. *Research Journal in Modern Languages and Literatures*, 2(2). Retrieved from https://royalliteglobal.com/ languages-and-literatures/article/ view/59

Mwathe, K. & Wafula, K. (2009).*Saving a precious lake through the media:a dossier of press coverage of lake Natron campaign (2006-2009).* Nairobi:Birdlife international Partnership. Ken.mwathe@Birdlife.or.ke

Nyamari R. K. (2016). *Mtindo katika utenzi wa katirifu*.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, UON. (Haijachapishwa)

Njoroge, T.K. (2012). *A comparative content analysis of agricultural information coverage by the standard and daily nation kenyan newspapers (Sept 2011-Aug 2012*).Unpublished Diploma Thesis.UON

Oelofse, L.E. & Wates, O. (2015). *Dhima ya vyombo vya habari kwako*. European Journalism Centre .ISBN/EAN 978-90-819305-1-2

Odongo, F.O. (2014). *Uchanganuzi wa uwasilishaji wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maseno. https://repository.maseno.ac.ke/handle/123456789/1114

Oduor, J.A.(2016). *An analysis of Kenya`s mainstream print media`s usage of objectification and anchoring to represent the kenyan international crimnal court cases in the Daily Nation and the Standard news articles*. MA Thesis, Maseno University, Unpublished.

Oluwakemi, O. & Omoniyi, T. (2015). Colour in learning: it's effect on the retention rate of graduate students. university, Ago-Iwoye, Nigeria, Department of Science and Technology Education, Olabisi Onabanjo. *Journal of Education and Practice*, 6(14), 2015. Retrieved from *www.iiste.org*

Omondi, L.N. (1992). *Linguistics*. Nairobi: Nairobi University Press

Ong`ute, R.N. (2014). *Uhakiki wa suala la uhifadhi wa mazingira katika tanzu teule za fasihi ya kiswahili ya milenia mpya*. Tasnifu, Chuo Kikuu cha Maseno. https://repository.maseno.ac.ke/handle/123456789/934

Outuoma, D.A. (2019). *Mtindo na maudhui katika uchanganuzi wa vibonzo kwenye gazeti la Taifa Leo*. MA Thesis, UON, Nairobi (Haijachapishwa)

Owala, S O. (2014). *Uchanganuzi wa matini zilizoteuliwa za ugaidi katika gazeti la Taifa Leo la Kenya kati ya Oktoba 2010-Novemba 2011*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Maseno (Haijachapishwa).

Owala, S O. *et al* (2013). Effects of terrorism news on the readers of newspapers:a case study of Taifa Leo Newspaper of Kenya. *Academic Research International*. ISSN-L:2223-9553.

Owala, S O. *et al* (2013). A study of terrorism discourse in Taifa Leo newspaper in Kenya. *Mediterranean Journal of Social Sciences*. ISSN 2039-9340. Vol.4 No.4

Ononye, S.F. (2014). *Style, lexical choice and media ideology in selected English- medium newspaper reports on Niger Delta conflict, 1997_2009*. Unpublished PhD Thesis: University of Ibadan, Nigeria.

Panane, J. (2012). *An Assessment of the quality of environmental information disclousure of corporation in China*. Elsevier Ltd. Disheng Dash Wu.Cc By-NC-ND www.sciencedirect.com

Patterson, T.E. (2013). *Informing the news:the need for knowlwdge –based journalism*. Joan Shorenstein centre on the press/Amazon.com Barnes noble.

Ponton, D. & Larina, T. (2017). Discourse Analysis in the 21st Century: Theory and Practice (11). *Russian Journal of Linguistics*: 2017 Vol. 21 NO. 17-21. http://journals.rudn.rull//linguistics.

Portner, P.H. (2009). *Modality: Oxford surveys in semantics and pragmatics*. New York: Oxford University Press.

Richardson, E.J. (2007). *Analysing newspapers: an approach from critical discourse analysis*. New York: Palgrave Macmillan.

Rube, A.(2021).*Perceptions of "progress" among journalists in kenya:an exploratory study*. MA Thesis. Malmo University.

Saeed, J. (2009). *Semantics*. Malden: Wiley-Blackwell Publishers.

Schafer, M.S.*et al* (2016). *Investigating mediated climate change communication:a best practice guide*. ZORA URL:https://doi.org 10.5167/uzh-131746. Jonkoping University. School of edn & communication Research Project No.6 2016 www.ju.se ISBN 978-91-8833-05-8

Shalini M. *et al* (2020). *Gender based violence during covid-19 pandemic: a mini-review. frontiers in global women`s health*/www.frontier sin.org

Simpson, P. (2004). *Stylistics: a Rsource Book for Students*. New York: Routledge.

Taylor, C. (2019). *How to analyze newspaper language*. wikiHow.com

Thapthiang, N. (2013). *An analysis of news reporting and it`s effects, using ibil model: lee gardens plaza and c.s pattani hotels cases*. www.sciencedirect.com

Timucin, M. (2010). Different language styles in newspapers: an investigative framework. In *Journal of Language and Linguistics,* Vol. 6 No. 2

Turner, G.W. (1984). *Stylistics*.Harmondsworth: Penguin

Tripathi, N. (2006). *Mass communication:concepts and processes*. New Delhi: Reference Press.

UNEP (2021). Mbinu za Kiasili ni Muorobaini wa Kukabili mabadiliko ya Tabianchi. news.un.org/sw/tags/mazingira. 14.1.2021.

Van Dijk(1998). *Ideology: A Multidisciplinary Approach*. London: Sage Publications

Varzari, J.K. (2001). *Revealing or remedying discrimination?:critical discourse analysis and environmental law in alberta*. MA in Communication Thesis,University of Calgary.National Library of Canada.0-612-65059-6

Verschueren, J (1999). *Understanding pragmatics*. New York: Oxford University Press.

Wakibia, J.(2020). *Tutunze mazingira kwa hali na mali*.unep.org/sw/habari-na – matukio/tukio/tutunze-mazingira-kwa-hali-na-mali.

Wamitila, K.W.(2003) *Kamusi ya Fasihi:Istilahi na Nadharia*.Nairobi:Focus Publications Ltd

Wamitila, K.W.(2007). *Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Wanyama, A. (2007). *Maudhui na mtindo katika utendi wa "Khuswala Kamuse".*Tasnifu ya Shahada ya Uzamili,Chuo Kikuu cha Kenyatta.Haijachapishwa.

Weche,M.O.(2000).*Children`s literature as an image force:A case study of Ezekiel Alembi`s books*. MA Thesis, Kenyatta University. Unpublished.

Wesana-Chomi, E. (2013). *Kitangulizi cha mofolojia ya Kiswahili*. Dar-es-Salaam: University of Dar-es-Salaam Press.

Xiaoquan, Z. *et al* (2011). Attention to science/environment news positively predicts and attention to political news negatively predicts global warming risk perceptions and policy support. *Journal of Communication* 61 (2011):713-731.

Xianzhong H. *et al*.(2015). Contrastive analysis of lexical choice and ideologies of news reporting the same accidents between chinese and american newspapers.*Theory and Practice in Language Studies*. ISSN17799-2591. Vol.5 No.11, pp 2356-2365

Ya-Wen L. (2016).Freeing the press:how field environment explainscritical news reporting in china.The University of Chicago. 0002-9602/2016/12201-0001 AJS Volume122 Number1(July 2016):1-48

https://www.unenvironment.org.ac.ke.Communication and Mass Media.21st May 2

**KIAMBATISHO 1: CHETI CHA IDHINI YA KUFANYA UTAFITI KUTOKA KWA NACOSTI**

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **812806**

Date of Issue: **04/May/2022**

**RESEARCH LICENSE**

**This is to Certify that Ms.. Nelly Nzula Kitonga of Maasai Mara University, has been licensed to conduct research in Nairobi on the topic: Tathmini ya Matumizi ya lugha na mtindo wa wasilishaji wa habari za mazingira katika gazeti la taifa leo la Kenya for the period ending : 04/May/2023.**

License No: **NACOSTI/P/22/17155**

**812806**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

National Commision for Science, Technology and Innovation

**KIAMBATISHO 2: BARUA YA IDHINI YA KUFANYA UTAFITI KUTOKA SHULE YA MAFUZU**

**Maasai Mara University**

BOARD OF POSTGRADUATE STUDIES

**OFFICE OF THE DIRECTOR**

**P.O. BOX 861 – 20500**
**Narok, Kenya** www.mmarau.ac.ke

**Tel: +254 – 20 -2066042**
**+254 – 20 - 8081874**

**13th April, 2022**

RESEARCH PERMITS SECTION
NACOSTI
UTALII HOUSE

**REF: NELLY NZULA KITONGA (DA05/4001/2015)**

We wish to confirm that the above named is a *bona fide* PhD student at Maasai Mara University pursuing a PhD in Kiswahili in the School of School of Arts, Humanities, Social Studies and Creative Industries. Her proposal research is *Tathmini ya matumizi ya lugha na mtindo wa uwasilishaji wa habari za mazingira katika gazeti la Taifa Leo la Kenya*'. She would like to apply for a research permit from NACOSTI before she can proceed for field work and data collection.

We further confirm that the candidate has adhered to all research protocol requirements of Maasai Mara University and the proposed research has been rated as having no known adverse impacts on the environment and does not pose any ethical concerns.

This is therefore to request your office to issue her with a research permit.

MAASAI MARA UNIVERSITY
P. O Box 861 - 20500
NAROK
13 APR 2022
DIRECTOR
BOARD OF POSTGRADUATE STUDIES

Faithfully yours,

**Prof. Romulus Abila, PhD.**
**DIRECTOR, BOARD OF POSTGRADUATE STUDIES**

## KIAMBATISHO 3: BARUA YA IDHINI YA KUFANYA UTAFITI KUTOKA KWA KAMPUNI YA *NATION MEDIA GROUP*

**Nation Media Group PLC**
Nation Centre,
Kimathi Street,
P.O Box 49010 G.P.O
Nairobi 00100 Kenya
Telephone: +254 20 3288000/1/2/3
Mobile: +254 719038000/ +254 732138000
Email: customercare@ke.nationmedia.com
Website: https://www.nationmedia.com


**Directors**
W. D. Kiboro, Chairman
S. Gitagama, Group Chief Executive
D. Aluanga
S. Dunbar Johnson (British)
S. Hassan
L. Huebner (American)
Y. Jetha (British)
T. Masasa (Tanzanian)
W. Mwangi
F. Okello
L. Otieno
A. Ramji (British)
S. Sejjaaka (Ugandan)
R. Tebiko


To:
Nelly Nzule Kitonga,
P.o Box 11054 – 00400.
NAIROBI.
October 26, 2023

Dear Ms Kitonga.

**<u>SUBJECT: REQUEST FOR PERMISSION TO USE THE CONTENTS OF THE *TAIFA LEO* NEWSPAPER FOR ACADEMIC RESEARCH</u>**

Thank you for your letter of 21/10/2023, requesting permission to use the contents of the *Taifa Leo* newspaper for your academic research towards a PhD.
We are happy to support your research by granting the permission sought, provided that the use of Taifa Leo content is for academic purposes only, and proper attribution is made.
We wish you success in your academic endeavors.
Best Regards,

Pamella Sittoni.
Group Managing Editor.

Group Divisions: Nation Newspapers, Nation Broadcasting, Nation Carriers, Nation Digital.